Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 3 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti, (Mhe. Jenista J. Mhagama ) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Taarifa ya Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 118

### Kukamilisha Ujenzi wa Shule ya Sekondari Kata ya Vigwaza

**MHE. HENRY D. SHEKIFU (K.n.y. MHE. ZAYNAB M. VULLU)** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Vigwaza wamefanikisha ujenzi wa shule ya Sekondari ya Kata ya Vigwaza, yenye wanafunzi 775 wanaosoma; pamoja na juhudi hizo bado kuna madeni ya mafundi na hitaji la Maabara na Maktaba ambayo wananchi kwa nguvu zao hawawezi kuyakamilisha;-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Maabara, Maktaba na miundombinu mingine muhimu katika shule hiyo?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la MheshimiwA Zaynab Matitu Vullu, (Mbunge viti) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, wananchi wa Kata ya Vigwaza na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kuweza kutoa fursa ya kupata Elimu ya Sekondari kwa jumla ya wananfunzi 775 katika Kata ya Vigwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa maendeleo kuhakikisha utoshelevu wa miundombinu ya shule ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika katika kutekeleza azma hii, mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia mwezi mei, 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilipata shilingi milioni 283.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 76.6 ni kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba za walimu, shilingi milioni 50 ni kwa ajili ya ukarabati wa shule ya Sekondari ya Bagamoyo na shilingi milioni 24 ni kwa ajili ya ununuzi wa *Mobile Labs. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imetengewa fedha kwa ajili ya miundombinu mbalimbali ikiwemo maabara shilingi milioni 108 na madarasa shilingi milioni 144.

Natoa wito kwa Halmashauri Kusimamia matumizi sahihi ya fedha hizi na kuhakikisha maelekezo ya Serikali kukamilisha miradi ya zamani yanazingatiwa kabla ya kuanza miradi mipya ikiwamo ukamilishaji wa ujenzi wa maabara na maktaba katika shule ya Sekondari Vigwaza.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina swali moja la nyongeza ambalo zaidi ni la kisera kwa niaba ya Wananchi wa Bagamoyo hasa wa Vigwaza. Sera ya inahimiza uanzishwaji sekondari za Kata ilipewa msukumo maalum mwaka 1906.

Mpaka mwaka 1907, msukumo huo kwa sasa unaonekana haupo kwa hiyo Halmashauri na wananchi wameachiwa jukumu la kujenga na kumalizia shule hizi. Serikali ina tamka nini katika kuhakikisha kwamba azma ile iliyokuwepo ya kuendeleza majengo yaliyojengwa yamalizike kwa msukumo unatolewa na Serikali?

**MWENYEKITI:** Hiyo Sera ninadhani kuna marekebisho yaliyofanyika mwaka 2007 ninadhani ili kuweka kumbukumbu sahihi. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu tafadhali kwa niaba ya Halmshauri zote katika nchi ya Tanzania, hili ni swali la kisera.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru sana kwa kufanya marekebisho na kwa sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambayo umefanya marekesho kwamba sera hii ya ujenzi wa shule za

sekondari nchini ilikuwa ya mwaka 2005/2006 mpaka 2007. Ninataka kutumia nafasi hii kuwapongeza wananchi Tanzania nzima kwa kazi kubwa ya kushiriki kikamilifu katika kujenga shule zetu za Kata ambazo sasa zimeanza kuonyesha mafanikio mazuri ya kuingiza vijana wengi katika shule hizi. *(Makofi)*

Matokeo tumeshayaona kama ambavyo pia tulileta vijana waliomaliza kidato cha sita hapa waliofaulu vizuri kupitia shule za Kata. Lakini bado pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi kwasababu vijana wetu sasa wanapata nafasi ya kukaa kwenye vyumba vya madarasa pamoja na changamoto tulizonazo. Lakini bado Serikali inao mkakati wa dhati kabisa kuhakikisha kwamba shule hizi zinapata mashiko ili ziweze kufanya kazi zake vizuri kama ambayo nimeeleza hapa. Katika kila Halmashauri nchini tumelazimika kuziongezea Bajeti kadri ambavyo wao wanaweka bajeti zao ili kurekebisha na kukamilisha miundombinu iliyopo ikiwemo maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza kuwa kwa sasa tunao mkakati pia wa kuboresha zile shule kongwe ambazo zilikuwepo kwa kuzipelekea milioni 50 kwa ajili ya ukarabati zirudi katika sura yake ya kawaida.

Lakini sasa pia tumeenda kwenye eneo ambalo tunachangamoto kubwa la elimu ya sayansi tumeshapeleka kila Halmashauri nchini milioni 24 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara tunaita ‘’*Mobile labs*” ambazo pia zimewahi kuonyeshwa pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua mwaka jana. Kwa

hiyo kila Halmashauri sasa ina fedha hiyo tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani katika kila Halmashauri kuhakikisha kuwa katika kila fedha tunazotuma zinatumika vizuri kama ambavyo tumekusudia, ahsante sana.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kuiuliza Serikali tatizo ambalo linafanana na hilo swali lililoulizwa hapo juu, limefanana kabisa na Jimbo la Babati Vijijini.

Serikali iliahidi kusaidia na kukamilisha ujenzi wa maabara, maktaba na miundombinu mingine katika shule mbili za Endakiso na Dohom ambapo kwa sasa hata bajeti zingine zikipangwa shule hizo mbili hazipangiwi bajeti yoyote na mpaka leo hii hakuna maendeleo yoyote. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kukamilisha shule mbili hizi za sekondari ya Endakiso na Dohom?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Kama ambavyo nimeeleza na inawezekana kabisa hizo zako mbili ziko kwenye mpango ule tuliokuwa tumeutangaza mwaka wa fedha mwaka 2011/2012 kwamba katika kila Halmashauri tumetenga shule mbili ambazo tutaziboresha na zitakamilika na katika mwaka huu wa fedha pia tumeshatenga fedha kwa ajili ya shule 264 ambazo zitaboreshwa kwa miundombinu

yake yakiwemo maeneo uliyoyataja ya maabara na maktaba.

Pia Halmashauri zenyewe kupitia mabaraza yao watakuwa wameshapanga Bajeti ya uboreshaji wa shule hizo ikiwemo shule ambayo ameitaja. Kwa hiyo, ni jukumu lenu sasa kwenye Halmashauri yenu kuhakikisha kuwa Bajeti mnayoipanga na fedha hii ambayo itakuja ambayo ni *top up* zote zifanye kazi kwa pamoja. Lakini bado tuendelee kuwasisitiza wananchi kushiriki kikamilifu katika kuchangia ujenzi wa miundombinu mbalimbali mashuleni kwetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata lakini pia ninafikiria Mheshimiwa Naibu Waziri kama unaweza ukatutengenezea orodha ya hizo shule ambazo zitakuwa *facilitated* na Wizara moja kwa moja ukatugawia Wabunge wote kabla ya bajeti yenu.

Itakuwa ni jambo la busara sana ili Waheshimiwa Wabunge wawe kwenye *position* ya kuelewa nini kinachoendelea katika kila Halmashauri. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, naona kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Mpina.

Na. 119

**Upungufu wa Watendaji wa Vijiji Nchini**

**MHE. JOELSON L. MPINA (K.n.y. MHE. SAID M. MTANDA)** aliuliza:-

Maeneo mengi ya vijijini nchini yamekuwa na upungufu mkubwa wa Watendaji wa Vijiji, hali inayochelewesha utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo.

(a) Je, ni vijiji vingapi vya Jimbo la Mchinga havina Watendaji wa Vijiji?

(b) Je, ni kwa kiwango gani ukosefu wa Watendaji hao umechangia kuzorotesha maendeleo ya wananchi kwenye Vijiji husika?

(c) Je, ni lini sasa Watendaji wa Vijiji wataajiriwa na kupangwa kwenye Vijiji husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya Kata / Vijiji nchini zina upungufu wa Watendaji wa Kata na Vijiji. Jimbo la Mchinga pekee lina upungufu wa watendaji

watano (5) wa vijiji. Vijiji hivyo ni Mvuleni ‘A’, Michee, Chilala, Komolo na Matapwa.

(b) Halmashauri zinao wajibu kwa kuzingatia Sheria kuteua Kaimu watendaji ili kujaza nafasi zilizo wazi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtendaji wa Kata/ Kijiji anapo kaimishwa kushika nafasi hiyo anao wajibu wa kuhakikisha majukumu aliyopewa yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Hata hivyo inapotokea matumizi mabaya ya Fedha za Umma au kutumia madaraka vibaya kwa maslahi binafsi, mtendaji huyo huchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Lindi imeomba kibali cha kuajiri watendaji wa vijiji kumi (10) ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi tano (5) zilizo wazi katika Jimbo la Mchinga.

Ajira za watendaji hawa sasa zitafanywa na Halmashauri zenyewe kwa kuomba kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma badala ya utaratibu wa zamani ambapo ajira hizi zilikuwa chini ya Sekretarieti ya Ajira ya Utumishi wa Umma.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri upungufu wa watendaji wa vijiji hivi upo na kwamba nafasi zao zimekuwa zikikaimiwa na baadhi ya watendaji

wengine Serikali au watu wengine wanaofanya shughuli zingine.

(a) Je, sasa atawathibitishia wananchi wa Mchinga kwamba mara watakapoleta kibali cha kuomba kuajiri watendaji hawa kitatoka mara moja bila kipingamizi?

(b) Kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la maslahi ya watendaji wetu hawa katika ngazi chini kwa maana ya watendaji wa vijiji na Kata nchi nzima.

Naibu Waziri atawathibitishia leo Watanzania hawa walioko kwenye Kata hizi kuwa maslahi yao sasa yataboreshwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao sawasawa, kwa kuwa kwa sasa hivi wanalipwa ujira mdogo sana.

**NAIBU WAZIRI,OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili nyongeza ya Mheshimiwa Mtanda, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti kama nilivyooeleza hapa na kama mlivyotusikia tulivyokuwa tunapitisha Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kada hizi kumi zilikuwa ziko kule kwenye sekretarieti kwenye Wizara yenyewe kada hizi sasa zimerudishwa kwetu sisi kwa hiyo ni kwamba kuna urasimu tena kuwa tutakuwa tunaomba kibali habari hii imekwisha.

Lakini hataweza mtu kuajiri bila kpata kibali kutoka Wizara ya Utumishi Ofisi ya Rais bado suala hili linabaki

palepale kwasababu huwezi kuajiri 20,30,50 kwasababu ina Bajeti *implications,* Kwahiyo, ninataka kumthibitishia Mheshimiwa Mpina kwamba baada ya maelekezo haya iko Sheria ambayo ilitupeleka kule Utumishi tunataka kufanya marekebisho ili Sheria ile iturudishe tena kule kwenye Halmashauri kwa kada hizo ambazo zinazungumzwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu maslahi Waziri wa Utumishi ndiye anayezungumza hapa. Mtakumbuka kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tulipitisha kitu kinaitwa *General Purpose grant* ilikuwa imeondolewa na Serikali lakini baadae Serikali ikakubali kupitisha tena ikarudishwa hii ndiyo ambayo inasaidia pia hawa watendaji anao wazungumza wa Vijiji na Kata, kuhusu maslahi yao kama yataboreshwa na kuwa mazuri mimi ushauri wangu ninamwomba Mheshimiwa Mpina haraka haraka apitishe hii Bajeti inayosemwa hapa akishapitisha Bajeti hii haya matatizo yatakuwa yamekwisha kwasababu tutaboresha pia na kuangalia huko kote mtamsikia atakapozungumza yeye mwenyewe.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona na mimi niulize swali dogo nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna ukosefu mkubwa wa Watendaji Vijijini na kwa kuwa wamekuwepo Watendaji wa Vijiji wengi ambao wana kaimu nafasi hizo hususani wa Wilaya ya Singida Vijijini.

Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani ili hao Watendaji ambao wame kaimu kwa muda mrefu na

ambao wameonyesha uwezo mkubwa wa kufanya kazi wapewe vibali vya kuajiriwa na kuwa Watendaji kamili, Mheshimiwa Naibu Waziri unasemaje kuhusu hili suala la Watendaji ku- kaimu kwa muda mrefu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti hizi nafasi ku-kaimiwa ni kweli kwanza ninapenda nikiri hapa mbele yake kwamba ni kweli kwamba ziko nafasi nyingi za Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji zinaonekana mpaka sasa hivi zina kaimiwa.

wengine tumeenda tukachukua walimu, wengine tumechukua maeneo s*ensitive* lakini *the bottom line is* kusema sasa kuwa huyu tunamfanya awe Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Kijiji tutaangalia sifa pia maana ninaweza kutamka hapa halafu kesho asubuhi unakuta mtu kachukuliwa huko kasukumwa pale halafu itakuwa mlisema kwamba tuchukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi hapa la kuzingatia ni hilo lakini tumezitaka Halmashauri zetu kupitia Makatibu Tawala wa Mkoa wa- *coordinate* vizuri hili zoezi waangalie wale ambao wana kaimu watuambie ni nani na walete mapendekezo yao ili na sisi walau tuweze kushiriki kwenye kusema sawasawa.

Na. 120

## Viwanja Vya Michezo Nchini

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA)** aliuliza:-

Kabla ya nchi yetu kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi viwanja vya michezo kumi na mbili(12) vilikuwa mali ya Watanzania wote lakini baada ya kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, viwanja hivyo viliendelea kumilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), na kwasababu wananchi walichangia viwanja hivyo husika pasipo kujali itikadi zao katika kipindi hicho:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa viwanja vile 12 vikarudishwa kwenye Halmashauri husika ili viwe sehemu ya mapato kwa Halmashauri hizo ambako kila mwananchi atafaidi matunda yake bila kujali itikadi zao?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina sababu za msingi za kuomba kuhamisha miliki ya viwanja 12

kutoka kwa mmiliki wake wa sasa na kuvikabidhi kwa Halmashauri kama inavyoshauriwa. Viwanja 12 vinavyozungumzwa sasa ni mali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama hicho kinavimiliki viwanja hivyo baada ya kufuata taratibu zote husika.

Hata hivyo, Serikali itakuwa tayari kuvipokea wakati wote kwa hatua zaidi kutegemea sababu ya kuvikabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu za Wizara yangu, viwanja hivi hutumiwa na Watanzania wote bila kujali tofauti za Kiitikadi na pia Mamlaka za viwanja hivyo hulipa kodi kwa mamlaka za kodi za maendeleo husika na hivyo kuchangia pato katika mfuko wa Serikali, fedha ambayo ni kwa huduma mbalimbali kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, kati ya viwanja hivyo 12 ni pamoja na kiwanja cha kumbukumbu cha Sokoine, Mbeya, CCM Kirumba Mwanza, Jamhuri Dodoma, Sheikh Amri Abeid Arusha, Mkwakwani, Tanga na vinginevyo.

(a) Kwa kuwa CCM siyo chama cha michezo na kwa mujibu wa kumbukumbu za Bunge tarehe 2 Novemba, 2007 Serikali ilikiri hapa Bungeni kuwa viwanja hivyo vilijengwa kwa nguvu za wananchi na kwa kuwa, Tume ya Nyalali mwaka 1992 ilipendekeza kuwa viwanja hivyo virudishwe Serikalini.

Je, ni lini CCM na Serikali watatekeleza mapendekezo ya tume ya Nyalali ya Mfumo wa Vyama Vingi kurudisha viwanja hivyo?

(b) Hivi karibuni vyombo vya habari vimenukuu taarifa za CCM zikikiri kushindwa kuviendesha viwanja hivyo na hivyo kuanza mchakato wa kutafuta wabia wa ndani na wa nje ya nchi kuviendesha viwanja hivyo. Sasa kama CCM imeshindwa kuviendesha ni kwa nini sasa viwanja hivyo visirudishwe Serikalini ili vikatumika kwa ufanisi na kwa manufaa ya Watanzania wote?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yaliyotolewa na Kamati ya Nyalali ni mapendekezo na kwamba viwanja hivi havikujengwa na wananchi vilijengwa na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, (CCM) na viwanja hivi vilijengwa kwa michango ya hiari na kujitolea. Kwa hiyo hili bado linathibitishwa pia na kesi iliyofunguliwa na Edson Mbogoro mwaka 2010 kesi Na. 16 ambayo Jaji Bubeshi alithibitisha kwamba viwanja hivi ni mali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Pili, si kweli kwamba CCM imeshindwa kuvihudumia viwanja hivi bali wanao uhuru wa kuamua ni namna gani ya kuviboresha na viwanja hivi bado vinatumika naamini kabisa kwamba Chama cha Mapinduzi kinao uwezo na mimi nimewahi kuwa Mweka Hazina kwa miaka minne hatujashindwa kuviendesha viwanja hivi. (*Makofi*)

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa sera za mapinduzi ni kuendeleza michezo na ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kinamiliki viwanja hivyo. Kwa kuwa, viwanja hivyo vinatumika na wananchi wote na ndiyo viwanja vikubwa katika nchi yetu na vinatumika mara nyingi sana, lile eneo la kuchezea *pitch* imeharibika na siyo nzuri.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuongea na Chama cha Mapinduzi ili Serikali iweze kutengeneza ile *pitch* kwa maana ya kuweka hata nyasi bandia?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye na ninapokea ushauri huo na CCM nafikiri wamepokea ushauri huo kwa namna ya kuweza kuviboresha viwanja hivyo. (*Makofi*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, hali iliyopo hivi sasa ya viwanja ambavyo vimetajwa na mwuliza swali la msingi inadhihirisha kabisa kwamba Chama cha Mapinduzi ambacho kinadai kwamba viwanja hivyo ni vya kwakwe, kimeshindwa kuvihudumia viwanja hivyo na hii ni ishara kabisa kwamba viwanja hivyo havikujengwa na wanachama wa Chama cha Mapinduzi peke yao isipokuwa viwanja hivi kihistoria vilikuwa toka enzi za mfumo wa Chama kimoja na Chama kimoja ilikuwa ni chama cha Watanzania wote.

**WABUNGE FULANI:** *Kelele*

**MWENYEKITI:** *Order, order,* naomba uende kwenye swali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Je, Serikali haioni sababu ya kuweza kuviondoa viwanja hivyo mikononi mwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kime-claime hivyo baada ya kuvipora viwanja hivi kutoka mikononi mwa wananchi ambao si wa wanachama wa Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana naye kwamba viwanja hivi vimejengwa wakati wa mfumo wa Chama kimoja na ulijengwa na wanachama wenye moyo kwa kujitolea na michango ya hiari.

Kwa hiyo, kama kuna wanachama ambao wanaona kutoka Chama cha Mapinduzi na kuviacha viwanja warudi ili wamiliki pamoja na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 121

**Chombo cha Kufuatilia Mjadala Kwenye TV/Radio.**

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza**:-**

Kumekuwepo na vipindi vingi sana vya majadiliano katika *TV* na *Radio* mbalimbali nchini vikishirikisha Wabunge, Watalaam wa fani mbalimbali

pamoa na wananchi wa kawaida ili kupata fursa ya kuishauri, kuikosoa na kuirekebisha Serikali yao:-

(a) Je, Serikali ina chombo maalum kinachofuatilia mijadala hiyo ili kuifanyia kazi ili kutatua kero na malalamiko ya wananchi yanayolikabili Taifa?

(b) Kama chombo hicho hakipo. Je, kwa nini Serikali inadharau juhudi hizo za Vyombo vya Habari na wadau kama Wabunge, Wataalam na wananchi ambao wana lengo la kuleta maendeleo kwa Taifa lao?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Habari ikishirikiana na vitengo vya mawasiliano vya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali ina wajibu wa kufuatilia vipindi vya majadiliano vinavyorushwa katika *TV* na *Radio* mbalimbali nchini, vyenye lengo la kuleta maendeleo kwa Taifa.

Hivi sasa tuna televisheni 26 na radio 86 ambazo zinaendesha majadiliano kwa Wabunge, watalaam na wananchi kwa nyakati tofauti. Wingi huu wa

televisheni na radio ni dhahiri kuwa ni changamoto kwa Idara ya Habari na vitengo vyake kufuatilia majadiliano yanayoendeshwa na vyombo vyote vya habari. Aidha, Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo imeanzisha tovuti ya wananchi inayoratibiwa na Idara ya Habari Maelezo. Kwa kupitia tovuti hiyo wananchi wa kawaida pia wanapata fursa ya kuishauri, kuikosoa na kuirekebisha Serikali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba Serikali inadharau jitihada za vyombo vya habari na wadau wengine bali inafuatilia vyombo hivyo kupitia katika vitengo vyake vya mawasiliano vinavyoratibiwa na Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, kupitia Idara ya Habari.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Nasikitika kwamba swali langu halikupata jibu sahihi na ningeweza kutumia Kanuni ya 46 lakini kwa kuwa naelewa kwamba niliuliza chombo ambacho kinaratibu na kufuatilia masuala haya kwa ajili ya utekelezaji.

Lakini kuanzisha tovuti watu wakaanza kupeleka mijadala tena na kushauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa naomba uende kwenye swali.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakwenda sasa kwenye swali. Vipindi vinavyotolewa mfano vipindi vya kipima joto, kipindi cha Baragumu na vipindi vya *Star TV*

vinavyotolewa na kuunganishwa na Dodoma, Dar es Salaam pamoja na ~~TBC~~ pia, vipindi hivi vina mafunzo makubwa ambapo Serikali inaweza ikajikosoa na kujitathmini wapi wamekwenda *wrong.*

Je, ikiwa chombo hiki hakipo nataka unihakikishie Waziri kwamba sasa Serikali ipo tayari kuunda hiki chombo kwa kuwa imeshakosekana na tovuti siyo chombo ambacho kinaleta ushauri?

Pili, waandishi wa habari na vyombo hivi ni mhimili wa nne usio rasmi wa Serikali na mhimili huu una mchango mkubwa kuelimisha jamii kwa namna mbalimbali.

Sasa kama Wizara yako inaratibu, uko tayari sasa kutuletea vipindi vyote na mambo yote haya kwa mpangilio wa kundi la siasa, michezo, mambo ya sayansi na vipindi vya kipimajoto ili na mhimili huu wa Bunge tuweze kuvipitia na kuangalia na kutathmini kipi kimetekelezwa na kipi hakijatekelezwa?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika jibu langu la msingi alitaka chombo kinachoratibu majadiliano, nasema chombo kinachoratibu ni Idara ya Habari na Taasisi zake ikiwepo Mamlaka ya mawasiliano. Kwa hiyo hao ndiyo wanaotupa kumbukumbu nini kimejadiliwa. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti la Pili; ni kwamba tumepokea ushauri wako nataka niseme tu kwamba habari hizi zote katika vyomvo vya habari zinafuatiliwa,

zipo habari za kuibua uovu, zipo habari za kuonesha kero, zipo habari za kushauri za watalaam wa kiuchumi.

Nataka nikuhakikishie kwamba Serikali muda wote inafuatilia majadiliano haya na kufanyia kazi. Vituo nilivyovitaja vya redio 86 wakati mwingine havisikiki Dar es Salaam viko katika Wilaya na hata Televisheni zipo zinazoonekana Dar es Salaam na baadhi ya mikoa na zingine ni za Halmashauri.

Kwa hiyo, Serikali iko makini inafuatilia majadiliano yote na kuyafanyia kazi.(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mwanahabari mwingine Mheshimiwa Juma Nkamia, hebu tumpe nafasi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Katika siku za karibuni vyombo vingi vya habari hasa televisheni vimekuwa vikionesha michezo ya kuigiza kutoka nje ambayo kwa hakika inapotosha mila na desturi za Mtanzania.

Je, Serikali kama inafuatilia kama Naibu Waziri alivyokiri, hili nalo hawalifuatilii ama hawalioni?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakata niseme kwamba Wizara yetu kama nilivyosema inafuatilia

kupitia *TCRA* na Idara ya Habari lakini pia tunayo Kamati ya maudhui ambayo inafuatilia filamu zote zinazokuja na vipindi vyote vinavyorushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea dokezo hilo kwamba kama kuna jambo hilo limetokea Wizara yangu inawezekana imeshalipokea halijafika hapa lakini tutalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kessy bado tuna muda wa kuchangia Wizara hiyo na tunakazi nzito mbele yetu. Naomba uniruhusu niendelee na swali linalofuata, tunahama kwenye Wizara hiyo ya Habari sasa tunaenda Wizara ya Maji na swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 122

**Ahadi ya Kusambaza Maji Kata - Itagano na Ihango**

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE** aliuliza:-

Katika Bunge la Tisa Serikali iliahidi kusambaza maji katika Kata ya Itagano na Ihango kwa kutumia chanzo cha maji cha mto Malagala.

Je, kazi hiyo ya kusambaza maji itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Itagano na Kata ya Ihango ni kata mbili zilizopo katika Halmashauri mbili tofauti ambazo zinatenganishwa na barabara. Kata ya Itagano ipo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Kata ya Ihango ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini. Chanzo cha kuhudumia Kata hizo ni mto Malagala kama aliyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Itagano imepewa kipaumbele na Halmashauri ya Jiji la Mbeya katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu. Mtaalam mshauri amefanya usanifu wa mradi kwa kutumia chanzo cha mto Malagala. Wakati wa utekelezaji wa mradi kwenye Kata ya Itagano, itawekwa sehemu ya maungio *tee junction* kwa ajili ya kupeleka maji katika Kata ya Ihango.

Katika mwaka 2012/2013, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imetenga shilingi milioni 236.1 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kata hiyo. Mkandarasi wa ujenzi ameajiriwa na sasa anafanya maandalizi ya kwenda katika eneo la kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini inatekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwenye vijiji 17 vya kipaumbele ilivyochagua.

Katika awamu ya kwanza, utekelezaji utahusisha vijiji vitatu vya Shongo, Igale na Iwalanje ambapo Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu amepatikana na ujenzi utaanza na kukamilika katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Miradi hiyo itagharimu jumla ya shilingi bilioni 1.1. Kata ya Ihango haikupewa kipaumbele na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini katika awamu ya kwanza ya programu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini inashauriwa kuingiza Kata ya Ihango kwenye vipaumbele vyake vya utekelezaji wa programu ya maji vijijini katika awamu zinazofuata.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri, lakini kwa kuwa Kata ya Itagano na Kata ya Ihango ni Kata ambazo ziko jirani na wenzao wa Kata ya Itagano wanapatiwa maji.

Je, Serikali haiwezi kutenga fedha ya dharura kwa ajili ya kuhakikisha kwamba na hawa watu wa Ihango nao wanapata maji kama wenzao wa Itagano?

Kwa kuwa Serikali katika Bunge lililopita iliahidi kwamba mradi huo utakapokuwa unafanyiwa usanifu hasa kwa upande wa Mbeya Mjini, basi wataunganisha kazi hiyo.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Kata ya Ihango ambao pia wangepatiwa maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoshauri hapa ni kwamba kwa kuwa hizi Kata zimepakana na kwa kuwa upande wa Jiji la Mbeya wameweka kipaumbele cha Kata ya Itagano kupata maji na chanzo cha maji ni cha mto Malagala ambacho ndiyo chanzo hicho hicho cha Kata ya Ihango iliyopo Mbeya Vijijini inatarajia kukitumia.

Kwa kuwa gharama za ujenzi kwenye kutega maji kwenye chanzo cha maji cha mto Malagala tayari zitafanywa na wenzetu hawa wa Mbeya Mjini, ina maana kwamba kazi inayobaki kwa Kata ya Ihango iliyopo Mbeya Vijijini itakuwa ni kuchukua maji kutoka kwenye ile *junction* na kuanza kazi ya ujenzi wa miundombinu na kusambaza.

Tunachoshauri ni kwamba katika ile miradi ya vijiji vitatu katika vijiji kumi, vitatu ambavyo vimepewa kipaumbele katika ile Halmashauri ya Mbeya Vijijini vimeongezeka Vijiji viwili kama alivyosema Waziri siku zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri vile vijiji viwili vinavyoongezeka viingizwe kwenye Kata hii ya Ihango ili viweze kufanya kazi ya kuepeleka maji kutoka kwenye ile *junction* ambayo itakuwa imetengenezwa na Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usanifu uliofanywa na Mbeya Mjini ni kweli kulikuwa na mkakati

huo kwamba vile vijiji vyote ambavyo vilikuwa pembezoni mwa Jiji la Mbeya vifanyiwe upembuzi yakinifu pamoja na sehemu za Mjini Mbeya kwa ajili ya kupata ufadhili wa Ujerumani.

Lakini masharti yalipokuja Ujerumani wakasema hapana watapenda sana kutoa fedha zao kwa ajili ya miradi ya Mjini. Kwa hiyo usanifu wa Vijiji hivyo umefanywa lakini itabidi miradi hii igharamiwe kupitia *WSDP* programu ya maji ambayo inasimamiwa na Wizara yetu na kama nilivyoshauri wakifanya hivyo wataweza kutekeleza mradi huu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa, matatizo ya maji katika Jimbo la Igunga yanafanana sana na matatizo ya maji katika Jimbo la Mbeya Vijijini, na kwa kuwa mradi wa kusambaza maji katika Kata za Mbutu, Isakamaliwa na Mwamashimba ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia umechelewa sana;

Je, Serikali itakamilisha lini mradi huu wa kusambaza maji katika maeneo haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Igunga kuna mambo mawili pale. Jambo la kwanza upo mkakati wa kutoa maji kuendeleza ule mradi wa Shinyanga na Kahama ili maji yaweze kufika pale Igunga. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali imetenga

bilioni moja kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa ile miradi ambapo Igunga ni mojawapo.

Lakini sehemu ya pili ni hii miradi ya Vijiji kumi, vipo vijiji ambavyo vimepewa kipaumbele na Halmashauri ya Igunga ambavyo itakuwa ni kati ya zile orodha ya zile Halmashauri ambazo zimepita na kwa sababu hapa sina naweza nikamwonesha tukitoka. Lakini tayari kuna Halmashauri 61 ambazo tayari zimeruhusiwa kuanza utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaomba orodha ya Halmashauri hizo 61 kabla ya Bajeti yetu ili kusudi Wabunge waanze kuzitambua ili kupunguza mjadala wakati wa hotuba ya Wizara ya Maji.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara inayofuata. Maswali yanahamia Wizara ya Viwanda na Biashara na swali hilo la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo.

Na. 123

## Ubinafsishaji wa Viwanda/Makampuni.

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza**:-**

Viwanda vingi vilivyoanzishwa katika awamu ya kwanza vimebinafsishwa au kuuzwa. Kwa mfano, kiwanda cha nguo cha Urafiki, Ubungo *Garments*, Ubungo *Spinning Mill, Polysacks*, Tanzania *Sewing Thread, Coastal Dairies (TDL)* na Kiwanda cha Zana za Kilimo *(UFI)* na hivyo kuathiri pato la taifa na ajira kwa wananchi.

(a) Je, kwa nini Serikali haikamilishi kushughulikia malalamiko ya mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa viwanda hivyo kwa miaka zaidi ya kumi sasa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa viwanda hivyo vilivyoacha au kubadili uzalishaji kinyume na mikataba na hivyo kuathiri miundombinu, kupoteza mapato na kupunguza ajira?

(c) Je, Serikali itafanya lini uchunguzi na kuweka mfumo thabiti wa usimamizi wa fedha kwa makampuni ambayo bado ina hisa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama i fuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wafanyakazi walioachishwa kazi katika viwanda vilivyotajwa na Mheshimiwa Mnyika, *Ubungo Spinning Mill 283, Polysacks 145, Coastal Dairies (TDL)* na Kiwanda cha Zana za Kilimo *(UFI)* 270 walilipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria. Aidha, madai ya iliyokuwa *Tanzania Sewing Thread Manufacturers Ltd.* yalilipwa kupitia ufilisi uliofanywa na Benki ya Rasilimali. Kiwanda cha

Maziwa cha *Tanzania Diries Limited* kiliwekwa chini ya ufilisi wa lililokuwa Shirika la Utafiti na Ushauri wa Maendeleo ya Viwanda *TISCO* ambapo wafanyakazi walilipwa mafao yao kwa mujibu wa Sheria ya Ufilisi.

Wafanyakazi wa kiwanda cha nguo Urafiki hawakupunguzwa kazi kwa sababu mkataba wa ubinafsishaji ulibaini kwamba wafanyakazi waendelee na ajira zao. Hata hivyo endapo ulazima wa kuwaachisha kazi ukijitokeza basi Serikali itabeba jukumu la kulipa mafao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwalipa mafao wafanyakazi waliopunguzwa kazi Serikali imeendelea kupokea madai ya mapunjo kutoka kwa waliokuwa wafanyakazi wa viwanda na mashirika mbalimbali yaliyobinafsishwa na yamekuwa yakishughulikiwa kulingana na hoja na vielelezo vinavyojitokeza.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Wizara yangu kwa kushirikiana na *Consolidated Holdings Cooperation (CHC)* kufanya uchambuzi wa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vimefungwa na kubadilishwa matumizi. Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa ili kujaddiliwa katika ngazi ya pili ya maamuzi. Hata hivyo, Serikali imewaruhusu baadhi ya wawekezaji kwa makusudi kubadili matumizi ya viwanda pale ambapo mabadiliko yalionekana kuwa na manufaa kwa Taifa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usimamizi wa fedha za makampuni yenye hisa zaidi ya 40

hukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *CAG* na taarifa kupelekwa kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya taarifa na hatua zake zaidi. Kitu ambacho kilikuwa hakifanyiki hapo mwanzo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sijaridhirika na sehemu (a) ya majibu kwa sababu nina vielelezo vya madai ya mafao na madai ya mapunjo ambavyo Wizara inavyo kwa zaidi ya miaka 10 bila kuchukuliwa hatua. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa kwenye sehemu (b) ya swali Serikali imeonyesha kwamba viwanda hivi vimefanyiwa uchambuzi na waraka umepelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na sehemu kubwa ya viwanda hivi vimefungwa na vijana wanakosa ajira na vinashindwa kuchangia kwenye pato la Taifa.

Sasa kwa kuwa hivi karibuni ilinukuliwa kwenye vyombo vya habari Rais Mstaafu Benjamin Mkapa akiwa Jimboni Ubungo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akisema kwamba sera ya ubinafsishaji ilikuwa na mafaniko makubwa lakini hali yenyewe ndio hii kwamba viwanda vimefungwa.

Je, Wizara iko tayari waraka huu utakapojadiliwa kwenye Baraza la Mawaziri kumshauri Rais kubatilisha mchakato wa ubinafsishaji ovyo ovyo uliogubikwa na ubinafsi ambao umelifikisha taifa hapa ili tuanze ukurasa mpya?

(b) Katika sehemu (c) ya jibu nashukuru kwamba Serikali imepinga kwamba ukaguzi umeanza kufanyika.

Je, Serikali iko tayari sasa badala ya taarifa hizi za *CAG* kupelekwa kwa msajili wa Hazina taarifa hizi kuletwa kwa Bunge ili kuondoa udhaifu ambao umejitokeza muda wa makampuni haya na makampuni mengine kama *UDA,* Kariakoo, Kibuku na mengine ambayo Serikali ina hisa kidogo taarifa zije Bungeni ili tuisimamie Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mnyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mnyika anashauri Baraza la Mawaziri limshauri Rais ambatilishe ubinafsishaji mimi nafikiri ni wazo lake lakini Baraza la Mawaziri hupokea waraka ambao una mapendekezo maalum.

Kwa hiyo, waraka ambao umeandaliwa ndio utakaoamua nini kifanywe kwenye Baraza hilo pamoja na hiyo ripoti ambayo imeletwa. Kwa hiyo, hili lisubiri nafikiri kama itaonekana kuna haja kutokana na tathimini hiyo basi majibu yatakuwa kama ulivyoshauri.

Kuhusu ripoti ya ukaguzi ya masharika ambayo asilimia chini 50 kuletwa Bungeni hili nalo ni jambo la kisera ambalo maamuzi ni baada ya mashauriano na hatua zitachukuliwa.

**MHE. REBECCA M MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa katika awamu hiyo hiyo ya kwanza kulikuwepo na viwanda ambavyo vilichangia sana katika kutoa ajira kwa wananchi kama vile *Kili-Textile, Sungura Textile, Mwatex* na kadhalika. Ningelipenda kujua viwanda hivi vilipatwa na nini? Je, Serikali ina mpango gani wa kuvirudisha katika uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rebecca swali ni moja tu, umeuliza mawili kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri ataamua kujibu moja kati ya hayo mawili, lini na kwa nini? Kwa hiyo, atajibu moja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nakujibu la nyongeza la Mheshimiwa Mngodo kama ifuatavyo:-

Viwanda vingi pamoja na mashirika ambayo yalibinafsishwa yalishindwa kujiendesha wakati ule na tatizo kubwa lilikuwa ni uendeshaji kwa maana ya utawala au menejimenti.

Kwa hiyo, pamoja na matatizo hayo ilikuwa Serikali pia ilikuwa na uamuzi wa kutoka kwenye biashara za moja kwa moja na kutaka sekta binafsi ichukue dhamana hiyo na ndio maana pamoja na kushindwa kujiendesha lakini pia pamoja mabadiliko ya sera ililazimika viwanda hivi vibinafsishwe. Ahsante sana.

Na. 124

## Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Elimu Zanzibar

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itaanzishwa Zanzibar ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wanaonufaika na mikopo hiyo?

(b) Je, ni vigezo gani vilitumika kujenga Vyuo vyote vya Taifa upande mmoja wa Muungano wakati elimu ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya wananchi wake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, (Mbunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Zanzibar umekamilika na ofisi imeanza kazi rasmi tarehe 1 Aprili, 2012. Ofisi hiyo ipo Kinanzini k aribu na Jengo la Benki Kuu ya Tanzania Mjini Unguja.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kila upande wa Muungano una Vyuo Vikuu. Inawezekana kukawepo na idadi tofauti ya Vyuo Vikuu kwa kila upande wa

Muungano kutokana na ukubwa wa eneo, lakini pia historia na matakwa ya waanzishaji wa Vyuo Vikuu.

Hata hivyo, bila kujali Chuo kipo sehemu gani ya Muungano, lengo lake ni kuwahudumia vijana wote kutoka pande zote za Muungano na wanaotoka nje ya Muungano bila ubaguzi ili mradi mwombaji awe na sifa za kitaaluma zinazohitajika katika chuo husika na kozi anayoiomba. Watoaji na waanzishaji wakuu wa elimu ya Vyuo Vikuu nchini ni Serikali na taasisi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kuna Vyuo Vikuu vya Umma vitano na Vyuo Vikuu Binafsi viwili na kwa upande wa Tanzania Bara kuna Vyuo Vikuu 11 vya Umma na Vyuo Vikuu Vikuu binafsi ni 34.

Uanzishwaji wa Vyuo Vikuu unategemea uwezo wa Kifedha wa Serikali lakini kwa kiasi kikubwa unategemea sekta binafsi ambayo imetoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa Elimu ya Juu pande zote za Muungano. Aidha, uanzishwaji wa Vyuo Vikuu unategemea uwepo wa wadau (wanafunzi wenye sifa, rasilimaliwatu, mtaji, wahadhiri, miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia) pamoja na madhumuni halsa ya kuanzisha Chuo Kikuu husika.

Kwa mantiki hii Vyuo Vikuu havianzishwi kwa maana ya kuongeza idadi bali kwa madhumuni maalum kutegemea mahitaji halisi. (*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza mawili mawili , kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wako vijana wenye uwezo na wanapata usumbufu mkubwa sana wa kupata mikopo na kufikia hadi kushindwa kusoma.

(a) Je, unaweza kulieleza taifa taratibu mahususi ambazo wanafunzi hawa watafuata kwa madhumuni kwamba hawatapata usumbufu na kuweza kupata mikopo?

(b) Je, kutokana na hali hii hatuoni kwamba katika upatikanaji wa mikopo kuna na kujuana au ubaguzi unaosababisha hata baadhi ya vijana wasipate mikopo na mifano hai ipo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utaratibu wa kukopesha wanafunzi wa Vyuo Vikuu suala hili linaeleweka. Lakini mtakumbuka mwezi wa Aprili, 2012 tulipokuja hapa kuleta sheria ya mabadiliko ya baadhi ya vifungu kwenye sheria hizi Wabunge wote mlisema kwamba hapana Wizara irudi ikaangalie upya vigezo vya kukopesha wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisikia na Kamati ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti Mama yetu Margareth Sitta, tayari suala hili lipo kwenye Kamati na Wizara inajiandaa kuleta vigezo hivyo ili lile litamkwe rasmi hapa Bungeni. Waheshimiwa Wabunge muone

Serikali ilivyoweza kujipanga namna ya kurekebisha baadhi ya vigezo vya ukopeshaji wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hilo ndio lilikuwa swali la msingi labda la pili lingine sikulisikia vizuri.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Kuhusu upendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama kuna upendeleo wowote namna ya kukopesha vijana hawa. Kinachotakiwa pale tunafuata vigezo vya kitaaluma na kozi anayochukua kijana.

Kama nilivyosema kwamba yawezekana likawa linaonekana kama upendeleo kwa sababu ya vigezo vilivyopo na Waheshimiwa Wabunge mlisema ninyi wenyewe kwamba tuangalie vigezo upya.

Kwa hiyo, hiyo ndio sababu inayopelekea sasa tuweze kuleta vigezo hizo *mini testing* kwa wakati ujao na kabla ya mwisho wa Bunge hili tutaleta vigezo rasmi vitakavyoanza kutumika kuanzia mwaka huu wa fedha.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Zanzibar ina wakazi kama 1,300,000 tunawazidi Mkoa wa Rukwa tuna watu milioni 1,600,000 na Zanzibar wamejengewa Ofisi ya Bodi ya Mikopo. Kwa nini Rukwa na Mikoa mingine ina watu

zaidi ya milioni 1,300,000 isijengewe Ofisi za Mikopo? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama alivyosema kwamba Zanzibar kuna idadi ndogo ya watu tumepanga Ofisi ya Bodi ya Mikopo kule lakini akawa anasema kwamba kwa nini na Sumbawanga na Mikoa mingine kama Mbeya nako tuweze kujenga ofisi hizo. Waheshimiwa Wabunge naomba tutambue kwamba Ofisi za Bodi za Mikopo tumepanga Dar es Salaam na hapa Dodoma na tujipange kufungua Ofisi hizo maeneo ya Mbeya, Mwanza na kule Arusha.

Lakini kikubwa hapa bado mpaka sasa hatujapata usumbufu wowote wa namna vijana wanavyojiunga na wanavyokopesheka hizi fedha kwa sababu kama nilivyosema kwamba sisi tunatumia mfumo wa kompyuta zaidi.

Lakini tumepeleka huduma ile Zanzibar kwa ajili ya mahusiano ya Kimuungano na hali yenyewe ya usafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Zanzibar. Tayari Ofisi hiyo imeshaanza kufanya kazi tangia tarehe 1 Aprili, 2012 kule Zanzibar. Ni namna moja ya kuimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Na. 125

## Kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Miundombinu ya Reli

**MHE. JUMA SURURU JUMA** aliuliza:-

Uimarishaji wa sekta ya uchukuzi nchini ni suala la uchumi endelevu hapa nchini na Afrika Mashariki hasa katika Sera ya Usafiri wa Majini, Barabara, Anga na Reli.

(a) Kutokana na umuhimu huo. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuunda mfuko maalum wa maendeleo ya miundombinu ya Reli, ambao utawezesha kuinua uchumi na masuala ya ukarabati wa mabehewa, njia za reli na madaraja?

(b) Kama Serikali itakubali kuanzisha mfuko huu. Je, Serikali itakuwa tayari kushirikisha wadau wa sekta ya usafiri wa reli wa huduma za abiria na mizigo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Reli Namba 4 ya mwaka 2002 iliyoanzisha *RAHCO* kifungu cha 18 kinaipa Taasisi hiyo mamlaka ya kuanzisha na kuendesha Mfuko wa Uendelezaji wa miundombinu ya Reli *(Railways Infrastructure Fund).*

Kwa sasa Wizara yangu inaandaa waraka kwa ajili ya kuanzisha Mfuko huo. Aidha, mara baada ya kukamilisha kwa waraka huo utawasilishwa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge itawashirikisha wadau wote wa Sekta ya Uchukuzi wakiwemo wanaotoa huduma za abiria na mizigo katika mchakato wa uanzishaji wa mfuko huo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nataka kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, ni kwa nini suala hili limechelewa kuanzishwa tokea ilipoanzishwa sheria mwaka 2002 na lini litakamilika kuanzishwa mfuko huu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tangu mwaka 2002 mpaka leo ni takribani miaka kumi. Kwa hiyo, inaweza ikaonekana kwamba suala hili limechelewa. Lakini ifahamike kwamba *RAHCO* ilianzishwa kwa madhumuni maalum wakati huo Shirika la Reli la Tanzania likiwa linaingiwa katika utaratibu wa ubinafsishwaji.

Mambo yaliyoendelea kati ya mwaka 2007 mpaka mwaka 2009 nadhani inafahamika kuwa

Watanzania wote tulivunja mkataba. Kwa hiyo, tukarudi nyuma tena pale tulipoanzisha shughuli hizi upya.

Kwa mantiki hiyo ule utaratibu uliodhaniwa wakati ule kwamba ungetumika katika endeshaji sasa hauna nafasi sana na ndio maana tunaandika waraka maalum ambao utazingatia hali ya sasa ya Shirika letu la reli kwa ujumla kwa maana ya *RAHCO* na *TRL* na sekta zingine za uchukuzi ili tuweze kuona kwamba mfuko huu utanufaisha sekta nzima ya uchukuzi badala ya *RAHCO.*

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala hili ni la kipaumbele cha juu sana katika Wizara, tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Na. 126

## Serikali Kulipa Fidia

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA** aliuliza**:-**

Upasuaji wa miamba wakati wa ujenzi wa barabara itokayo Kagoma hadi Lusahunga katika eneo la Kalebeza na nyumba za wakazi wa eneo hilo zimeathirika na milipuko ya miamba hiyo:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa walioathirika na zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kuwa kumekuwepo na athari za milipuko ya baruti wakati wa kulipua miamba iliyokuwa kwenye eneo la ujenzi wa barabara katika maeneo ya vijiji vya Kalebezo, Ng'ambo na Nyarukongogo katika Wilaya ya Biharamulo Mkoani Kagera.

Baada ya milipuko mnamo Oktoba, 2010 Wakala wa Barabara Mkoani Kagera (*TANROADS*) ilipeleka mtalaam wa milipuko aliyetoka Ofisi ya Kanda ya Ziwa Victoria iliyoko Mkoa wa Mwanza. Mtalaam huyo aliweza kubainisha mali zilizoathiriwa na milipuko hiyo ya baruti kama ifuatavyo:-

Kati ya wananchi 45 katika Vijiji vya Kalebezo, Ng'ambo na Nyarukongogo Wilayani Biharamulo waliolalamikia kuwa nyumba zao na mali nyinginezo zimeathiriwa na milipuko ni walalamikaji 25 tu ambao mali zao zilionekana kuwa zimeathirika na milipuko hiyo ya baruti na walalamikaji 20 waliobaki nyumba zao athari zake hazikutokana na milipuko ya baruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya mtaalam huyo ilipelekwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Biharamulo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo mnamo tarehe 24 Januari, 2011 ambaye aliwapatia taarifa hiyo wananchi husika ambao nakala ya taarifa hiyo ilipelekwa pia Katibu

Tawala wa Mkoa wa Kagera na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Nyumba na mali nyingine za wananchi hao 25 walioathirika na milipuko hiyo zilifanyiwa uthamini na mthamini wa Serikali (*Valuer*) kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Taarifa ya tathimini ilitumwa kwa Mhandisi Mshauri tarehe 10 Juni, 2011 ili itoe maelekezo kwa Mkandarasi kwani ndiye anayestahili kulipa. Mkandarasi atakuwa amelipa fidia kwa wahusika ifikapo mwezi Septemba, 2012.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba niseme wazi kwamba taarifa hii, majibu haya, hayaendani na hali halisi ilivyo. Swali.

(a) Kwa kuwa baada ya tathmini ya kwanza ilionekana wananchi wengine hawakuridhika na hiyo tathmini na wakajitokeza kulalamika na hivi ninavyoongea ni wiki moja imepita tena huyu *valuer* ameenda kufanya tathmini nyingine. Je, hamwoni kwamba tathmini iliyofanyika ilikuwa na mapungufu?

(b) Kwa kuwa Mkandarasi huyu anaelekea kumaliza kazi na hapa mnajibu kwamba mwezi Septemba ndiyo atalipa, hauoni kwamba ni kuweka wananchi mashakani kwamba malipo yao hayatafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Dkt. Anthony Mbassa, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza kabisa taarifa kwamba wananchi hawakurithika na tathmini sinayo, tunachosema ni kwamba tumeshafanya tathmini kuonyesha kwamba athari za mlipuko maana yake hapa tuna vitu viwili kwamba kuna athari za mlipuko halafu na ile thamani ambayo imefanyiwa tathmini. Sasa hiyo nyingine ambayo anaizungumza hatujaipata.

(b) Naomba nimwondoe wasiwasi kwamba pamoja na kwamba Mkandarasi anakwenda vizuri na ujenzi wa barabara, amepewa maagizo na bado yuko *site* kwa hiyo suala hilo atalitekeleza kama Serikali anavyoagiza.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge nilishatoa rai toka swali lililopita sitoruhusu maswali ya nyongeza na mliona nilifanya hivyo kwa Mheshimiwa Juma. Kwa hiyo sitaendelea kutenda haki kama maswali mengine nitaongeza maswali ya nyongeza.

Naomba nimalize sasa niende kwenye swali la Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lakini namwona jirani yake na kaka yake, Mheshimiwa Senator Professor Kapuya, atauliza swali hilo kwa niaba ya Mheshimiwa Saidi Nkumba.

Na.127

## Hitaji la Umeme- Vijiji vya Sikonge

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MHE. SAID J. MKUMBA**) aliuliza:-

Vijiji vya Usanga, Mole, Chabutwa, Ipole na Mpombwe vimeombwa na vinakidhi viwango vya kupatiwa umeme:-

Je, ni hatua gani imefikiwa hadi sasa ya kuvipatia Vijiji hivyo umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Kwanza nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi alivyoibadilisha Sikonge na kuwa moja ya Wilaya zinazovutia kimaendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwenda katika Vijiji vya Usanganya, Chabutwa na Ipole utatokea Sikonge Mjini, umeme wa Mole utatokea Kijiji cha Tutuo na umeme wa Kijiji cha Mpombwe utatokea Mpombwe *Centre*. Gharama za kupeleka umeme katika Vijiji hivyo ni shilingi bilioni 3.8 na gharama hizi zitatumika kujenga kilomita 94 za njia ya umeme ya msongo wa KV 33 na ufungaji wa *transfoma 12.* Jumla

ya wateja 500 wanatarajiwa kupatiwa umeme katika mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *REA* ipo katika hatua za maandalizi ya awamu ya pili ya mradi kabambe wa umeme Vijijini na Vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vimejumuishwa katika mradi huu utakaoanza kutekelezwa katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2012/2013 na inategemewa kukamilika baada ya miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Vijiji vya Sikonge vinafanana kabisa na Vijiji vya Wilaya mpya ya Kaliuwa vilivyoko katika Kata za Ushokola, Ubisiganga, Zugimlole, Ukazaroho, Igwisi, Igagala, Kamsekwa, Kaliowenye, Ugunga na kwa kuwa *REA* walishakuja na kufanya tathmini.

Je, ni lini Vijiji hivi navyo vitapatiwa umeme kwa utaratibu huu?

(b) Kijiji cha Usinge kiko kilometa 90 kutoka Makao Makuu ya Kaliuwa, ripoti ya *REA* ilipendekezwa kwamba hapa wapatiwe *generator* kubwa ya umeme

na vile vile nilikuwa nimemwalika Mheshimiwa Waziri aje atembelee na azungumze na wananchi wa Usinge.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja na lini atatekeleza ahadi ya kupeleka *generator* kubwa usinge?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Professor Juma Athuman Kapuya, kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini kupitia *REA* inayo miradi mingi ya kuhakikisha inasambaza umeme katika Vijiji na maeneo, *centres* mbalimbali nchini na miradi hii tumeipanga katika awamu tofauti.

Lakini katika awamu ambayo tutaanza katika mwaka wa fedha huu wa 2012/2013 ni Vijiji hivi nilivyovitaja ndivyo vimo kwenye mradi na tutakapoleta hotuba yetu ya Bajeti, viko Vijiji vingine kwa maeneo mengine nchini ambayo yataguswa na mradi wa *REA* ambao tumegawa kwa uwiano kwa nchi nzima.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge asubiri wakati wa Bajeti ya Wizara yetu yako maeneo ambayo katika Mkoa wa Tabora tumeyaainisha ambayo tutayatekeleza katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 na kama Vijiji alivyovitaja havitokuwemo, basi tumevichukua tutaviweka katika awamu inayofuatia. *(Makofi)*

(b) Swali la pili ameuliza ahadi ya *generator* katika Kijiji cha Usinge. Nimechukua ahadi hii na mimi nitazungumza na wenzangu Wizarani ili kuangalia utekelezaji wa ahadi hii na nimhakikishie tu kwamba sisi kama Wizara ya Nishati na Madini, tuko tayari kutembelea maeneo mbalimbali kukagua miradi ya maendeleo na nimhakikishie kwamba tutapanga naye kulingana na kalenda ya shughuli za Bunge, tuone lini tutakwenda Usinge kuangalia maendeleo katika Kata ya Usinge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge ajenda ya maswali kwa siku hii ya leo imekwisha.

Kwa hiyo, kabla hatujaendelea na ajenda nyingine naomba nitoe matangazo. Kwanza naomba niwatambue wageni ambao wako ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa siku ya leo.

Mgeni wa kwanza kabisa ni mgeni wa Mheshimiwa Spika na nitaomba pale alipo aweze kusimama ni Ndugu Nestory Matiku. Wageni wanaofuata ni wageni wa Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mwenyekiti wa Bunge na Mbunge wa Peramiho na hawa ni kama wafuatao. Kwanza ni Ndugu Rajab Hassan Mtiula, yeye ni Diwani wa Kata ya Mpitimbi na Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Songea. Naomba Mheshimiwa Rajab Mtiula asimame.

Lakini ameongozana na Ndugu Vedastus Martin Mfikwa, huyu ni Diwani wa Kata ya Mkogotema, lakini ni Katibu wa Madiwani wa Chama cha Mapinduzi

katika Halmashauri yetu na ni Katibu Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, naomba Ndugu Vedastus naye asimame.

Lakini wameongozana na Mke wa Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya Margareth Mtiula, ningeomba na yeye asimame. Ameongozana na Afisa wa Serikali za Mitaa kutoka Mkoa wa Ruvuma anaitwa Christina Kumwenda. Ningeomba Dada Christina asimame. Nawashukuru sana, karibuni sana Mheshimiwa Mwenyekiti ukiona sipo sipo kule Wilayani, mambo yenyewe ndiyo kama unavyoyaona hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wanaofuata ni kama wafuatao. Mheshimiwa Naibu Waziri Majaliwa anao wageni wake ambao ni Madiwani wa CCM 28 kutoka katika Halmashauri ya Ruangwa. Wageni hawa 28 ni viongozi wa CCM naomba wasimame hao Madiwani 28 wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Ruangwa. (*Mafoki*)

Lakini wameambatana na Madiwani wenzao kutoka Chama cha CUF naomba na wao wasimame. Wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri huyu Mwenyekiti wa Halmashauri ana jina zuri sana, anaitwa Mheshimiwa Songea, ana jina zuri sana Mwenyekiti huyo. *(Makofi)*

Lakini ameambatana na Watendaji watatu (3) kutoka katika Halmashauri hiyo hiyo hiyo. Naomba na wao wasimame. Kwa hiyo, Halmashauri hiyo ina ushirikiano wa kutosha sana. Wote wanafanya kazi

kwa pamoja na kiongozi na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge wako wanafunzi 86 na Walimu wao kutoka shule ya Msingi Lugalo, Dar es Salaam naomba wasimame. Lakini wako wageni wengine nadhani ni wa Mheshimiwa Mpina hawa, hawa ni washiriki 23 wa *Miss Higher Learning Institution* wakiongozwa na Miss Agnes Mathew. Naomba na wao wasimame, Miss Agnes Mathew tungeomba wasimame, Ma-Miss wako jamani hapa, wameungana na sisi katika siku hii ya leo. Naomba watupungie mkono tuwaone kwa kweli nadhani Waheshimiwa Wabunge hawajaona vizuri. Waheshimiwa Wabunge naomba muwatazame vizuri, hawa wasomi wamekuja kuungana nasi leo hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Tunaona Wajumbe 17 wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam wakiongozwa na *President* wao Ndugu Beatus Mtani naomba hao wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wako pale ndani. Kwa heshimiwa ya Rais wao, ningeomba Mheshimiwa *President* upunge mikono yako ili tuweze kukutambua, ahsante sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 6 kutoka shule ya Sekondari ya Jamhuri naomba nao wasimame kama wapo hapa ndani, tunao wanafunzi wengine 34 kutoka *Tanzania College of Early Education* na hao sijui wako sehemu gani. Lakini nadhani watakuwa labda bado hawajaingia na tunaona wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma naomba wasimame kama

hawajasimama basi na wao watakuwa bado, oh! Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninao pia wageni wa Mheshimiwa Faith Mitambo, hawa ni Viongozi kutoka Kijiji cha Kikuliungu Jimbo la Liwale na wamekuja hapa kushughulikia mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji chao na pori la akiba la Selou kule Liwale. Ningeomba na wao wasimame sijui watakuwa wamesimama wapi? Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mitambo nawashukuru kwa kuja kujumuika na sisi.

Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe matangazo ya kazi. Tangazo la kwanza limeletwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ananiomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa leo tarehe 3 Julai, 2012 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi namba 227 jengo la Utawala.

Mheshimiwa Professor David Homeli Mwakyusa, yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Mifugo, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa watakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 3 Julai, 2012 saa saba mchana. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 219 jengo la utawala. Kwa hiyo, naomba sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kikao saa saba Ukumbi Namba 219.

Nimeombwa pia na Mheshimiwa Charles Mwijage, huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Nishati na Madini, ameomba Wajumbe wa Kamati Ndogo ya Nishati na Madini kukutana leo tarehe 3 Julai, 2012 saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa C. Kwa hiyo, hawa nao wanaombwa wakutane ili waweze kupitia masuala mbalimbali ya kibajeti.

Waheshimiwa Wabunge nafikiri baada ya matangazo hayo sasa nimwite Katibu ili tuendelee na ajenda inayofuata.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi natumia Kanuni ya 47 kutoa Hoja ili tuweze kujadili suala la madaktari ambalo linaendelea hapa nchini, kwa sababu hatuwezi tukaliacha Serikali imeamua kuacha, inatumia ubabe, madaktari wanaendelea kugoma na watu wanakufa. Sasa kama Bunge tusipoingilia kati suala hili tukalijadili, tukatoa na maamuzi, itakuwa ni kinyume na tutakuwa hatuwatendei haki wananchi.

Kwa hiyo, naomba kutoa hoja naomba Wabunge wenzangu mniunge mkono ili tuweze kujadili suala hili. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI**: Noamba Mkosamali ukae na Wabunge wote mliosimama mkae. Mheshimiwa Mnyika mwongozo unaofuata?

**MHE. JOHN. J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1).

**MWENYEKITI**: Kanuni gani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(1) ambayo naomba naisoma: "Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia, Sheria nyingine za nchi, Kanuni zingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge na Mila na Desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania".

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote Spika alishatafsiri neno "mapema" ambalo liko kwenye Kanuni ya 68(7) kumaanisha jambo lolote ambalo limetokea katika siku ya karibuni.

Sasa naomba mwongozo wako kwamba jana katika mkutano wa Bunge, Mwenyekiti wa Bunge, alitoa maneno yafuatayo kwa Wabunge wawili, kwa Mheshimiwa Machalli Mbunge wa Kasulu Mjini, alisema aache kimbelembele, anadandia hoja na anajitafutia umaarufu na kwangu akasema kwamba moja alisema

kwamba nimeshindwa kujibu taarifa iliyokuwa imesemwa jambo ambalo sio la kweli. Kwa kuwa sikupewa nafasi ya kujibu taarifa ya Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, lakini pili akasema kwamba nawashwa, sijui nawashwawashwa vipi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya maneno yameleta hasira sana kule kwa wananchi na wananchi wa Ubungo kule wameona haya maneno ni sawa wamekashifiwa wao au wameambiwa wao na naamini hata wananchi wa Kasulu Mjini haya maneno ni kama wameambiwa wao. Sasa Kanuni zetu za Bunge Kanuni ya 64 (2).

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa nenda sasa kwenye mwongozo kwa sababu ulishasema.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nataka kuomba mwongozo kutokana na Kanuni ya 64 (2) inatoa nafasi tu kwa Mbunge kutaka utaratibu kwa mambo yanayohusu Mbunge mwingine.

Sasa kwa jambo ambalo limemhusu Mwenyekiti, kukiuka Kanuni ya 64(1) (a) kusema mambo yasiyokuwa ya kweli, kukiuka Kanuni ya 64 (f) kusema vibaya kwa lugha ya matusi kwa Mbunge mwingine, kukiuka Kanuni ya 64 (1) (g), kutumia lugha ya kuudhi na kudhalilisha wengine.

Maneno ambayo vilevile yanakiuka Ibara ya 6, ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Naomba

Mwongozo wako, Wabunge tuchukue hatua gani kwa hali kama hiyo?(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hiyo Miongozo miwili. Lakini kwanza naomba niseme kwamba, Waheshimiwa Wabunge, nafikiri wote tunajua Kanuni zetu zinatuelekeza nini katika suala lolote ambalo linatokea hapa Bungeni.

Kwanza kabisa nikianza na Mwongozo wa Mheshimiwa Mkosamali, kwanza Mheshimiwa Mkosamali na yeye amevunja Kanuni kwa sababu, suala ambalo lilishafanyiwa Maamuzi na Mheshimiwa Spika, limeshafanyiwa Maamuzi. Kwa hiyo, unapotaka kurejea maamuzi ambao yalishatolewa *Rulling* na Mheshimiwa Spika, na wewe mwenyewe pia unakuwa unakiuka Kanuni kwa makusudi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, kwenye suala hili la Madaktari, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika, alishatolea maamuzi. Tena hata mimi ninashangaa sana Waheshimiwa Wabunge, wanaendeleza sana suala hili. Nilikuwa ninaomba, kwa mujibu wa Kanuni zetu, kama kuna mtu hajaridhishwa bado na maamuzi yanayohusu suala hilo, zipo taratibu nyingine za Kikanuni humu ndani, anaweza akalileta suala hilo sasa kwa kutumia njia nyingine ya Kikanuni kuliko utaratibu unaondelea sasa wa kuoneshana ubabe wakati mwingine na maneno ambayo kwa kweli, hayajengi heshima ndani ya Bunge letu. Zaidi ya hapo yanatufanya tu sasa humu ndani tuishie kugombana zaidi kuliko kujenga umoja wa kuwatetea hao Madaktari ama kuwatetea

Watanzania ambao wamekuwa wakiathiriwa na mgomo huo wa Madaktari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *Rulling* yangu katika hili, Mheshimiwa Mkosamali, hata wewe unakiuka Kanuni kwa sababu, tayari Maamuzi yalishafanyika. Kama Mheshimiwa Mkosamali, unaona kwamba, maamuzi yale yaliyokwishafanyika hayakukidhi wewe, tafuta Kanuni nyingine humu, tena ziko nyingi tu, sitaki kuwasomea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, nitapoteza muda wa wale ambao wanataka kuchangia Hotuba hii muhimu sana. *(Makofi)*

Vinginevyo, ningewasomea Kanuni moja baada ya nyingine, kwa mtu ambaye, hajaridhika na maamuzi afanye nini. Sasa nikianza hiyo kazi, kwanza hata mimi nitakuwa sijitendei haki kwenye hiki Kiti kwa sababu, tayari hata Mheshimiwa Mkosamali mwenyewe, ilitakiwa nianze na yeye kumhoji kwa sababu, ya kuvunja Kanuni. *(Makofi)*

Kwenye suala hilo jingine la Mheshimiwa Mnyika, nitalitolea Maamuzi baadaye, ama siku nitakayoona inafaa. Katibu, tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na (Utawala Bora) Pamoja na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu)

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Ninaomba niendelee kusisitiza kwamba, Maamuzi yote niliyoyatoa nimeyatoa kwa mujibu wa Kanuni na ninalindwa na Kanuni.

Kwa hiyo, ninaomba tusipoteze muda wa wananchi, tuendelee na Hoja yetu na Mjadala uendelee. Kwa sasa ninamwita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekifu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia. Naanza kuchangia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF. TASAF* niwapongeze sana kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakitekeleza miradi ya maendeleo nchini. Jimboni kwangu, wananchi wangu mnajua kwamba, tumejenga barabara nyingi sana za *TASAF.* Barabara ile inayochongwa sasa ya Tindabuligi – Longarohiga – Mwandu – Isangijo, barabara ya Mwabusalu kwenda Mwaukoli, barabara ya Itinje kwenda Mwafuguji. Barabara hizo zote zinaendelea kujengwa na nyingine zinatarajiwa kujengwa na Mfuko huu wa *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze *TASAF* kwa kazi nzuri ya kufungua mawasiliano ya Vijijini, kuviwezesha Vijiji kuwasiliana, kuziwezesha Kata kuwasiliana. Niombe sana kwamba, Mfuko huu wa *TASAF,* umekuwa ukifanya kazi nzuri, leo tunaenda kwenye Awamu ya III, ni vizuri sana uendelee

kuongezewa pesa, ili uendelee kutekeleza majukumu yake sawasawa. Niipongeze timu ya *TASAF* pale Wilayani, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuleta maendeleo, ya kuharakisha maendeleo kwa wana-Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kujitathmnini wa Umoja wa Afrika *(IPRM).* Kwamba, inasikitisha, sisi Tanzania, ni nchi ambayo ni ya mfano. Nimeenda maeneo mengi katika Vikao vingi, Vikao vya Bunge la Afrika, lakini Vikao vikubwa vya Kidunia, kama ule wa Korea ule wa Wahisani; tulikuwa na Mheshimiwa Mkullo, *by then,* kule Korea ya Mashariki. Tanzania inasifiwa kwa kazi nzuri ambayo tunafanya, lakini ni kwa nini *IPRM* toka tujiunge mwaka 2004, leo ni miaka 8, hatujalipa michango yetu tunayotakiwa kulipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni limefikia bilioni 1.25 hadi sasa. Sababu za kwanini, fedha hizo hazilipwi, wakati kila Mwaka wa Fedha, tunatenga fedha kwa ajili, ya kulipa kule. Fedha hizi huwa zinaenda wapi? Ni kwa nini hatulipi, hatuchangii katika Mpango huo wa Kujitathmini kwa Umoja wa Afrika *(IPRM)*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa *(PCCB)* yaani *TAKUKURU.* Katika Jedwali lao walilowasilisha kwenye Taarifa iliyowasilishwa na Waziri, kuanzia Julai, 2011 hadi Mei, 2012 kesi zilizofikishwa Mahakamani zilikuwa kesi 134, lakini kesi tulizoshinda ni kesi 46 tu. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, *TAKUKURU* wenyewe hawako makini katika tuhuma na kesi ambazo wanazifungua Mahakamani. Maana yake ni kwamba,

wanakurupuka katika kufungua kesi na kuzipeleka Mahakamani, mwisho wa siku zinakosa ushahidi wakutosha. Mwisho wa siku Taifa linaingia gharama kubwa ya kulipa gharama za kesi na pengine kuwalipa wale tuliowashitaki. Kwa sababu, unamshitaki mtu wakati ukiwa huna ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri zaidi kujua na kuchunguza kwa kina kabla ya hatua nyingine zinazofuata, hadi kumfikisha mtu Mahakamani, kuliko hivi ambavyo tunakurupuka. Kwa sababu, kesi 134, kushinda kesi 46 tu, sio jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulisisitiza leo, na siku hiyo bahati nzuri nililiuliza hapa Bungeni, sikupewa majawabu, nadhani leo nitapewa majawabu, nikiamini kwamba, Mkurugenzi wa *TAKUKURU* leo yupo. Maswali yangu yote haya, leo yatajibiwa. Kumekuwa kukiripotiwa wizi wa kutisha hapa nchini, fedha nyingi za Watanzania zinazotorishwa kwenda katika Mabenki kule Ulaya. Nilizitaja taarifa ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na Taasisi mbalimbali, ukiacha Taarifa za *CAG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa iliyowasilishwa *The Global Financial Integrity Report of 2008, with the Heading of Ilicit Financial from Africa, Hiding Resource of Development;* taarifa hii inabainisha wazi kwamba, Tannzania, imepoteza trilioni 16.6 ambazo zimefichwa nje na Wafanyabiashara pamoja na Watendaji wa Serikali. Sasa, lakini vilevile, utafiti uliofanywa na akina

Ndikumana na Boyo, katika mwaka huo wa 2008 na wenyewe unathibitisha hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa iliyotolewa majuzi na Taarifa hizo zote bahati nzuri ninazo hapa, Taarifa iliyotolewa juzi ya *1 Billion Dollar Question,* ambayo na yenyewe inathibitisha kwamba, kila mwaka Tanzania, imekuwa ikipoteza bilioni 478 kila Mwaka wa Fedha, kwa ajili ya *ilicit capital flow account.* Nazo hizi zinaenda kufichwa katika Mabenki kule nje. Lakini Taarifa ya mwisho ni ile Taarifa ya *Swiss Central Bank* na *Swiss National Bank,* ambayo wameitoa ikisema kwamba, Tanzania, kuna Watanzania 6 tu kule Uswisi, ambao wameweka kwenye akaunti za Uswisi, bilioni 315.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya Waziri, aliyoisoma hapa Bungeni, kitu hicho hakijatajwa, wala *TAKUKURU* wenyewe hawajasema wanalishughulikia vipi suala hili. Fedha hizi za Watanzania, nyingi sana, katika nchi masikini kama hii zingeweza kuwepo hapa nchini na zikasaidia sana kusukuma suala la maendeleo, kusukuma na kupunguza utegemezi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa na Dunia imejipanga vizuri hivi sasa kwamba, hakuna mahali popote ambapo Mtendaji wa Serikali au Mfanyabiashara anaweza kwenda kuficha fedha za umma. Kwa hiyo, popote pale kwa kutumia mfumo ulioanzishwa na *World Bank,* ambao kwa jina maarufu unaitwa *Stolen Asset Recovery Star Initiative.* Ambayo hii, inawezesha mahali popote kuzi-*trace* fedha za

wananchi zilizoibiwa, kuzitaifisha na kzuifilisi na kuzirejesha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninajiuliza, *PCCB* wanashindwa wapi kuhakikisha kwamba, fedha za Watanzania zilizoibiwa, zinataifishwa kwenye Mabenki kule na kurejeshwa hapa nchini? Benki Kuu, wanajua akaunti za kila Mtanzania, alizofungua nje, utata uko wapi? Mpaka sasa hivi, Watanzania hawajaelezwa fedha hizo ni za akina nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu, inajua akaunti zote za Watanzania, zilizo nje. Mpaka leo *PCCB* hawajasema, *TAKUKURU* hawajatuambia. Taarifa imewasilishwa hapa, hatujaambiwa kama Bunge, fedha hizi zinazozungumzwa ni fedha za aina gani? Zimeendaendaje? Ziko halali kule ziliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo, najua kabisa Mkurugenzi wa *TAKUKURU* ananisikia vizuri. Bwana Hosea yupo, ananisikiliza vizuri; alete majibu yakutosha ya kuwaeleza Watanzania, fedha hizi ni za akina nani? Zimeibiwa lini? Zitarejeshwa lini nchini? Ili tuweze kuendelea na mkakati wa shughuli za maendeleo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango. Naongelea Tume ya Mipango, suala la Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka mitano (5). Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka mitano (5), toka ulivyowasilishwa, tulifanya marekebisho katika Majedwali yale, lakini mpaka sasahivi marekebisho hayo hayajaletwa hapa Bungeni. Vitabu bado

vinawasilishwa vikiwa havina marekebisho yale tuliyoyafanya. Tulifanya marekebisho kwa mfano tukasema, Benki ya *TIB* pamoja na Benki ya Kilimo, badala ya kupelekewa bilioni 100 kwa miaka 5, zipelekewe bilioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitabu mpaka sasa hivi, haijafanyiwa marekebisho hayo. Kitabu bado kinaonesha vilevile kama tulivyosema mwaka jana, mpaka sasa hivi. Ni kwa nini, hatuletewi marekebisho hayo tuliyoyafanya ya msingi mpaka sasa hivi vitabu vinasema hivyo na ni kipindi cha mwaka mzima sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Kazi. Taarifa zilivyowasilishwa, Kitabu cha Mpango, ukiangalia katika Bajeti ilivyowasilishwa na Tume, bajeti yetu hii, na kama Taarifa ya Kamati ya Fedha ilivyozungumza, iliyosomwa majuzi na Mheshimiwa Mwenyekiti Andrew Chenge. Ukisoma Taarifa hii, utagundua ni fedha tu pekee zilizotengwa na Serikali, ndizo zilizooneshwa kwenye jedwali, lakini miradi yetu inatekelezwa na wabia, inatekelezwana Serikali.

Kwa hiyo, ilitakiwa pia katika jedwali hili ionekane, Sekta binafsi yenyewe itachangia kiasi gani kwa kila *item.* Lakini vilevile *item* zilizooneshwa ni zile zilizopewa pesa tu. Lakini *item* ambazo hazijapangiwa pesa, hazijaoneshwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaleta mkanganyiko mkubwa katika ufuatiliaji na utekelezaji wa Mpango wenyewe. Kwa sababu, Mpango ambao hauwezi kuu-

*trace* sasa. Mpango unaainisha wazi kazi zitakazofanywa kwa kila *item,* ukienda kwenye jedwali. Ilitakiwa iwasilishwe hivyohivyo hata zile *item* ambazo hazikupangiwa fedha mwaka huu, zingeainishwa halafu zikawekewa 0 kwamba, hazikutengewa fedha.

Lakini zile zinazotekelezwa na watu binafsi au sekta binafsi na zenyewe zingeoneshwa na watu binafsi hao wanachangia fedha kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa pia kwamba, utafiti wa matumizi ya Serikali; Tume ya Mipango, ilituambia wakati inawasilisha hapa kwamba...

*(Hapa, kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** ... itahakikisha kwamba, inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba, inapunguza matumizi yake ya kawaida. Tume mpaka sasa hivi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele ya pili. Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili, naomba uheshimu Kiti.

Tunaendelea na Mchangiaji anayefuata. Mheshimiwa Henry Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Injinia Mohamed Habib Mnyaa.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mungu, lakini nafsi yangu inanisuta nisipokukushukuru wewe pamoja na Spika na wote ambao wanajaribu kutuasa na kujaribu kutafuta

njia nzuri ya kuliendesha Bunge. Nimekaa Bungeni, miaka 10 nikaondoka, nimerudi tena Bungeni, nimekuta yanayofanyika ni tofauti sana. Niwaombe wenzangu, kwa upande mwingine kwamba, kukosoana na kukosolewa ni kitendo cha maendeleo. Lakini, basi, kauli na lugha hazioneshi sura ya utamaduni wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kuchangia katika eneo ambalo tunachangia leo, nianze kusema kwamba, Baba wa Taifa alisema, ili nchi iendelee inahitaji mambo manne (4) ambayo ni ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Sasa leo tunazungumzia eneo kubwa ambalo ni shughuli za Ofisi ya Rais. Ni ukweli kwamba, kama ilivyosemwa katika ukurasa wa 71 kwamba, ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu, tunahitaji pamoja na mambo mengine, utumishi wa umma unaozingatia misingi ya utawala bora, ambapo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zitatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za umma na taasisi zinazohusika ziko katika Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizi mbili nilizozitaja za mwisho, siasa safi, watu na uongozi bora, ziko Ofisi ya Rais. Mimi kwa kuchangia niseme tu kwamba, Wabunge wengi, wamezungumzia maeneo ya uhafifu, lakini mimi nijielekeze katika utaratibu kwa ushauri tu. Kwanza ninaomba ile Ofisi ya Urasimishaji Rasilimali, bado naamini haijatenda haki na pengine kwa kweli inahitajika sana kufanya juhudi za kurekebisha mambo yaende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoelewa urasimishaji mali, nia ni kupunguza umasikini na kuwasaidia wananchi waweze kupata kipato cha kupunguza umasikini huo, wapate kitu kinachoitwa dhamana. Mimi niliamini katika maeneo ambayo yangechaguliwa, yale maeneo ambayo inaonekana kabisa wananchi wako tayari, lakini kuna vizingiti vya maendeleo yao; kwa mfano maeneo yenye ardhi ndogo, kama Lushoto, nilitegemea kabisa maeneo kama haya yangepewa umuhimu na Serikali, ili wananchi warasimishe rasilimali zao kwa kuwapa Hati Miliki za Asili. Yale maeneo madogomadogo, waweze kuwekeza na waweze kupata Hati za kuwasaidia na waweze kuondoa umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa sielewi wenzetu wa Kitengo hiki, ni vipaumbele gani vinatolewa? Ningependa nipate jibu. Maana Wilaya tu zinachaguliwa, unasikia, hakuna *transparent* inayotosha. Hakuna mahali ambapo maeneo yale ambayo nayo yanaonekana ni muhimu, yanaguswa. Nasema wote ni Watanzania na wote tunapenda kuguswa. Lakini mimi ninafikiri katika kugawa, unamgawia yule aliye na tatizo zaidi, kuliko yule ambaye anacho na ana uwezo wa kujiendeleza, hapati haki. Hilo naomba, ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kwa kushauri. Kuna mapungufu machache katika Menejimenti ya Utumishi. Ukweli, juhudi zinachukuliwa kuongeza mishahara. Basi ni vizuri, kama Serikali ilivyoahidi, iishi kwa kauli yake; maisha ni magumu, wananchi wanahitaji kwa kweli, kuangaliwa.

Basi mishahara iendelee kuangaliwa na iangaliwe na tamko litolewe. Pamoja na kwamba, Sera inasema tusitamke, lakini ni vizuri, ni utamaduni wetu kwamba, unapofika mwezi wa sita hivi, tunaposoma Bajeti, wananchi wanaandaliwa. Ninajua yako madhara yake kwamba, bei zinaweza kupanda, watu wakaanza kupandisha bei, lakini ni vizuri wananchi wakaandaliwa kwamba, mwaka huu angalao, *minimum wage* itakuwa ni kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunategemea ongezeko la mshahara kiasi hiki. Maana hizi hela tunaziona bilioni 3, trilioni 3 ni nyingi, lakini nikiangalia utumishi na mambo yaliyopo, sio nyingi, tungependa ziwe trilioni 15, ili kila mtu apate mshahara tunaotaka. Lakini kwa sababu ya uwezo mdogo wa Serikali, ndio hicho.

Lakini hicho kidogo kinachotajwa kisifichwe, wananchi wajue. Hayo mambo mengine ya kupanda kwa bei ni wajibu wa Serikali, kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utendaji wa Serikali. Ni ukweli usiopingika sasa hivi utendaji umeshuka sana katika ngazi zote, wala haihitaji kuuliza. Ukienda Mahakamani, ukienda Hospitalini, Jeshini, ukienda kwenye Serikali, watu wako *lesser fair,* yaani ni yale mambo ya kawaida. Hakuna msukumo wa kujali kazi.

Nchi haiwezi kwenda. tunaweza tukatenga fedha nyingi sana. Lakini kama wanaotekeleza hawana msimamo wa kutekeleza, tunafanya kazi bure.

Mimi naishauri Serikali isimamie taratibu za kuisimamia Serikali, taratibu za kusimamia Watumishi ziimarishwe. Viongozi wawajibishwe, tusimwajibishe Waziri tu huku juu, hawa wa ngazi za chini, wanawajibishwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli si rahisi kwa Waziri kumfahamu kila mmoja na utendaji wake, anahitaji msaada sana kwa watendaji wengine ngazi za chini kutoka kwenye Halmashauri, Mikoani, wanahitaji msaada sana. Sasa hawa wanawajibishwaje? Ndiyo tukubaliane kila kiongozi aliye na nafasi yake a-*deliver* na kama hawasilishi matokeo mazuri aondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi katika maeneo nyeti, tunalo tatizo, sasa hivi zinajengwa zahanati, katika Jimbo langu mimi nina zahanati tatu ziko tayari lakini hakuna watumishi. Sera inasema tujenge zahanati kila kijiji, sasa naomba tuongeze *speed* ya wataalam na suala hili nasubiri Waziri wa Afya aje azungumze, sikupewa watumishi, aniambie tukafunge zile zahanati, tunaumia, wananchi wametoa nguvu, wamejenga zahanati, inafika mahali hawapati watumishi, zahanati zimekaa tu kama eneo la Mkuzi, kuna maeneo mengi tu katika Jimbo langu ambapo wamekosa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Sekretarieti ya Ajira, nafurahi kwamba Serikali imeamua kurudisha ajira huko ambako ziko, kurudisha kwenye Halmashauri na Mikoa, jambo hili litendeke haraka. Moja ya upungufu wetu ni kutamka mambo na inachukua muda mrefu sana kuyatekeleza. Hii inaondoa hata ari ya kazi. Hivi kuna tatizo gani la kuleta sheria haraka ili watumishi waajiriwe katika ngazi wanakohitajika? Tatizo liko wapi? Kila siku tunaahidi sheria itabadilika, maamuzi yameshafanyika, si vizuri, mimi nafikiri kwa utendaji mzuri ni kuamua na kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TASAF, TASAF* kwa kweli inafanya kazi nzuri lakini wasimamiaji wake bado wana matatizo. Katika Jimbo langu Lushoto kuna maeneo mengi miradi ya *TASAF* imeanzishwa lakini watumishi waliokuwemo mle wamekuwa wajanja, wamewalaghai wananchi, wamechukua fedha, wameondoka, miradi ile haikujengwa na wamehamishwa. Sasa mimi nitampelekea Waziri *list* na ninataka wachukuliwe hatua*. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Ya kwanza!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba *TASAF* pamoja na kazi nzuri na

malengo mazuri yaliyowekwa kwa ajili ya utendaji wake, madhumuni yake lakini utendaji, wafanyakazi wake waangaliwe kwa undani. Ninayo mifano na nitamletea Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni kuiomba Serikali ijitahidi, Ofisi ya Rais ni taasisi na ukitaka uheshimike ni lazima wewe baba kwenye nyumba uonyeshe mfano. Mimi naomba sana, Ofisi ya Rais ni sehemu ya heshima na kwa kweli hakuna nchi ambayo haiheshimu Ikulu, ukiona nchi hawaheshimu Ikulu hao watu wana matatizo, ni uasi. Basi kauli tunazotumia kuhusu viongozi wetu ziheshimu maadili ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuropoka na kuonyesha uwezo wako wa kupanua mbavu, si tabia njema kwa Watanzania lazima tusitahiane. Mimi nina wazee nilioanza nao Bungeni hapa, Mzee Mrema pale, Cheyo hata na Bwana mdogo Mbatia, hatujawahi kukemeana hivi na si sifa unapobebwa na Polisi wa Bunge wakutoe huko nje, ni aibu kwa Watanzania, hatuna utamaduni huo, hao wanaotaka kuuleta wanatupeleka kubaya. Makosa yapo na yeyote atakayepewa mamlaka naye atapata changamoto lakini hatutoi changamoto na matatizo kwa kukemeana, kuzomeana bila aibu. Mimi nawasihi sana wenzangu, nia iwe njema, ni kushauri Serikali yenu, Serikali yenu sikivu watasikia. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia

nafasi hii ambayo nilitakiwa niipate jana lakini kwa dharura za Kibunge sikuweza. Kwanza, nitoe tanibii, haijapata kutokea duniani mtu kupanda choroko akavuna mbaazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yaliyotokea jana Bungeni ambayo ni fedheha kwa Bunge ni katika yale mambo ya aibu ambayo tusingeyategemea lakini ndicho tulichopanda kwa hivyo nafikiri Watanzania nao watajifunza na tutajikosoa baadaye kwa pande zote*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli Mbiu ya Chama cha Wananchi *CUF* inasema 'haki sawa kwa wote'. Nitumie fursa hii leo kuitendea haki ofisi hii ya Rais. Katika kuitendea haki, nianzie hasa hiki kitu kinachoitwa utawala bora. Kila jambo katika dunia lina misingi na nguzo zake. Utawala bora una nguzo nane, ndiyo inapatikana kujengwa kwa utawala bora. Nguzo ya kwanza ushirikishwaji yaani *participation*, huo ndiyo utawala bora. Utawala bora unajengwa na nguzo ya pili utawala wa sheria, *rule of law*. Utawala bora unajengwa na nguzo ya tatu uwajibikaji, *accountability*. Utawala bora unajengwa kwa nguzo ya usawa kwa wote *equity and exclusiveness*. Utawala bora unajengwa na nguzo ya uwazi, *transparency*. Utawala bora unajengwa na nguzo ya huduma kwa wakati, *reponsiveness*. Utawala bora unajenga kwa nguzo ya tija na ufanisi, *efficiency and effectiveness*. Utawala bora unajengwa kwa nguzo ya kujenga makubaliano, *consensus building*. Hapo ndipo tutapata pa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011 ya hivi karibuni. Katika ripoti hii kuna dosari kumi na tatu za Serikali Kuu na tukimaanisha Serikali Kuu ofisi hii ya Rais inahusika, ofisi ya Waziri Mkuu inahusika, Ofisi ya Makamu wa Rais inahusika, hiyo ndiyo mizizi mitatu ya hili jiti kubwa, zilizobaki Wizara ya Nishati na Madini, Ujenzi hayo ni matawi ya hili jiti. Kwa hiyo, shina ni hizo tatu. Sasa ikiwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katoa dosari kumi na tatu ambazo kwa uchache wa muda huu wa kuchangia siwezi kuzitaja zote lakini ninukuu mbili kwanza kwa taarifa yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kutotekeleza mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa katika miaka uliyopita, hiyo ni dosari ya Serikali Kuu. Lakini nyingine inasema hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 nanukuu, hesabu jumuifu za Taifa zilionyesha shilingi bilioni 461,500 milioni na kuendelea halafu mkopo shilingi bilioni 579, 280 milioni na kuendelea kama dhamana ya Serikali. Kwa wastani kiasi hiki cha dhamana ni sawa na asilimia 96.8 ya mikopo yote iliyotolewa. Huu ni ukiukwaji wa kifungu cha 13(1)(b) cha Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya Serikali ya 1974 iliyorekebishwa mwaka 2004 ambayo inaeleza dhamana si zaidi ya asilimia ya fedha zote zilizokopwa asilimia 70. Sasa tujiangalie, ikiwa Serikali Kuu inafanya hivyo na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali imesema hivyo, tutaweza kulaumu Halmashauri kinachotendeka kule, ikiwa shina picha ni kama hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata zile dosari zilizotolewa miaka iliyopita pia Serikali Kuu imeshindwa kujirekebisha. Kwa hiyo, hapa ndipo tunapopata picha ya utawala ya bora kwa kuanzia kwa sababu mwenye nyumba ikiwa matendo yake mabaya kama ni ya ulevi, kama ni ya zinaa, kama ni ya namna gani leo mtoto atakapofanya yale una uwezo gani wewe wa kumuonya ukaweza kumzuia? Picha ya Serikali Kuu ni hii je, tunashangaa yanayotendeka katika Halmashauri na sehemu zingine huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, naomba kunukuu ukurasa wa 26 wa kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Utawala wa Bora, kuna kipengele cha nne kinasema madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 54,010, yenye thamani ya shilingi bilioni 72,351 milioni na kuendelea yamelipwa. Jedwali namba sita linaonyesha huku. Sasa madai ya mishahara yamelipwa, tunazungumza utawala bora, nguzo moja ni huduma kwa wakati, *responsiveness* maana yake Serikali inakiri kulikuwa na malimbikizo ya mishahara, jedwali limeonyeshwa na kila kitu kimeonyeshwa na ndiyo kinatolewa taarifa yamelipwa. Hiyo ni nguzo moja imekosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, tukija katika sehemu nyingine ya *accountability*, uwajibikaji, tumeshuhudia mara ngapi Wizara, Mawaziri kwa Mawaziri kulalamikiwa, nani amechukua hatua angalau yeye mwenyewe akasema najiondoa, *accountability,* hatujajenga utamaduni huo. Wazee wetu zamani wapo waliofanya, Mheshimiwa Lowassa alifanya hapa, baada ya kuona nini akajiondoa,

*accountability*, lakini leo wanaofuata hakuna kitu kama hicho, *accountability* hiyo ni nguzo moja ya utawala bora, tujitathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilisema Tanzania ni nchi ya kumi na nane katika *rule of law,* katika nchi 53, ya kumi na nane katika *Mo Ibrahim Index*, tulikuwa tunazungumza kwa sababu vigezo vyenyewe viko hapa na tukijitathmini ndiyo tutajikuta tuko mbali. Kitu chochote utakachukichukua, ukiangalia la uwazi lina tatizo, ushirikishwaji una matatizo, kuna ushirikishwaji wa kibaguzi unaokwenda kitabaka, wa kichama, wa nini, ushirikishwaji wa umma katika mambo chungu nzima ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni tatizo, ni vyema ofisi hizi, ya Mheshimiwa Rais na Mawaziri wake watatu, ofisi ya Waziri Mkuu na Mawaziri wake watano pamoja yaani watatu na Manaibu Waziri ofisi ya Rais, Makamu wa Rais, zote zifike mahali sasa zijitathmini, waangalie dosari hizi zilizopo, zijitathimini ili kupiga hatua mbele lakini utawala bora bado kuna matatizo kwa vigezo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 48, ninukuu kidogo, amezungumzia Mradi wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, MKURABITA, baadaye akazungumzia kwamba kwa upande wa Zanzibar kufanya urasimishaji wa ardhi, miji na kujenga uwezo katika Halmashauri za Miji halafu kuna Wilaya kataja mbili na Miji mitatu, biashara na huko ardhini hii hadithi imekuwepo zaidi ya miaka saba nyuma na ilifika *stage*

MKUMBITA hawa wakaenda Pemba eneo la Kaskazini ikabidi baadaye waende Kusini ikatokea mgongano baina ya SMT na SMZ, kilichotendeka hatukukijua, hawa watu wa MKUMBITA mwingine mmoja sijui akapigwa uhamisho akapelekwa sijui wapi huko hakuonekana, hakuna chochote kinachoendelea. Hizi stori ....

**MWENYEKITI:** Ni MKURABITA sio MKUMBITA?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nakushukuru sana kwa tanbihi yako hiyo, kwa hiyo kila mwaka tunaletewa ripoti sijui utafanywa hivi MKURABITA, sijui mashamba yao yatafanywa hivi, biashara zao lakini hakuna kinachoendelea, ni tatizo lingine lile lile la utawala bora na kutokuwajibika. Nikuombe Mheshimiwa Waziri leo uniambie hasa hawa watu wa MKURABITA watakuja lini katika Wilaya ya Mkoani, Jimbo la Mkanyageni pamoja na Wilaya zingine za Pemba isiwe stori za miaka saba za namna hii na ikiwa hawatokuja kwa safari hii ina maana Mungu akitujalia na uzima bajeti ijayo tutaonana hapa Bungeni. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunivumilia na nafikiri utani...

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alizimiwa microphone kwa vile alionekana anaendelea kuchangia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, naomba Waheshimiwa Wabunge mnisaidie, kengele yako ya pili ikishagonga basi ujue muda wako wa kuchangia umeisha. Sifurahii sana hii tabia ya Kiti ya kumkatisha mtu na kuzima *microphone* yake kutoka hapa nilipo, kwa hiyo, naomba sana ushirikiano wenu. Naomba nimwite Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa uweza wake na mimi leo hii nimepata fursa kujadili hotuba hii muhimu kwa Serikali hasa katika ofisi inayogusa Watanzania wengi, wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa kuniombea kila siku nami nawaambia ya kwamba tumejipanga kwa ajili ya kuitetea Wilaya yetu na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa lugha yetu, kule nyumbani kuna lugha moja inaitwa Bangusilo, Kizaramu Bangusilo maana yake ni jambo la kupakaziwa. Kwa hiyo, hata ukienda katika nyumba ya mtu, ukifika barazani utakuta kapeti fulani hata ukiwa na matope yako unafutafuta pale maana yake ile ndiyo Bangusilo. Kwa nini nasema hivi? Naomba sana

Wabunge wenzangu na nawaomba sana Watanzania kipindi hiki kinatakiwa tuwe imara kwelikweli na tuwe makini kuliko jambo lingine lolote. Kwa kweli napenda kuwapa pole wagonjwa wote waliokuwa katika hospitali zetu na familia zao zote, mimi kwa binafsi najisikia huzuni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpa pole ndugu yangu Ulimboka kwa madhara aliyoyapata na sisi kama Watanzania wote tuweze kumpa pole mwenzetu kwa hilo lililompata. Lakini naomba kuzungumzia jambo lifuatalo, naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina, ni kina nani waliohusika na hili ndiyo maana nimesema Bangusilo, kuna wengine wanaitakia shari nchi yetu ya Tanzania, anaweza akatafuta fursa kwamba tatizo liko wapi ili mradi waweze kuwasha moto kwa Watanzania waweze kuichukua Serikali yao. Mimi napata mashaka sana hapa kwa sababu kuna wengine inawezekana wana maslahi binafsi katika suala zima la mgogoro wa Madaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu ana maslahi binafsi katika mgogoro wa Madaktari, inawezekana wanaweza wakafanya jambo lolote ili mradi kuipaka matope Serikali. Lakini si kuipaka matope Serikali, lengo kuu ni kuhakikisha kwamba Tanzania hatukai katika maeneo salama. Watanzania watakapopata hasira, vurugu zikitokea maana yake Tanzania siyo salama tena. Katika hili naiomba sana Serikali iende kwa umakini kujua ni akina nani waliohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwaomba Wabunge wenzangu, mimi sikufurahishwa na kwamba hali imetokea na tumeona mgomo ule kwa mujibu wa sheria Mahakama imetoa utaratibu lakini watu mpaka tumo Bungeni humu tunasema tupo nyuma yenu, tutahakikisha tunapambana, siyo kauli nzuri kwa Watanzania. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**MHE. SELEMANI S. JAFFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutoa hilo, kwamba Watanzania tunaijenga Tanzania yetu kwa ajili ya mstakabali wa nchi yetu. Sasa naomba kuendelea, Tanzania yetu hii...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Nani amesema Kuhusu Utaratibu? Mheshimiwa Mnyika, Kanuni inakuruhusu kuzungumzia utaratibu wakati mtu anazungumza, taarifa ndiyo inayomkatisha mtu kuzungumza na siyo utaratibu. Naomba uendelee Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema haya kwa uchungu kwa sababu najua kwamba Watanzania wanapata shida huko mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wetu katika Halmashauri zetu na maeneo mbalimbali wanapata

shida na naomba Waziri mwenye dhamana ujue kwamba tuna matatizo makubwa sana ya Maafisa Utumishi katika maeneo mbalimbali. Kuna wafanyakazi wengine kila siku wako maofisini kudai maslahi yao, wengine wanadai kupandishwa vyeo lakini kuna Maafisa Utumishi wengine ni wazembe, hawataki kuwajibika kwa mujibu wa taratibu zinazotakiwa na hili ndiyo maana nawaambia kila mwaka tunazungumzia madeni ya wafanyakazi kutokana na uzembe wa Maafisa Utumishi na hili lipo wazi. Leo hii tunasema matatizo yamekwisha lakini ukienda katika Halmashauri utakuta Walimu wanalalamika, Manesi wanalalamika, Mabwana Shamba wanalalamika na Watendaji wa Vijiji walalamika na Maafisa Utumishi wapo. Kuna wengine wamebadilishiwa mshahara lakini wakati mwingine toka apandishwe anakaa miezi mitato au sita mshahara wake haujaingizwa katika kompyuta, mtu amekalia meza tu, anapoteza muda wakati watumishi wapo vijijini wanapata shida. Namwomba Waziri mwenye dhamana uwapitie Maafisa Utumishi ili wale wazembe, tunaomba ututolee ili mradi tuondoe malalamiko ya watumishi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nililisema mwaka jana kwamba jambo hili linasababisha hata kuleta mambo ya rushwa na rushwa mbaya zaidi ni rushwa ya mapenzi, ni hatari kwelikweli. Ina maana mtu mwingine ni lazima ambembeleze mtu ili ampatie stahili yake, hili jambo si sawasawa. Nasikitika kwa sababu wakati mwingine Walimu utakuta wanaacha kufundisha shuleni wamejazana Wilayani ili kudai haki zao. Hili jambo si sawasawa kabisa! Kwangu Kisarawe,

Manesi wanalalamika sana katika hili na Walimu wangu wanalalamika katika hili, naomba Waziri mwenye dhamana uhakikishe kuwa unapitia Halmashauri zote ili kuhakikisha utaratibu unakaa vizuri na Maafisa Utumishi wanatenda kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia inaonekana mwaka huu kutakuwa na ongezeko la mishahara, mwaka jana nililisema pia, hata tukiongeza mishahara, mishahara hii jamani tunatofautiana, kitendo cha kuongeza 1% unakwenda kwa 15%, mtu aliyekuwa anapata mshahara wa shilingi 200,000/= ukimuongezea 10% maana yake atapata nyongeza ya mshahara wa shilingi 20,000/= na yule anayepata shilingi 2,000,000/= maana yake anapata nyongeza ya shilingi 200,000/=. Nasema utaratibu huu hauko sawasawa, kwa nini ile mishahara ya chini tusiongeze kwa asilimia kubwa na ile ya juu tukaongeza kwa asilimia ndogo? Tutakuwa tumewatendea haki hawa wafanyakazi ambao wanafanya kazi ya hali ya chini kwelikweli. Leo hii unamuongeza 20%, Mkurugenzi akiwa analipwa shilingi 2,000,000/= mfano, maana yake utamuongezea karibuni shilingi 400,000 wakati yule mfanyakazi wa chini, mwenye kima cha chini anayepata shilingi 200,000/= maana yake utamwongezea shilingi 40,000/= ambapo hujamsaidia chochote katika mazingira magumu anayoishi. Naiomba Serikali isikie hili na ikijua kwamba hili ni tatizo la wafanyakazi wetu na sisi tunaguswa na wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima tuwalilie na katika bajeti hii hatutakubali mpaka

tujue kwamba utaratibu utakuwaje kwa wafanyakazi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine la wastaafu wetu, wastaafu wanamaliza kazi, wametumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini anapomaliza kazi kufuatilia kupata stahili yake katika Mifuko ya Jamii imekuwa ni tatizo kwelikweli, watu wanalalamika. Kwa hiyo, nawaomba sana watu wa *LAPF* na *PSPF* wanisikilize. Kwa mfano, kuna mama yangu mmoja toka mwezi wa pili mpaka sasa hivi *document* yake ipo *LAPF,* Makao Makuu, amefanya kazi katika hospitali ya Wilaya, mama amestaafu hata hela ya kula hana watu wanamzungusha, mnataka hongo au mnataka nini? Naomba watu wa *LAPF,* wale wafanyakazi wangu wote wa Kisarawe ambao *document* zao zipo Makao Makuu mpaka leo hawajalipwa, nitazifuatilia na Waziri nitakukabidhi, kuna uzembe katika maeneo mbalimbali, hatuwezi kuiendesha Serikali watu wakipata shida wakati wameitumikia Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna watu wengine walikuwa wanalipwa *pension* zao, bahati wakabadilishwa kutoka miezi sita kwenda miezi mitatu. Kuna kipindi fulani nilipata taarifa kwamba miezi karibu minne hawajapata malipo yao, naomba Serikali iliangalie hilo ili kuhakikisha kwamba watu wanapata fursa ya kulipwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni sensa. Nashukuru sana mwaka huu tunakwenda katika zoezi la sensa ili mradi tuweze kujitambua na tuweze

kupanga mipango yetu ya maendeleo kwa mustakabali wa nchi yetu. Lakini sensa hii, naomba kutoa maoni kwamba mimi nafurahi sana kwamba sasa hivi tuna vijana wengi wamemaliza Vyuo Vikuu na wengine *Diploma*, wengine *Form Four* na wengine *Form Six* wapo mtaani. Kwa nini katika suala zima la kuhesabu watu, tusiwashirikishe Walimu na watu wengine kama vijana hawa ambao wengine wamekata tamaa kabisa mtaani? Naomba vijana wetu waliomaliza Vyuo Vikuu, waliomaliza *Diploma* zao na waliomaliza elimu za *Form Four* tuwachanganye na Walimu ili waende kufanya zoezi la kuhesabu watu yaani sensa ili na wao wapate mkate wao wa siku japo wakumbuke kwamba tumepata elimu yetu na Serikali yetu tumeitumikia vizuri na mwaka huu tumehesabu watu. Najua kuna sheria lakini sheria hiyo ni mtu na yeye yuko katika kijiji chake na ana wazazi wake na ana mtendaji wa kijiji, ni lazima hawa watu tuweze kuwahusisha ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kumalizia katika suala zima la uadilifu. Tuna tatizo kubwa, taarifa ya fedha katika kipindi kilichopita hapa tumeona kwamba kuna wizi katika Halmashauri zetu lakini watu hawachukuliwi hatua stahili. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba wale watu wote walioiba pesa za wananchi, Serikali iweze kuwachukulia hatua ili mradi kila mwananchi ajue kwamba kweli Serikali yao imefanya kazi kubwa na ya kutosha, mimi nasema hili haliwezi kushindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba tuanzishe *Financial Communication Protocol* ambayo itamsaidia Mbunge, Mwenyekiti wa Halmashauri kupata taarifa zote za kifedha kwa kila mwezi, *Bank Reconciliation*, Mbunge awe anajua kwamba *transaction* gani mwezi huu zimepita katika Jimbo lake. Mwenyekiti wa Halmashauri anapata taarifa hizo kwa kuweka *Financial Communication Protocol* ambayo itatumwa kwa Mkurugenzi, Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wa Halmashauri. Hii itakuwa ni *database* ya ku-*monitor* mikataba yote na *payment* zote zinazofanyika katika Halmashauri, maana sasa hivi utaratibu wa *CAG* anakagua miradi iliyofanyika miaka mingi. Tukifanya hivi, tutafanya *monthly control* ya *financial system* katika nchi yetu na hii itatusaidia sana kulinda pesa za wananchi wetu na mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nilikuwa sijisikii vema kwani nilikuwa naumwa lakini namshukuru Mwenyezi Mungu ameniwezesha nimezungumza haya machache, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika ulikuwa sahihi, *I am sorry* nilichanganya Kuhusu Utaratibu na Mwongozo. Naomba useme ulichokuwa unataka kusema.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *justice delayed is justice denied*. Nilikuwa na jambo wakati ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nimeshakwambia kwamba *I am sorry* kwa sababu nilishachanganya mambo mawili sasa sijui…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru siendelei na hilo.

**MWENYEKITI:** Haya endelea na ulichokuwa unataka kusema.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nataka lile la kwake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo ulishalitolea maelekezo lakini mchangiaji alikuwa anaendelea kuchangia kinyume na Kanuni, alikuwa akiendelea kukiuka Kanuni kuhusu suala la mgomo wa Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ni ruksa na ni vizuri ikawa ruksa wachangiaji kujadili jambo hili basi itolewe ruksa watu waweze kujadili, kutoka na hali mbaya iliiyopo jambo hili lijadiliwe, isije ikawekewa mipaka wakati wengine wanaachiwa wanalijadili tu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Mnyika kusema hicho anachokisema, mimi naomba niendelee kutumia Kanuni yangu, Kanuni ya 5(1) ambayo imenipa mamlaka ya kufanya

maamuzi kwa kusikiliza kile kinachoendelea Bungeni na kuweza kukipima kina mtazamo gani na hali gani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba suala hili tumelisema kwamba lifungwe mjadala kwa maana ya hali iliyotokea jana, kwa sababu hali iliyotokea jana ilikuwa ni hali ya kuomba Miongozo katika kulumbana na namna *speech* zilivyokuwa zinazungumzwa upande mmoja na mwingine ilikuwa si afya kwa Bunge letu. Lakini suala hilo linaweza kuongelewa na mtu yeyote hapa anaweza akasimama kuliongelea suala hilo kwa utaratibu ambao siyo wa uvunjaji wa Kanuni na mimi kama Kiti atakayeongea mwingine nitaendelea kupima anazungumza kwa mipaka ipi ya Kikanuni? Kanuni yangu hii ya 5, inanipa nafasi ya kupima na kujua nini kifanyike katika kila mazungumzo yatakayoendelea. Bado tuna wachangiaji wengine hapa wataendelea lakini kama watatturudisha katika hali iliyotokea jana, ni wajibu na ni lazima Kiti kisimame imara na kuona utaratibu unafuatwa.

Mheshimiwa Mnyika, kwa jinsi alivyoongea Mheshimiwa Jafo huwezi kufananisha na mazungumzo yaliyokuwa yanaendelea ndani ya Bunge jana, lazima tuwe *fair*, Mheshimiwa Mnyika ni lazima tuwe *fair* hata hiyo *justice* tunayoidai jamani ninawaomba Waheshimiwa Wabunge isiwe inavuka mipaka kudai vitu vingine ambavyo vimevuka mipaka. Kwa lugha aliyoitumia Mheshimiwa Jafo huwezi kufananisha na lugha ya wachangiaji waliochangia jana na wala sitaki kurejea kuwataja majina na ninaomba niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mkiheshimu Kiti,

mimi ni mtu mzima ninafanya kazi kwa Kanuni na nimekuwa nikitoa hayo maelekezo kwa kutaka nidhamu ya Bunge ibaki vizuri kama ilivyo.

Kwa hiyo, ninaomba sana tuendelee kuchangia na kwa kweli mtu atakayekiuka mipaka kama ilivyokuwa jana basi Kiti hiki hakitasamehe iwe ni upande wowote ule. Naomba mniache niendelee na Kiti na niendelee kusimamia shughuli za Bunge. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour ajiandae.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Madaktari kwa niaba ya Chama cha Wananchi *CUF* kwa Madaktari kukubali maelekezo ya Rais na kurejea kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanya hivi kwa sababu roho na pesa ni vitu viwili tofauti sana.

**TAARIFA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa! Mheshimiwa Kombo naomba uketi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa masikitiko sana, naomba kutoa taarifa

kwa mzungumzaji. Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari leo, Madaktari Bingwa wametoa kauli wamesema kwamba Rais amepotoshwa na wamekataa kukubaliana na kauli ya Rais kwa kuwa Rais amedanganywa. Kwa nini Bunge letu haliingilii kati lipate taarifa sahihi ili tufanye maamuzi sahihi? Tunaendelea kupotoshwa!

**TAARIFA**

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Juma! Subiri Mheshimiwa Kombo, taarifa zote unapewa, kwa hiyo wewe ndiye mwenye kuzikubali au kuzikataa. Mheshimiwa Juma Nkamia!

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini Bunge linaendeshwa kwa Kanuni na taratibu, Bunge haliendeshwi kwa kuzingatia vyombo vya habari vimesema nini. Mtoa taarifa aliyesema sasa hivi, juzi hapa alikariri gazeti akisema kwamba gazeti fulani limetoa habari fulani na ni habari ambayo si sahihi. Sasa tukiendelea namna hii kuendesha Bunge kwa taarifa za namna hii, tuwe tunasikiliza vyombo vya habari vinasema nini hatuwezi kufika na pia tumechoka, tumechoka. Tumekuwa tukikaa kimya, kelele kila siku, hatuwezi kuendesha Bunge namna hii kwa kusikiliza vyombo vya habari vinasema nini.

**TAARIFA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika naomba uheshimu, ulipokuwa unatoa taarifa yako hakukuwa na mtu aliyekuwa anakukatiza. Naomba umsubiri amalize.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma umemaliza?

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Gekul taarifa!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukapuuza vyombo vya habari, jana tu Madaktari bingwa ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul unampa taarifa nani?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Nampa taarifa Mheshimiwa Kombo. Ni jana tu Madaktari Bingwa wametangaza mgomo kwa sababu hawana wasaidizi na tumesisitiza kwamba Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na Ripoti ya Kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu iletwe hapa Bungeni ili tuijadili kwani Watanzania wanapoteza maisha. Kwa hiyo, Madaktari wanaendelea na mgomo, tusipuuze na Bunge lisipuuze hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Mnyika, naomba nimalize hizo taarifa kwa sababu naona tuelewane kwanza kisha ndiyo tuendelee.

Mheshimiwa Mnyika, wewe umetoa taarifa ya kwanza sasa kabla taarifa hiyo haijapokelewa unaendelea tena na taarifa nyingine nadhani hizo taarifa zote mnampa mchangiaji lakini mnapompa mchangiaji hizo taarifa naomba nisome Kanuni ya 68(8) ambayo inasema hivi:-

*"Vilevile, Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema "taarifa" na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema, ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema kuketi kusikiliza taarifa hiyo".*

Kanuni ya 68(9) inasema:-

*"Mtoa taarifa atakapomaliza na kuketi, Spika atamuuliza Mbunge aliyekuwa akisema mwanzo kama anakubali au haikubali taarifa hiyo kabla ya kumruhusu kuendelea kuchangia hoja yake".*

Sasa ninyi mmeshatoa taarifa kwa hiyo na mimi natekeleza wajibu wa Kikanuni, ninamuuliza Mheshimiwa Kombo hizo taarifa unazikubali? Kama huzikubali nijue ili niweze kufanya maamuzi ya kuendelea na shughuli zangu.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zote hizo mimi nazikataa na ninakataa kwa sababu ningezikubali lakini kwa

maelezo ya jana na kitabu chao kilichozungumzia maelezo haya, wao walikataa kwamba hawahusiki na masuala haya ya kuwakampeni Madaktari lakini leo bado Madaktari wanakubali kurudi kazini wao wanasikitika kwa nini wanarejea kazini, kwa hiyo, nakataa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni naomba kuzifunga taarifa zenu na sasa namruhusu mchangiaji aendelee, Mheshimiwa Kombo endelea!

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Madaktari kwa kuona na kuweza kufanya hesabu kwamba pesa na roho ni kitu tofauti sana. Wazee wetu, ndugu zetu, wake zetu na kadhalika ambao walipata matatizo makubwa ya mgomo uliopita wanajua sasa Madaktari kwamba kweli suala ambalo walikuwa wanataka kulifanya halikuwa la haki. Namshukuru Rais kwa hekima zake alizozitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena na kwa niaba ya Chama changu nawapa hongera Madaktari na Rais kulimaliza tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba huwezi kupata roho nyingine lakini unaweza ukapata pesa nyingi sana na zikamalizika na ukapata nyingine. Tuwatazame Watanzania na tuitazame nchi yetu inapata heshima gani, itaonekana ina kiasi gani, watu wanaifahamu vipi na leo migomo sijui kwenye shule, sasa ni migomo kwa Madaktari na kesho migomo

itakuja mpaka ndani ya nyumba zetu. Tukiwaambia hawa wake zetu watupikie watasema sipiki, sasa hii migomo inaanza kwa sababu ya kuchocheachochea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nawaomba sana wananchi wa Jimbo langu la Chakechake, tumekaa miaka 50 kwa manung'uniko kwamba Katiba hii haitupi haki Watanzania wote, nawaomba waende wakachangie watoe sifa na ubaya wa Katiba hii ambayo imepita na inayokuja sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala tatu, nashukuru na ninaomba kuwaomba *TASAF* ambao katika kitabu cha Kamati yetu, *page* ya 21, tumezungumzia suala la *TASAF* Awamu ya II. Awamu ya I, imetekelezwa vizuri, imefanya kazi nzuri na sasa hii Awamu ya II, naiomba pia iwe na kazi nzuri ili kuendeleza maisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Tulipendekeza kwenye Kamati yetu kwamba Sheria hii na Kanuni zibadilishwe ili Kamati iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni mfuko wa Rais wa Kujitegemea na Kuwakwamua Wananchi wa Chini. Ni wazo zuri la Rais lakini bahati mbaya sana linatumiwa kisiasa. Wanaochukua, CCM wanafanya mfuko huu kama ni wao na hata wanaopewa hii mikopo basi ni CCM, haionekani kama mfuko huu ni mfuko wa watu ambao hali zao za maisha ni za chini. Naomba sana Waziri anapokuja awaambie CCM wenzake kwamba

huu mfuko si wao bali ni mfuko wa wananchi wote wa Tanzania na nina ushahidi akitaka nitampeleka katika Mkoa wangu. Unakaliwa na vikao vya chama vya CCM nani apewe na nani asipewe. Bahati mbaya sana tuliungana kwenye Serikali hatukuungana kwenye vyama, kwa hiyo, chama hiki kikongwe bado kinatuyumbisha, hakitaki kuona kwamba mfuko huu ni mfuko wa wananchi wote na bahati mbaya mtu anakopeshwa shilingi 30,000/= au 40,000/= au 50,000/= atajikomboa vipi kiuchumi katika matatizo haya? Mkoa mzima unaletewa sijui shilingi milioni tatu (3,000,000/=) Serikali ya Zanzibar inaongeza milioni mbili (2,000,000/=) zinakuwa milioni tano (5,000,000/=). Sasa utamkopesha mtu shilingi 50,000/= au 60,000/= akajikomboe na nini huyo? Akinunua pakiti moja ya mchele shilingi 55,000/= mkopo wote umekwisha. Sasa sijui anaenda kulipa nini! Nilifikiri tuliangalie vizuri na ninalitetea hivyo kwa sababu ni wazo zuri ambalo Rais amelifikiria. Tuna *TASAF*, mfuko huu ungetusaidia sana kuondoa matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yametoka kwenye Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala. Sasa nimepata nafasi ya kuzisaidia Wizara hizi tatu na tumetoa mapendekezo haya ambayo ni ya msingi sana. Tunaomba Serikali ishughulikie suala hili kutokana na mapendekezo yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo namalizia la tano, tumesema ni vizuri Wabunge wa Majimbo yote tukashirikishwa katika *TASAF*. Muundo uliopo hivi sasa ni wa kutafuta Wabunge wawili wa Kisiwa kizima cha

Zanzibar na Pemba, sijui huku Bara muundo wao uko vipi. Sasa sisi ndiyo tunaoona maendeleo ya lile Jimbo na ndio tunawashawishi watu wafanye kitu gani lakini sisi si wajumbe wa mfuko wa *TASAF*, tunakuja kupokea taarifa kwenye Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala. Ni vizuri sana Wabunge washirikishwe ndani ya Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia wale ambao wanafikiri wanaweza wakatusaidia kwa mawazo yao ya kibabe au kwa mawazo finyu, naomba sana watusaidie kwa utaalamu wao. Wale wengine ni Wabunge wa Mjini na sisi tukiishatoka shamba tunapita pale kuja Bungeni, leo wakianza ubabe humu ndani tutaogopa kupita pale. Inawezekana na wananchi wao wanatusubiri watufanyie hivyo hivyo. Sasa ninachoomba, tuwe kidogo kama sisi ambao tunaweza kujua kuwa hiki ni kibaya na hiki ni kizuri. Wawe kama Chama cha CUF abacho kina ustaarabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti kubwa ni kwamba Chama hiki kinaongozwa na msomi, Profesa, lakini hicho Chama kingine ni *Disco Joker*. Sasa *problem, problem*, natafuta taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, hebu zima hiyo *microphone* yako.

**MBUNGE FULANI:** Afute hiyo kauli.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye ninayeongoza Kiti, sasa msinifundishe nini cha kufanya.

Nimesimama nikijua naongoza Kiti. Nimesimama nikijua ninaongoza Bunge kwa mujibu wa taratibu na Kanuni tulizonazo.

Mheshimiwa Kombo maneno uliyomaliza nayo kwa mujibu wa Kanuni si maneno mazuri, ni maneno ya kuuzi. Viongozi wote wa Vyama katika nchi ya Tanzania wana heshima na wanaheshimika na wanachama wao. Hujasema ni kiongozi gani ambaye ni *Disco Joker*, hujataja chama wala jina la kiongozi, lakini umesema kiongozi anayeongoza chama. Sasa viongozi wanaoongoza vyama ambao tunao humu ndani ni Mheshimiwa Mrema, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mbowe na pia Mheshimiwa Cheyo, ukiacha wale wengine wengi ambao wako nje ya Bunge. Kwa hiyo, sasa kuita viongozi hawa kwa sababu hujataja chama wala jina la kiongozi na kufanya hiyo *generalisation* ya kusema kwamba, kiongozi anayeongoza chama ni *Disco Joker*, jamani Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli niridhike kwamba neno hili ni la kuudhi. *(Kicheko)*

Ningekuomba Mheshimiwa Kombo uifute kauli hiyo ili tuweze kuendelea na shughuli nyingine na kama hutaifuta basi Kiti kiweze kuchukua hatua.

**MHE. MUSSA H. KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunielewa kama mimi mwenyewe nilivyokuwa nimekusudia. Nafuta msemo huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kombo. Waheshimiwa Wabunge hii ndiyo nidhamu ya Bunge. Kama mtu unakosea na kuteleza na unapoongozwa

na Kiti kufanya hivyo lazima nikiri kwamba Mheshimiwa Kombo nakushukuru na hii ni nidhamu ya Bunge. Nadhani huko mbele tutaendelea kujifunza vizuri.

Naomba nimwite mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. Ningeomba kusisitiza Waheshimiwa Wabunge muendelee kuchunga kauli zenu na namna mnavyochangia hapa Bungeni.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuchangia katika Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na hali ya maisha ya watumishi. Hivi sasa kufanya kazi Serikalini inaonekana ni nafasi isiyopendwa na wafanyakazi wengi kutokana na maslahi mabovu, mishahara finyu na mzigo mkubwa wa kodi. Mpaka hivi sasa ni Taasisi mbili tu za Serikali ambazo wafanyakazi wanapendelea kuzifanyia kazi; *TRA* na *BOT*. Wafanyakazi wa *TRA* na *BOT* wako tayari kufanya kazi maisha yao yote na wako tayari kulia pale unapofika wakati wa kustaafu lakini wafanyakazi wengine wote waliobakia hawana tena mapenzi na nafasi zao wanazofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitatoa mfano wa Walimu. Mwalimu anapoingia pale kazini kuwafundisha wanafunzi, lengo lake ni kwamba wale wanafunzi waelewe na waweze ku-*pass*. Anakuwa na hamu na shauku kubwa kuona wanafunzi wake wote

aliowafundisha katika darasa lake au wanafunzi wote aliwafundisha wana-*pass* lakini hivi sasa kuna tofauti kubwa. Mwalimu anakwenda kazini *just* aonekane kwamba amekwenda kazini. Ili mradi achukue chaki achorechore watakaoelewa wameelewa na wasioelewa basi. Hii inatokana na ugumu wa maisha kwani mshahara wanaoupata ni kidogo mno. Kwa hiyo, Walimu waliishakata tamaa na wanakwenda shuleni ili waonekane tu kwamba wamekwenda, lakini wanafunzi hawafundishwi na matokeo yake wengi wanafeli. Sababu mojawapo ya kufeli kwa wanafunzi ni kwamba Mwalimu hachukui *attention* kubwa ya kuwafundisha wale watoto wakaweza kufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hizi shule za Serikali ni za watoto wa wanyonge. Wazee ambao wana kipato kikubwa hawapeleki watoto wao katika shule za  Serikali bali shule za *private*. Tuwaoneeni huruma hawa wanyonge jamani. Tuwawezeshe hawa Walimu kwa kuwa mshahara wao ni mdogo, angalau tuwawezeshe kupokea mshahara wa shilingi laki tatu (Sh.300,000/=) baada ya kuondoa makato yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitazungumzia kuhusu pensheni. Hivi sasa kufanya kazi Tanzania au katika Serikali limekuwa ni jambo baya kwelikweli. Hawa wazee wetu wa zamani au hata sisi si kwamba tulishindwa kwenda kufanya kazi katika *private sector*, bali tulikuwa na uzalendo na ndiyo maana tukaamua kufanya kazi Serikalini.  Sasa wafanyakazi hawa wamefanya kazi kwa muda wa miaka 30 na sasa wanadai haki yao ya pensheni, lakini wanazungushwa. Kwa nini hamji na mfumo mzuri ili mtu

anapomaliza muda wake wa kazi na kustaafu apewe fedha zake kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahoji hilo kwa sababu tayari mwajiri anajua mwezi fulani mfanyakazi huyu anastaafu, kwa nini asimtengenezee mafao yake ya uhakika kwa wakati? Mfanyakazi anapata usumbufu wakati ameshastaafu na anataka akae nyumbani apumzike lakini kila siku inabidi aripoti pale kazini kwa lengo la kudai mafao yake kama vile ni mfanyakazi. Naiomba Serikali iwaone huruma hawa watu ambao wamejitolea maisha na muda wao kwa miaka kadhaa na katika mazingira magumu ya ugumu wa maisha lakini bado wakabaki na kuendelea kufanya kazi humo humo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa watumishi ambao wamepata kashfa ya ubadhirifu. Zoezi lililopo hivi sasa mtu akipatikana na kashfa ya ubadhirifu huwa anahamishwa kutoka sehemu ile kwenda sehemu nyingine. Sasa kila nikitazama hii sioni mantiki yake. Je, kumpeleka maeneo mengine mnategemea na kule akafanye ubadhirifu? Kwa nini hamchukui hatua za kumpeleka kwenye vyombo vya sheria ili kama amefanya ubadhirifu huo ahukumiwe na kupata adhabu ili iwe fundisho kwa wengine lakini badala yake zoezi lililopo hivi sasa yule mtu anahamishwa kutoka sehemu ile na kupelekwa nyingine. Kwa hiyo, naishauri Serikali mtu akionekana amefanya ubadhirifu asihamishwe kwenda sehemu nyingine akaenda kuharibu na kule, au akawafundisha na wale walioko nao wakaharibu, badala yake ni vizuri sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi lawama nilizotoa lakini Serikali inapofanya mazuri lazima niipongeze. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali. Baada ya Kamati ya Katiba na Sheria kutoa mawazo yake kwamba wanafunzi wanapomaliza masomo waende JKT, Serikali ilikubali na sasa imeishaanza kuwapeleka wanafunzi JKT. Lakini hapohapo natoa msisitizo kwamba, kwa kuwa nafasi zenyewe ni chache mno na wanafunzi wanaomaliza shule ni wengi basi Serikali ihakikishe inatoa nafasi za JKT kwa uwiano ili kuepuka nia hiyo nzuri kuleta migogoro chungu nzima na malalamiko kwamba, Serikali imepeleka watu wa fulani, imewaacha hawa, imepeleka wa CCM, wa CHADEMA wameachwa. Ninachoomba ni kwamba, kuwe na uwiano mzuri wa hawa wanafunzi watakaopelekwa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilifarijika sana kusikia kwamba huko JKT kuna somo la uzalendo. Hili ni somo zuri sana. Hata hivyo, inanishangaza kwani viongozi wengi waliopo madarakani waliopitia huko JKT na wakasoma hili somo la uzalendo lakini wao ndiyo wamekuwa mafisadi wakubwa. Kwa hivyo, ninaishauri Serikali kwamba somo hili la uzalendo litolewe kwa upana ili kila mtu alifahamu na taifa liepuke kuwa na viongozi mafisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kukaa, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia

hoja iliyoko mbele yetu. Mimi kwa kuanza ningependa ku- *declare interest*, mke wangu ni mfanyakazi wa Serikali. Siku moja aliniomba kwenda shule, nikamruhusu. Aliporudi cheo hakikupanda. Akaniomba kwa mara ya pili, nikamwambia bwana eeh, kasome ujasiriamali uje ufuge kuku. Akakataa, unajua wanawake wa siku hizi wanaweza kukataa. Akaenda akasoma *Post Graduate Diploma* akarudi lakini cheo hakikupanda na wala daraja halikupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitolea mfano mimi mwenyewe kuonesha uzito wa tatizo hili. Wafanyakazi wanaokwenda kujiendeleza ni vyema wanaporudi Utumishi muwape stahiki zao ili ziweze kutoa motisha. Yako malalamiko kwamba, watu wamepoa, idara zote zimepoa, lakini mojawapo ya mambo yanayowafanya wafanyakazi wapoe ni kwa sababu wanapofanya mazuri hatuwatambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma kidogo mambo ya utumishi hivyo ninayajua. Mfanyakazi anapofanya jambo zuri na wewe kiongozi wake ukatambua, huyo mfanyakazi ataongeza bidii. Tutambue nafasi za wafanyakazi watafanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza mjadala, nimeyapitia maandiko yote haya, mwaka jana wakati wa bajeti tulianzisha mpango wa dharura kumaliza tatizo la umeme. Nashawishika kuishawishi Serikali yangu kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, tuanzishe mfuko wa dharura wa kuweza kumaliza madai na malimbikizo ya wafanyakazi. Kitafutwe kiasi kikubwa

cha fedha tumalize matatizo yao kwa sababu yako madhara makubwa; Walimu wanasema mimi malimbikizo yangu miaka mitatu, minne, hawezi kufanya vizuri kwa sababu hakuna motisha. Naomba Serikali ilifikirie hili. Utumishi fikirieni na mtengeneze namna ya kumaliza suala hili kwa sababu hamna namna ya kulificha. Huwezi kulificha katika itikadi, huwezi kulificha katika mahusiano, kwanza mimi na-*declare interest,* Katibu Mkuu wa Utumishi ni Mjomba wangu. Eeh, kwa hiyo huwezi kulificha wakati wowote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia Mjomba mimi sitachangia kwa sababu naogopa kuzuia shilingi ya wapwa zangu lakini inafikia hatua inalazimika useme kwa sababu wafanyakazi watalalamika, Walimu watalalamika. Kwa hiyo, ninachoomba ili wote tufaidike, tutengeneze mfuko wa dharura, tuanishe ni akina nani wamepunjwa mafao yao na tuweze kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji ufanisi wa Serikali. Wenzangu wamezungumzia nafasi ya watumishi, watendaji wa Vijiji, Kata na wale wa Tarafa. Narudia kuiomba Serikali yangu kwamba, hawa watu wanaostahili muwaweke kwenye nafasi zao lakini hawa watu muwape majukumu na tuwe tayari kuwawajibisha tutakapokuwa tumewapa zana na maelekezo bora ya kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yanayofanyika, uharibifu wa mazingira, kushindwa kukusanya nguvu za wananchi katika maendeleo

inatokana na kwamba ule mfumo wa utumishi wa wafanyakazi wa Serikali haukusambaa vizuri. Kwa upole kabisa na ninajitahidi kabisa, naishauri Serikali yangu mlitekeleze hili. Hatuhitaji kwenda Marekani kutafuta mtaalam wa Utumishi. Mtumishi *WEO, VEO*, hawa watu wanapatikana. Kuna vijana wengi, zile ajira milioni moja (1,000,000) tutazipata kirahisi kwa kuchukua vijana wenye *Certificates*, *Diploma* tukawapatia nafasi za utendaji lakini msiwatupe kwenye nafasi zile, muwatafutie na nyenzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuomba tena Watendaji wangu hasa Maafisa Tarafa wa Mkoa wa Kagera hawana vyombo vya usafiri. Kuna Katibu Tarafa mmoja wa Nshamba ili aende Rutoro inabidi mimi nitoe fedha, inabidi nimpe Pikipiki yangu atembelee. Muwasaidie na wale walioko pembezoni. Nawasemea watu wa pembezoni, mzungumzie Makatibu Tarafa. Unajua Katibu Tarafa wa Ilala na Katibu Tarafa wa Muleba ni tofauti. Muwazungumzie hawa watu wa pembezoni. Msiwatupe kule halafu mkataka wa- *perform*, hawawezi ku-*perfom*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie TAKUKURU. Nazungumzia TAKUKURU kwa nia ya kuwashauri. Wananchi hawajui michakato, *formula* na *methodologies* za kazi za TAKUKURU. Wananchi wanachotaka ni kuona kwamba, rushwa haipo. Tarehe 27 Mei, 2012 walikuja Polisi wakafika pale Izigo wakawakamata vijana waliokuwa na pikipiki wakawatoza shilingi elfu hamsini hamsini. Wale vijana wakanipigia simu, nikawaambia mimi Mbunge siwezi kuwafanya lolote, ni Polisi wa Muleba. Sasa kwa

wananchi wa Izigo kuona kwamba TAKUKURU Inafanya kazi ni kutonyang'anywa fedha zao. Nimekuwa nikilalamika kuhusu suala la Polisi na watu wa uvuvi wanavyowaonea watu wangu katika visiwa vya Ziwa Victoria kule Ghoziba. Watu wa Iyumbo wataelewa Serikali inafanya kazi pale Mbunge atakapomwambia *RPC* wa Kagera kuna Polisi amepiga mtu, nyavu zimechomwa, mtu aliyehusika apelekwe Mahakamani. Wataelewa TAKUKURU inafanya kazi kama hawatatoa na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na *methodologies* za Bwana Hosea mnazozitumia kwa wananchi ni ile *perception*, watu wanakuonaje? Unaweza ukafanya kazi kwa kutumia *methodologies* za Ulaya lakini kama watu hawaoni rushwa ikiondoka hawatawatambua. Naishauri kwa upole TAKUKURU siyo kwamba nawaogopa, siwaogopi! Mimi ni mtenda mema. Ila ninawaambia watu wanaona kuna rushwa katika Ziwa Victoria, kama alivyosema mjukuu wangu hapa Vincent Nyerere kwamba kuna watu wamerundikana kuanzia Dar es Salaam mpaka Mtukura wanakusanya fedha mtaani. Sasa hao wanaoomba fedha barabarani sisemi muombe kwa kificho, lakini inakuwa haileti staha. Kwa hiyo, hayo mambo ndiyo yanauma, muangalie maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mishahara hewa, watu wa Utumishi mimi ninawaombea bajeti yenu ipite, lakini ili kutujengea heshima sisi, kusudi kutuponya sisi, wale vinara waliokuwa wanaendesha zoezi la mishahara hewa mtuletee hapa tuwajue. Haiwezekani shilingi bilioni tisa (Sh.9 bilioni) zikaondoka,

mishahara hewa tusijue nani ali-*recommend*, nani ali-*approval* na nani alicheki, hii haina itikadi, tungependa kujua nani huyo ali-*approval* hizo shilingi bilioni 10 zikaondoka. Tungependa suala la mishahara hewa liweze kwisha, lakini kwisha ni lazima tujue nani anawajibika na anayewajibika tusingependa kuletewa vidagaa. Kuna rafiki yangu mmoja amesema hapa leteni sangara mkubwa mseme huyu ndiye aliyewajibika tuweze kumwajibisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuleta wataalam kutoka nje, limezungumzwa katika taarifa ya Mheshimiwa Stephen Wasira kwamba kuna wataalam wataletwa kutoka nje watakwenda Kilosa kufundisha watu wa Kilosa namna ya kulima kitaalam, naipongeza Serikali yangu kwa wazo hilo nzuri lakini ningeomba hao wataalam wa kutoka China au Wakorea au Vietnam muwalete na Kagera kusudi wafundishe watu wa Kagera namna ya kulima mpunga, namna ya kulima ndizi bila kupata huu ugonjwa wa mnyauko, waje watusaidie liwe zoezi la nchi nzima. Wachina wapo, Wakorea wapo na Vietnam wapo mnapoamua kuwaleta, hili si suala la majaribio kwamba Wachina ni wazuri katika mambo ya kilimo, si suala la kujaribu walete wengi, mtuletee watu wa Vietnam waje watufundishe kufunga samaki kusudi tuweze kuleta tija kwa kasi. Miaka 50 hatuna muda wa kusubiri, unasikia masimango na vijembe vinavyopigwa, hatuwezi kusubiri. Hilo suala ninaipongeza Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uanzishwaji wa JKT, ninaunga mkono uanzishwaji wa JKT, umuhimu kwangu katika kuanzisha JKT, yamekuwepo

mazungumzo ya Serikali kwamba JKT itaanzishwa na baadhi ya vikosi vichache zitawekwa mpakani, ningeomba kwenye Mkoa wangu wa Kagera anzisheni JKT, weka vijana mpakani kuweza kuzuia hawa watu wanaopitapita kwa sababu mpaka wa kwetu upo-*pores,* una matundu mengi, tuweze kuzuia watu wanaoingia ovyo, tuweze kuzuia watu wanaoingiza mifugo ovyo kusudi vijana waende pale, wasaidie vijana wenzao namna ya kuzalisha, waonyeshe hizi mbinu bora za JKT na mbinu bora za Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo mengi, ningeomba niunge mkono hoja nikiwa na imani kwamba Serikali yangu itazingatia hayo, nimetekeleza shughuli ya ushauri, nimewashauri TAKUKURU mkitekeleza hayo na watu wakapata stahiki zao, mambo yataenda vizuri. Naomba niunge mkono hoja, naomba muipitishe hii bajeti ya Mjomba wangu kusudi wapwa zangu wasinielewe vibaya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwijage lakini tunaweka kumbukumbu sahihi, tunapitisha hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Uhusiano na Uratibu isije ikabakia kwamba unaunga hoja ya Mjomba wako kwenye *Hansard*, uko mbele *Hansard* inaweza isitambue kuunga mkono kwako kwa hoja ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kushiriki kwenye kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais. Nitajikita katika maeneo makubwa matatu. Kabla ya kujikita, pia niwashukuru sana Wanakorogwe. Niwashukuru kwa uvumilivu wao na niishukuru Serikali hiihii na utawala wake bora. Baada ya kelele ambazo tulizipiga mwaka jana, mwaka huu watu wa Mikongeni *cheque* zinaendelea kuandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Serikali hii kwa utawala wake bora leo hii tumeingia kwenye mpango mahsusi wa kurekebisha Mji wetu wa Korogwe na kupata kiasi kizuri cha fedha kwa ajili ya maendeleo. Ni Serikali hii kwa utawala wake bora tumeongeza miradi ya maendeleo. Lakini kama sehemu ya angalizo niliwakumbusha wakati wa kuchangia hoja ya bajeti kwamba tunapewa *ceiling* baadaye tunaambiwa kwamba tupeleke *special request*. Mtindo ule unatufanya Wabunge, Wakurugenzi na hata wananchi kwenda kugombania goli na hatma yetu inakuwa chini ya mkono wa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda sasa nichangie kuhusiana na bajeti hii hasa kwenye lile eneo la *TASAF*. Korogwe ina maeneo mawili ya kiutawala, katika ukurasa wa 80 wa Kitabu cha Bajeti nimeona ikizungumzwa Korogwe DC, basi nitumie fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwamba Wilaya ya Korogwe ina maeneo mawili ya utawala ambayo ni Korogwe Mji na

Korogwe Wilaya na kadhalika. Tatizo hilohilo nimeliona kwenye eneo la Wilaya ya Muheza pale ambapo Mkinga imehusishwa na Wilaya ya Muheza. Mkinga ni Wilaya na ni Halmashauri inayojitegemea. Kwa hiyo, ipo haja ya kufanya urekebishaji kidogo ili na sisi tuweze kupata fursa kama ambazo zinatokea kwa watu wengine. Fedha za miradi iliyopita na hata fedha zilizoongezwa kwenye miradi iliyobakia, naomba mliangalie kwa umakini kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kadhalika niende kwenye sehemu ya Utumishi. Nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutupa Mkuu wa Mkoa na kadhalika kunipa Mkuu wa Wilaya kijana, mwenye nguvu, rafiki yetu na mdogo wetu lakini niseme ipo haja ya kuongeza nguvu katika kuwapa semina Wakuu wa Wilaya. Katika maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kwamba pamoja dhamana hii msikae kwenye viti vile mkawa ni wapiga kampeni. Pamoja na dhamana hii msiende kugombana na Wabunge. Pamoja na dhamana hii waheshimuni Wenyeviti wa Halmashauri mnazokwenda kuzikuta. Pamoja na dhamana hii kaangalieni uovu wa watendaji na pale wanapofanya vizuri muwape kile wanachostahiki kwa kuwasifia. Nirejee tena kutoa ushauri, Wakuu wa Wilaya wapya na Wakuu wa Mikoa wale wachache mjaribu kuuzingatia kwa sababu huko tunakokwenda kunaweza kukaleta mtafaruko mkubwa baina ya *public*, Halmashauri na nyie kama watendaji mliopewa dhamana na *Executive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie *PCCB*, niwapongeze sana *PCCB*

niliyasema haya kwenye mchango wangu mwaka jana na nazidi kuwapongeza tena mwaka huu kazi mnayofanya ni nzuri. Lakini kuna mahali hapa mnajichanganya, itakapotokea kwamba kuna kesi ya rushwa inayomtuhumu fulani Athumani Ali, halafu kesho Athumani Ali anapewa *appointment* ya kuwa labda Katibu Tarafa au kuwa Mkuu wa Mkoa na huku kuna *allegation* ya kesi nyingi za *PCCB* mnamweka mahali pabaya Mheshimiwa mwenye kufanya uteuzi pale ambapo kesi itafikia mahali pa kwenda Mahakamani, kama mwenye dhamana ya kuteua amekwishakumpa uteuzi huyu tunafanyaje? Lakini pia sisi kama *public* kule chini tunahitaji kuona kwamba tuhuma na *allegation* za waziwazi ambazo zimepelekwa mbele au ule ukamataji uliofanywa na Idara ya TAKUKURU ungeweza kutuletea matunda ili tuweze kukomesha matatizo yaliyopo. Mathalani unamteua Nassir leo kuwa Mkuu wa Wilaya na huku ana kesi na tuhuma ambazo zipo *PCCB* ina maana uteuzi utakapotoka kutakuwa tunam-*complicate* yule mwenye madaraka. Sasa ningewasihi tu mjitahidi kumaliza viporo vya kesi zilizopo na tuangalie maeneo mapya ili haya mambo yasije yakajirudia. Nina uhakika ndugu yangu Hosea umeyasikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais. Mimi ningependa nishauri hivi, hii bajeti iliyoletwa sasa kwa huko tunakoelekea basi iongezwe zaidi ili Mheshimiwa Rais awe ana sehemu kubwa ambayo inahusu ahadi zake sijui kama nimeeleweka. Ni kwamba Rais akitoa ahadi ya maji pale Korogwe Mjini na mradi wa maji ni shilingi bilioni sita basi zile shilingi bilioni sita ziingie kwenye bajeti ya

Mheshimiwa Rais. Utaratibu uliopo sasa wa kuchukua ahadi za Rais na kuzibandika kwenye Wizara husika unaturejesha nyuma kwenda kugombea goli tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa John Magufuli juzi akijibu swali langu la nyongeza wakati nilipouliza ahadi ya Rais kuhusiana na barabara. Akasema bajeti yetu imeongezeka kutoka shilingi bilioni 300 kwenda shilingi bilioni 400, lakini ni bajeti hiihii ambayo tuliipitisha mwaka jana haikukidhi. Sasa ahadi ya Rais inapelekwa kwenye kapu la Wizara na matokeo sasa isipotimizwa tunarudi nyuma tena kwa wananchi kuonekana kwamba Rais wakati ule akiwa mgombea alitudanganya, kuna hali kama hiyo. Sasa mimi ningeshauri Ofisi ya Rais, jambo la msingi la kufanya, Mheshimiwa Rais anapotoa ahadi ya barabara ya kilomita mbili na nusu wahakikishe kwamba gharama za barabara kilomita mbili na nusu ziingie huko na watafute timu maalum ya kuweza kuzisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Utumishi, Kanali Mwijage amezungumzia kuhusiana na mishahara hewa lakini nataka nijikite pale ambapo tuliamua kwa makusudi kabisa kama Taifa kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Wakati ule akiongoza Mzee Rugunyamheto na kadhalika Mheshimiwa Mbunge wa Ngara kama sikosei tumeboresha vizuri maslahi ya wafanyakazi, lakini kuna mahali hatukutoa kipaumbele hasa kwenye suala zima la *succession plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizunguka kwenye Wizara mbalimbali, sina uhakika na Utumishi lakini kwenye Wizara mbalimbali na Idara mbalimbali za Serikali kuna ombwe au *vacuum* kubwa kwelikweli. Ukiangalia vijana wa miaka 27 unawatafuta Serikalini, vijana wa miaka 32 unawatafuta Serikalini na kwenye Idara mbalimbali na hata wale wa miaka 40, kuna mahali hatukwenda sawa, tufanyaje ili kwenda *speed* hatimaye kuweza kuziba mianya hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeingia neema, tumejaliwa, sasa nizungumzie gesi, bado tunazo leseni ambazo tumezitoa 28 hebu tuulizane leo na taarifa zinazotolewa ya kwamba kuna vijana gani wa Kitanzania wanaoshiriki moja kwa moja kwenda kufanya *seismic studies* au wanaoshiriki kwenye uchimbaji kule hata kwa ile kazi ya chini kabisa ya kupiga *anti-oxidant* kwa maana ya *anti-rust* kwenye mabomba ya gesi, hakuna! Taarifa tunazosomewa hapa na viongozi wetu pamoja na kuwa *verified* na *TPDC*, lakini *TPDC* hawana *representative* kule chini. Tunaambiwa kuna uchimbaji unaendelea baharini, taarifa zote anatuletea mwekezaji kwenye meza na kwenye kompyuta, hii si sahihi. Wakati umefika sasa tufanye juhudi za makusudi kabisa za kuweza kusukuma vijana wa Kitanzania kama uwezo wa kuwasomesha ndani hatuna tuangalie uwezo wa kutafuta nguvu nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono sana hoja hii na naomba ushauri wangu uzingatiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Nassir kwa kujali muda. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, namwita sasa James Mbatia halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Madelu na atamalizia Pindi Chana.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji au kasi ya sayansi na teknolojia duniani zinatupa sana shida Mataifa ambayo yanajulikana kama au nchi za Ulimwengu wa Tatu. Mtindo ambao bado tunaendelea nao wa kiutawala na ukiangalia mifumo yetu ya elimu ambayo ni kopi katika mataifa ambayo yanafikiri yanatuandalia na sisi tunakopi tunayaendeleza, inatupa matatizo makubwa sana. Hivi tukiamua kufikiri kwa mapana, tuangalie lengo la nane la milenia na *global partnership* na kama tunaweza tukasema *let us think globally and act locally* tukiona dunia ya kwamba ni kwetu hapa Tanzania utaona tunazo changamoto nyingi sana ambazo inabidi tuweze kuzi-*address* sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi tunayoijadili, Ofisi ya Rais ukiangalia mamlaka yake aliyonayo Kikatiba, ukiangalia nafasi mbalimbali au Taasisi ambazo zipo chini ya ofisi yake, utendaji wote kwa pamoja kwa ujumla wake kwenye Ofisi hiyo, unatia shaka kama kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia inaendana na kasi ya utendaji katika ofisi hii. Nasema hivyo kwa sababu mwaka 1933 katika *Montevideo Convention* walipoweka zile tabia nne za dola na sisi tunajikita

kwenye tabia ya tatu hasa ya utawala ukianza watu, ardhi, utawala na mahusiano ya nje. Hapa kwenye utawala tunayo mihimili mitatu, yapo mambo ya msingi ya kugawanya madaraka haya katika mihimili hii mitatu. Ukizungumzia mathalani kwenye Katiba yetu, Ibara ya 9 au ukiangalia tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu, haki ya mwanadamu kuishi, haki ya uhai wa mwanadamu ambaye hakuna raia yeyote mwenye haki au Taasisi yoyote au chombo chochote cha kuondoa maisha ya mwanadamu yeyote na Tanzania tumeridhia tamko hili. Tunazungumza kwenye Ibara ya 9 (a) suala la utu. Kwa mfano, maisha ya Mtanzania yeyote yakiondoka iwe ni ajali kwa makusudi, iwe ni migogoro iliyopo sasa hivi mathalani ya Madaktari, huwezi kuzungumzia kutokana na migawanyo ya madaraka basi tuache uhai huu uondoke kwa sababu mhimili huu hauwezi kuingilia mhimili huu, kwa sababu maisha ya mwanadamu huwezi ukayaweka kwenye gharama ya kitu chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema haya kwa makusudi kabisa kwa sababu janga tulilonalo kama Taifa inabidi kufikiria upya mfumo wetu wa kiuongozi, mfumo wetu wa kiutendaji, kuna matatizo makubwa. Nasema kuna matatizo makubwa kwa mfano, bajeti yote ya wafanyakazi mishahara inaonekana kwamba ni shilingi trilioni 3.78, ongezeko lake kutoka bajeti ya mwaka jana ni asilimia 15.6 ambazo takribani ni shilingi bilioni 500 lakini kuna mfumuko wa bei ambao ni zaidi ya asilimia 17.8. Kwa hiyo, utaona ongezeko lenyewe linaonekana wapi ukiweka kwenye hizi takwimu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuangalie tunazungumza changamoto zipo nyingi. Je, mishahara ya wafanyakazi hawa ipatikane wapi? Mfumo wetu wa misamaha katika sekta mbalimbali za kodi, mifumo yetu ya misamaha ikoje? Ukiangalia na ukipata takwimu za Hazina yenyewe kuanzia mwaka 2007 mpaka mwaka huu misamaha ya kodi imefikia takribani shilingi trilioni 5.05 ambayo ni zaidi ya mishahara yote ya wafanyakazi kwa mwaka huu wa fedha tunaojadili hapa, misamaha ya kodi ya mwaka huu wa fedha uliomalizika mwezi Juni. Kuanzia mwezi Julai mpaka mwezi Februari, mwaka huu ilikuwa takriban shilingi trilioni 1.048 ambapo msamaha huu wa kodi ungeongezwa tu kwa wafanyakazi kwa mwaka huu migogoro yote hii ingekwisha ambazo ni zaidi ya shilingi trilioni moja ambalo lingekuwa ni ongezeko la takribani asilimia 30 ya mishahara ya wafanyakazi na tungeondoka kwenye migogoro hii ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipobadilisha tabia zetu na hasa kwenye zile kanuni za kuwa na tabia ya ufanisi, tukaenda kasi kama wenzetu, hatutafanikiwa. Tabia ya kwanza, ya maadili; ya pili, ya uadilifu; ya tatu, ya uwajibikaji; ya nne ya kuheshimu sheria na taratibu tulizojiwekea na ya tano kuheshimu haki za binadamu. Kwa sababu kila mwanadamu anaheshimika kwa utu wake, sitapenda watu wasipende kufanya kazi. Tukiri kwamba, tunasema sana, lakini yale tunayoyasema hatuyafanyii kazi na pia suala la kuzingatia muda, (*time management*), tusipoutawala muda hatuwezi tukatawala kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano mingi, ahadi kwa mfano za Rais. Ahadi aliyoitoa Kibondo Mjini mathalani ya kilomita moja na nusu ya lami mpaka leo hii haijatekelezeka. Haki ili itendeke na ili uweze kupata amani lazima uone haki ikitendeka kwa sawa. Mwenyekiti Mheshimiwa Mrema hapa anasema ametumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa tu, lakini haki yake ikoje na ukiangalia hili tamko la ulimwengu la haki za binadamu, haki inatakiwa isiwe ya kibaguzi. Lakini mzee wetu huyu hapa anapata shilingi 800,000/= kwa miezi sita, unaweza kuona hata matibabu yake atayahudumia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukubali kwamba, mfumo wetu una matatizo na kama una matatizo tufanyeje? Naomba ukiangalia taarifa ya Utawala Bora ya Serikali ni ile ya mwaka 2007/2008, sasa tunajipima vipi kwenye vigezo vya sasa vya utawala bora? Niseme kwamba, inabidi tukubali kuwa, tukishirikiana sote kwa pamoja, kwa mfano, majanga yanayolisibu Taifa letu, leo hii tunapozungumzia janga la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam mathalani ambapo kwa kila siku tunapoteza takriban shilingi bilioni nne za Kitanzania, kwa mwaka mmoja ni takriban shilingi trillioni 1.46. Wakati ukiwa na janga mnafanya kazi kama *team work,* je, Ofisi ya Rais ikiagiza vyombo vyake vyote ikiweko TAKUKURU, Usalama wa Taifa, Jeshi na Wizara zinazohusika wakifanya maamuzi ndani ya mwezi mmoja msongamano huu utakwisha, tutajiondoa ile hasara tunayoipata takriban ya shillingi bilioni nne kila siku itaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo janga leo hii la ukabila, udini, ubaguzi wa rangi, huyu ametoka wapi na kuna majanga mengine ni ya kujitakia sisi kama binadamu na kuna majanga mengine ni ya Mwenyezi Mungu. Hatuwezi tukamsingizia Mwenyezi Mungu kwa majanga tunayojianzishia sisi wenyewe kwa mfano, ya ukabila, ya ubaguzi wa rangi na kadhalika. Sasa janga lolote likitokea inabidi tulifanye wote kwa pamoja *as a team work* na kama ni *team* ya pamoja, lazima tukubali kwamba mambo ya msingi lazima yawe *above political affiliations* na tusipofanya hivyo tutakuwa tunalumbana siku baada ya siku, nani mwenye mawazo bora kuliko mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingesema hivyo, hapana, lakini tuone kwamba Taifa likisambaratika sote tunasambaratika. Kwa hiyo, tuwe na msingi. Ukiangalia na Walimu wanavyopambana leo hii, mambo ya migogoro ya wanafunzi, mikopo ya elimu ya juu tangu mwaka 1990. Nakumbuka nilifukuzwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1992 kwa ajili ya kutetea migogoro hii hii ya mambo ya wanafunzi ya elimu ya juu na mpaka leo zaidi ya miaka 20 tumeshindwa kuitatua. Kwa hiyo, lazima tukubali kwamba, kuna tatizo hapa katikati. Tukubali kwamba makosa yetu ya jana wahenga walituambia hivyo yanatusikitisha, je, mafundisho yetu ya leo tunayafanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tena na nisisitize kwamba tukifanya kazi kwa pamoja Taifa hili litasonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia muda huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbatia na nakushukuru kwa kujali muda na kuwa makini. Kwa kweli nakupongeza sana kama Kiongozi wa Chama.

Waheshimiwa Wabunge naomba nimwite msemaji anayefuata, kama nilivyosema anayefuata sasa ni Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba Madelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Lakini nina uhakika Mheshimiwa Pindi Hazara Chana ndiyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho leo na bado naendelea kufanya mawasiliano na Waheshimiwa Mawaziri kuona na kujua wanajipanga namna gani ili waweze kujibu hoja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba Madelu.

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niseme na Watanzania wakati nachangia mada tuliyonayo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa manufaa ya Watanzania wote na kwa manufaa ya heshima ya Bunge hili, Bunge hili ni chombo cha juu sana ambacho kinaishauri Serikali, kinaisimamia Serikali na wakati mwingine kinaweka maazimio. Sasa kwa ajili ya ukubwa wake ule ningeomba Kiti chako aidha kitoe agizo ama kitoe ushauri ama kitoe maelekezo kwenye

baadhi ya maeneo yaliyoandikwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani kwenye mada hii ambayo yamejaa uchochezi na yamejaa udhalilishaji kwa baadhi ya kada za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 27, Kambi ya Upinzani imejumuisha na imewatuhumu Walimu kwa ujumla wao. Walimu wa Shule za Msingi pamoja na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tupeleke vizuri. Ukurasa wa ishirini na ngapi?

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 27 kwenye kitabu cha Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye mada tulizonazo mbele, *paragraph* ya tatu ameweka na mabano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwanza limenifedhehesha sana kwa sababu Walimu ni watu ninaowaheshimu sana, linasomeka namna hii: “Walimu wa Shule za Msingi hufanya biashara mashuleni wakati wa masomo.” Hii ni tuhuma kubwa sana kwa watu ninaowaheshimu na nina uhakika hata kama wapo sio Walimu wote, huwezi ukaandika Walimu wa Shule za Msingi wanafanya biashara mashuleni wakati wa masomo. Hii ni tuhuma kubwa sana.

Lakini pia …

**TAARIFA**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, natumia kanuni ya 64 (1). “Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge:- (a) Mbunge yeyote hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli”.

Mzungumzaji ambaye amemaliza kuongea sasa hivi anasema kwenye taarifa yake kwamba, Kambi ya Upinzani tumesema kwamba Walimu wote wanafanya biashara, nataka tu kumpa taarifa kwamba si Walimu wote ni baadhi ya Walimu wanauza biashara na akitaka mfano tutampa, asilidanganye Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mbunge kwa mujibu wa kanuni, sitakiwi kusema, wewe ndio unayetakiwa kupokea taarifa ama kuikataa. Sasa nisiingilie kati ingawa na mimi nina hiki kitabu hapa. Kwa hiyo, nirudishe taarifa kwako kwa mujibu wa kanuni ili uweze kuipokea taarifa hiyo iliyoletwa na Mheshimiwa Sungura ama kuikataa na mimi nitoe maamuzi ya kuendelea na mchango wako ama kutokuendelea na mchango wako.

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyenipa taarifa labda arudi darasa la kwanza akafundishwe kusoma. Nimesema hivi imeandikwa kwenye taarifa yao na nimewasomea. Kwenye taarifa hii sio natoa kichwani, kwenye taarifa wameandika Walimu wa Shule za Msingi hufanya biashara mashuleni wakati wa masomo, kwenye kitabu nimesoma humu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 64 (1)

**MWENYEKITI:** Iliyokiukwa ipi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: 64 (1)(a) na 64(1) (f) na 64(1)(g).

**MWENYEKITI:** Haya zisome.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu kutokutoa mambo yasiyokuwa ya ukweli.

**MWENYEKITI:** Naomba uzisome zote uzisome kama zilivyo Mheshimiwa Mnyika. Umesema 64(a).

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** "Bila ya kuathiri Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. (f) Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge mwingine yeyote. (g) Hatatumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyekuwa akichangia amesema kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani imeandika kwamba Walimu wote na ametumia neno Walimu wote wa Shule za Msingi na tunaweza tukarudi kwenye *Hansard* tutaona neno "wote". Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba

nikusomee maana yake anasoma kipande kidogo anaacha baadhi ya maneno.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Mnyika wewe ngoja kwanza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naomba nikusomee kwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika naomba uketi. Naomba Mheshimiwa Mnyika wewe umeongoza, kanuni uliyoitumia si kanuni inayokufanya wewe u-*justify* ukweli. Hii kanuni namba 64 (a) yenyewe inasimama kama ilivyo. Ungerudi kwenye ile kanuni nyingine ambayo, Mheshimiwa Mnyika naomba hebu tuelewane, unamtuhumu Mbunge kwa kusema uongo wewe ndio sasa unatakiwa u-*justify* ule uongo ambao unasemwa na Mbunge, hilo la kwanza.

Lakini la pili, naomba hebu mnisubiri, nataka twende taratibu, umesema kwamba hatatumia lugha ya matusi kwa Mbunge ama mtu mwingine yeyote. Sasa nilikuwa nafikiri uende pia hapo ndio useme hayo matusi pia yaliyotokea, halafu useme pia ile lugha ya kuudhi iliyotumika kwa sababu umetaja vipengele hivyo. Ukishasema Mheshimiwa Mnyika kaa chini suala la kusoma hapa atasoma mtu anayepewa Mwongozo na aliyepewa Taarifa. Wewe utaniambia tu vipengele vilivyokiukwa ili sasa niweze kutoa *ruling* yangu na aliyepewa taarifa aweze kusema kwa mujibu wa utaratibu.

Sasa Mheshimiwa Mnyika ukiwa unaniongoza kwa utaratibu unaotaka wewe, wewe tena ndio usome alichokuwa anasema mtu, wewe ndio useme kanuni

zilizokiukwa sasa na mimi kazi yangu hapa itakuwa ni kufanya nini. Tugawane majukumu Mheshimiwa Mnyika kwa kulingana na taratibu za kikanuni. Sasa wewe umeainisha hapa kanuni zilizokiukwa na mimi nakubaliana na wewe; ya kwanza umesema kwamba hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli, haya hiyo tumemaliza. Umesema kwamba taarifa hizo alizosema na umetaja neno "wote" ambalo halipo kwenye kitabu, hiyo umemaliza. Hebu nenda sasa kwenye ile uliyosema hatamsema mtu vibaya kwa lugha ya matusi. Hebu niambie hiyo lugha aliyoisema, halafu nenda kwenye ile (g) Mheshimiwa Mnyika ndiyo tunakwenda hivyo. Sasa ukitaka na wewe ndio uwe Mwenyekiti na wewe ndio mchangiaji, hatutakwenda.

**MBUNGE FULANI:** Acha ukada!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu iingie kwenye rekodi neno moja tu, neno moja tu. "Kambi ya Upinzani imetumia neno "mfano" kutokana na mishahara midogo, imetumia neno mfano ambalo huyu hakulisema.

Sasa nirudi kwenye haya maeneo mengine na Mwenyekiti katika Mwongozo wako naomba usome *paragraph* yote usisome mstari aliosoma yeye.

**MWENYEKITI:** Hebu Mheshimiwa Mnyika kaa, keti, keti. Hivi Mheshimiwa Mnyika sijui kama unanielewa, kwa sababu sasa natoa Mwongozo huu kwa mara ya mwisho. Nimekukubalia, nimekwambia Mnyika lete hoja zako na umeniambia kwamba unaleta hoja zako kuhusu utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 64.

Mheshimiwa Mnyika nimekuambia sawa twende 64, umesema kanuni iliyokiukwa ni 64(a) na 64 (f).

*(Hapa Mheshimiwa Mnyika alisimama kutaka kuzungumza)*

**MWENYEKITI:** Ngoja subiri, huwezi ukasimama wakati naongea, unavunja kanuni pia na nitachukua maamuzi mengine ukisimama kabla sijamaliza. Lakini Mheshimiwa Mnyika umesema kanuni nyingine iliyovunjwa ni kanuni ya 64(g), nimekwambia Mheshimiwa Mnyika ,ni kweli kanuni hizo, sasa wewe naomba ukisaidie Kiti kujua kanuni hizo zilivunjwa namna gani, Mheshimiwa Mnyika naomba unisikilize. Kwa sababu sasa natoa Mwongozo kwako kwa mara ya mwisho, ukikiuka Mwongozo huu utakuwa hukitendei haki Kiti.

Umesema kanuni namba 64(a), Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anachangia hajasema ameipa taarifa ambazo hazina ukweli na pale umesema kwamba kwenye taarifa ambazo hazina ukweli ameongeza neno “wote” na kwenye taarifa ya Kambi ya Upinzani neno “wote” halipo, hilo la kwanza tumemaliza.

Nakuomba unaposimama sasa nenda moja kwa moja kwenye (f) iliyokiukwa inayosema” “Kwamba hatasema vibaya ama kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote.” Naomba hiyo lugha uniambie ukimaliza hapo nenda moja kwa moja kwenye (g), ukitaka tena maneno mengine ya kunizungusha Mheshimiwa Mnyika sasa sitakubaliana

na wewe.  Ndiyo maana nimesema niache Kiti nifanye kazi yangu, wewe fanya kazi yako ya Mwongozo na aliyepewa Taarifa asubiri jambo la Taarifa na Mwongozo aliopewa.  Sasa ukitaka kufanya yote matatu wewe unavunja kanuni na unadharau Kiti. Nimemaliza, naomba Mwongozo wangu uzingatiwe, haya endelea.

**MBUNGE FULANI**:  Acha ukada!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele 64(1)(f) kinasema "Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi.  Sasa amemsema vibaya Mbunge aliyempa taarifa na amemsema vilevile kwa kuvunja kifungu (g) inayohusu lugha ya kuudhi na kudhalilisha, kwamba arudi darasa la kwanza akasome tena.  (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwigulu kwenye lugha hiyo ya kumrudisha mtu darasa la kwanza ni lugha ya kuudhi naomba uifute.  Halafu kwenye ile unayoambiwa kwamba hujasema sawasawa, eeh hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.  Sasa nakurudisha usome kifungu kile ulichokuwa unakisoma halafu u-*justify* ukweli wako, lakini futa kwanza ile lugha ya darasa la kwanza.

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta hilo neno, kwa hiyo nitawasomea mimi mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Unafuta neno gani?

**MHE. LAMECK L.N. MADELU**: Nafuta neno la kumrudisha darasa la kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *paragraph* hii niliyowasomea hata kama ni mfano hakuna neno baadhi someni vizuri nyinyi wenyewe, hakuna neno baadhi badala yake imeandikwa tu mfano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu naomba uisome kama ilivyo kwanza.

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Nawasomea kama ilivyo. Sentensi inasema hivi anasema “Walimu wa Shule za Msingi hufanya biashara mashuleni wakati wa masomo” Mimi ndio nasema hii ime-*generalize.* (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unitunzie na muda wangu. Lakini imeendelea vile vile wakasema: “Pia Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Umma hufanya kazi za muda katika vyuo vingine tofauti na kule walikoajiriwa”. Hii nayo ni *accusation* kubwa sana kwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitakiomba Kiti chako kiweke kumbukumbu sawasawa ili tusiwaonee Walimu kwamba wanafanya biashara wakati wa masomo. Hii si kweli na ni lugha ambayo kwa kweli inawaonea, haiwatendei haki Walimu na kwa kweli sikutegemea lugha kama hii itoke kwenye Chama cha Upinzani ambacho kinajinasibu kwamba kinawatetea wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nitaiomba Kiti chako kiwatake wasahihishe. Wamesema mali za umma ukurasa wa pili *paragraph* ya pili wanasema: "Mali za umma imeingia katika kashfa mbalimbali zinazohusu rasilimali za nchi kuporwa. Sasa sentensi ambayo nitakiomba kiti chako kitoe maelekezo inasema, "Lakini Usalama wa Taifa hatujawahi kusikia popote...

**MWENYEKITI:** Iko sehemu gani Mheshimiwa Mwigulu kwa sababu mambo hayo lazima tuelewane vizuri.

**MHE. LAMECK L.N. MADELU:** Ni ukurasa wa pili *paragraph* ya pili, Ofisi ya Rais. Wamesema nchi yetu imeingia katika kashfa mbalimbali zinazohusu rasilimali za nchi kuporwa, lakini nenda kwenye sentensi iliyoanzia na lakini, wanasema: "Lakini Usalama wa Taifa hatujawahi kusikia popote wamehusika katika kuzuia mchakato huo japokuwa wanakuwa na taarifa za kutosha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama wa Taifa kwenye nchi yoyote ni Taasisi nyeti sana na ni roho ya nchi. Kwanza Usalama wa Taifa haufanyi kazi kama *traffic* ambao kila mtu anaweza akawaona.

**TAARIFA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma kifungu cha 64(1): "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na

kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge. Mbunge, nasimamia (a), hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mzungumzaji anayezungumza naamini ana uelewa, tunaposoma taarifa kuna kitu kinaitwa *context*, anayejaribu kupotosha umma anasoma *out of context,* nina mashaka na elimu yake, anataka kuwapotosha Watanzania, asome kwenye *context* ya hotuba ya Kambi ya Upinzani, asisome mstari mmoja, anapotosha umma.

**MBUNGE FULANI:** Aache ukada!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Asiingize siasa kwenye mambo ya muhimu kama haya.

**MWENYEKITI:** Naomba waropokaji mumpe nafasi niliyempa nafasi. Mheshimiwa Mbunge, sasa hapo mmenichanganya hata mimi. Wewe umesema taarifa, una kitabu cha Kanuni hapo? Hebu chukua kitabu chako cha Kanuni. Mheshimiwa Msigwa taarifa iko katika Kanuni ya 68(8). Hebu soma hicho kifungu Mheshimiwa Msigwa, Waheshimiwa Wabunge hebu subirini, tusameheane, ngoja twende kwa taratibu ndiyo tutaelewana vizuri. Mimi nakaa, wewe soma.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nimesoma 64(1).

**MWENYEKITI:** Nimekuelekeza usome Kanuni ya 68(8). *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** 68(1).

**MWENYEKITI:** Msigwa, hebu Mchungaji 68(8).

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Inasema: “Vile vile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa, kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo.”

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa wewe umeniomba taarifa kwa mujibu wa Kifungu cha 64(1). Sasa kwa sababu taarifa ambayo sio sahihi wewe nakukatalia siwezi kutoa Mwongozo wowote kwa sababu hujafata Kanuni. Nikurejeshe Mheshimiwa Msigwa mara nyingi wewe unagombana na mimi kwenye kiti. Unasimama bila kusoma na kujua Kanuni zinaelekeza nini. Kwa hiyo, utaratibu huo mara nyingi unakufanya uende katika Kanuni ambazo sizo na ndiyo maana nikakuomba leo usome mwenyewe 68(8) inayohusu taarifa.

Hii naifanya kwa sababu moja kubwa, kumekuwa na *message* zinazopelekwa nje kwamba kiti mara nyingi kinawaonea baadhi ya watu. Lakini hiyo nataka kuithibitisha hapa kwamba utaratibu ni kwamba, kila Mbunge anayesimama ni lazima ajue anatumia Kanuni namba ngapi. Kwa hiyo, Msigwa kwa kuwa Kanuni yako uliyotumia na kwa kuwa umenichanganya hapa wala siwezi kujua nishike kuku ama yai, naomba niendelee na mtu aliyesimama. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 64(1)(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayezungumza ili aelewe kwamba anachokisema anakitambua; alikuwa Mtumishi wa Benki Kuu ambayo ilikumbwa na kashfa ya ufisadi wa *EPA* na sasa ni Mweka Hazina wa Chama cha CCM inayotuhumiwa kwenye wizi wa pesa za Kagoda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika nenda kwenye hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kambi ya Upinzani kwenye Mkutano wa Tisa wa Bunge.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mnyika, naomba ujielekeze kwenye hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo najielekeza kwenye hoja. Lakini Usalama wa Taifa hatujawahi kusikia popote katika kuzuia au kuhusika kwenye kuzuia. Kwenye Bunge hili, Kambi ya Upinzani ilileta ushahidi wa Barua ya Usalama wa Taifa kwenye kashfa hiyo ya *EPA* ambayo anaifahamu vizuri. Usalama wa Taifa ukizuia jambo lisije Bungeni kujadiliwa badala ya kuibua ufisadi, kuzuia ufisadi usitokee, ushahidi huo uko ndani ya kumbukumbu za Bunge na ukitaka nilete ushahidi zaidi nitaleta ushahidi wa namna gani matukio ya uhalifu na hili ni lalamiko ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa. Baadhi ya Watumishi wa

Usalama wa Taifa wanatoa ushirikiano, wanatoa taarifa viongozi wa juu yao hawazishughulikii taarifa na katika Hotuba ya Ofisi ya Rais, hii tunayozungumza, haijatuonyesha popote Idara ya Usalama wa Taifa ilipozuia matukio ya uhalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mchangiaji atambue huo ukweli na aache propaganda na aache siasa kwa sababu yeye ni mmoja wa watuhumiwa.

**MBUNGE FULANI:** Na pia aache ukada. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba uthibitishe hilo kwamba na yeye ni mmoja wa watuhumiwa kabla sijatoa Mwongozo na kama unao uthibitisho kwamba na yeye ni mmoja wa watuhumiwa naomba utoe uthibitisho huo kama huna ufute kauli yako ili niweze kufanya maamuzi ya kinachofuata ili tuendelee na kazi za kuwawakilisha wananchi. Mheshimiwa Mnyika una uthibitisho wa kwamba Mheshimiwa Mwigulu ni mmoja kati ya wanaotuhumiwa?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa mmoja wa watumishi wa Benki Kuu...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mnyika umesema hapa na kulithibitishia…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Niambie kwanza niseme tuhuma gani ninazo dhidi yake na nitoe ushahidi wa hizo tuhuma. Nimesema ni mmoja wa watuhumiwa.

Niruhusiwe niseme anazo tuhuma gani na nitoe ushahidi wa hizo tuhuma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, umesema kwamba unao ushahidi, naomba unisikilize kusudi utakaponijibu ujibu Mwongozo nitakaokupa kwa mujibu wa taratibu. Mheshimiwa Mnyika umesema hapa na kulithibitishia Bunge, Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Umesema unao ushahidi na umelithibitishia Bunge kwamba yeye Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba ni mmoja wa watuhumiwa katika kesi hizo za *EPA*. Sasa na mimi nakupa siku saba ulete ndani ya Bunge tuhuma zinazomgusa Mheshimiwa Mwigulu. (*Makofi*)

*Order please,* nasema *order please.* Narudia kusema siku saba, nataka tuhuma zinazomgusa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba. (*Makofi*)

Naomba *order*, Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize zinazomgusa yeye katika kesi hiyo ya *EPA*. Naomba tuhuma zinazomgusa Lameck Nchemba Mwigulu ndani ya siku saba. Mheshimiwa Mwigulu endelea!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwa mujibu wa Kanuni ya 68 inaniruhusu niweze kuonesha.

**MWENYEKITI:** 68 ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, 68(1), inaniruhusu niweze kuonesha kama kuna Kanuni zozote zinazovunjwa na ili Bunge liweze kutekeleza wajibu wake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu jana hadi leo Kanuni nyingi sana kupitia mlango huu wa Kanuni 68(1) zimekuwa zikuvunjwa sana na pengine matumizi ya kuhusu utaratibu na miongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unataka kusema Kanuni zote zinazoanguka kwenye 68.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaka kukuonesha Kanuni zinazovunjwa humu ndani ni nyingi ndiyo maana sitaki kusema tu kwamba, niruhusu tu nijaribu kueleza nini kinachoweza kikasaidia Bunge lako liweze kufanya kazi vizuri. Lakini Kanuni zinazovunjwa ni nyingi mno kwa sababu mahali penye Utaratibu mtu anaomba Mwongozo, mahali penye Mwongozo mtu anaomba Utaratibu. Sasa kuna vitu kama hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ukae. Nafikiri unalo jambo la msingi lakini na wewe

utusaidie kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni hata wewe unatakiwa kutusaidia kujua Kanuni gani. Angalau mfano, wa Kanuni moja na nyingine nyingi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inasema hivi; Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu. Nimefanya hivyo; ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema ananyamaza na kukaa chini na Mheshimiwa Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu iliyokiukwa. Nimesema ni maeneo mengi, Kanuni zote zinazohusu Mwongozo au kuhusu Taarifa. Zote zinakiukwa na ndipo ninapotaka kufafanua ili kukisaidia Kiti chako.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yanayosemwa hapa kwanza kabisa yanakwenda kinyume na taratibu na kanuni zako ambazo wewe unazisimamia na ningekuomba sana kwamba maneno haya kwa sababu yanatumika vibaya yanapoteza muda wa Bunge kwa sababu Bunge lolote duniani linaongozwa na shughuli zake za siku hiyo kwenye *Order Paper*. Hapa tunahama kwenye shughuli ya siku hiyo tunaanza mwongozo, utaratibu, mwongozo kiasi kwamba tunakula muda wa wachangiaji wengi ambao wangeweza kusaidia Serikali kama jukumu la Bunge linavyotakiwa kuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana kwamba, kwanza kabisa hata utaratibu wa mtu kusema mtu haruhusiwi kusema kwa jambo hilo zaidi ya mara moja humu ndani ya Bunge, isipokuwa tu kwa mazingira maalum ndiyo anaweza kusema juu ya jambo zaidi ya mara moja. Sasa kama mtu ataruhusiwa kusema huyo huyo kutoka asubuhi mtu anamwangalia huyo huyo hata wanaotizama hilo Bunge lako watachoshwa. Mimi nikuombe sana tumia Kanuni zile vizuri. Mtu haruhusiwi kusimama kwa jambo hilo hilo mara tano, mara sita linawachosha watazamaji wengine, linawachosha wasikilizaji na hivyo Bunge lako kwanza linashuka kiwango kwa sababu watu wamechoshwa huko nje na vituko vinavyoendelea humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuoneshe kwamba baada ya hapa ukienda kupitia vizuri utakumbuka kwamba Kanuni nyingi sana zimerukwarukwa, ni vizuri niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanatuamini sana hebu tufanye; kwa sababu Bunge linaanza na uwasilishaji wa Kambi zote, mnakwenda mtu anachangia, watu waachwe kila mtu aseme ya kwake amalize, baadae kwenye majumuisho Serikali itajibu. Sasa hapa imekuwa kama ni mahali ambapo ni mdahalo ambao hauna *conclusion*. Naomba sana Kiti chako ki-*control* mazingira haya ili Bunge liweze kufanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kila Mbunge anayesimama hapa ni fundi mzuri wa Kanuni ingawa wote bado tunatakiwa kuendelea kujifunza

Kanuni hizi vizuri. Kwa hali hiyo, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge pamoja na mambo yote hayo baadaye lazima huwa narudi kwenye Kanuni yangu ya 5(1) ambayo ndiyo inanipa nguvu sasa kufanya maamuzi kulingana na masuala yote ambayo yanaendelea. Kwa mujibu wa mamlaka ya Spika au Mwenyekiti kama Spika kwa Kanuni namba 5(1), naomba sasa mijadala yote hii inayoendelea sasa ifungwe. Mheshimiwa Mwigulu malizia mchango wako na hapo baadaye tutaendelea na hatua inayofuata.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema nimalizie, lakini ndiyo nilikuwa naanza tu na muda ndiyo umekwenda hivyo na nilipewa taarifa kwamba walipanga kuhakikisha wanafanya hivyo ili nisiongee kwa sababu nawabomoa sana.

**MWENYEKITI:** Naomba ujikite kwenye mchango wako.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Kwanza kwa utangulizi tu kwa ile ambayo imetokea hapa. Yale yaliyotokea Benki Kuu 2004/2005, nilikuwa Chuo Kikuu na nimekwenda Benki Kuu tarehe 1 Oktoba, 2006. Kwa utangulizi tu. Kwa hiyo wakati yanatokea, nilikuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu na hata mlango wa Benki Kuu nilikuwa siujui. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichokuwa nakisema umeshakipata usome ile *paragraph* na utoe maelekezo yanayostahili. Lakini jambo lingine ambalo

nataka nilisemee hapa ukijiangalia kwenye kioo ukakuta una matope kosa sio la kioo. Hii sentensi imerudiwarudiwa hapa na kwenye hotuba iliyopita ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alisema kama vile Chama cha Mapinduzi ndiyo kimekuwa kikifanya propaganda ya ukabila na ukanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wana macho na wana masikio, hili jambo la ukanda limeletwa hapa na aliyekuwa anatoa taarifa leo, ukurasa wa 36, akasema Waziri alijibu kirahisi kwamba wote wanaolalamikia ndiyo wanaojihusisha na jambo hilo. Yeye akasema huu ni mzaha. Nimeona hili nalo niliwekee kumbukumbu. Ukigeuka tu upande walipo hapa hapa Bungeni na karatasi ninayo hii hapa, nitakupa inayoonesha jinsi walivyokuja kila mmoja na ndugu yake kwa kiwango kikubwa. Hata wakikaa hapa hakuna tofauti wanapokaa sebuleni kwenye vikao vya ukoo kule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu naomba uketi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwigulu kwa mujibu wa Kanuni hata kama hao unaowataja wamekuja kwa utaratibu huo wa kiundugu na mambo mengine, lakini huwezi ukamaliza kwa kusema kwamba kama vile wako sebuleni. Naomba ufute sebuleni halafu uendelee na utaratibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu naomba usikilize Kiti, naomba ufute hiyo kauli uliyoisema ya sebuleni kwa sababu sio lugha ya Kibunge.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba ufute kwa sababu sio lugha ya Kibunge.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naifuta.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Utaratibu mtatoa baadaye, naomba uendelee.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naifuta ile kauli, lakini nataka niwaelezee Watanzania kwamba hili jambo la ukabila si kwamba tunalifanyia propaganda, lipo. Kwa mfano, hata kwenye vile Viti, kati ya vile Viti Maalum tisa; Shinyanga wenye Majimbo manne wana Mbunge mmoja wa Viti Maalum.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu naomba ujikite kwenye hoja maalum.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI**: Nimesema nitatoa utaratibu baadaye.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu jikite kwenye hoja.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba Mwigulu ufute hoja hiyo uendelee na mchango wako.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtu anayeomba utaratibu atasimama kwenye kiti bila kupiga kelele. Kwa hiyo, mtu anayesimama na kuwasha *microphone* pia kwenye Kanuni someni, hairuhusu. Naomba mfuate utaratibu.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilifuta lile. Hili jambo lichukuliwe kwamba sio propaganda. Sio propaganda na kwa uhalisia wake lipo na watu wanapotaka Serikali isilite humu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uendelee na bajeti.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili la leo niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwasaidie Watanzania. Bunge ni chombo kikubwa sana na kwenye haya ambayo tumeyaona sehemu moja wapo hapa ni sehemu ya TAKUKURU. TAKUKURU imetusaidia vijana wengi sana kufika Bungeni kwa kuzuia rushwa wakati wa uchaguzi. Lakini kwenye vyama vikwazo ambavyo inakumbana navyo leo hii tunaona kuna kesi nyingi zimerundikana, wamefanya uchunguzi lakini kesi tunasema hazijatolewa maamuzi. Ndugu zangu, TAKUKURU sio Mahakama, hawa wanafanya jukumu lao wakishamaliza wanapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, ikitoka kule ndiyo inakwenda Mahakamani. Mahakamani Bajeti huwa tunazipitisha sisi wenyewe, kesi zinarundikana Mahakamani. Kwa hiyo, kama tunataka tusaidie chombo hiki kwanza tukipatie bajeti ya kutosha. Pili, nitaleta Muswada Binafsi ambao utaongelea kuanzishwa kwa Mahakama ya Uhalifu wa Kiuchumi ili hata kama Bajeti itakuwa ni ndogo iwe imetengwa kwa ajili ya kesi zinazohusiana na hili. Lakini pia tunatakiwa kama Bunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwamuda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili kwa mujibu wa maelekezo ya Makatibu. Naomba umalize.

**MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii kweli shughuli, lakini wakati mwingine ni shughuli pia yenye tija na afya. Afya ni kuonesha kila Mbunge umaarufu wake katika kuzijua Kanuni na kutokuzijua Kanuni sawasawa. Kwa hiyo, wakati mwingine hii inatusaidia kwa sababu katika mchezo wowote lazima kuwepo na kanuni za kuweza kuongoza mchezo. Kwa hiyo, hiyo pia huwa inasaidia kuona tunaongozaje mchezo wetu kwa mujibu wa Kanuni.

Sasa nilisema akimaliza Mheshimiwa Mwigulu atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana, lakini simwoni hapa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba yangu kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara zilizowasilisha hotuba za bajeti zao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi zina changamoto nyingi sana za kiutendaji ambazo zinalalamikiwa na watumishi wa umma, changamoto ambazo zimeweza hata kusababisha wakati mwingine kuchochea migomo katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo ni vizuri Serikali ingeziangalia kwa umakini ili kuleta ustawi wa nchi yetu na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kuwa kumekuwepo na migomo au matishio mbalimbali ya migomo kwa baadhi ya kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko mengi ambayo watumishi wa umma wanayalalamikia ni pamoja na suala zima la maboresho ya maslahi ya wafanyakazi yakiwemo mishahara, posho mbalimbali ikiwemo posho ya mazingira magumu, pamoja na malalamiko kutoka wa wafanyakazi, pia yapo malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi wakizilalalamikia baadhi ya taasisi za umma kujihusisha na vitendo vya rushwa au huduma mbaya. Baadhi ya taasisi hizo ni kama Hospitali, Mahakama, Halmashauri zetu, Wizara ya Ardhi, Polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo niliyoyazungumza ningependa kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ijaribu kualnisha yale maeneo yenye mazingira magumu kwa wafanyakazi ikaweka vivutio maalum. Pili, itafute njia ya kuimarishWa kwa maadili ya watumishi wa umma sehemu za kazi ili kupambana na tatizo kubwa la rushwa. Pia sheria itungwe kuwabana watumishi wanaovujisha siri za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na uwajibikaji kwa watumishi wale wasiowajibika basi wawajibishwe na wale viongozi wasiotimiza wajibu wao nao wawajibishwe ili kulinda utawala bora na maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kupotoka kukubwa sana kwa maadili ya Taifa letu na viongozi wengi kujilimbikizia mali. Upo utaratibu wa viongozi wetu wa umma kujaza fomu kwa ajili ya kutaja mali zao. Labda utaratibu ungeangaliwa, kiongozi anapoanza uongozi mali zake, pia utaratibu huo anapofikia tamati ya uongozi wake pia ajaze fomu ili kujua katika uongozi wake amemaliza akiwa na mali kiasi gani. Huwa najiuliza hawa TAKUKURU kweli wanafanya kazi yao inavyotakiwa? Kuna baadhi ya viongozi wamekuwa wakituhumiwa kujilimbikizia mali za umma, tuhuma hizo zimekuwa zikitolewa na vyombo vya habari na tumeshuhudia viongozi wengine kukiri sasa TAKUKURU wanafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kesi nyingi sana zimekuwa hazipati ufumbuzi za TAKUKURU na tumeshuhudia baadhi ya Maofisa wa TAKUKURU wakituhumiwa na wao kwa rushwa na pia kuwalinda baadhi ya viongozi. Je, chombo hiki tutakiamini vipi? Mpaka wananchi wengine kuwabadilishia jina na kuwaita TAKUKURA, hii ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa kada hizi wangeangaliwa kwa umuhimu wake ili waajiriwa wawe safi ili kuleta imani kwa chombo hiki. Pia chombo hiki kiwezeshwe ili kiwe na nyenzo za kisasa na ikiwezekana ofisi ziwepo katika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la MKURABITA lipewe kipaumbele ulingane na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria na Serikali isambaze

mpango wa MKURABITA kwa nchi nzima kuliko inavyofanyika hivi sasa ambapo Wilaya huchaguliwa kutumia vigezo vilivyofanyiwa tathmini na elimu itolewe ili wananchi wapewe haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie maadili ya viongozi, yaangaliwe upya. Ni vema uwepo utaratibu wa kufungua Chuo cha kuwaandaa viongozi kama ilivyokuwa zamani kwa Chuo cha Kivukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwaamini wataalam wetu kwa kufanya kazi kwa kutegemea taaluma ya utawala tu haitoshi, ni vema maadili na miiko inayosimamia utendaji ifunzwe kama ilivyo. La sivyo, sekta ya utumishi wa umma itaendelea kushindwa kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iboreshe Sheria ya Maadili ya Viongozi. Mgongano wa kimaslahi kati ya viongozi wa kisiasa na biashara zao ndiyo umetufikisha mahali hapa tulipo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona taarifa za viongozi kuhusu ukiukwaji wa maadili ya kujilimbikizia mali zinazidi kutolewa na kusambazwa kwa umma wakati huo huo Tume imekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, ni vema viongozi wa umma wakazingatia maadili ya kazi

katika utendaji wao wa kila siku, hasa kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwatazame watendaji mbalimbali wa kada ya chini ambao wengi wao wako vijijini, hii ndiyo njia pekee ya kuboresha maisha ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa kunipa afya njema na ufahamu wa kuandika kuchangia hoja hii. Pia nakupongeza wewe binafsi na timu yako kwa kuliendesha Bunge hili kwa uadilifu pamoja na kuwa mapungufu ya kibinadamu hayaepukiki, kwani hakuna mkamilifu ila Mwenyezi Mungu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama wa Taifa ni Idara nyeti sana na muhimu sana kwa usalama wa nchi yoyote ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu na unyeti wa idara hii ni lazima Serikali itoe kipaumbele cha pekee kwa idara hii ili iendane na mabadiliko ya teknolojia. Idara hii sasa iboreshwe, iimarishwe na ifanye kazi kwa juhudi na kisayansi zaidi ili kukidhi haja ya kuwa na usalama wa Taifa wenye viwango vya karne ya 21 ambayo ni karne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya sasa ya utandawazi ina hujuma nyingi sana zitokanazo mara

nyingine na ushawishi wa Mataifa mengine; hasa Mataifa makubwa ambayo yana hulka ya unyonyaji. Idara hii sasa ni lazima iwe makini zaidi na yenye macho makali ya kuyaona haya. Idara hii pamoja na jukumu kubwa ililonalo la kuhakikisha usalama wa viongozi wakuu wa Serikali, lakini pia ina jukumu la kuangalia usalama wa rasilimali zetu zisitoroshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Usalama wa Taifa ina jukumu pia la kuangalia usalama wa uchumi wetu. Uchumi wetu ukiwa imara inakuwa nafuu kuangalia usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoroshwaji wa fedha nje. Idara hii ina jukumu la kuchunguza fedha zinazotoroshwa na kupendekeza Serikalini namna bora ya kudhibiti. Lakini pia idara hii ichukue hatua kwa wanaohujumu uchumi wetu. Utoroshwaji wa dhahabu na madini mengine ya thamani, idara hii inawajibika kuzuia kwani huo ni uhalifu wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii ichunguze fedha shilingi 315 bilioni zilizoko katika mabenki ya Uswisi. Taarifa zitolewe wazi, wahusika wachukuliwe hatua na fedha hizo zirudishwe Hazina ili zisaidie wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wahabeshi. Idara hii ina jukumu la kujua kiini cha biashara hii *(human trafficking)*. Vinara wa biashara hii ambayo inaonekana ina mizizi mirefu na iliyokomaa wakamatwe na sheria ifuate mkondo wake ili kukomesha uharamia huu. Uchu wa kujilimbikizia fedha

hata haramu ni hatari kwa usalama wa Taifa letu! Watu hawa wanaosafirishwa wanaweza wakawa ni mamluki na wanaweza kutuletea madhara makubwa ndani ya nchi yetu hasa wakati huu ambao kuna watu wanaotaka madaraka *by hook or by crook*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naiunga mkono hatuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Mfuko huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania hasa wale ambao kipato chao cha siku hakitoshi kuendesha maisha yao.

Mfuko huu una changamoto nyingi sana, ya kwanza Mfuko hauwafikii wananchi wenye shida ya maisha. Utoaji wa mikopo ni wa kujuana, hivyo hauleti matokeo yaliyotegemewa. Hivyo, tuhakikishe kuwa mikopo hii inawafika walengwa. Changamoto ya pili ni kuwa wanakopeshwa hawarejeshi mikopo kwa wakati na wengine hawarejeshi mikopo yao kabisa. Hii inasababisisha wajasiriamali wengine wasipate mikopo. Naiomba Wizara ichukue hatua za dhati ili kurekebisha changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TAKUKURU bado chombo hiki hakifanyi majukumu yake inavyotakiwa. Bado rushwa haijapungua hata kidogo. Mara zote hungojea tatizo liripotiwe, halafu wao wakachunguze.

Hawana ubunifu wowote wa kuchunguza vitendo vya rushwa wao wenyewe na kuwapeleka watuhumiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima muelekeo wa taasisi hii ubadilike ili uweze kufanya kazi vizuri zaidi na kuweza kupunguza ulaji rushwa.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Celina O. Kombani na Mheshimiwa Stephen Masato Wasira kwa hotuba zao kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo dalili za mfumo wa usalama na ulinzi wa nchi kuzorota. Hii inadhihirishwa na matukio ambayo yamekuwa yakitokea kwa kadri ya miaka mitatu mpaka mitano iliyopita bila hatua madhubuti kuchukuliwa na vyombo vya usalama na ulinzi. Mifano ya matukio hayo ni:-

Kumekuwa na wahamiaji haramu ambao wamevuka mipaka ya nchi katika maeneo ya Kigoma, Kagera, Kilimanjaro na maeneo mengine. Kwa taarifa zilizopo wahamiaji hao, hasa eneo la Kagera, wameingia nchini wakiwa na mifugo na wameanzisha migogoro na wenyeji. Kwa taarifa zilizopo, viongozi wa Wilaya na Mkoa wameshindwa kabisa kutatua tatizo hili la wahamiaji haramu.

Matukio mengine ni yale yanayotokea katika Kata ya Bunju, Boko, Madale na kadhalika Dar es Salaam. Wavamizi wamekuwa wakivamia maeneo hayo ya watu na kubomoa nyumba zilizojengwa na kuchoma mashamba, halafu kuyauza maeneo hayo. Wenye maeneo wamejitahidi kufuata taratibu kwa kuripoti Polisi, kwa Mkuu wa Wilaya na Mkoa hadi kwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa, lakini hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahalifu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina kauli gani kuhusu uhalifu huu ambao umevishinda vyombo vya usalama kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, katiba ya sasa ya Muungano wa Tanzania inatambua nafasi ya wanamgambo katika usalama na ulinzi wa nchi. Je, ni lini wataweka kwenye ajira rasmi katika utumishi wa umma ili watekeleze majukumu yao kikamilifu na kwa kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu uliopo kwenye Halmashauri kuajiri watu kwa vipindi vifupi vifupi mathalani, katika Halmashauri ya Bukombe, kuna watumishi kama hao takriban 20 kwenye kada ya walinzi, Sekretari au Mhazili, Afisa Msaidizi ambao wameajiriwa kwa vipindi vifupi toka 2003 mpaka sasa. Swali, kwa nini watumishi hawa wasiwekwe kwenye ajira ya kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafao, kuna wastaafu wengi ambao hawapati pensheni zao kwa

wakati. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Bukombe wapo wastaafu zaidi ya 100 katika kada mbalimbali ambao hawakupata pensheni yao ya Julai mpaka Disemba 2011 ingawa wamepata malipo ya Januari mpaka Machi 2012. Je, kwa nini mpaka sasa wastaafu hawa hawajapata malipo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa matatizo yanayoukabili utumishi yapo yafuatayo:-

- Watumishi kutofanya kazi kwa bidii na kujituma na kwa masaa yaliyopangwa;

- Watumishi kutoripoti mahali walipopangiwa na badala yake wanabadilisha wenyewe au kuomba uhamisho kwa sababu zisizo za msingi; na

- Waajiri kutoingiza taaarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kujiuliza ni kwamba, hatua zipi zimechukuliwa kwa mambo hayo?

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia na kuishauri Serikali katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Katika hili kumekuwa na malalamiko ambayo hayaleti tija katika Halmashauri zetu. Hili linatokana na ukweli kwamba ajira zote lazima zipitiwe na ama kutangazwa na Tume na Sektrearieti ya Ajira na pia suala zima la kutoa vibali kwa baadhi ya kada kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba sekretarieti hii ipo kisheria, basi ni vyema sheria hiyo ikaangaliwa upya na ikiwezekana urudishwe utaratibu uliokuwepo hapo awali ili iweze kutoa fursa sawa kwa Watanzania wote wa mjini na vijijini kwani bado kuna baadhi ya maeneo ambayo mawasiliano bado si mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni muundo wa utumishi wa wachumi, kwa maana ya utaratibu wa kuajiriwa na kupandishwa cheo au vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana 2011/2012, nilichangia na kuulizia namna ya mfumo ulivyo na bado majibu yake hayakuwa ya kuridhisha. Niliongelea hili kwani suala zima hapa ni namna ya kuwapata Maafisa Mipango ambao wengi wao wamekuwa hawapati nafasi hizo na nafasi hizo kujazwa na wachumi. Je Maafisa Mipango ambao kwa mfano wanatoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini wanapatiwa kazi gani kwani wao wamekuwa wamejikita zaidi katika mipango ya maendeleo vijijini ambapo ukiangalia sana wao ndiyo wanatekeleza sera za kumuondolea umaskini mwananchi wa kijijini. Je Serikali inasema nini kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sifa ya kuingilia kwenye nafasi hizo kwa mfano kuajiriwa wenye Shahada ya Kwanza ambao wamejiimarisha *(major)* katika mojawapo ya fani. Uchumi, Takwimu, Sayansi ya Uchumi Kilimo (*Bsc. Agr. Economics & Agribusiness*)

nafasi hii ni Mchumi Daraja la II ama la I na mengineyo. Katika hili malalamko yanakuja pale masharti yanaposema ama yanapoelekeza kwamba mtahiniwa awe ametoka katika Chuo fulani kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ni kwamba, je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo inawabagua baadhi ya watahiniwa ambao labda kati ya masomo waliyosomea si *major* lakini ama *minor* katika fani husika? Je, kwa kuviainisha baadhi ya vyuo tu, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wanafunzi wanaosoma vyuo vingine ambavyo aidha ni vya nje ama vingine vya humu nchini? Serikali inatoa tamko gani kuhusu hili kwani lengo ni kuongeza na kupanua ajira kwa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Mishahara na Maslahi katika utumishi wa umma. Katika hili ni vema Serikali ikaangalia upya mfumo wa upandishaji vyeo hasa kwa walimu na namna ya malipo yaani mishahara iangaliwe upya kwa kuangalia viwango vya elimu na si kusema kwamba kada fulani ya kazi ndiyo muhimu kuliko kada au fani nyingine na pia muda wa mtumishi aliokaa na kutumikia eneo lake la kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni suala la uzoefu *(experience)* labda sio chini ya miaka mitano, hili nalo linazuia kutoa nafasi kwa watumishi wapya yaani wanaotoka katika vyuo hivyo ni vyema Serikali

iangalie upya muundo wa ajira kwa kada na fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Ofisi ya Rais Menejimenti na Utumishi wa Umma. Pamoja na pongezi hizo nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kuhakikisha tatizo la watumishi hewa linaondolewa kabisa. Sekretarieti ya ajira isishughulikie na ajira ya Serikali za Mitaa badala yake, hiyo ifanywe na taasisi ambazo kisheria zina mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kupunguza gharama ya kuendesha Serikali ili kubakiza fedha za kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kumaliza migogoro inayojitokeza inayohusu maslahi ya wafanyakazi kwa njia ya mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais ifuatilie na kuondoa dosari zinazohusu Ofisi ya Rais zilizotajwa kwenye ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa TAKUKURU inafanya kazi nzuri ingefaa bajeti yake iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie utendaji kazi wa watumishi wa umma wasiowajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikaondokana na gharama kubwa za ukodishaji na ukarabati wa majengo kwa taasisi ambazo hazina majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukue hatua za viongozi kutenganisha biashara na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie watumishi wa umma wasiowajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilete taarifa ya Kamati Teule iliyoundwa na Bunge ili suala ya David Jairo na wenzake liweze kumalizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe fedha zinazotokana na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea uwafikie wananchi wanyonge ili waweze kuondoa umaskini wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe maelezo ya watumishi waliohusika katika wizi wa *Deep green, Kagoda, IPTL*, Meremeta na mikataba mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iendelee na utaratibu wa shughuli za kutengeneza na kutoa hati miliki za kimila kwa wamiliki wa mashamba.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni dhana ya kisasa ya kuuelezea uwezo wa Serikali kutumia rasilimali *(resources)* za Taifa kwa kuleta maendeleo kwa kuzingatia maadili, utamaduni

na sheria za nchi. Aidha, utawala bora unahitaji uwazi *(transparency)* ili ukubalike kwa wale wanaotawaliwa ambao ndiyo pia wanaolipia utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taasisi zinazomsaidia Rais kutawala, kwa ufupi wa mchango wangu najikita kwa Taasisi ya Usalama wa Taifa na Taasisi ya TAKUKURU. Naamini taasisi hizi ni muhimu sana katika dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu taasisi hizi zimeonekana kama taasisi za Ofisi ya Rais na zenye usiri mkubwa. Maoni yangu taasisi ni za umma na nguzo muhimu za utawala bora na Taifa. Hivi karibuni tumetunga Sheria ya Taasisi ya Usalama wa Taifa *(TISS)* na TAKUKURU (2007) kwa nia nzuri ya kuimarisha taasisi hizi. Aidha, kupanuka kwa utawala wa Vyama Vingi uwazi, mawasiliano *(media)* na mashinikizo ya Kitaifa *(Global – Publisher)* kwa nia nzuri au mbaya, kunaleta changamoto mpya za taasisi hizi. Muundo wa Taasisi hizi uliokidhi awali, haukidhi changamoto za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupambana na hali halisi ya mazingira ya ndani ya nje ya nchi, kuna umuhimu wa kuangalia upya muundo na uhuru *(International Independence)* ya taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo ya kuangalia ni jinsi Wakurugenzi wa taasisi hizi wanavyopatikana, bajeti zao ziwe wazi na wawajibike ipasavyo kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Umuhimu wa taasisi nasisitiza kwa kuamini utabiri kwamba tuendako hata Rais wa nchi anaweza kulazimishwa kuwajibika

kwa kutumia taarifa za Taasisi hizi na ni vizuri mamlaka na uhuru wa vyombo hivi ukaangaliwa upya na sheria zirekebishwe kuwapa nguvu ya kisheria kufanya kazi zao kwa uhuru zaidi na weledi bila vikwazo isipokuwa vikwazo *(limitations)* vilivyowekwa wazi na sheria, haitoshi kuendeleza dhana ya ushauri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watumishi ambao wanatumikia nafasi mbili kila mmoja; kiongozi wa siasa na mtumishi wa umma. Kumekuwa na hofu nyingi kwa watumishi wa umma wale ambao wanagombea nafasi za Udiwani kwa Vyama vya Upinzani kusumbuliwa na Serikali, vile vile kumekuwa na vijana ambao ni viongozi wa CCM na wanafanya kazi katika Halmashauri. Naomba Waziri katika majumuisho aliweke hili wazi, nafasi zipi watumishi wanapaswa kushiriki na kwa taratibu zipi ili kuondoa mkanganyiko uliopo kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichangie katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Ni lini Serikali itafunga hizi Ofisi za Sekretarieti kwenye mikoa yote nchini kwani wafanyakazi wa Serikali wapo nchi nzima, kuiachia ofisi hii ibake Dar es Salaam na Dodoma ni kuwatesa watumishi kinauli, kifedha na kupoteza muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu ajira za Watumishi wa Serikali. Naishauri Serikali irudishe ajira za

watumishi wasaidizi kama watendaji wahudumu wa ofisi, madereva zirudishwe Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusiana na mishahara hewa, ni aibu kwa Serikali kuwaambia umma wa Tanzania kuwa, kuna mishahara hewa, huu ni uzembe wa Serikali, kwani pamoja na mfumo *(HCMIS)* ambao ni 80% ya watumishi *data* zao zimekwishaingizwa lakini cha kushangaza mishahara hewa imezidi kupanda hadi bilioni tisa. Waziri atuambie wale waliohusika na utaratibu wa mishahara hewa wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala bora, kumekuwa na mwingiliano mkubwa sana kati ya uteuzi wa Mheshimiwa Rais, kuwateua Wabunge kuwa Wakuu wa Wilaya, huku ni kulipunguzia Bunge nguvu kwani tayari humo humo kuna Mawaziri, Manaibu, *RCs, DCs*. Naishauri Serikali nafasi za *RCs, DCs,* wateuliwe watu wengine nje na Bunge ili kuongeza wigo wa ajira.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili waliotoa hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Wamewasilisha kwa umakini mkubwa na uwazi. Napenda kutoa pongezi nyingi kwa vyombo ambavyo viko chini ya Ofisi ya Rais, Idara ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU. Ni kutokana na kazi zao nzuri ndiyo maana nchi yetu imebaki kuwa kisiwa cha amani katika bahari iliyofufuka. Demokrasia na uhuru na uwazi vimejengeka kwa haraka na kwa uimara zaidi kutokana na utendaji mzuri wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU ina kazi ngumu ya kuendesha mapambano dhidi ya rushwa na wameifanya kazi hii vizuri pamoja na ufinyu wa bajeti. Ningependa kuwakumbusha TAKUKURU ahadi yao ya kujenga ofisi pale Nachingwea. Nachingwea ni Wilaya kongwe lakini TAKUKURU haina ofisi ya kueleweka. Naomba tafadhali TAKUKURU wajenge ofisi katika Wilaya ya Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwasilisha hotuba yake yenye maslahi ya watumishi Tanzania. Kwa kuwa viwango vya mshahara vinapishana kutokana na kada au sehemu ya kuajiri ingawa watumishi wenye ajira ya mwanzo kutoka chuo kikuu kimoja wanapata mishahara tofauti, hii inasabisisha baadhi ya kada kukosa watumishi bora kwani wengi wanakimbilia kada zenye maslahi au mshahara mzuri. Hivyo, naishauri Serikali kuhakikisha kuwa, waajiriwa wote *(first appointment)* wapewe mshahara sawa, kusiwepo tabaka la waajiriwa kama wahasibu kulipwa mshahara mkubwa na wengine kama kilimo wanapata mshahara mdogo, tabaka hili liondoshe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu MKURABITA; kwa vile mradi huu ni wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge, naiomba Serikali iharakishe mradi huu ili waliokusudiwa wanufaike hasa wanyonge kwani ndiyo

njia pekee ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania kwa kutumia mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Awali ya yote napenda kuwapongeza Mawaziri wote pamoja na watendaji wao waliofanikisha kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

MKURABITA, Awamu ya kwanza (I), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, kwa kiasi kikubwa mpango huu wa umeshindwa kuleta matumaini kwa Watanzania wanyonge wanaoishi vijijini ambao walitegemea kuwa watapata hatimiliki za kimila za ardhi zao ili nao waweze kukopesheka na kuondokana na hali ngumu za maisha walizonazo. Mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji tangu mwaka 2008 MKURABITA ulipoanza hadi leo hakuna hata kijiji ama mwanakijiji yeyote aliyepata hatimiliki ya kimila. Je, MKURABITA kweli utaweza kumkwamua Mtanzania maskini kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utumishi wa Umma, katika bajeti ya mwaka 2011/2012 Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 72, kifungu cha

tano, alieleza kuwa kuna pesa inatengwa kwa ajili ya kukamilisha utaratibu juu ya kupatikana ekari 200 za ardhi katika Kijiji cha Ikwiriri kwa ajili ya kufungua tawi jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mchakato huu umefikia wapi, ardhi Ikwiriri imepatikana au bado na kama imepatikana; je, Ujenzi wa tawi jipya la Chuo cha Utumishi wa Umma, Ikwiriri utaanza lini?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maoni kuhusu utawala bora na hali halisi ya dhana hii hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi kubwa la Jeshi la Polisi kuua wananchi pasipo sababu za msingi, aidha, kwa *interest* zao wenyewe au kwa kutokujua nini wanatakiwa kufanya, zaidi polisi kazi yake ni kulinda raia na wala sio kuua raia hovyo hovyo. Inasikitisha kuona Watanzania wasio na hatia wanaendelea kuuawa. Kinyume kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba Serikali ichukue hatua ili kukomesha mauaji haya ya wananchi hasa katika Mkoa wa Mara ambapo tumeshuhudia mauaji katika Miji ya Mugumu na Tarime, Rorya, Mwanza na kwingineko Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kugusia kwa masikitiko makubwa sana kasi kubwa ya ubambikaji wa kesi kwa wananchi wa Tarime na Rorya unaofanywa na askari wa kikosi maalum *(task force)* ambao wapo kwenye kanda maalum ya Tarime na Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii gereza la Tarime limejaa mahabusu kuzidi uwezo wa gereza kwa zaidi ya mara tatu. Unakuta watu au raia wamekamatwa kwa makosa madogo madogo kama vile uzururaji lakini wakishafikishwa kituoni hugeuziwa kesi na kuandikiwa *armed robbery* au *murder* na hii hutokana na ukweli kwamba wakishakamatwa huombwa kutoa fedha laki mbili hadi laki tano za Kitanzania, wakikosa hawa wanadamu wanateswa sana hata wengine wanahasiwa na kubambikiwa hizo kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeshuhudia kesi yenye dhamana hazitolewi na kupelekea watu kurundikana magereza, nguvu kazi ambao zinaacha familia zikiteseka, maana wao ndiyo *bridal earners*, hii ni kinyume kabisa na haki za binadamu. Itafika wakati raia watachoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani na kuamini kuwa ombwe hili la maaskari kukamata wananchi na kuomba rushwa ili waachiwe ni dhahiri linatokana na mafao madogo kwa askari hawa huku wakifanya kazi ngumu kuliko malipo wanayopata. Tumeshuhudia malimbikizo ya malipo au posho kwa askari wa kada ya chini pamoja na watumishi wengine wa umma kama walimu. Hii ni hatari sana kwa uhai wa nchi yetu kwani watumishi hawa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia uhalisia na matamshi ya viongozi wa Serikali ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi na yale inayoyatenda ni vitu viwili tofauti.

Inakatazwa watumishi wa umma kujihusisha na vyama vya siasa, lakini utashangaa mfano hai walimu wa shule za msingi kwenye Kata ya Susuni Wilayani Tarime ni wanachama wa CCM na si tu wanachama bali ni viongozi wa Kata wa CCM. Sasa hapa nini ni nini? Majina ya walimu hao ni Philipo Ngogo, Katibu Uchumi CCM, Tawi la Keroti, Mwalimu wa shule ya msingi Kiongera; Mwalimu Senye wa Matamankare Shule ya Msingi ambaye ni Katibu Uchumi, Kata ya Susumi. Wengine ni Mwalimu Magesa wa Nyabinongo Shule ya Msingi na Mwalimu Pius wa Kliongera. Hii ni kinyume kabisa na utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali imekuwa ikikemea dini kutojihusisha na siasa, lakini cha ajabu Serikali hii imeendelea kukumbatia upande mwingine ambao baadhi ya makabila kama Wakurya huwasikiliza na kuamini kwa kile wanachokisema na huu upande ambao kazi zake ni sawa sawa na dini ni wazee wa mila. Serikali ya CCM pamoja na viongozi wa CCM wamekuwa wakiwatumia sana hawa wazee wa mila tena mbaya zaidi wote ni wananchama hai wa CCM. Sasa hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa hili ni mzee wa kimila wa Kata ya Susuni, Wilayani Tarime, Mzee Changua Mtongori ambaye ni mwanachama hai wa CCM na amekuwa akitumiwa katika chaguzi kutoa matamko na kukemea koo zile katika kampeni za CCM, huku akivaa kofia ya uzee wa mila. Ameshaalikwa hadi Ikulu na Mheshimiwa Rais na mara kadhaa kaja Bungeni na aliamrisha vijana kutoa ng'ombe kama tuzo kwa Mwenyekiti wa CCM alipata

shamra shamra za uchaguzi. Hii ni kubariki na lazima isimamishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu watumishi wa Serikali kukosa maadili au utashi wa kuhudumia wateja. Yaani utendaji kazi wa Serikali ni wa kusuasua sana ndiyo maana *production rate* yetu ni ndogo sana. Serikali *service rate* yake ni dakika 30 kwa mteja, wakati kwa huduma hiyo hiyo kwa makampuni binafsi ni dakika tatu kwa mteja, kwa maana uzalishaji kwenye kampuni binafsi 100 zaidi ya ule wa Serikalini. Yaani ni aibu, inabidi utazamwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu wa takriban miaka kumi sasa kumekuwa na tatizo kubwa la watumishi wa umma kuwa na mgogoro wa kutaka kuongezewa mishahara ili waweze kukidhi haja inayotokana na kupanda kwa maisha. Kwa upande wangu nakubaliana na kilio hiki na naomba Serikali kusikiliza kilio hiki cha muda mrefu cha watumishi hawa wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madai haya halali ya watumishi, naomba Serikali iangalie suala hili kwa upande wa pili ambao watumishi wengi kama si wote huchukua mikopo mikubwa kupitia mishahara yao na hatimaye kusababisha watumishi hao kukosa

mishahara ifikapo mwisho wa mwezi. Kitendo cha kukosa mshahara kinasababisha watumishi hawa kuhangaika kutafuta riziki ya kujikimu na kuacha shughuli zao za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili naiomba Serikali iwaambie waajiri wafuta taratibu za mikopo kwa kuwapa watumishi mikopo isiyozidi 30% ya mshahara. Kwa kufanya hivi kutasababisha watumishi waweze kuwa na 70% ya mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiahidi kuwa posho ya mazingira magumu ipo kwenye mchakato na itatolewa hivi karibuni. Tangu Serikali itangaze mchakato huo hadi sasa hakuna lolote linaloendelea. Ni vizuri basi kama mchakato huo hauwezekani, Serikali itangaze waziwazi bila kuficha kuwa imeshindwa kutoa fedha hizo kwa sababu ambazo watazitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la baadhi ya watumishi kutolipwa mishahara yao baada ya kuhakikiwa. Tatizo hili linasababisha watumishi hawa kuishi maisha magumu sana kwa zaidi ya miezi mitano sasa. Naiomba Serikali iweze kuangalia kwa undani ni sababu zipi zinasababisha watumishi hawa wa muda mrefu kukosa mishahara yao. Endapo kuna viongozi wa Wilaya wanaosababisha hali hiyo itokee basi Serikali ichukue hatua kali dhidi yao na kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanapewa mishahara yao na kutokana na adha kubwa wanayoipata watumishi hawa waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine la watumishi wa umma kukaimu kwa muda mrefu. Sheria za utumishi zinaeleza wazi kuwa mtumishi yeyote anayekaimu kwa muda wa miezi sita kama ana sifa; anatakiwa kuthibitishwa kwenye wadhifa huo na kama hana sifa basi anatakiwa aidha kuendelea kuangaliwa tena kwa muda wa kuondolewa kwenye wadhifa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano ya watumishi wa Wilaya za Kilosa, Rufiji na nyinginezo kuna maafisa wengi ambao wamekuwa wanakaimu kwa zaidi ya miaka minne sasa. Viongozi hawa wanakaimu nafasi kubwa kama vile Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya, Kaimu Afisa Elimu wa Wilaya, Kaimu Afisa Mipango wa Wilaya. Nafasi hizi ni nyeti mno na wamekaimu kwa muda mrefu. Naiomba Serikali itoe maamuzi kuhusu watendaji hawa ama wathibitishwe au waondolewe kwenye nyadhifa hizo endapo wameonekana hawafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu kuhusu bajeti ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napoteza kazi inayofanywa na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kwa kazi nzuri wanayofanya katika kurasimisha ardhi vijijini sambamba na kujenga uwezo kwa Halmashauri mbalimbali. Zoezi hili ni zuri, ila nashauri Halmashauri nyingi zifanyiwe utaratibu huu ili kuwawezesha

wananchi hasa walioko vijijini waweze kukopa kwa kutumia hati za kimila za mashamba na nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri inayofanywa na *TASAF* hapa nchini. Halmashauri nyingi na vijiji vinaweza kuibua miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa madarasa, zahahati na kadhalika. Mpango huu umesaidia kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya *TASAF* ya jamii kwa kaya maskini sana katika Halmashauri za majaribio za Wilaya ya Bagamoyo, Chamwimo na Kibaha ni vizuri sasa upanuliwe katika Wilaya nyingine zikiwemo Wilaya ya Makete, Wanging'ombe na hususan vijijini. Program ya *TASAF* pia imefanya vizuri katika programu za UKIMWI, mradi huu uendelee ili kuwawezesha vijana kuweza kujiajiri na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kwa kuunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Bajeti imeandaliwa kwa makini na inakidhi matarajio ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri yenye kueleweka. Pia naomba nitoe pongezi za dhati kwa kuanzishwa kwa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naotoa pongezi kwa TAKUKURU kwa kazi nzuri wanayofanya. Sasa hivi hata vigogo wenye makosa wanashtakiwa, hiyo ni hatua kubwa. Hongera! Viongozi Mafisadi kushughulikiwa ni hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa walimu wote kwa kazi nzuri wanazofanya. Nashauri mishahara ya walimu iboreshwe na mazingira yao ya kazi yaboreshwe. Walimu wana mishahara finyu, mazingira magumu, nyumba duni na wengi wao wako vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Pension* za wastaafu hasa wa Afrika Mashariki, wamezuia njia, wamelala barabarani, wametembea bila nguo yote hayo hayajasaidia, nini kinazuia Serikali isiwalipe? Wastaafu wasaidiwe, walipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapunjo ya mafao, wastaafu walipwe haki zao na ninyi ni wastaafu watarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa anavyoongoza nchi yetu. Niwapongeze Mawaziri wote wa Ofisi ya Rais, hususan Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Stephen Wassira na Mheshimiwa George Mkuchika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Ofisi ya Rais na watendaji wote. Kazi inayofanywa ni nzuri ila kasi

zaidi iongezwe. Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na kauli mbaya ambazo zimekuwa zikiipaka matope Idara ya Usalama wa Taifa kwamba imeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Ni ushauri kwamba mapitio yafanyike ili kutathmini kwa ajili ya kuondoa kasoro zozote zitakazobainika, kwani ni chombo muhimu sana kisichopaswa kupakwa matope hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuliongelea ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa mujibu wa takwimu ni kwamba kuna takriban asilimia saba ya viongozi wa umma ambao hawakurejesha fomu za Tamko la Rasilimali mwaka 2011. Ningependa kufahamu zaidi ya kuandikiwa barua na kutakwa watoe maelezo ni hatua gani itachukuliwa dhidi yao ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uhakiki wa rasilimali na madeni ya viongozi, ni muhimu kwa sekretarieti hii kupewa mamlaka ya kupata taarifa muhimu za kibenki na kuitaka *TRA* na *BRELA* ili iweze kuhakiki vema rasilimali. Lakini pia, ni vema baada ya uhakiki kufanyika, ni muhimu kufahamu hatua ambazo waliokutwa na mali na madeni kinyume na taratibu, wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watumishi wengi tu ambao hawaguswi na Sheria Namba 398 ya Maadili ya Viongozi wa Umma na wamekuwa wakienda kinyume na taratibu, kanuni na matakwa ya sheria kuhusu Maadili umefika wakati sasa watumishi wote walazimike kutekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa umma, ni muhimu watumishi wakapata uthibitisho wa ajira zao kama sheria na kanuni zinavyohitaji. Kwani wengi wamekuwa wakichelewa kuthibitishwa kazini na wengine wamecheleweshwa kupandishwa vyeo wanavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara mbalimbali zimekuwa zikiomba vibali vya kuajiri watumishi, lakini vibali hivyo vimekuwa havitolewi kwa wakati jambo ambalo limekuwa likisababisha usumbufu kwa Wizara, taasisi na idara za Serikali. Hivyo basi, Idara inayohusika na utoaji wa vibali waongeze kasi yao ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa malimbikizo na mapunjo ya mishahara ni suala lingine ambalo linapaswa kushughulikiwa kwa kina ili kupata suluhu ya kudumu. Malipo haya ni haki stahiki ya watumishi hivyo ni muhimu sasa Serikali ijitahidi kukamilisha malipo ya madeni haya ili kuondoa usumbufu wanaoupata watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuanzisha Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, ni muhimu watakaoteuliwa kutumikia katika Bodi hii wakawa ni wale wenye sifa na uzoefu utakaosaidia katika utendaji kazi wa Bodi hii. Aidha, ni muhimu pia kwa wawakilishi wa Vyama vya wafanyakazi wakatoa uwakilishi ili kutumia uzoefu wao na kutoa ushauri kuhusu misingi ya miundo ya mishahara katika utumishi wa umma na kutoa

mapendekezo juu ya mishahara, posho na maslahi kwa ajili ya mihimili mitatu ya Dola na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* naishauri Serikali ifanye hatua za haraka za kuanzisha Mfuko wa TASAF kwa awamu ya tatu ili wananchi wapate maendeleo.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu utawala bora. Utawala bora ni kichocheo cha maendeleo katika jamii. Pamoja na Serikali kutumia fedha za ndani na wafadhiili kwa kutoa elimu ya utawala bora kwa watendaji wa Serikali ngazi zote, inasikitisha baadhi ya watendaji wa Serikali hukiuka dhana zima ya utawala bora na kuzorotesha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa Kijiji cha Ruaha, Kata ya Ruaha,Jimbo la Mikumi. Kijiji kubaki hakina Mwenyekiti wa kijiji miaka miwili na hivi karibuni msimamizi wa uchaguzi alitangaza uchaguzi mara ya tatu sasa, lakini huahirisha bila sababu yoyote na wakati wagombea baadhi walishafanya kampeni kwa ratiba aliyotoa na uteuzi aliofanya. Kitendo hicho kinasababisha hasara kwa wananchi na kupelekea vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni eneo lenye malalamiko mengi toka kwa wananchi kuhusu uporaji ardhi, migogoro ya mipaka, ambao husababisha vurugu, vilema, mapigano na vifo kama ilivyotokea Kilosa, Ulanga na kwingineko katika Wilaya za Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanasababishwa na ukosefu wa ushirikishwaji wa wananchi katika masuala yanayowahusu. Serikali ni vema ikafuatilia na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara hewa, wakati watumishi waliopo kazini wanakosa mishahara na stahiki zao, lakini kuna wimbi kubwa la mishahara hewa. Mfano, wapo walimu wengi kazini lakini hawajalipwa fedha za mizigo, fedha za kujikimu za siku 14 na za familia zao. Hawaambiwi chochote, walimu wamejawa na manung'uniko na kukosa ufanisi katika kazi zao. Leo tunajiuliza elimu inashuka, hiyo ni sababu mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya wafanyakazi, pamoja na Serikali kutoa taarifa ya ulipaji madeni lakini ni vizuri angeainisha ni madeni yapi yaliyolipwa kwani kuna malalamiko mengi ya wafanyakazi ambao hawajalipwa hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utumishi wa umma, upandishaji wa vyeo na kukaimu kwa muda mrefu katika Halmashauri. Nashauri Serikali iweke utaratibu wa wazi kuhusu upandishaji wa vyeo na

vigezo viwe wazi ili kuondoa mazingira ya rushwa. Kuhusu kukaimu katika Halmashauri kwa muda wa miaka saba, Serikali ni vema ikafanya marekebisho ya muda wa uzoefu kutoka miaka saba (7) hadi mitatu (3) najenga hoja kuwa wakati vigezo hivyo vinawekwa idadi ya wasomi wa shahada na kadhalika na kabla ya kupata shahada hufanya mazoezi kwa vitendo, hawakuwepo wa kutosha sana wakati huo ni cheti na diploma. Hivyo, ili kuboresha utendaji, watendaji wanaoajiriwa wapunguziwe miaka ya uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Pensheni kwa wastaafu, pamoja na Serikali kufanya marekebisho ya kima cha chini cha pensheni Julai, 2009 kiwe 83,500/= lakini hadi leo wastaafu hao wanalipwa Sh. 50,000/= kwa mwezi, naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya *LAAC* katika kazi zetu za Kamati ni pamoja na kukagua hesabu na miradi, pia kupitia ukaguzi wa *CAG* na kutuongoza kiukaguzi. Vile vile kusimamia Halmashauri kujibu hoja zote za ukaguzi ambapo nyingi zinahusu fedha za umma. Ingawa kwa msisitizo Kamati hutoa adhabu ya onyo au tozo ya 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuu kutojibu hoja za ukaguzi zinazohusu fedha za umma ni hatari kwa maendeleo ya Taifa, hivyo hoja zote zijibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mashirika ya Umma, Viwanda na maslahi ya wafanyakazi waliostaafu. Ningependa kupata majibu kuhusu

waliokuwa wafanyakazi wa *Polytex* Morogoro wapatao 1,200 lakini mpaka leo hawajalipwa mafao yao ya kustaafu. Waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero wamo waliostaafishwa lakini hawajalipwa. Waliokuwa wastaafu wa *TAZARA* kwa miaka mingi hawajalipwa na hawajui hatma yao. Naishauri Serikali itoe ufafanuzi wa malipo ya watumishi hao na wengine.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kuwa na mpango mzuri wenye nia ya kuboresha sekta ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri katika kuboresha sekta hii muhimu:-

Kwanza, katika kupandisha daraja na vyeo watumishi wa umma, nashauri Serikali iangalie upya mfumo huo kandamizi ambao sasa watumishi wengi wanalalamikia na nilichangia kirefu jana tarehe 2/7/2012 kuwa bado Serikali haijawatenda haki kama ilivyofanya na kuboresha maslahi ya walimu na kutoa waraka maalum. Mtumishi anapokwenda kujiendeleza kimasomo kwa kukopa, au kulipiwa na mwajiri na akikamilisha elimu yake na kupata mfano *degree* akirudi kazini hapandishwi cheo na kuongezewa mshahara, bali anashuka kutoka *Senior Officer* kuwa *Junior Officer* na mshahara kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda masomoni anakuwa katika *scale* ya *TGS E* au *F* lakini anaporudi anakuwa anashuka kutoka *TGTS E* au *F* kuwa *TGTS – D* bila kujali ametumikia Serikali miaka

mingapi na pia akitoa cheti au vyeti vyake alivyojiendeleza atashuka daraja na mshahara na hataweza kufikia daraja alilofikia awali kwa sababu baada ya muda mfupi atakuwa amestaafu. Inaathiri mshahara, pensheni, mafao ya uzeeni na pia kuondoa morali kazini na nia ya kujiendeleza na kusababisha wale wanaomaliza masomo kutaka kuhama kwenda *(Private Sector)* sekta za binafsi au hata nje ya nchi. Naomba Serikali iangalie upya na kulipatia ufumbuzi tatizo hili kama ilivyotatua kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Utumishi iendelee kutoa elimu juu ya *customer charter* ili wateja au wananchi waweze kupata elimu juu ya haki yao na kuboresha huduma kwa jamii hasa katika ofisi za umma. Ofisi nyingi za umma kwa sasa hawafuati utaratibu wa msingi wa kutoa huduma bora na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni Sekretarieti ya Ajira, Taifa. Naishauri sehemu hii nyeti iboreshwe zaidi na bajeti yake iongezwe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, wapatiwe nyezo zote za kufanya kazi na pia wafungue ofisi katika kila Mkoa na kwa sasa hata kila kanda. Iwe ni *data* benki ya watumishi wote chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali kwanza kabisa izibe mwanya wa kutoa vibali vya kuajiri watendaji wa Vijiji, Kata na Afisa Tarafa katika Wilaya zote nchini, ni tatizo sugu wakati watendaji wanakaimu vijiji zaidi ya kimoja na Kata hivyo hivyo, cheni ya uongozi inakatika na wanapata mianya ya kukwepa

kufanya kazi kwa uadilifu na kikamilifu pamoja na Serikali kupeleka miradi hadi ngazi ya Vijiji na Kata bila hawa watendaji kuwepo miradi haitasimamiwa vizuri na mrejesho kuwa mbaya. Pia katika kuajiri hawa Watendaji wa Vijiji, tunashauri mwendelee kuajiri wa kidato cha nne au sita bila kigezo cha kuwa na cheti au diploma ili sehemu nyingi nchini zipate watendaji hao kwani mazingira magumu yanafanya tusipate watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume au Ofisi ya Maadili ya Viongozi wa Umma, tunashauri ofisi hii ipatiwe bajeti ya kutosha ili waweze kuelimisha jamii juu ya maadili ya viongozi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ikitolewa kwa jamii, tutapata viongozi waadilifu na watatumikia umma wanavyopaswa kufanya. Leo wengi wa watumishi wa umma na viongozi wanaofanya kazi kinyume na utaratibu na pia maadili yao binafsi pia hauridhishi. Wanaweza kuwa na tabia mbaya kimaadili lakini kwa sababu Watanzania waliokuwa wengi hawajui maana ya kiongozi na maadili ya kiongozi mfano, mlevi, mzinzi, mwenye lugha chafu na pia tabia zingine mbaya. Ofisi hii ikipatiwa bajeti na ianzishe kitengo cha elimu kwa jamii kwa kufika kila kona ya nchi hii na kutoa mfano jamii itakuwa ndiyo msaidizi wa Serikali kutambua na kuwataja viongozi wenye maadili mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iharakishe kutoa fedha ya wastaafu ambayo ni haki yao ya msingi wameshatumikia nchi kwa muda waliostahili kuchangia na wao pia ni muda muafaka

wapate stahili zao waweze kuitumia kwa manufaa yao. Wakiwa wanalipwa kwa wakati basi hata tamaa ya kuiba na kujichukua maamuzi mabaya wakiwa kazini kabla ya kustaafu haitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia suala la Tume ya Mipango ya Taifa, ifanye kazi kwa kupita katika maeneo mbalimbali nchini na kukutana na wadau mbalimbali ili waweze kupanga mipango kwa kipaumbele cha eneo husika, kila eneo linachangamoto zake na vipaumbele vyake. Kila idara ya Serikali na wadau wake wapate muda wa kukaa na Tume ya Mipango ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala ya utawala bora, naomba Serikali iendelee kutoa elimu bila kuchoka na kuboresha elimu zaidi, tutapata mafanikio makubwa. Kuna mifano mingi ambayo inaonesha kuwa misingi wa utawala bora haifuatwi, kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kutotendewa haki ama kwa kuchelewesha huduma wanazostahili kupatiwa au kutopatiwa kabisa huduma anayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu juu ya uwazi katika maamuzi, mapato na matumzi ya ngazi zote za Serikali hasa Halmashauri, Kata na Vijiji itolewe ili malalamiko mengi yaliyopo yapatiwe ufumbuzi. Wananchi wangejua vema utawala bora wangeweza kufuatilia masuala ya maendeleo na mchango wao wanaotoa kwa ajili ya maendeleo. Pia haki zao za kupata huduma mbalimbali kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mchakato wa kupata Katiba mpya pia kupongeza Kamati ya Katiba kuanza kupokea maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa pongezi nyingi kwa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yako kwa uhahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili nimeombwa na wapiga kura wangu kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wastaafu wameomba kuongezewa pensheni toka shilingi 50,000 mpaka shilingi 100,000 kwa mwezi.

Pili, Watendaji wa Vijiji na Kata wameomba waboreshewe maslahi yao.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati Katiba, Sheria na Utawala, kwa misingi hiyo, naungana na Maoni na Ushauri wa Kamati.

Baada ya kusema hayo, naomba nisisitize yafuatayo:-

- Gharama ya uendeshaji Serikali ipunguzwe kwa kupunguza ukubwa wa Serikali; Wizara zipunguzwe kwa kuunganisha baadhi ya Wizara.

- Uwajibikaji; Watumishi wengi wa Serikali katika utoaji huduma hawana umakini na huchelewesha utoaji huduma, matokeo maendeleo au huduma duni hutolewa.

- Watumishi wa Serikali wanatumikia Chama Tawala badala ya kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria na Taratibu. Hili linasimamiwa na Wakuu wa Wilaya ambao pia ni *Political Managers* wa Chama Tawala (CCM).

- Maofisini hakuna nidhamu; watumishi wanasikiliza miziki ofisini, wanatazama *TV* ofisini na wanavaa nguo zisizo za heshima.

- Serikali ilipe mafao ya wastaafu hasa walimu.

Mhesehimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri kwamba ili kuondoa na kukwepa malumbano yasiyokuwa ya lazima, Serikali ifanye kazi yake kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni na siyo kwa kuwafurahisha Wanasiasa.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake nzuri ya mwisho wa mwezi Juni 2012 hususan msimamo wake kuhusu mgomo wa Madaktari. Msimamo alioutoa Mheshimiwa Rais kwamba, Madaktari waamue moja,

aidha, kutumika kwenye Hospital za Serikali ama waache watafute *green pastures* sehemu zingine. Msimamo huu ni sahihi kabisa na naishauri Serikali kwamba, msimamo kama hii ingepaswa kuchukuliwa haraka ili kudhibiti fujo na uchochezi unaofanywa kwa makusudi ya kuidhoofisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za uhamisho wa Wafanyakazi wa Serikali zitengwe kiasi cha kutosheleza na kukidhi kanuni na taratibu za uhamisho wa watumishi kila wanapofanya kazi kituo kimoja kwa muda wa miaka mitano *(maximum).* Watumishi wengi hususan wa ngazi ya kati na chini, hawahamishwi kwa sababu ya kukosa mafungu ya kuwezesha uhamisho. Aidha, agizo la Serikali kuwa Mtumishi aihamishwe mpaka alipwe kwanza, limeleta kisingizio cha kutowahamisha kabisa watumishi hata wazembe na wabadhirifu.

Wengi wa Watumishi hawana tofauti na Wanakijiji wanaowahudumia kwa sababu wanapokuwa wamekaa muda mrefu, hukosa tija na kusahau wajibu wao na kujiingiza katika mambo yasiyofaa na wengine kujihusisha na masuala ya kisiasa. Nashauri ule utaratibu wa zamani wa kuwahamisha watumishi baada ya miaka mitatu *(minimum)* na miaka mitano *(maximum)* kutoka kituo kimoja kwenda kingine ufuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU hivi sasa inafanya kazi nzuri ila bajeti yake bado ndogo. Kuiongezea asilimia nne tu haitoshi. Zama hizi za Utawala Bora na Haki za Binadamu kinahitajika

Chombo madhubuti cha kupiga vita rushwa ili haki itendeke kwa raia na mgawanyo sawa wa rasilimali za Taifa hili lenye utajiri mkubwa. Itengewe fedha za kutosha ifanye kazi kwa ufanisi na kwa haraka zaidi na maamuzi yake yatoke haraka na yaonekane kwa wananchi. Taasisi hii inahitaji fedha za kutosha. TAKUKURU wawe wanapatiwa fedha zote wanazohitaji kila mwaka bila kupunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Ofisi ya Rais ambayo ndiyo imebeba maeneo muhimu ya nchi yetu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mawaziri na Wataalamu walioko chini ya Ofisi ya Rais, kwa kuweza kuwasilisha Bajeti ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la usalama katika nchi yetu. Kumekuwa na matukio mengi katika nchi yetu yanayohatarisha usalama wa nchi yetu. Hivi majuzi tumeona kwenye vyombo vya habari watu waliokuwa wanasafirishwa kwenye lori wakitokea Somalia na baadhi kupoteza maisha. Hapa ndipo maswali yanapoanzia; hivi kweli Usalama wa nchi yetu unafanya kazi gani au unafanya kazi ya kuangalia usalama wa chama kilichopo madarakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliona kwenye vyombo vya habari, Wabunge wa CHADEMA walivyovamiwa na kupigwa vibaya. Haya yameendelea tena hivi majuzi kwa kiongozi wa Madaktari, Dkt. Ulimboka; Taifa hili tunalipeleka wapi?

Tunaomba Idara ya Usalama wa Taifa ifanye kazi yake ili kuondoa hofu ambayo Watanzania wanayo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa aliijenga nchi hii tukawa na mshimakamo mkubwa bila kujali dini zetu au makabila yetu, lakini nchi inakokwenda sasa ni kubaya na hili linanisikitisha zaidi linasemwa na Viongozi tena wa ngazi ya juu, Wabunge, hii ni hatari kwa Taifa. Juzi tukiwa tunachangia Bajeti ya Waziri Mkuu, alisimama Mbunge mmoja akasema umejengwa mtandao wa Wachaga katika Halmashauri na Wachaga hao wanaiba hawachukuliwi hatua wanahamishiwa katika Halmashauri nyingine. Kibaya zaidi, Mawaziri walikuwa wanapiga makofi kuashiria kwamba suala hilo lina ukweli. Kama ndivyo ni kwa nini watu hao hawachukuliwi hatua zinazostahili kuliko kuhukumu Wachaga wote hata ambao siyo wahusika katika wizi huo? Sitetei wizi na ninapiga vita watu wanaotumia ofisi zao vibaya na si kabila la mtu huyo.

Suala hili nalo naomba Usalama wetu wa Taifa ufuatilie, tujue huo mtandao uliojengwa ulijengwa na nani ili hatua kali ziweze kuchukuliwa kwa haraka. Hatutaki tuanze kugawanyika kwa taarifa ambazo hazina ukweli ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala linaloendelea kwa muda mrefu katika nchi yetu nalo ni migomo kila kukicha, ukitazama kwenye vyombo vya habari utaona taarifa hizo. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwa ni vizuri ikakaa na Watumishi wake wasikie matatizo yao, mwone jinsi ya

kuyatatua, kuliko hivi sasa kinachoendelea ni kutupiana lawama kuwa kuna kikundi cha watu wanaowaambia watumishi wagome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tukifanya hayo, nchi yetu itakuwa na amani ya kweli na maisha bora yataweza kuonekana.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kuwa miongoni mwa Wabuge waliohudhuria katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza na Utawala Bora. Tanzania ni miongoni mwa nchi adimu duniani na hasa katika Afrika ambayo imeweza kudumisha amani na utulivu. Ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi bora ya amani na utulivu ni haki, usawa na Utawala Bora. Kwa hiyo, Serikali inapaswa kusimamia haki za Watanzania pasipo kubaguliwa. Serikali ipambane na rushwa na ufisadi, ambavyo ni hatari kuvunja Misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki lakini ufisadi unavuruga kila kitu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwa TAKUKURU; TAKUKURU wanapaswa kufanya kazi zao kwa umakini na uadilifu, wahusike katika shughuli zao za kila siku kwa watu wote. Wenye madaraka na wasio na

madaraka, maskini na matajiri, wote watendewe haki. Kwa kuwa TAKUKURU ni Chombo kinachopambana na rushwa na ufisadi, basi wao wanatakiwa kuwa safi na wawe mfano kwa jamii. Kitendo cha kusikiliza aina mbalimbali za ufisadi ndani ya Tanzania, mafisadi hawakamatwi na kuwajibika kwenye vyombo vya sheria wala hawajulikani ni akina nani. Siyo jambo jema katika nchi yenye Utawala Bora. Fedha ya ufisadi inapatikana, wahusika hawapatikani hii inatia doa Utawala Bora na ndiyo hujenga dhana mbaya kwa wananchi na kujiuliza maswali mbalimbali ambayo hayapati majibu.

(a) Je, mafisadi hawa ni watu gani?

(b) Je, mafisadi hawa ni watu maskini?

(c) Je, mafisadi hawa ni miongoni mwa Viongozi wa Nchi?

(d) Je, mafisadi hawa ni matajiri au ni akina nani na kwa nini hawakamatwi wakafikishwa kwenye Vyombo vya Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie suala la Watumishi hewa. Suala hili linaisababishia

Serikali hasara kubwa, karibu bilioni tisa za mishahara zimelipwa kwa Watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watumishi hewa ni mbinu mojawapo inayotumiwa na mafisadi kutafuna fedha za Watanzania bila kutoa jasho lolote huku Watanzania walio wanyonge wakiendelea kufa kwa umaskini uliokithiri na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali ichukue hatua madhubuti ya kukomesha tatizo hili la Wafanyakazi hewa. Naiomba Serikali, wahusika wa kashfa hii wachukuliwe hatua mara moja ili iwe fundisho kwa yeyote aliye na nia ya kuchezea fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi wengi hawajui Miiko ya Uongozi, hawajui wajibu wao na ndiyo maana wizi na ubadhirifu wa mali za umma unazidi kuendelea kwa kasi kubwa sana hasa katika utoaji wa zabuni katika Taasisi za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa inakithiri katika Sekta hizi za Umma; kama Serikali haitajipanga vizuri kuzuia na kukomesha rushwa ndani ya Taasisi za Serikali, basi nchi hii itashindwa kusonga mbele.

Mhesimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana la Waajiriwa wa Serikali kutokuripoti katika sehemu zao za kazi walizopangiwa; mfano, Walimu, Madaktari na Mabwana Shamba, hawa wanaathiri sana utendaji wa kazi. Tatizo hili linaathiri sana katika Sekta ya Elimu, kuna upungufu mkubwa wa Walimu katika baadhi ya Shule

za Kata. Vile vile Madaktari na Mbwana Shamba. Naishauri Serikali suala hili walione kuwa ni tatizo kubwa linaloathiri utendaji wa kazi kwa kiasi kikubwa; hivyo basi, litafutiwe ufumbuzi ili lisiendele kuathiri zaidi.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la Watumishi wa Umma Serikalini; Watumishi wa Serikali ambao wapo pembezoni kwa mfano Walimu, wamekuwa wakikopa fedha kufuata mishahara yao mijini na wakifika mijini wanalipia gharama ya malazi, chakula na kadhalika. Huo mshahara wanaoufata pia haukidhi mahitaji yao na wanaishia kulipa madeni.

Je, ni lini Serikali itahakikisha Watumishi wa Umma wanasogezewa mishahara yao karibu ili kuepuka usumbufu wanaopata na gharama wanazozipoteza kufuata mishahara yao mjini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyakazi hao ambao wapo pembezoni, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu; hawana vitendea kazi, makazi yao hayaridhishi kama Watumishi wa Umma; na vile vile wanakuwa wanavunjika moyo, kwa mfano, kama Walimu wamekuwa hawawafundishi watoto wetu madarasani na badala yake wanatumikisha biashara zao madarasani. Lini Serikali itaonesha kwa vitendo kuboresha mishahara ya Watumishi wa Umma ambao wapo pembezoni kwa kuwajengea nyumba bora za kisasa waondokane na kero hizo na wawajibike kwa Watanzania wanaowatumikia kwa nyadhifa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la Watumishi hewa limekuwa kero, naiomba Serikali ihakikishe inakagua Wizara zote na Wafanyakazi wa Serikali ambao wanahusika na suala hili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Wastaafu Serikalini; kuna Wazee ambao wamelitumikia Taifa hili kwa uadilifu bila kuiibia Serikali, wamesahaulika na wengine hawajalipwa mafao yao mpaka leo. Wamekuwa wakiteseka bila ya kupata huduma za kijamii na hata kusahaulika na wanapokufa Serikali inakuwa ndiyo ya mwanzo kutaja nyadhifa zao na sifa kemkem. Cha kushangaza, wakati wa uhai wao hawakuwatendea haki kwa kuwalipa mafao yao kwa wakati mwafaka na kuwaenzi. Je, ni lini Serikali itawalipa Wazee hao wastaafu wanaodai Serikalini na kuwaenzi kama Viongozi Wastaafu waliolitumikia Taifa hili kwa uadilifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ubadhirifu mkubwa katika Halmashauri zetu. Serikali ihakikishe inakagua Halmashauri zote na wanaobainika na ubadhirifu huu wa mishahara ya Watumishi wa Umma, wachukuliwe hatua za Kisheria. Halmashauri nyingi, Viongozi wao wamekuwa siyo waadilifu katika vyanzo vya mapato na wanaobainika wachukuliwe hatua za Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ni muhimu na ipo chini ya Ofisi ya Rais na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na

Rushwa (Namba 11) ya Mwaka 2007. Cha kushangaza, Chombo hiki hakiwashughulikii wala rushwa na wanaohujumu mali za umma. Rushwa zimekuwa zikitolewa nje nje na wanaofanya uovu huo wanajulikana lakini hawachukuliwi hatua. TAKUKURU imekuwa ikinyamaza na badala yake wamekuwa wakiwashughulikia wala rushwa wadogowadogo na kuacha kuwachukulia hatua wala rushwa wakubwa wakubwa Serikalini na Viongozi wa Kisiasa wanaojihusisha na vitendo vya kifisadi.

Je, ni lini TAKUKURU watafanya kazi kwa vitendo bila kumwogopa mtu na wale wote watakaobainika kujihusisha na rushwa wachukuliwe hatua za kisheria na kuondoa dhana ya Watanzania waliokosa imani na kuona TAKUKURU inahusika moja kwa moja na wala rushwa na wanaohujumu uchumi wa Taifa hili?

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuboresha maslahi ya wafanyakazi na pia kudumisha na kuboresha Utawala Bora, ningependa nishauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwiano wa mishahara lipewe msisitizo ili kuwepo na viwango ambavyo havina tofauti kubwa kati ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali na ndani ya Vyombo hivyo kama ilivyo sasa. Hili litapunguza tofauti kubwa za maisha na kuimarisha moyo wa kujitolea na kuondoa vichochezi vya migomo na maandamano, kila kikundi kikifikiria njia ya kuneemeka wao kimapato ya mshahara dhidi ya wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurejesha nidhamu kazini na kukuza uzalendo, Maafisa wote wa Serikali na Taasisi zake ambao hawakupitia Jeshi la Kujenga Taifa, wapangiwe kufanya hivyo. Mipango kama hili ilikwishafanywa hapo zamani na kuwawezesha Viongozi kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma muhimu za maendeleo katika nchi yetu hutolewa vijijini kwa kutumia Walimu, Maafisa Afya, Maafisa Ugani na kadhalika. Kumekuwepo na tatizo kubwa la Maafisa hawa kutokuishi kwenye maeneo hayo kwa sababu mbili kuu:-

(a) Watendaji hao kuamua kutokuishi sehemu hizo hata pale ambapo wanapatiwa nyumba.

(b) Serikali kutowapatia Watendaji hao nyumba; athari za jambo hili limejitokeza kwenye matokeo ya mitihani Wilayani Tanga, ambapo kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kwenye matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne yamekuwa mabaya sana mwaka 2011, kiasi ambacho shule nyingi hazikuwa na ufaulu wa Daraja la Kwanza wala la Pili na hata huo ufaulu wa Daraja la Tatu na la Nne ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iyashughulikie kikamilifu matatizo (a) na (b) niliyoyataja hapo juu, kwa kusimamia nidhamu ili Maafisa waishi vijijini humo na kwa kutekeleza ujenzi wa makazi ya Wafanyakazi hao.

**MHE. ANNA M.J. MALLACK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais inasimamia Baraza la Mawaziri na Tume ya Mipango, ambayo ndiyo Msingi Mama wa Bajeti ikiwemo kupanga Miradi ya Maendeleo, masuala ya TAKUKURU, Utumishi wa Umma na Bajeti ya Mipango ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Usalama wa Taifa na Ikulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na TAKUKURU kushindwa kuchukua hatua za dharura na haraka kukabiliana na wapokea rushwa na watoaji rushwa, tupendekeze kuwa TAKUKURU kiwe Kitengo ndani ya Jeshi la Polisi ili wawe wanakabiliana na janga la rushwa, tofauti na sasa TAKUKURU walivyo wazito kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi hii ya Rais imebeba pia Utawala Bora na sote tunaelewa kuwa Utawala Bora ni ule unaozingatia haki na sheria. Watumishi wengi sasa hivi hawazingatii haki na Sheria kiasi kwamba, wanakiuka na kukosa maadili katika Utumishi wao na kutumia madaraka vibaya. Mfano, kuna Mkurugenzi mmoja ambaye jina tunalo, kwa kutozingatia Sheria na Haki za Watoto, alitumia madaraka yake vibaya kwa kuwatoa watoto wa shule tena kipindi cha masomo darasani na kuamuru wakazoe takataka katika majalala makubwa yanayozolewa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuzingatia afya za watoto wadogo hao, aliwazolesha takataka katika majalala makubwa na yaliyobeba kila aina ya uchafu

bila kuvaa viatu hata *gloves.* Wazazi walilalamika na kulaani vikali swala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, huo ni Utawala Bora kama siyo kutumia utawala vibaya? Kama ametumia madaraka vibaya kwa kuwatoa watoto darasani kuzoa taka bila viatu wala *gloves*, kwa watoto wadogo hao wakati magari ya Halmashauri yapo; Serikali inachukua hatua gani kwa Mkurugenzi huyo?

Naishauri Serikali iwe makini na watu wa aina hii kujali afya za watoto ni muhimu sana na ni bora kuzuia kuliko kutibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ijaribu kulipa madai ya Madaktari na Walimu wanayodai ili kuepusha migomo inayotokea sasa kwani inazadharaulisha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha, siungi mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kero nyingi sana kwa Watumishi wa Umma na urasimu mkubwa wa Idara Kuu ya Utumishi na kupunguza ari ya kufanya kazi kwa watumishi na wakati mwingine kutoziba nafasi zilizo wazi kwa wakati kwa sababu hizo za uzembe na urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kambi ya Upinzani yameitaka Idara Kuu ya Utumishi ishughulikie Watumishi wa Serikali Kuu pekee, kwa sababu ya kutokuwepo na ufanisi na kuleta malalamiko mengi na

Watumishi wa Serikali za Mitaa wajitegemee na kadhalika Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nikatolea mfano; Bodi za Vyombo mbalimbali vya Umma vina mamlaka Kisheria kuajiri, kufukuza na kupitisha viwango vya mishahara na miundo yake. Mamlaka haya yanatenguliwa na Idara Kuu ya Utumishi kuthibitisha lakini inawachukua muda mrefu kuthibitisha bila sababu na kuwaweka watumishi katika hali ngumu wanapandishwa vyeo bila nyongeza za mishahara kama ilivyo kwa Shirika la Magazeti *(TSN),* ambayo ni Magazeti ya Serikali. Pia hata watumishi wa Serikali Kuu kama Walimu wanapandishwa madaraja na kucheleweshewa nyongeza za mishahara na kusababisha madai ya nyongeza hizo na kufanya kero ya Walimu kutomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo ya utatuzi wa kadhia hii ambayo ni kero kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara Kuu ya Utumishi inachelewesha kutoa vibali vya ajira kwa wakati hasa katika maeneo yenye upungufu wa watumishi kama Walimu wakati wapo Walimu waliostaafu na bado wana uwezo wa kufanya kazi kutopata fursa hiyo kwa wakati na upungufu huu kutojazwa na kuendelea na malalamiko ya ukosefu wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kutokuwepo na kumbukumbu sahihi za Watumishi wa Umma na kusababisha malipo ya watumishi hewa,

lakini pia hupata usumbufu wa kulipwa mafao yao kwa kutokuwepo kumbukumbu sahihi kwa wakati; hivyo, nitapenda kujua hatua zilizochukuliwa kukabiliana na tatizo hili na utayari wa Idara Kuu ya Utumishi kugawanywa ili dhana ya kung'atua madaraka iwe na maana, vinginevyo, unatoa haki upande mmoja na kunyang'anya upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kombani, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri wa Utumishi. Hii inaonesha wazi kuwa, wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuongelea Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwani kuna baadhi ya Viongozi wa Umma, wanapojaza Fomu za Maadili hawajazi mali zote walizonazo na kujaza baadhi tu ya mali. Mfano, mali za vijisenti zimechukuliwa hatua gani mpaka sasa kwani kwa kuacha watu hawa bila kuwachukulia hatua yoyote ndiyo hupelekea watu wengine kuchukua hatua ya kupora mali za Serikali kwa kuona wenzao hawajachukuliwa hatua yoyote. Sasa basi kuna kila haja ya kuleta Sheria ya Ufilisi wa Mali za Umma zilizoibiwa ili kuwatia adabu pale mtua anapopora mali ya umma, isiishie kufikishwa mahakamani tu ni lazima kuchukuliwa hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu Utawala Bora utachukua muda mrefu kufanya kazi, kwani ukitaja Utawala Bora ni lazima ujali Utawala wa Sheria, kama Sheria zitapindishwa Utawala Bora haupo na kutakuwa na Bora Utawala. Kama wezi wa kuku wapo jela ni vipi wezi wa pesa za rada ambao hadi leo wapo nje na tunadiriki kusema eti chenji ya rada? Hii ni aibu sana tena sana, tuna kila sababu ya kuwashughulikia kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia juzi tu kumeokotwa maiti na watu walio hai hapa Dodoma ambao walikuwa wanapitishwa kwa njia haramu kuelekea nchi jirani; huu ni unyama ambao Watanzania tumefikia kufanya tunajua hakuna tutakalofanywa. Lazima Serikali iwe imara hata watu wanaofanya vitendo hivyo wataogopa na kutii Sheria kwa hiyari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya Watumishi ambao siyo waaminifu, tunaambiwa mishahara hewa; inatoka wapi? Makeshia au Wakurugenzi hawajui kama hawa watu hawapo? Lazima tuchukue hatua stahiki kwa mishahara hewa na sasa ikome kabisa. Uwajibikaji uwe wazi ili kuleta ufanisi. Kwa kuwa baadhi ya Wakurugenzi hutoa upendeleo kwa wafanyakazi ambao wanajiendeleza kwa kuomba ruhusa kwenda kusoma, baadhi yao huchukulia ujamaa, ukabila au sababu nyingine kuwabagua Watumishi kupata elimu. Baadhi ya Wafanyakazi hulipiwa ada na mambo mengine yote, baadhi hulipiwa ada tu na wengine hunyimwa vyote

hata kama kuna Sheria ya kufanya kazi miaka isiyopungua miwili na wale wanaosomeshwa wengine wanakuwa hawajakidhi vigezo vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kidogo MKURABITA, dhana halisi Wananchi walio wengi hawaifahamu ni bora tukawawezesha Wananchi kufahamu dhana nzima. Pia Wananchi wengi wanashindwa kurasimishiwa ardhi na nyumba kutokana na gharama kubwa za upimaji shirikishi; ni bora Serikali itenge pesa za kutosha kwenye eneo hili ili Serikali yenyewe ichukue jukumu hilo na pia itoe elimu ya kutosha ili Wananchi wa Tanzania waweze kutoka katika umaskini wa kutupwa ambao unawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itakuwa makini na wale wote wanaofanya kazi kwa kutoa huduma kwa Wananchi chini ya Mwamvuli wa Serikali wakitimiza wajibu wao, tutatoka tulipo. La muhimu ni kujitolea na kufanya kazi kwa Sheria, Kanuni na Taratibu, hali zitabadilika, ni lazima sote tujitume kwa bidii na maarifa, tukifanya hivyo tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa pamoja na Watendaji wao wote, kwa Hotuba zao nzuri zenye kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURUBITA) ndiyo mkombozi wa wanyonge vijijini;

kwani mwananchi mnyonge anakuwa na ardhi yake kwa njia ya kurithi na kumiliki kimila, lakini mnyonge huyo hana faida ya umiliki wa ardhi hiyo. Ili kumkomboa mnyonge kwa kupitia MKURABITA huwa inakuwa vigumu kutokana na migongano ya Sheria yenye upungufu mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba ofisi iharakishe kwa kuleta Bungeni Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 14 ili ziweze kufanyiwa marekebisho kwa manufaa ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na utendaji kazi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, lakini bado haujakomaa. Ilibidi kupanua wigo wa kazi zake siyo kuangalia Viongozi tu. Kwa nini kuna kada Serikalini zina vitambi noma kwa kuchota fedha za Serikali; mfano kada ya uhasibu, manunuzi na wanaoshughulikia Mikataba ya Serikali?

Angalia vijana ambao uajiri wao mfupi lakini tayari wanamiliki nyumba, magari na kadhalika, ukiangalia mishahara yao midogo wala hawawezi kukopa benki wakaweza kumiliki vitu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Maadili wajipange na wafanye tathmini ya kazi zao na kufuatilia baadhi ya kada nyeti Serikalini kwa kukagua mali walizonazo wamepata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba TAKUKURU iendelee kufanya kazi zake kitaalam zaidi, kwani uwezo

wa kazi bado ni mdogo na unahitaji watendaji kazi wake kupata mafunzo ya utendaji kazi zao ndani na nje ya nchi. Vile vile isibakie na Ofisi hapa Dar es Salaam lakini pia ifungue Ofisi Mikoani, kwenye Ofisi za Halmashauri ili kupanua wigo wa kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kukusanya Fomu za Maadili ya Viongozi pia iwe inafanya tathmini ya wale wote waliowakagua kuliko kukaa kimya na kusitiriana. TAKUKURU huzinduka pale jamii imeona na kupiga kelele, suala kama hilo linakuwa na ushahidi duni. Hata hivyo, TAKUKURU iongeze bidii ya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu kwenye Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu), ambayo imetayarishwa na kuwasilishwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi tariban asilimia 75 wanaishi vijijini na shughuli yao kubwa ni kilimo. Hivyo, hutegemea sana ardhi. Mpango huu wa MKURABITA unabainisha kwamba, unaweza kuwa mkombozi kwa Wananchi hawa wa vijijini ambao rasilimali kubwa wanayomiliki ni ardhi kama dhamana katika mikopo katika Vyombo vya Fedha lakini wengi bado wanakabiliana na changamoto ya upatikanaji wa Hati Miliki ya Kimila katika ardhi zao wanazomiliki. Zoezi hili la kuwapatia Hati Miliki bado linasuasua katika Halmashauri nyingi

kutokana na ufinyu wa Bajeti katika Mpango huu wa MKURABITA. Naishauri Serikali iongeze fungu la Mpango huu katika Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nijiunge na baadhi ya wachangiaji juu kutoridhishwa na utendaji wa *TASAF II*, ambapo baadhi ya changamoto zilizosababisha utendaji duni kwa *TASAF II* ni suala la kuhamishia shughuli na *Management* ya *TASAF* katika Halmashauri huku aidha hakuna Watumishi ambao wanawajibika moja kwa moja na *TASAF.* Kwa mfano, Mhasibu na Mweka Hazina wa Halmashauri ndiyo pia anasimamia na kutekeleza shughuli za *TASAF.* Hii kwa kiasi kikubwa imeathiri utendaji na usimamizi wa *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mfuko huu wa *TASAF* unategemea kuanza Awamu ya III, yaani *TASAF III,* ninaishauri Serikali awamu hii ijitegemee katika utendaji kama Taasisi kuliko ilivyo Awamu ya II. Hivyo basi, *TASAF III* katika Halmashauri zifanye kazi kama Taasisi inayojitegemea. Aidha, kabla ya utekelezaji wa awamu hii, Wananchi waandaliwe jinsi gani wao watashiriki katika *TASAF III.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) ni Msingi na Mhimili Mkuu wa Maendeleo ya Taifa lolote linaloendelea au lililoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya jambo ambalo linapaswa kushughulikiwa kwa nguvu zote ni suala la rushwa au kama ambavyo wengi wetu sasa hivi tunaliita ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa inahujumu maendeleo *(sabotage of national development)*, ni adui wa haki na ni kikwazo kikubwa katika kuleta usawa kijamii nchini. Jambo hili linahitaji nguvu ya pamoja ya makundi mbalimbali kupambana nalo. Tanzania tuna rasilimali nyingi sana; madini, misitu, wanyama (mbuga za wanyama), mifugo, ardhi na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iweze kuendelea ni lazima izingatie Kanuni za Utawala Bora, ambazo maandishi mbalimbali yanaeleza kwa kina kuwa zipo nane.

- Ushirikishwaji *(Participation)* - Wananchi wote na wadau wote washirikishwe katika mambo yote yahusuyo maendeleo.

- Utawala wa Sheria *(Rule of Law)* - Inadhihirishwa na uwepo wa Mahakama Huru na usawa mbele ya Sheria na utekelezaji wa Sheria kwa kuepuka hisia na kuzingatia haki za binadamu, kuepuka rushwa na kadhalika.

- Uwazi *(Transparency)* - Serikali kuwa wazi kwa Wananchi na watu wote kwa kutoa taarifa kwa wakati na iwe sahihi.

- Uwajibikaji *(Accountability)* - Maafisa wa Serikali kujenga desturi ya kuwajibika kwa matendo yao ili kuleta ufanisi maeneo ya kazi.

- Usawa *(Equity and Inclussiveness*) - Kuweka mizania iliyo sawa kwa watu wote; watoto, vijana, wanawake na kadhalika katika mambo muhimu ya kimaendeleo.

- Huduma kwa wakati *(Responsiveness)* - Taasisi za Serikali na Binafsi ziwahudumie wadau kwa wakati sahihi.

- Tija na ufanisi *(Efficiency and Effectiveness)* - Taasisi zijaribu kufikia malengo yaliyokusudiwa bila kuharibu mazingira.

- Kujenga makubaliano *(Concensus)* - Kujaribu kuweka mijadala ya wazi na nia nzuri ili kuleta maelewano ya pamoja bila kujadili utofauti wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Serikali ikiyazingatia haya, nchi yetu itapiga hatua kubwa sana kimaendeleo na wakati huo huo imani itakuwepo kwa wote.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), imezungumzia mambo mengi mazuri na ya maana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa hayo naomba nichangie machache.

Kwanza, napenda kuzungumzia kwa kifupi Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 52, kifungu cha (41)(i), kinaelezea kutoa huduma ya mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wakati mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo na madhumuni ya kutoa mikopo ni mazuri sana katika kuwasaidia watu wenye kipato cha chini na kuwatoa katika dimbwi la umaskini uliokithiri. Pesa hizi sasa zimekuwa na changamoto kubwa kwa sababu ya urasimu mkubwa uliopo wa kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile mantiki hasa ya pesa hizi sasa haionekani, watu wamekata tamaa kiasi kwamba hata mikopo hii haizungumziwi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali irudishe vuguvugu na harakati juu ya suala zima la mantiki ya pesa hizi na wanyonge wajenge matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lengine ni suala zima la tishio la migomo. Migomo ni jambo ambalo linaweza kurudisha nyuma kasi ya maendeleo ya Taifa lolote Duniani. Mgomo wa Madaktari na mgomo wa Walimu katika nchi yoyote ni hatari sana. Katika nchi yetu hivi sasa tumo kwenye mgomo wa Madaktari na mgomo wa Walimu unafukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali pamoja na juhudi zote inazochukuwa, iongeze juhudi ya mazungumzo kati ya Viongozi wa Madaktari na Walimu ili kunusuru hali nzima juu ya maisha ya watu na hatua ya watoto wetu katika suala zima la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kutekwa kwa Dkt. Ulimboka, limezua hisia tofauti nchini na vitendo hivyo huwa vinatokea hata kwa Viongozi wa Kisiasa kupigwa na kujeruhiwa na watu wasiojulikana. Hii ni changamoto kubwa kwa Serikali; hivyo, naishauri izidi kuwa makini juu ya mambo haya na mfano wa haya kwani yanaweza kutujengea chuki na uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufungua Ofisi Zanzibar, naipongeza Serikali kwani itarahisisha kupatikana kwa huduma na pia kupatikana kwa ajira kwa baadhi ya watu. Vilevile itaondoa hata changamoto na suala zima la malalamiko juu ya Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kutekeleza shughuli za Wananchi. Napenda kuchukua fursa hii, kuongelea suala la wastaafu katika nchi yetu. Kumekuwepo na hali ya kuwasahau sana wastaafu hawa ambao wamelifanyia kazi na wamelitumikia Taifa hili na sasa wanahangaika na maisha magumu sana huko waliko baada ya nguvu zao, elimu yao na

ujuzi wao kuutumia katika kuijenga nchi hii. Inasikitisha sana, leo hii wastaafu hawa wamegeuka kuwa wategemezi na kwa namna nyingine ombaomba. Jambo la kushangaza ni kuona wamesahaulika kabisa!

Jambo la kujiuliza je, hawa wastaafu hawakuwa watumishi halali?

Je, mafaili yao yalikuwa yanaandikwa kwa kalamu ya risasi na sasa yamefutika au nyaraka zao zimechomwa moto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasikitisha sana na inaleta wasiwasi mkubwa hata kwa watumishi walio kazini sasa, maana baada ya kustaafu hawajui hatima ya maisha yao ya uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazee ambao wameishia kulipwa nauli na mpaka sasa hawajawahi kulipwa mafao yao hata kidogo. Wamehangaika kufuatilia bila mafanikio, hata kile kidogo walichoweza kukitunza wamekitumia kuhangaikia na kufuatilia mafao yao bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai yangu kwa Serikali kutafakari kwa kina jinsi gani ya kuwasaidia wazee hawa ili waweze kuongeza muda wa maisha badala ya kuwasababishia mahangaiko na maisha magumu na hatimaye kuwapunguzia maisha kwani hawa ndiyo wanaotunza wajukuu na watoto waliotelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la mirathi; suala hili wahanga wakubwa ni akina mama lakini kubwa sana ni pale ambapo mhusika alikuwa Mtumishi wa Serikali na bado viambatanisho halali vimeandaliwa lakini cha ajabu bado suala la usimamizi wa mirathi linabaki kuwa kitendawili kikubwa na kigumu kuteguliwa. Hawa akina mama ndiyo walezi na wasimamizi wa familia, bado pamoja na kusongwa na familia makandokando ya wanandugu kuhusu urithi, mapato na mali ya familia, bado Serikali inazidi kumwongezea huyu mama msongo mwingine wa mawazo akate tamaa na mwisho kuaga dunia pasipo walau kupata hata senti moja ya nguvu ya aliyekuwa mwenza wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai yangu kuwa sasa Serikali inapaswa kuangalia makundi haya mawili kwa namna ya pekee. Hii itasaidia kuwapa maisha bora hawa wajane na wastaafu. Hali hii isipofanyiwa kazi vizuri, tutajikuta tunaongeza wimbi kubwa la wategemezi, wimbi kubwa la watoto wa mitaani na hivyo kupelekea Taifa kuingia katika janga jingine ambalo ni utegemezi usio na suluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itunze takwimu sahihi ya watumishi wake, pindi wanapostafu waweze kuishi maisha bora na pia suala la mirathi liwekewe utaratibu maalumu na wa haraka ili haki iweze kutolewa mapema, kwani familia husika zinapokea msiba wa kuondokewa na jamaa yao na pia msiba mwingine wa kukosa kufaidika na nguvu ya ndugu yao, mwenza wake au mwanafamilia ambayo ameitumia katika Taifa hili.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi na ustawi wa jamii hauwezi kuimarika ikiwa mikataba na tafiti zinazofanyika hazitekelezwi kwa wakati. Mfano, hatuwezi kuendeleza taaluma na kuongeza ujuzi kuiwezesha Tanzania kuwa na nguvu za kiushindani na suala zima la mikataba hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali baada ya kuchukuwa hatua ya kubinafsisha viwanda na kukosekana kwa nishati ya umeme, kumechangia uuwaji wa viwanda Tanzania na kuikosesha nchi mapato kwa kiasi kikubwa, jambo ambalo limeuwa hata ajira kwa Vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina hekta 29,400,000 lakini cha kusikitisha inalima hekta laki nne; hivyo, uwezo wa kilimo na kufikia kilimo cha kibiashara utapatikana wapi. Hatuwezi kusonga mbele kufikia katika maendeleo kama hatujaweza kuangalia upungufu uliotokea nyuma na kuupatia ufumbuzi unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kujenga na kuimarisha uwezo wa watumishi ni pamoja na kuwapatia mishahara ambayo itawawezesha kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu, jambo ambalo litajenga mazingira mazuri ya utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais (Sekretarieti ya Ajira) imesema katika Utumishi wa Umma itafungua Ofisi Zanzibar kwa ajili ya ajira za Muungano. Tunataka

kujua Ofisi hiyo itafunguliwa lini kama siyo ndoto za kufikirika?

Miaka 49 ya Muungano, Zanzibar inafikiriwa kufunguliwa Ofisi ya Ajira ya Muungano leo kutoka 1964 mpaka leo 2012 kama suala hili siyo dharau kwa Wazanzibari ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali zinazohusiana na Muungano ni vyema zikazingatia heshima ya pande zote mbili za Muungano na lazima zielekezwe pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, fedha za rada haziwahusu Wazanzibari, imeleta sitofahamu kule Zanzibar na hata sisi baada ya kupata undani wa jambo hili kwamba kulichukuliwa asilimia fulani kutoka kwa Wizara ambayo siyo ya Muungano na karibu asilimia zaidi ya 85 ilitokana na Wizara ya Ulinzi, imetufanya tupoteze imani kwamba Muungano unatuendea kinyume Wazanzibari kwa kutotuhusisha na fedha za rada ambazo zinatuhusu. Wazanzibari ni washirika na hatupaswi kutolewa kwenye ushirika huu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana MKURABITA siyo mpya nchini mwetu, yapo mafanikio kadhaa yaliyopatikana lakini bado tuna changamoto nyingi; kwa mfano, urasimishaji ardhi kufanyika katika maeneo

kadhaa nchini na hati kadhaa kutolewa. Hata hivyo, upo urasimu mkubwa katika mchakato mzima wa hati hizo, wakati mwingine waombaji wa hati hizo huombwa rushwa na Maafisa wanaohusika.

Pili, lipo tatizo pia la Taasisi za Fedha kama vile Benki kukataa kupokea Hati za Kimila kama dhamana ya mikopo. Hili ni tatizo, naomba Serikali ilifuatilie suala hili.

Tatu, kasi ya utekelezaji wa MKURABITA iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Miradi mingi chini ya *TASAF I* na *II* haukuwa mzuri sana, usimamizi wa Miradi mingi uliachwa chini ya usimamizi wa wanavijiji ambao wana utaalamu kidogo sana. Matokeo yake, Miradi mingi kama vile majengo ya zahanati na shule yalijengwa chini ya kiwango. Wakati mwingine baadhi ya majengo yalilazimika kufumuliwa kama Zahanati ya Isenzanya, Kata ya Nambinzo, Mbozi. Sekondari ya Kapele, Kata ya Kapele Mbozi, bweni lilifumuliwa na kadhalika. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Awamu ya Tatu ya *TASAF* ilenge kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa *TASAF I* na *II.* Aidha, urasimu upunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kazi nzuri. Hata hivyo, nashauri ijengewe uwezo zaidi ili iweze kukabiliana na Viongozi wasio waaminifu. Wapo

Viongozi ambao nina imani huficha baadhi ya mali zao au huziandikisha kwa majina ya ndugu zao. Aidha, mali nyingi hupatikana kwa njia zisizo sahihi. Nashauri pia wale wanaopatikana na makosa nchini ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, wachukuliwe hatua kali kwa mujibu wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri kuwa na Chombo Maalum kwa ajili ya kuajiria Watumishi mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Hata hivyo, inaonekana Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma sasa badala kutatua matatizo ya ajira hasa katika Halmashauri za Wilaya, Miji Manispaa na Majiji, kimeleta urasimu mkubwa sana. Ucheleweshaji ajira na kufanya nafasi nyingi Vijijini, Katani na Wilayani, kuwa wazi muda mrefu sana na hivyo kuathiri utendaji kazi katika maeneo hayo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ajira kama za Madereva, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na Wahudumu katika maeneo mbalimbali waajiriwe na Halmashauri husika. Kwa kufanya hivyo, tutaajiri Watumishi ambao watakuwa tayari kufanya kazi katika maeneo wanayotaka. Urasimu wa ajira hizo pia utapungua na hivyo kuongeza ufanisi wa kazi katika maeneo hayo. Serikali iache kuhodhi kazi ambazo kimsingi ni za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ni Chombo muhimu sana katika nchi yetu. Tume ya Mipango huandaa Mpango wa Maendeleo katika vipindi mbalimbali kama miaka mitano au kumi au kumi na tano na kadhalika. Hata hivyo, Mipango mingi

inayopangwa na Tume, kwa sehemu kubwa haieleweki kwa Watanzania wengi, ndiyo sababu hata utekelezaji wake huwa mgumu sana. Hivi unapogawa vipeperushi vilivyochapishwa kwa Lugha ya Kiingereza ni kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi ya Tume ya Mipango ni kuishauri Serikali kuhusu vipaumbele vya Kitaifa. Vipo vipaumbele lukuki; hivyo, kusababisha fedha kidogo za maendeleo kwa Taifa letu kutawanywa katika maeneo mengi sana. Kwa mtazamo wangu, matokeo yake au *impact* kwa maendeleo ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Tume iishauri Serikali ije na vipaumbele vichache kama vile miundombinu, maji, nishati, kilimo na afya. Kwa kufanya hivyo ni rahisi kuona matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa mchango kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), kwa Mwaka 2012/2013.

Katika aya ya tisa, Tume imeeleza kwamba, imeandaa Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/2012 - 2025/2026); pamoja na Mpango huo kuridhiwa na Bunge na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, naomba Mpango huo uletwe Bungeni

kuthibitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) na (3) ili kuwezesha Bunge kusimamia Serikali kuhakikisha utekelezaji. Katika aya ya ishirini na moja, Tume imeeleza kwamba, iliandaa mfumo wa kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013, mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais itoe maelezo ni kwa nini mfumo huo haukuandaliwa mwezi Februari 2012 na Mpango wa mwaka kuandaliwa mwezi Februari kama Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge zilivyohitaji? Matokeo ya udhaifu huu ni Mfumo, Mpango na hata Bajeti ya 2012/2013 kutozingatia Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kwa vipaumbele vilivyopaswa kutekelezwa kwa mwaka 2012/2013. Mfano, kwa mwaka 2011/2012 na 2012/2013, jumla ya shilingi bilioni zaidi ya mia moja zilipaswa kutengwa kwa kilomita 96 za barabara za kupunguza foleni Dar es salaam (rejea ukurasa wa 147 wa Mpango). Hata hivyo, mpango wa mwaka na bajeti imetenga bilioni kumi tu kwa mwaka 2012/2013. Aidha, ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa ajili ya kupunguza kero ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa upande wa maeneo yanayohudumiwa na Ruvu Juu ulipaswa kutengewa jumla ya shilingi bilioni takribani 72 kwa mwaka 2011/2012 na 2012/2013.

Hata hivyo, kiwango kilichotengwa kwa ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ni kwa ajili ya kulipa fidia na hakikamilishi ujenzi. Hivyo, Rais kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa Tume ya Mipango na Mwenyekti wa Baraza la Mawaziri, ashughulikie udhaifu uliojitokeza na

kuwezesha ongezeko la fedha kwenye bajeti kwa mujibu wa mpango ili kutimiza pia ahadi ambayo Rais alizitoa kuhusu barabara na maji Dar es salaam na kutangaza kwamba utekelezwaji ungekamilika mwaka 2013.

Kwa upande mwingine, Tume ya Mipango iishauri Ofisi ya Rais na Baraza la Mawaziri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ambao utajadiliwa mwishoni mwa Mkutano huu wa Bunge ili kupunguza kodi kwenye bidhaa zinazochangia katika mfumko wa bei na ongezeko la gharama za maisha kwa Wananchi na wakati huo huo kupanua wigo wa vyanzo mbadala vya mapato. Tume ya Mipango ifanye hivyo kwa kuchambua michango ya Kamati, Kambi ya Upinzani na Wabunge, tuliyoitoa katika Mkutano huu wa Nane wa Bunge wakati wa kuchangia Bajeti. Tume ya Mipango ichukulie kwa uzito michango tunayoitoa Wabunge, kwa kuwa mchango ninaouwasilisha sasa niliuwasilisha kwa Ofisi ya Rais mwezi Julai mwaka 2011 na Aprili, 2012. Hata hivyo, michango hiyo haikuzingatiwa kwenye Mfumo na Mpango wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara za 33 mpaka 45 za Katiba ya Nchi zimetoa madaraka na mamlaka makubwa ya Rais, yenye athari kubwa kwa maisha ya Wananchi. Madaraka na mamlaka hayo yanajitokeza pia katika sura ya tatu na sura ya tano kwa kiwango hata cha kuathiri Mihimili mingine ya Bunge na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka na madaraka hayo yanapaswa kudhibitiwa wakati wa Mchakato wa Katiba Mpya. Wakati mchakato huo ukiendelea, Ofisi ya Rais iongeze nguvu katika kusimamia Serikali kutekeleza maoni na mapendekezo ambayo tuliyatoa kwenye Mkutano wa Nne na Bunge, tarehe 4 Julai na 5 Julai 2011 kuhusu masuala ambayo yalipaswa kuwa yametekelezwa kwenye Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Baadhi ya masuala hayo ni pamoja na hatua iliyofikiwa katika uchunguzi wa tuhuma za ufisadi wa Meremeta, Tangold, Deep Green, Kagoda na Richmond, ambayo ni masuala ya Kitaifa.

Kwa upande wa Jimbo la Ubungo, hatua za Idara ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU kuhusu malipo kwa Kampuni ya Twiga Chemicals kuhusu biasharaa haramu na hujuma katika miundombinu ya maji na kuhusu urejeshwaji wa viwanja vya wazi vilivyovamiwa hasa katika Kata ya Sinza. Vyombo husika vimshauri Rais kuwezesha hatua kuchukuliwa.

Katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2012/2013 ya Ofisi ya Rais, pamoja na hayo ninayorejea kusisitiza yatekelezwe kutokana na Bajeti ya 2011/2012 ni kama yafuatayo:-

Mosi, Ofisi ya Rais (Ikulu) na Baraza la Mawaziri, lirejee kupitia upya Muswada wa Sheria ya Fedha wa 2012 ili kuufanyia marekebisho makubwa yenye kulenga kupunguza kodi kwa bidhaa zinazoongeza mfumko wa bei na kupanua wigo wa mapato kwenye vyanzo mbadala. Hatua hii itaongeza mapato kuelekezwa kwenye Miradi ya Maendeleo na

kupunguza ugumu wa maisha kwa Wananchi. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza kodi kwa wafanyakazi na kupanua wigo wa mapato katika rasilimali ikiwemo madini na gesi kama tulivyoshauri tarehe 15 Julai, 2011.

Pili, Ofisi ya Rais (Ikulu) na Baraza la Mawaziri liingilie kati migogoro iliyomo kwenye Vyuo Vikuu hususan Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM).* Kuna upotoshaji mkubwa kuhusu suala la kusimamishwa kwa wanavyuo; ni vizuri Ofisi ya Rais kutokana na ahadi ya 2007 na Ripoti ya Tume iliyoundwa na Rais juu ya Elimu ya Juu na Taarifa iletwe Bungeni. Aidha, Ofisi ya Rais (Ikulu) na Baraza la Mawaziri kwa pamoja wasimamie utekelezaji wa ahadi za Rais alizozitoa katika Jimbo la Ubungo mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Mwanzoni mwa 2010, Rais alitembelea Kimara Bonyokwa na kuahidi visima vya dharura kuchimbwa na pia Barabara ya Kimara – Mavuminza – Bonyokwa inayounganisha Manispaa ya Kinondoni na Ilala na kuchangia katika kupunguza foleni kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo ina hali mbaya sana kwa sasa na pia haijapandishwa hadhi, pamoja na mimi kama Mbunge kutumia njia zote za Kiofisi kufuatilia kupitia Manispaa ya Kinondoni, Bodi ya Barabara Mkoa wa Dar es Salaam na Wizara ya Ujenzi. Suluhisho kwa barabara za pembezoni ni kuwezesha nyongeza ya bajeti kutoka bilioni kumi mpaka bilioni mia moja kwa barabara zilizotajwa kwenye Ilani ya CCM na Mpango wa Miaka Mitano kwenye ukurasa wa 14, zenye jumla ya kilomita mia moja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu ya kisheria iliyonayo TAKUKURU lakini suala la rushwa bado linaonekana kuongezeka na hasa katika maeneo ya kutolea huduma kwa watu, na yameanza kujengeka mazoea kuwa bila kutoa chochote, basi huduma hautapata na/au utapata huduma chini ya kiwango. Jukumu lingine la kisheria ya Taasisi hii ni kuishauri Serikali namna bora ya kuziba mianya ya rushwa, na hatujaona mipango halisi ya taasisi hii ya namna bora ya kuishauri Serikali. Bado dhamira ya Serikali haipo katika kupambana na suala ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali inapaswa kubuni mikakati mipya yenye lengo la kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la rushwa. TAKUKURU iweke wazi mipango au mikakati yake ya kuishauri Serikali kuhusu suala la rushwa ili tupate kujua tatizo lipo wapi, ni kwa Serikali au TAKUKURU?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo halisi la MKURABITA bado halijafikiwa na hasa katika Wilaya nyingi nchini. Suala la Ardhi vijijini, bado wananchi wengi hawajaweza kumiliki ardhi na/au kwa vibali vya kisheria au kwa hati za vijiji. Suala la ujenzi wa masijala za ardhi vijijini kwenye Halmashauri, bado inasuasua na hakuna mkakati wa dhati wa kufanikisha na kusimamia zoezi hili. Ni vyema suala la ujenzi wa masjala ya ardhi liwekwe katika mpango mkakati wa Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba suala/mkakati wa MKURABITA lifike mpaka vijijini palipo

na wananchi wengi ambao ni wanyonge wanaohitaji kumiliki rasilimali walizonazo au wenye (wananchi) fursa kubwa ya rasilimali walizonazo ambazo wanahitaji kumiliki. Masijala za Ardhi ziwekwe katika Mipango ya Halmashauri ili iweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF)* bado haujafikiwa, na riba inayotolewa inalingana na Taasisi nyingine za kifedha. Dhamira ya kumsaidia mnyonge ipo wapi ilhali hakuna unafuu wa riba ya mikopo? Nashauri kwamba riba inayotolewa na Mfuko huu ipunguzwe ili dhamira ya kuwasaidia wananchi wa hali ya chini wainuke kiuchumi, ionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekretarieti ya Ajira, vyema sekretarieti hii iwe inaajiri nafasi za juu, lakini kwa kada za chini ni bora ajira hizi ziachiwe mamlaka zenyewe, mfano Halmashauri za Wilaya na Taasisi nyzingine za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuongelea kuhusu Menejimenti ya Utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira vinachelewa sana kutolewa, hivyo kunapelekea Halmashauri nyingi kuwa na upungufu wa watumishi hasa katika kada ya watendaji wa vijiji na Kata. Nashauri kwamba tatizo hili la ucheleweshaji wa vibali utazamwe upya na/au kubadilisha mfumo wa utoaji wa vibali husika. Panapotokea migogoro ya utumishi, mamlaka au mtu husika anapokata rufaa kwa

mamlaka za juu yake, uamuzi huwa unachelewa sana. Ni vyema maamuzi/rufaa zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo panakuwepo na sheria za utumishi zinapofanyiwa marekebisho, wataalamu wenye taaluma ya utumishi washirikishwe kutoa maoni yao kabla ya sheria husika kurekebishwa. Hii itasaidia kutoa uhalisia wa changamoto wanazokutana nazo wataalamu husika ili kuboresha kada ya utumishi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora ni vyema liwe linafanyiwa tathmini katika Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kupima utendaji wa Serikali kama unaendana na misingi ya utawala bora, ili kuleta ufanisi uliokusudiwa wa utawala unaofuata misingi bora ya utawala.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Ndani ya hotuba hii katika ukurasa wa 55 Serikali imejipanga kutumia Sh. 3,781,100,000,000/= kugharamia malipo ya mshahara, upandishwaji vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara. Suala la madai ya malimbikizo kwa watumishi bado ni tatizo kubwa hasa katika Halmashauri. Katika Wilaya ya Geita wako watumishi katika Sekta ya Elimu na Afya wanayo malalamiko makubwa sana kuhusiana na kutolipwa malimbikizo haya. Kwa vile katika bajeti hii fedha zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo, naomba sasa mara baada ya kupitisha bajeti hii, watumishi wenye kudai malimbikizo yao walipwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wapya wanaoajiriwa kwenye Halmashauri, inachukua muda kuwekwa kwenye *payroll* kiasi kwamba watumishi hawa wanaishi mazingira magumu. Mfano, Walimu wapya waliopangwa mwaka 2011/2012 walipata shida sana kiasi kwamba iliathiri hata utendaji kazi katika baadhi ya Shule za Sekondari za Geita, wengine walipiga simu kuhitaji msaada. Naomba Serikali iweke utaratibu ulio bora wa kuwalipa fedha za kujikimu *(advance)* ili watumishi hawa waendelee na majukumu yao bila manung'uniko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya hotuba kipengele cha 47 ukurasa wa 56 inazungumzia sera ya malipo ya mshahara na motisha kwa watumishi wa umma. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali inaandaa mwongozo wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Napenda kuupongeza utaratibu huu. Swali langu ni: Je, mwongozo huu utakamilika lini? Ni lini watumshi walio katika mazingira magumu wataanza kunufaika na utaratibu huu? Napenda kupata ufafanuzi huu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupendekeza pia motisha hii iangalie vizuri kada mbalimbali za watumishi. Kwa mfano, Waratibu wa Elimu Kata, Wakuu wa Shule za Sekondari wapewe *responsibility allowance* kwa maana wanayo majukumu makubwa ya kutembelea na kuangalia utendaji kazi wa watu wengine. Wapewe usafiri hata kama kwa kuwawekea

utaratibu mzuri wa kukopeshwa pikipiki ili watekeleze majukumu yao katika ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa Umma, utaratibu wa usaili uliopo kwa sasa wa kufanyika Dar es Salaam unawanyima fursa Watanzania wengi walioko pembezoni. Katika bajeti ya mwaka huu 2012/2013 sijaona kama kuna uwezekano wa kuanzisha Ofisi ya Sekretarieti za ajira Mikoani kwa mwaka huu wa fedha. Je, Ofisi za Sekretarieti za Ajira Mikoani zitaanza lini? Vile vile zipo ajira ndogo ndogo mfano Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata ambazo kwa ushauri tu, usaili ungefanyika kwenye Halmashauri husika kuliko hivi sasa kwamba lazima Sekretarieti ya Ajira ihusike. Hii itasababisha urasimu usiokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumekuwa na kero mbalimbali hususan kwenye Taasisi ya Utumishi wa Umma (Afya). Kumekuwa na malalamiko ya kukosekana kwa Bodi ya *Ocean Road Hospital/Cancer Institute,* suala ambalo linasababisha *Management* kua-*abuse* sheria kwa kuwa tu hawana Bodi inayo wa-*control*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wakurugenzi wanamiliki hospitali binafsi ambazo zinaratibu magonjwa sawa na wanayotibu *Ocean Road cancer institute*. Je, hapo hawaoni kuwa kuna *conflict of interest* ambayo inapelekea upotevu wa vifaa, muda na rasilimali watu wa taasisi hiyo kwa kufanya kwenye Taasisi zao? Serikali inatupa jibu gani juu ya uanzishwaji wa Bodi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya *uniform allowance* kwa wafanyakazi kwa takribani miaka mitatu iliyopita, badala ya kupewa Sh. 120,000/= walipwa Sh. 80,000/= tu. Haya ndiyo yanachangia migomo hii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa Kigoma, watumishi wamekuwa na malalamiko yao, mojawapo ni kukosekana kwa usiri kwa watumishi wanaoishi na VVU hasa inapofika kipindi cha kulipwa fedha za kuwasaidia lishe na matibabu, kwa kuwa wanapewa kupitia Ofisi ya Mhasibu wa Mkoa badala ya hundi kama Waraka wa Serikali unavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la kukosekana kwa posho za *overtime allowance.* Kwa kuwa muda wa kuingia kazini umehama kutoka 2.00 usiku hadi 12.30 jioni, hadi saa 3.30 asubuhi, nashauri kuwepo na malipo ya ziada kutokana na muda wa ziada wa kufanya kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la wafanyakazi kutokulipwa madai ya *on call allowance*, likizo na matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora, kumekuwa na tatizo la baadhi ya watumishi wa Serikali ku-*abuse* sheria na kusababisha matatizo kwa wananchi, hususan Wizara ya Ardhi, kutoa hati mbili mbili, kuuza maeneo ya watu, na hata pia maeneo ya mipakani. Pia kumekuwa na wimbi la wahamiaji haramu, lakini wanatoa rushwa, wanaingia hususan Mkoa wa Kigoma, na inapoanza kamata kamata wanakamata raia wema wa Tanzania. Tume ya Utumishi iunde Tume ya Kuchunguza Maafisa Uhamiaji mipakani ili kupunguza migororo nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa la kuwa na mainjinia, wathamini, *surveyor.* Ni wachache sana, hivyo hawakidhi matakwa ya majukumu yaliyopo. Tatizo kubwa kuliko yote ni ukosefu wa Afisa Ardhi wa Manispaa, hivyo tumeazimwa na watu wa Mkoani, lakini hana mamlaka ya kutoa hati. Serikali inatuambiaje juu ya mwaka huu wa fedha? Wananchi wanashindwa kufanya *transfer* ya nyumba na viwanja vyao.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita sana katika kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha mishahara na maslahi ya Walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakuu wanaishi katika mazingira magumu sana kiasi kwamba kazi ya kufuatilia utolewaji Elimu Bora inakuwa ngumu kwa kuwa kila ukimbana Mwalimu atimize wajibu wake,

anakujibu kuwa mishahara ni midogo na mazingira ya maisha ni magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa Serikali itamke kauli na kutangaza kuwa ajira ya utumishi wa Ualimu iitwe kwa umaalum wake *special civil servant,* yaani ajira/utumishi wa ualimu uwe *special* na huduma zake zisilinganishwe na kada nyingine ukiachilia udaktari ambao utumishi wake nao ni *special* na mishahara, mafao, maslahi yake ni tofauti na kada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza *Teacher's Professional to be categorized* katika uwiano wake. Mfano mzuri ni huu, Walimu wenye shahada moja au shahada mbili za elimu wanatofautiana mishahara kwa daraja sawa, elimu sawa, uzoefu sawa, kasoro ni mazingira ya kazi, yaani huyu ni mkufunzi chuoni, na yule ni Mwalimu wa Sekondari. Je, hatuoni utofauti huu unaleta ubaguzi kwa Walimu wa Sekondari wakati huku kwenye sekondari pia *A-level* yaani Kidato cha Sita nao wanafundisha vijana wanaofanana kielimu hasa wakufunzi wanaofundisha walimu *Grade III A*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi japo nikipata nafasi pia nitasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitapenda kuongea mengi ambayo najua yataongelewa na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kuhusu kitengo cha nidhamu kwa Walimu *TSD*. Kwa kweli kitengo hiki kimekuwa kikikosa fedha kabisa au kupata fedha pungufu na isiyofika kwa wakati na kuwakwamisha majukumu halali ya ufuatiliaji wa nidhamu na uwepo wa Walimu mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko mengi na ya msingi kuhusu ushukaji thamani wa kiwango cha elimu kutokana na kitengo hiki kutowajibika vizuri kutokana na ufinyu wa bajeti na fedha kidogo inayopelekwa kwenye kitengo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kabisa katika bajeti hii basi, kwa nchi nzima, kitengo hiki kitakuwa na fedha na kuongezea watumishi kwani hali siyo nzuri na kama kweli tuna nia ya dhati ya kuinua kiwango hiki cha elimu kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea kero ambayo imepelekea kushusha hadhi ya uaminifu kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara hewa, napenda sana kupata ufafanuzi wa tatizo la kuwalipa mishahara watumishi waliokufa au kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili imekuwa chungu sana masikioni mwa wananchi wasiopenda

kuona fedha za umma zinaingia mifukoni mwa watu wasio waaminifu na kupotea wakati kuna mahitaji mengi makubwa na ya msingi ambayo hayatatuliwi kwa kukosekana fedha, huku fedha nyingi zikipotea mikononi mwa wanaojipangia na kuchukua mishahara hewa, huku inajulikana vizuri kwa taarifa ya watumishi wanaostaafu na kufariki, huwa taarifa zao zipo. Inakuwaje hadi leo bado kunakuwa na wimbi la mishahara hewa?

Mheshimiiwa Mwenyekiti, ningependa sana katika majumuisho ya hotuba ya Waziri na majibu yake, basi tupate ufafanuzi katika jambo hili. Pia napenda kupata taarifa ya mikakati na hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhusu mishahara hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna malalamiko mengi ya watumishi wastaafu; napenda kuona kuna maandalizi mazuri sana ya watumishi ambao wanastaafu na wamestaafu, basi maisha yao ya ustaafu hayawi majuto kwa wao kuwa watumishi wa umma hapo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi na rahisi, ni Mheshimiwa Augustino L. Mrema. Yeye alilitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa sana na ikapelekea yeye kupewa cheo cha Naibu Waziri Mkuu, na akafanya vizuri kazi yake, amekuwa akilialia hapa Bungeni kuwa hajalipwa stahili zake japo kikatiba hakuwemo katika wale wenye stahili, lakini mchango wake umekuwa ukitambulika na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alifanya kazi yake vizuri, yupo ndani ya Bunge lako, ni vipi waliopo nje?

Mheshimimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuona katika majibu ya Waziri, basi azingatie hayo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa kazi nzuri ambazo zimefanywa na Wizara hii hasa katika uboreshaji wa shughuli za utumishi wa umma, napenda tu waangalie na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mishahara. Watanzania wanaajiriwa, wanapata mishahara midogo ambayo haikidhi gharama za maisha. Inafaa posho zote zijumuishwe na ziwe mishahara, na *base* ya mshahara ibadilishwe. Hatua hii itaondoa sana dhana ya posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira nyingi kama Katibu Tarafa, Watendaji Kata/Vijiji zipo tupu. Watu wanakaimishwa tu. Utaratibu ufanywe zijazwe ili kusimamia fedha vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za Watendaji Kata/Vijiji, madereva, zifanyike katika ngazi za Halmashauri, Benki zinafanya hivyo. Mkurugenzi ameaminiwa kutunza fedha nyingi, sioni kwa nini asiaminiwe kuajiri katika ngazi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara yake kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yao. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo la Mfuko wa *TASAF* kuhusu utendaji wake wa kazi ndani ya Jimbo langu la Urambo Magharibi. Mwaka 2006/2007, Kijiji cha Kazana Upate, kilichopo Kata ya Igagala, Tarafa ya Kaliua, Wilaya ya Urambo, kiliibua mradi wa ujenzi wa Shule ya Msingi ambayo gharama ilikuwa ni Shilingi milioni 34. Wananchi hawa walifanya hivyo kwa kuzingatia taratibu na maelekezo yote ya *TASAF*. Kwa kuzingatia taratibu hizo hizo, wananchi wa kijiji hiki cha Kazana Upate walipaswa kuchangia Shilingi milioni tano na Mfuko wa *TASAF* kuchangia Shilingi milioni 29 tu. Kwa kuzingatia kuwa wananchi hawa walikuwa na hamu sana na mradi huu, walijituma zaidi na kukusanya matofali, mchanga na mawe vyenye thamani ya Shilingi milioni sita. Huo ulikuwa ni mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kwamba, mpaka leo hii Mfuko wa *TASAF* haujatoa hata senti moja, huu ni mwaka wa tano. Matokeo yake, tofali zimeanza kuharibika, mawe yameanza kupotea na mchanga kusambaa. Kwa kweli hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imewavunja sana moyo wananchi wa kijiji cha Kazana Upate, inakuwa vigumu sasa hivi kwa sisi viongozi kuwahamasisha wananchi hawa wa Kijiji hiki kushiriki tena katika kazi za

kujitolea ili kujenga na kuendeleza Kijiji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aone aibu, hii kero aiondoe kwa kuhakikisha haki inatendeka, kijiji kipate mgao wake kutoka *TASAF*, na hasa ukizingatia kuwa *TASAF II* inafikia ukingoni. Ikilazimika, basi mzigo huu ubebwe na *TASAF III*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri aliainisha kazi zilizotekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni pamoja na kutoa huduma kwa Rais na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma nyingine iliyotolewa kwa Mheshimiwa Rais ni ushauri katika maeneo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, jamii, sheria na uhusiano wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo kufanyika, kuna jambo moja kubwa ambalo Serikali imelisahau nalo ni ulinzi wa heshima ya Rais. Kuna mitandao ya jamii ambayo imekuwa ikimdhalilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuchukuliwa hatua zozote za kinidhamu. Ni kweli Serikali inadai kuwa na *freedom of speech* katika vyombo vya habari, lakini pamoja na uhuru huo ni wajibu wa ofisi husika kumlinda Rais kwa kuhakikisha kuwa mitandao ya jamii haitumiki kumtukana Rais kila kukicha. Jambo hili limemdhalilisha Rais na Watanzania kwa ujumla,

ukizingatia kuwa Rais wa nchi yoyote ile ana haki ya kupwa heshima yake anayostahili kama Mkuu wa Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Idara husika ikilisahau hili, nadhani wakati sasa umefika kumpa Rais ulinzi stahiki ikiwemo kulinda heshima yake na hatimaye kulinda heshima ya nchi yetu kama ilivyokuwa wakati wa Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu MKURABITA, zoezi hili ni zuri, lakini linatekelezwa taratibu sana, kiasi kwamba wananchi hawaoni *impact* yake, na wananchi wengine hawaelewi MKURABIRA ni nini. Zoezi hilo liende sambamba na utoaji elimu kwani zoezi ni zuri na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali inabidi izi-*convince banks* zilizopo zipokee/zikubali hati za kimila kama dhamana ya kupatia mikopo na iletwe sheria iainishe wazi kuwa hati za kimila zitatumika katika kukopeshea kama dhamana ili wanyonge nao wakopesheke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TAKUKURU, wanafanya kazi nzuri, wananchi wanatambua wakitoa au kupokea rushwa wako hatarini. Lakini bado baadhi ya watumishi sio wadilifu, wanashirikiana na watoa rushwa, hivyo kupoteza imani kwa wananchi. Hali hii hujitokeza zaidi kwenye kipindi cha uchaguzi. Alikutwa Afisa wa TAKUKURU, kabla hajakwenda kwenye tukio,

anawasiliana na *suspect* ili aondoke, akifika hakuna kinachoendelea, ushahidi unakuwa umepotea. Maadili ya kazi yao yazingatiwe, pia wawe non *partisan* kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri TAKUKURU wafanye *special duty*, dhidi ya askari wa barabarani ambao rushwa *is order of the day*. Kama tunavyofahamu, *report* inaonyesha Jeshi la Polisi Tanzania ni namba moja kwa rushwa. Kwa hiyo, ni muhimu TAKUKURU wajikite katika kuzuia na kupambana na rushwa iliyokithiri katika Jeshi hilo la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wazo la Kambi ya upinzani Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU uteuzi wake ufanywe na Kamati ya Taifa ya Uteuzi na athibitishwe na Bunge. Lakini kama bado, ipo haja ya kuteuliwa na Rais, lakini athibitishwe na Bunge. Kwa upande wa *report* za TAKUKURU ziletwe na zijadiliwe na Bunge kama ilivyo kwa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Serikali imesema takriban watumishi 92 elfu wanapandishwa cheo. Kumekuwa na tatizo la watu kupanda madaraja katika ajira zao lakini kiwango cha malipo ya mishahara na stahili mbalimbali haziendi sambamba, matokeo yake watumishi hao hulazimika kuidai Serikali matokeo yake Serikali kuwa na madeni mengi, lakini vile vile migogoro huzuka. Hivyo, wakipanda vyeo na malipo yao yawe yameandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara iendane na hali halisi ya mfumuko wa bei uliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi hewa, hili bado ni tatizo zaidi. Shilingi bilioni moja imelipwa kwa watumishi waliokufa na walioacha kazi na kustaafu. Serikali iwe na *data base* ya utambuzi wa watumishi halali walio katika ajira. Vile vile inaonekana upo mtandao kuanzia ngazi ya chini hadi juu ya ulaji wa fedha za umma kupitia watumishi hawa. Nashauri wahusika wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma, wengi hawafanyi kazi masaa manane kama *job description* zao zinavyowataka. Mwaka mzima wanafanya mambo binafsi na kuongea na simu/kupiga soga ofisini. Uwajibikaji ni mdogo, lakini pia sababu ndogo yaweza kuwa ni kukosa motisha na mshahara isiyokidhi. Hivyo wanakwenda nje ya ofisi kujitafutia kitu cha ziada cha kukidhi mahitaji ya mwezi, kwani mishahara huisha kabla ya mwisho wa mwezi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mawaziri wa Nchi – Menejimenti ya Utumnishi wa Umma, Utawala Bora na Uhusiano na Uratibu kwa kukabiliana na changamoto zote za maeneo yao ya uongozi. Aidha, napenda pia kuwapongeza Watendaji wao wote kwa kuwasaidia Mawaziri wao vizuri kumudu kuongoza na kuendesha Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri ufuatao:-

Mosi, nashauri kwamba Menejimenti ya Utumishi iboreshe na kuimarisha *Human Resource Management* kwenye sekta zote za umma, iachane na matumizi ya Watendaji wa Sekta ya Utawala – *DADPS* kwenye sehemu ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu vishiriki kwa kuwatumia zaidi *Acadamicians* jambo linaloleta matatizo ya haki za kiutumishi kwa watumishi. Ihakikishe *Human Resource Officer/Managers* wanapewa nafasi stahili ya kutumia taaluma zao badala ya kukandamizwa na wakubwa wao vyuoni humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matatizo ya kiutumishi vyuoni chanzo chake ni kuwadharau wataalam wa fani hii. Hali ya kiutumishi kwa watumishi wa *DUCE*, MUCE na kadhalika. Haipo sawasawa kutokana na mtindo wa *CEOs*/Wakurugenzi wa Utawala kuwa sio wabobeaji kwenye *Human Resources Management*. Kauli itolewe yenye msisitizo ya kuwajali na kuwatumia vizuri wenye kada hii popote walipo.

Pili, muda wa kutoa vibali vya ajira uangaliwe. Kuna kuchelewa sana kupatikana kwa vibali kiasi hata wale wenye kada muhimu hukaa kitambo kidogo wakingojea ajira pasi sababu za msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nasisitiza watumishi wa kada za chini ajira zao ziwe *Decentralised* badala ya kufanywa Makao Makuu. Watumishi kama madereva, wahudumu na kadhalika wanaweza kushughulikiwa na Halmashauri.

Nne, kumekuwa na tatizo la watumishi kulalamika kwa kuibiwa mishahara yao benki kufuatilia mishahara hiyo kupitia benki. Sababu ni nyingi, hasa ugeni wa matumizi ya *TEHAMA*. Nashauri Menejimenti ya Utumishi kwa kushirikisha na Wizara ya Sheria kuandaa na kuleta Sheria ya *Cyber Crimes* Bungeni ili isaidie kupunguza wizi huo wa mishahara kwa njia ya *TEHAMA*.

Tano, kwa kuwa Serikali imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali watu kwa lengo la kuweka usahihi wa rekodi za rasilimali watu, ni vyema uandaliwe utaratibu wa kupita kila Wilaya na Idara ili wafanyakazi warekebishe taarifa na kumbukumbu zao ili tusipate matatizo ya watumishi wanaotarajia kustaafu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu mkubwa wa wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Serikali ina mpango gani wa kuwapa posho? Maana wanafanya kazi kuliko hata Watendaji wa Vijiji na mara kwa mara Watendaji huwa hawapo kwenye vituo vyao vya kazi, wanavizia mwisho wa mwezi tu kuchukua mishahara yao. Huwa hawakai vituoni hata kwa miezi mitatu mpaka mitano, hasa Watendaji wa Vijiji vya Mwambao mwa Ziwa Tanganyika, nimewahi kutoa taarifa kwa Mkurugenzi bila mafanikio yoyote yale. Kwa hiyo, ni bora kuwe na Mwenyekiti kuliko kuwa na Watendaji wanaokula pesa bila kazi. Hata Watendaji wa Kata huwa hawakai kwenye Kata, na wengi wao wamejiingiza kwenye biashara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kuwa Wenyeviti wapewe posho angalau Sh. 50,000/= kwa mwezi. Wana kazi kubwa sana. Naomba nipewe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Serikali hulipwa mishahara yao kila mwezi kama haki yao ya Utumishi, lakini haiangalii jinsi gani huo mshahara unamfikia mtumishi wake. Baadhi ya watumishi wanatumia robo ya mishahara yao ili kufuata hiyo mishahara yao. Kwa mfano, watumishi wanaoishi kando ya Ziwa Tanganyika wanatumia vipando vya *boat,* kisha gari na kulala kwenye *guest* kwa siku kadhaa kwenda na kurudi, akisalia na robo tatu tu ya mshahara yao: Je, Serikali haioni kama inawaingiza watumishi kwenye madeni na wanakuwa hawana mori wa kazi?

Pia kuhusu miradi ya *TASAF* katika Wilaya ya Nkasi *TASAF* ilikuwa na miradi mingi ya kutosha, lakini miradi hiyo hailingani na pesa zilizotolewa na huo mradi. Miradi mingi ilihujumiwa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifuatilie miradi yote ya *TASAF* ya Wilaya ya Nkasi tangu ilipanza, itaona hakuna kilichofanyika ila ubadhirifu mtupu na kuneemesha Waratibu wa *TASAF*.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais DKT. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuingoza nchi yetu kwa utulivu na amani. Nawapongeza Mawaziri wote

wanaomsaidia Rais katika Ofisi yake kwa kuwasilisha vizuri bajeti katika ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya UKURABITA ni nzuri na ilitegemewa kujibu changamoto nyingi zinazotukabili hasa ardhi inavyoweza kumkomboa mwananchi kupitia Urasimishaji wa Ardhi na Mali za wananchi. Suala la kurasimisha ardhi, bado halijashughulikiwa kikamilifu, kwani maeneo mengi bado urasimishaji haujafanyika, hasa Wilaya ya Singida na Ikungi ikiwa ni pamoja na Jimbo la Singida Magharibi. Kasi ya suala hili ni ndogo sana na sababu zinazotolewa na Serikali ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Halmashauri ya Wilaya ya Singida haina fedha za kuwezesha kutengeneza kazi ya urasimishaji;

(b) Uhaba wa wataalam na vitenda kazi; na

(c) Kutoanzishwa kwa Masjala ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotekelezwa kwa suala la urasimishaji linawanyima wananchi fursa ya kujipatia mikopo inayoweza kusaidia kujipatia maendeleo. Ningependa kujua dhana hii imetekelezwa vipi katika Halmashari ya Singida na kwanini kasi ya utekelezaji ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tatizo la fedha litatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, ukweli ni kwamba wananchi wengi

hawaufahamu hasa vijijini. Nashauri kwamba Serikali iutangeze mfuko huu ili ujulikane ikiwa ni pamoja na kutoa vipeperushi na vipelekwe Wilayani na vile vile Semina kwa Madiwani zitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madai ya watumishi hasa Walimu, sasa linakera. Hivi kulikoni? Kero hii haipatiwi ufumbuzi. Kwanini maelekezo ya Serikali kutolimbikiza madeni hayatekelezwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwahamisha watumishi wanaofanya ubadhirifu katika eneo moja na kuwahamishia eneo lingine ukomeshwe. Bali wahusika waadhibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban zaidi ya vijana laki sita hawana ajira na bado kuna vijana wengi wanategemea kumaliza Vyuo hivyo. Ni dhahiri namba hii itapanda. Cha kusikitisha, vigezo vinavyotumika ili kijana apate kazi, anatakiwa awe na uwezo *(experience)* wa kazi usiopungua miaka mitatu. Tujiulize bila kupata ajira, huu uzoefu wanautoa wapi? Hii inapelekea vijana wengi kujiingiza kwenye biashara haramu za madawa ya kulevya, hata kuwa majambazi na watoto wa kike kujiingiza kwenye biashara za uchangudoa ambayo ni hatari kwa afya zao, ukizingatia kasi ya ugonjwa wa VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali ihakikishe wanatoa waraka wa kuajiri Mashirika, Ofisi za Umma; kwa kuanzia, kigezo cha uzoefu kiondolewe katika ajira, waangalie akifanya *interview* aajiriwe, atapata tu uzoefu akishaanza kazi. Kwa nini wastaafu wanaongezewa mkataba wa kufanya kazi wakati kuna vijana tele wanaosubiri kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara hewa, hili ni tatizo kubwa. Ni lini Serikali itamaliza tatizo hili? Ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliosababisha uzembe huu?

Mheshimniwa Mwenyekiti, kuna kundi la vijana wapo tayari kujiajiri, wale waliomaliza Vyuo vya Ufundi, lakini mtaji ndiyo tatizo na wengi hawana dhamana ya kupeleka benki, na wachache walionazo bado riba katika mabenki yetu ni kubwa mno kuanzia asilimia 81 mpaka 22. Je, kwa riba hii kubwa, kweli Serikali ina nia ya kuhakikisha vijana wanaweza kujiendeleza?

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mie kuchangia katika Ofisi ya Rais kuhusiana na bajeti ya mwaka 2012/2013 kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuanza na wafanyakazi wanaokaimu nafasi mbalimbali kwa muda unaozidi mwaka mmoja kama sheria ya kazi inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tabia au tatizo limeshakuwa sugu kwa kiwango cha kusikitisha sasa. Hii

inasababisha mtumishi husika kutojipanga katika mfumo mzima wa maisha yake inakosababishwa na hofu au woga wa kutoondolewa madarakani siku na wakati wowote atakapoteuliwa mtu mwingine kushika nafasi hiyo au kushindwa wakati wa *interview* ya nafasi hiyo na kusababisha yeye kurudia nafasi yake ya zamani kama itakuwa haijajazwa au kama ataweza kupita tena. Mfano mzuri ni kwa Mkuu wa Chuo wa sasa wa Chuo cha Uhasibu Arusha ambaye alikaimu nafasi hiyo tokea tarehe 1/11/2008 kutoka aliyesimamishwa na uongozi wa juu wa Chuo hicho, yaani Wizara ya Fedha anajulikana kwa jina la *URIO* (aliyesimamishwa), na aliyekaimu ambaye sasa ni Mkuu wa Chuo Prof. Johannes Monyo, alikaimu nafasi hiyo kwa miaka isiyopungua mitatu baada ya kupata barua mwaka huu kwamba amekuwa Mkuu wa Chuo toka tarehe 1/11/2011. Hii inatokana na kufanya *interview* na kubahatika kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni la baadhi ya watumishi kutumia lugha au njia zozote za udanganyifu kuhakikisha wanapata uhamisho katika maeneo ya kazi waliyopangiwa na hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Wahasibu wawili waliopangiwa eneo la Longido Mkoani Arusha kutoweka eneo la kazi bila taarifa. Tukio hili lilitokea miezi ya Septemba na Oktoba mwaka 2011 na mmoja alitoweka na taarifa zake, hadi leo hajajulikana yupo wapi. Huyu anaitwa Gabriel Mkonyi. Wa pili anaitwa Mchungazi Kabonaki ambaye alizumguza na watumishi wa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Arusha

(Mama Itanisa) ambaye alikataa kumpa uhamisho, lakini baadaye alifanikiwa kumzunguka mama huyu kwa baadhi ya maofisa wake hapo Mkoani na kufanikiwa kupata barua ya uhamisho ya kuhamia Mkoani Tanga eti kwa kazi maalum na barua hiyo ilisaniwa na Nkya. Je, Ofisa huyu hafahamiki hata ashindwe kuchukuliwa hatua za kinidhamu hadi leo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, Wilaya zetu za pembezoni hazitapata maendeleo kama hali hii itaendelea na hatua zozote za kisheria kutokuchukuliwa. Naomba sana tuzisaidie Wilaya hizi ili ziweze kuendelea pia. Kama inashindikana, wazawa ndiyo wapangiwe maeneo hayo ili kukwepa hii adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Celina Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Capt. (Mst) George Huruma Mkuchika - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mheshimiwa Stephen Massato Wasira - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, (Mahusiano na Uratibu) kwa moyo wao wa kupenda utendaji wa pamoja *(team work)* na maandalizi mazuri ya bajeti ya Wizara. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Capt. George Mkuchika kwa utendaji mahiri ambao umetambuliwa na Mheshimiwa Rais na hivyo kuwateua kuongoza Wizara nyeti zilizo chini ya Ofisi yake. Hongereni sana kwa uchapaji wenu wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Makatibu Wakuu wote wa Ofisi ya Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi - Mheshimiwa Balozi Ombeni Sefue na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia utekelezaji wa sera na sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nathibitisha kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu vibali vya ajira: Miaka iliyopita Serikali ilikuwa na utaratibu mzuri sana wa kuidhinisha ajira ambapo vibali hutolewa kupitia ikama na bajeti ya mishahara, ikiwa na maana kuwa mara baada ya ikama kuidhinishwa na Utumishi na fedha kuidhinishwa Hazina na kupata baraka za Bunge kupita bajeti ya Serikali na Wizara inayohusika, hakukuwa na sababu tena ya kurudi Utumishi kuomba kibali kingine.

Urasimu ulianzishwa na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa umma imekuwa ikigharimu Serikali kiasi kikubwa sana, kwani hata vibali vinapoombwa huchukua muda mrefu mno, kiasi cha mwaka wa fedha kuweza kwisha kabla ya kibali kutolewa. Ili kuimarisha utendaji kazi Serikalini, utaratibu wa zamani urejeshwe. Utumishi iwe na jukumu la kuidhinisha ikama na kuachia mamlaka za ajira ziendee na hatua zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa sekta ya ardhi ina upungufu wa wataalam wapatao 650 ambao ni sawa na asilimia 24 na mahitaji halisi ya sekta nchini. Hali hiyo imekuwa sababu ya kero ya wananchi kutopata huduma stahiki za upangaji wa matumizi ya ardhi, upimaji na umilikishaji ardhi, usimamizi wa utekelezaji sera na sheria mbalimbali na kadhalika. Ili kuondoa kero hii, ni vizuri Serikali iruhusu wahitimu wa Vyuo vya Ardhi nchini waajiriwe moja kwa moja badala ya kusubiri mpaka vibali vipatikane kwa Wizara au Halmashauri moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Maafisa ambao wamekuwa wakikaimu nafasi kwa zaidi ya miaka miwili, mfano mzuri ni nafasi ya Kamishna wa Ardhi ambayo imekuwa wazi tokea mwaka 2010. Utumishi ndiyo sababu ya kuchelewa kujaza nafasi hiyo. Pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kuhakikisha kuwa Rais hashauriwi kuteuwa watumishi wasio wadilifu kushika nafasi, utaratibu ungebadilishwa ili kuwepo na mawasiliano ya moja kwa moja baina ya Wizara ya Sekta na Ofisi ya Rais kwa masuala ya upekuzi badala ya kupitia utumishi. Vile vile ni vizuri Wizara iwasilishe mapendekezo ya uteuzi kwa Mheshimiwa Rais kupitia Katibu Mkuu Kiongozi badala ya kupitia Utumishi ili kuondoa urasimu usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna mifuko mingi sana iliyoanzishwa kwa lengo la kuwezesha wananchi kujitegemea kwa kukopeshwa ili kuanzisha miradi mbalimbali. Kwa mfano, *Mwananchi Empowerment Fund* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, na kadhalika; nashauri kuwa mifuko hii iunganishwe ili kupunguza

gharama za uendeshaji na hivyo kuwapunguzia wadau wake mzigo wa riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi bora ya wafanyakazi yamekuwa changamoto kubwa na kuzua mtafaruku katika utendaji wa watumishi wa umma kama Walimu, Mahakimu, Madaktari nikitaja tu wachache, lakini watumishi wengi wa umma wamekuwa wakilalamika sana kwamba maslahi yao ni duni, hivyo ustawi wao na familia zao umeathirika kwa namna moja au nyingine. Nashukuru kwamba bajeti hii kwa mwonekano wake imeangalia haki ya watumishi hawa. Kilichobaki ni utekelezaji thabiti ili nao waweze kutekeleza majukumu yao, siyo kwa kufuata misingi ya sheria na taratibu za kazi tu, bali kwa moyo wenye ari, weledi na maadili mema katika kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa bajeti nzuri ambayo inajali hali bora ya kazi, haki na wajibu kwa watumishi wa umma. Bajeti hii ni nzuri na imezingatia ushauri mwingi uliotolewa katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na mimi

katika bajeti ya mwaka jana. Maslahi ya wafanyakazi wa kada zote, utawala bora na maendeleo ya watumishi kielimu pamoja na matarajio ya kuendelea kuboreshewa hali zao na maendeleo yao kazini yamezingatiwa. Nakiri kwamba bajeti hii inatekeleza kwa dhati Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatambua umuhimu wa rasilimali watu katika Maendeleo ya Taifa letu.

Matumaini ya wananchi ni kuona sasa wafanyakazi wa umma kwa kutatuliwa kero mbalimbali watatimiza wajibu wao kwa kutoa huduma bora kwa wananchi. Nategemea malalamiko ya wananchi kuhusu kudaiwa kutoa rushwa ili wapate huduma ambayo ni haki yao, yatakoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kuishauri Wizara iendelee na mikakati ya kubuni hali ya kuboresha maslahi ya watumishi, kupandisha vyeo kwa haki, uhamisho wa tija na siyo kukomoana ili wataalamu wengi katika fani ya Madaktari, Wahandisi, Maprofesa na kadhalika waweze kutulia na kulitumikia Taifa badala ya kwenda kutafuta maslahi bora katika nchi nyingine wakati wamesomeshwa kwa pesa za wananchi wa Tanzania kwa matumaini kwamba watalitumikia Taifa hili.

Mheshimniwa Mwenyekiti, kuna tatizo sugu la watumishi wa umma wanaopangwa kufanya kazi maeneo mbalimbali hususan vijijini kutokwenda kuripoti katika maeneo yao ya kazi. Suala hili limepelekea kuwepo na uhaba mkubwa wa watumishi wa fani mbalimbali katika maeneo haya, hivyo kudumisha maendeleo na kusababisha kero na malalamiko mengi

ya wananchi kwa kukosa huduma mbalimbali. Nashauri kwamba Wizara ijitahidi kuboresha maslahi na kuweka vichocheo na motisha *(incentive)* za kufanyia kazi vijijini ili watumishi watakaoajiriwa na kupangwa kufanya kazi maeneo ya vijijini waweze kuwa na ari ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado napenda niendelee kutoa kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini kuhusu upungufu mkubwa wa watumishi. Naendelea kuomba kwamba Jimbo la Kibaha Vijijini lipatiwe wataalamu wa Kilimo, Nishati na Umeme, Miundombinu, Biashara, Huduma za Jamii, Elimu, Afya na wachumi. Sambamba na hili, naomba huduma za jamii ziboreshwe ili wataalam hawa waweze kuja kufanya kazi katika Jimbo hili na pia wavutiwe kuendelea kuishi na kufanya kazi. Bajeti hii ya mwaka 2012/2013, ni nzuri, inazingatia ustawi wa wafanyakazi, hivyo tunategemea utumishi uliotukuka kutoka kwao. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiongeza Serikali kupitia *TASAF* ambayo imekuwa ikifanikisha miradi mingi hapa nchini katika maeneo mbalimbali, mfano katika Jimbo la Kisesa, miradi mingi ya barabara kama ile ya Sakasaka - Butuli, Mwandu, Isangijo, Mwabusalu – Mwaukoli, Lingeka – Mwabulutago, Mwaukoli – Ntobo, Masanga – Malwilo, Tindabuligi – Matale na kadhalika imefanikishwa kupitia mfuko huu. Hivyo, naipongeza timu ya *TASAF* ya Wilaya ya Meatu jinsi inavyosimamia miradi hii. Mfuko huu unapaswa kutengewa fedha za kutosha ili uweze kuendelea kutekeleza miradi mingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kujitathmini wa Umoja wa Afrika *(APRM)* ulianzishwa kwa lengo la kusimamia mwenendo wa uongozi na utendaji mzuri wa maeneo manne yakiwemo ya demokrasia na siasa, uchumi na uongozi kama ilivyo ada katika *organization* nyingi, mwanachama anapaswa kuwa hai kwa kujihusisha na mambo mbalimbali katika *organisation* ama kwa kujishughulisha na shughuli mbalimbali za oganaizesheni, kulipia michango husika na kadhalika.

Tanzania tukiwa kama wanachama wapya katika chombo hiki, pia tulilazimika kuwa tunachangia, lakini kama nchi hatukufanya hivyo tena kwa kipindi kirefu tangu tujiunge 2004 na kufanya tulimbikize madeni na kufikia kiasi cha Dola za kimarekani 800,000 sawa na Shilingi bilioni 1.258, Tanzania ni nchi pekee katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati inayodaiwa fedha nyingi ikilinganishwa na majirani zake ambazo zinadawa kiasi cha fedha kwa Dola za Marekani kwenye mabano, Rwanda (300,000); Zambia (20,000); Kenya (1000) na Uganda (400,000). Kwa nini Tanzania hatukuwa tunalipa michango yetu katika *APRM* kwa mwaka wa fedha wakati tumekuwa tukitenga fedha kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasema fedha za matumizi mengine zipunguzwe, sikukurupuka, kwani *finance bill* bado haijapitishwa na hivyo siyo sahihi kusema kuwa, kwa kuwa mapendekezo ya bajeti yamepita kwenye Kamati na hivyo Bunge halina nafasi ya kufanya marekebisho kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, kwani kama Kamati zina kauli ya mwisho,

hivyo hapa Waheshimiwa Wabunge nawashangaa, tunafanya nini hapa?

Mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge tufungashe vilivyo vyetu twende nyumbani, kwani kwa kauli ya Waziri, kazi zimekwisha. Kwa maana hiyo, sisi tunakuwa ni mihuri tu ya bajeti iliyokwishapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), taarifa na takwimu zilizoainishwa katika jedwali la kwanza katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inaonyesha kuwa kwa kipindi cha Julai, 2011 hadi Mei, 2012 kesi zilizoshindwa Mahakamani ni 56. Kesi zilizoondolewa Mahakamani ni 32 huku kesi zilizoshinda ni 46 tu. Hii inamaanisha kuwa kesi nyingi zinazofunguliwa na TAKUKURU ni za kukurupuka kwani nyingi zimekuwa zikikosa ushahidi wa kutosha Mahakamani na kulisababishia Taifa hasara kubwa. Hivyo, TAKUKURU wawe makini katika uchambuzi na uchunguzi wa tuhuma mbalimbali kabla hawajafikisha kesi Mahakamani kwa wakati, kwani tatizo lingine ni kwamba tuhuma zikipelekwa TAKUKURU huchukua muda mrefu kuchunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kwamba, rushwa na wizi wa waziwazi wa fedha za umma tuhuma hizo hazichunguzwi na taarifa zake hazitolewi ili Taifa lifahamu. Licha ya taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Mashirika na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi, yamekuwa yakitoa taarifa ya jinsi fedha za umma

zinavyoibiwa na zinavyotoroshwa nje ya nchi. Mfano, *The global financial intergrity (GFI) Report of 2008 with the heading: "Illicity Financial Flows from Africa: Hidden Resources for Development."* Ripoti hii ilibainisha kuwa kwa miaka 39 (1977 - 2008) Tanzania ni nchi ya 13 kati ya nchi 20 zinazoongoza kwa utoroshaji wa fedha za umma na kuficha nje na kwamba kwa kipindi hicho Tanzania imepoteza Shilingi trilioni 11.6 ambazo zimefichwa nje na wafanyabishara na Watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata matokeo ya utafiti uliofanywa na akina Ndikumana na Boyce katika mwaka 2008 umefanana na ule wa *GFI – 2008. The one bilioni Dollar Question with the heading "How can Tanzania stop losing so much revenue,"* inaonyesha kuwa Tanzania inapoteza Shilingi bilioni 478 kutokana na *illicit capital flow account* kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, The Swiss Central Bank and Swiss National Bank zimetoa taarifa hivi punde kuwa Watanzania sita wanamiliki akaunti zenye thamani ya Sh. 315.5 bilioni nchini Uswisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Waziri, haijaonyesha hata kushutushwa na taarifa hizo, kwani hakuna mahali popote ambapo imeelezea wala kuainisha hatua zozote zitakazochukuliwa juu ya wizi huo wa fedha za umma uliofanyika mpaka sasa. Pia ni mikakati gani Serikali iweke kuweza kubaini na kuujulisha umma wa Watanzania na Bunge juu ya watu wanaohusika na utoroshaji huo wa fedha za umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu wanajua kwa majina akaunti zote na fedha ambazo Watanzania wanamiliki katika mabenki nje ya nchi, iweje hadi leo TAKUKURU hawajatoa taarifa yoyote? Hii inaleta mashaka kwa chombo hiki muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoroshaji huu mkubwa wa fedha za umma inapunguza akiba ya fedha za kigeni, inaongeza mfumuko wa bei, inapunguza ukusanyaji wa kodi, inapunguza uwekezaji, fedha hizi zingeweza kutumika kwa manufaa ya Watanzania wote katika jitihada za kuongeza kasi ya utoaji huduma kama maji, afya, elimu na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuwezesha ukuaji wa kilimo, miundombinu na viwanda. Wakati Watanzania wengi wakiteseka na lindi la umaskini, fedha nyingi zinaishia katika mifuko ya wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zilizoamua kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa fedha zilizotoroshwa na kuwekwa katika mabenki *(developed country financial centres)* zinataifishwa na kurejeshwa nchini. Nchi hizo ni kama Nigeria, Peru na Ufilipino. Pia Benki ya Dunia baada ya kuona kuwa suala la wizi wa fedha za Umma katika nchi zinazoendelea linazidi kuongezeka kila siku, ndipo ikaamua kuanzisha mkakati maalum wa kurejesha rasilimali zilizotoroshwa. *Stolen Asset Recovery (STAR) Initiative Challenges, Opportunities and Action Plan (2007),* mkakati huu unaiwezesha nchi au Wakala wa Kimataifa kufuatilia, kutaifisha na kufilisi na hatimaye kurejesha raslimali hiyo katika nchi iliyoibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, marekebisho tuliyofanya wakati tukijadili mpango wa maendeleo hayajaingizwa hadi sasa katika kitabu. Mfano, Benki ya Raslimali tuliazimia kupeleka Shilingi bilioni 500 badala ya Shilingi bilioni 100 na Benki ya Kilimo. Vilevile, marekebisho haya hayajaonyeshwa mpaka sasa katika kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi mpango kazi ulivyowasilishwa katika jedwali la miradi ya Kitaifa ya kimkakati mwaka 2012/2013 umedhihirisha mapungufu makubwa ya uwasilishaji wa taarifa, kwani katika mpango wa miaka mitano umeainisha miradi na gharama ya fedha zitakazotumika. Huku miradi mingine ikigharamiwa na Serikali kwa asilimia mia moja na mingine Serikali kwa ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo haikutengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013 haikuanishwa katika jedwali na hivyo kufanya kazi ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango kuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali limeanisha miradi na gharama itakayogharamiwa na Serikali kwa fedha za ndani na za nje, lakini haijaonyesha mchango wa sekta binafsi. Hii inaleta mkanganyiko na wasiwasi mkubwa wa kutekeleza mpango kama ulivyopangwa. Hapa jumla kuu ya miradi ya maendeleo ingesomeka Shilingi trilioni 8.6 badala ya Shilingi trilioni 4.5 ilivyoainishwa katika jedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa, Serikali imeshindwa kupunguza Matumizi ya Kawaida na hata katika bajeti ya mwaka huu imedhihirisha hilo. Tume ya Mipango katika Mpango wa Miaka Mitano iliahidi kufanya utafiti ili kuiwezesha Serikali kupunguza matumizi yasiyo na tija *(recurrent expenditure).* Kazi ambayo hadi sasa haijafanyika na hata katika bajeti yao haijaainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza ikapunguza matumizi mengineyo kama posho za safari (ndani na nje ya nchi) ununuzi wa magari ya kifahari warsha na semina mafuta, pango, mafunzo, *furniture*, viburudisho, ikiwa jumla ya fedha zilizotengwa katika eneo hili ni Shilingi trilioni 1.76 ambazo zinaweza zikapunguzwa na kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza ukubwa wa Serikali, hivi sasa kumekuwapo na utitiri wa mashrika ya umma na kwamba karibia kila siku yanaanzishwa mapya. Ruzuku ya Serikali katika mashirika haya ya umma imefikia Shilingi trilioni 1.7. Utafiti wa kina unahitajika ili kuweza kubaini umuhimu wa kuendelea kuwa na mashirika ya umma mengi yanayozidi 200. Hivyo, mashirika haya yanatakiwa kufanyiwa tathmini ili kuweza kufuta baadhi ya mashirika yasiyokuwa na tija katika Taifa, pia kuyaunganisha mashirika mengine ambayo kwa namna moja au nyingine yana lengo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shughuli nyingi za Wizara ya Elimu kuhamishiwa katika Wizara ya

TAMISEMI na hivyo Wizara ya Elimu kubaki na shughuli za kisera: Je, kuna haja ya kuendelea kuwa na Wizara yenye umbile kubwa ambalo kwa kiasi kikubwa limepunguziwa shughuli?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia juu ya watumishi wa umma. Napenda kuishauri Serikali kuweka wazi na haraka utaratibu wa '*incentives*' vivutio kwa Wilaya za pembezoni kama Kibondo ili waajiriwa wapya wakubali kwenda kufanya kazi huko na utaratibu huo uwe uko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa ushauri kwa Serikali kulipa madeni yote kwa haraka na kuepuka kuhamisha wafanyakazi bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, napenda kuishauri Serikali kupanua wigo wa kuangalia mali za viongozi kwenda hadi kwa watumishi wa umma. Kwani kuna watumishi wengi wa umma wenye mali nyingi kuliko uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sekretarieti hii haichukui hatua stahiki mfano zaidi ya Madiwani 1800 hawakutii Sheria ya Maadili kwa Viongozi wa Umma lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa umma. Napenda kushauri vibali vya ajira vitolewe kwa wakati.

Pia utekelezaji wa Halmashauri kuajiri Wahudumu na Madereva ufanyike kwa haraka. Pia Wizara itoe mwongozo wa *qualifications* ambazo zitazingatiwa nchi nzima kwa Wahudumu na Madereva.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye mipango na mikakati mizuri kama ikitekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa mchango wangu kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Naipongeza Wizara kwa kuzindua utekelezaji wa Awamu ya III ya *TASAF*. Kwenye miradi hii ya *TASAF* ni muhimu sana kukusanya takwimu za awali *(baseline data collection)* kwa ajili ya kupima mafanikio ya utekelezaji baadaye kwa sababu kuna baadhi ya Halmashauri na vikundi vinakuwa vya kifamilia na pesa hizo za miradi huliwa tu bila kuwanufaisha wananchi waliokusudiwa. Kwa kuhakiki vikundi hivyo vya ujasiriamali itasaidia kuimarisha shughuli zao ziendelee kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni migogoro baina ya Serikali na watumishi wake. Kwanza niunge mkono maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa Serikali ishirikishe watumishi wa umma katika maamuzi yanayowahusu watumishi hasa maslahi yao. Madai ya watumishi wa umma yanaongezeka kwa kasi huku yakiambatana na vitisho vya migomo ya kuishinikiza Serikali. Naomba nipendekeze kuwa Serikali kwanza

ipokee madai ya watumishi na kuyafanyia kazi japo kwa kuweka bayana kila stahili yao ili kusiwe na manung'uniko lakini pia kuyafanyia kazi. Migomo inayotaka kujitokeza kwa kutafuta kiini cha migomo hiyo, ufanyike utafiti wa kina ni kitu gani na ni nani wanaochochea migomo na kuchukuliwa hatua, kwani kuna manung'uniko kuwa kuna baadhi ya Vyama vya Siasa vinachochea migomo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya watumishi yanayoendana na hali ya maisha ya sasa bado ni duni sana, hayaendani na kauli mbiu ya Rais ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Kiwango kinachotarajiwa kuongezwa mpaka Sh.170,000/= bado ni kidogo hakiendani kabisa na hali ya maisha ya sasa kutokana na mfumuko wa bei kuwa juu. Kiwango hiki kidogo cha mshahara ndicho kinachosababisha ufisadi na watu kutowajibika ipasavyo. Lakini pia kuwe na mfumo ambao utaweza kuwabana watumishi wawajibike kwani watumishi wengi hawafanyi kazi, ni wavivu, watoro makazini lakini wanahitaji mishahara mikubwa bila kuzalisha, hivyo kuwe na utaratibu wa kuhakikisha watumishi kweli wanawajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kwenye Halmashuri zetu kwenye upande wa watumishi hasa wanapokwenda kuongeza ujuzi. Watumishi wanapokwenda kuongeza ujuzi na kuripoti makazini wanapelekwa kwenye Kata bila kujali ujuzi wao walioongeza hali inayopelekea wengi wao kukata tamaa na kuacha kazi. Ninamwomba Waziri anapokuja kufanya majumuisho aniambie utaratibu

ukoje, mtumishi anapokwenda kuongeza ujuzi akirudi anarudishwa palepale au kuna utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri alitolee ufafanuzi kwani jambo hili ni muhimu sana. Kuna malalamiko mengi hasa kwenye Halmashauri, watumishi wengi wanalalamika kuwa Wakuu wa Idara wanapendelea hasa pale Ofisi Kuu anapokuwa na watu wenye Diploma na wenye ujuzi mkubwa kama *Degree* na *Masters* wanapopelekwa kwenye Kata na wanakata tamaa na kuacha kazi na Halmashauri zinabakia bila wataalam. Naomba Waziri alieleze kiuwaziwazi ili watumishi walifahamu vizuri.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu ni muhimu sana, naiunga mkono hasa ukizingatia dhana pana ya Serikali ya kuboresha mishahara ya watumishi wake (aya 45), hali ya watumishi Serikalini ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na vuguvugu lililopo la Madaktari na Walimu, ni vyema tukajipanga kuona mishahara yao wote inaboreshwa na mishahara ya taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 38 (b), nchi yetu inakabiliwa na janga kubwa la mapambano dhidi ya rushwa. Rushwa inapoota mizizi basi hakuna kinachopona. Serikali hutingishwa, vyombo vya kiusalama hutetereka na pakawa na Serikali mbili, Serikali Tawala na ya Wala Rushwa. Hii ni hatari sana, tunashuhudia yanayojitokeza nchi za Marekani ya Kusini, suala hili ni baya sana. Nashauri Serikali itenge

mbali Mahakama za wala rushwa ili kesi zao ziendeshwe kwa umakini zaidi kuliko zinavyoendeshwa hivi sasa na ikiwezekana kesi zimalizike si zaidi ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Mahakama kuna hizo kesi zote za waagiza unga, mihadarati, nazo zishughulikiwe na Mahakama Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pawepo na Mahakama Maalum vilevile kwa wauaji wa maalbino, kesi zote za ubadhirifu wa fedha za umma na zile zilizothibitishwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*). Hizi zote zisipite katika mkondo wa Mahakama za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hapatakuwa na ufumbuzi wa kesi hizi kwa aina yake, rushwa nyingine itazuka Mahakamani na Magerezani. Nchi itachafuka na haitatawalika. Naomba hili lionekane na hatua muafaka ziwe zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Serikali ilivyojipanga kushughulikia suala la ardhi na marekebisho ya baadhi ya vipengele vilivyokuwa na utata. Ardhi ni jambo muhimu sana na *assets* endelevu kwa wananchi matajiri au maskini lakini suala hili linataka mipango maalum kuwasaidia wamiliki lisiwe tu ni la kuwa na ardhi bila ya kuiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na maelezo niliyoyatoa hapo juu, lakini wananchi wanapaswa kupangiwa mipango mahsusi ya kilimo na ujenzi na makazi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja hii tunayoijadili sikuona *sector* ya uvuvi inapangwaje ili kusaidia kipato cha Mtanzania au kuinua pato la nchi kwa ujumla wake. Bahari, mito ni hazina tosha kuleta ajira kwa Watanzania alimradi mipango kabambe itaasisiwa ambayo itatoa ajira na kuondoa umasikini vijijini na mijini.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kuhusu watumishi hewa. Kwa kuwa kuna watumishi hewa ambao wanasababisha nchi kupata hasara kubwa ya mabilioni ya fedha za Kitanzania kupotea, hadi sasa ni watumishi hewa wangapi wamebainika na fedha kiasi gani zimeokolewa? Je, Serikali imeweka utaratibu kudhibiti na kukomesha hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *PAYE*, kwa nini watumishi wa umma wanaendelea kutozwa kodi kubwa wakati mishahara yao ni midogo? Serikali inao mpango gani wa kupunguza kodi wanayokatwa watumishi wa umma katika mishahara yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, upungufu wa watumishi nchini hususan Wilaya za pembezoni kama Serengeti, kwa kuwa watumishi wanaojiriwa na Serikali wengi wao hawapendi kwenda Wilaya hizo, Serikali ina mkakati gani ili kuweka uwiano mzuri wa watumishi nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *Management Audit.* Kutokana na usimamizi hafifu kwa watumishi wa umma,

hali hii imesababisha tija kazini kuwa chini sana mbali na Serikali kuanzisha utaratibu wa *OPRAS* hali bado si ya kuridhisha katika ufanisi na tija kazini na nidhamu ndogo kazini. Je, Serikali iko tayari kupitia upya juu ya kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa watumishi wa umma ili kuongeza tija na nidhamu kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, uteuzi wa Wakuu wa Idara, ili kuwa na uongozi madhubuti na imara, ni vizuri uteuzi na ajira ya viongozi wa ngazi hii (*Heads of Departments*) uwe wa uwazi na makini, pia *vetting* ifanyike. Hali hii itasaidia kujenga uadililfu, uaminifu, kuongeza tija kazini na nidhamu ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, mishahara na marupurupu kwa watumishi wa afya wakiwemo Madaktari kuwa kidogo sana. Kwa vile migomo katika kada ya afya imekuwa ni ya mara kwa mara, hii ni kielelezo cha kutoridhika na wanachokipata mfano mfomo wa kwanza ulikuwa mwaka 1974, wa pili mwaka 1991, wa tatu mwaka 1995, wan ne mwaka 2002, wa tano mwaka 2005, wa sita mwaka 2012 kwa mwaka huu ni mara tatu ukiwemo huu unaoendelea, hali hii inatisha na si salama kwa nchi yetu. Je, ni kwa nini Serikali haijalifanyia suala hili utafiti ili kujua kiini hasa cha migomo hii ni nini? Ni vizuri sasa *seriously* Serikali iunde Tume ya kudumu ya kufuatilia kwa ukaribu hali ya mshahara na mafao kwa watumishi wa afya.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwepo katika Bunge

hili Tukufu nami nikiwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima za Bunge hili Tukufu, nami nichukue fursa hii, nichangie hotuba hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais ndiyo yenye dhamana na mamlaka ya kusimamia shughuli zote za kiusalama za umma wa nchi hii. Idara hii ya Usalama ina wajibu wa kusimamia na kuhakikisha inazingatia kwa umakini katika kusimamia na kulinda maslahi ya nchi na umma wake badala ya kusimamia na kulinda maslahi ya viongozi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeingia katika kashfa mbalimbali zinazotuletea kuteketeza uchumi na rasilimali za nchi hii kama vile rushwa na matumizi mabaya bila usimamizi mzuri wa fedha za umma (uzembe), wizi wa kiholela kwenye mashirika ya umma na kadhalika. Hujuma hizi baadhi huwa zinaonekana na nyingine ushahidi wake huwa unapatikana lakini vyombo vya usalama tunanyamaza kimya. Ushauri wangu, naomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi iache kuwaelimisha watumishi wa umma na kuwaandaa kutumikia umma wa Watanzania kwa kuchanganya siasa katika utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la bajeti la mwaka jana 2011/2012 lilitangaza hadharani kashfa za aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Katibu wake jambo ambalo Maafisa Usalama kazini walikuwemo na wala hawakutoa habari hizi hadi suala

hili limegunduliwa na Kamati ya Bunge. Je, chombo cha usalama hakikuwepo? Naomba Serikali ibadilike na ichukue tahadhari kubwa kulinda mali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni pamoja na utawala wa sheria yaani kuendesha mambo kwa heshima, kulinda na kufuata Katiba na sheria nyingine za nchi. Hali ilivyo sasa kwa mwonekano wa juhudi za kufuata utawala wa kisheria kwa kiasi fulani kwa ngazi za kitaifa hata hivyo kwa ngazi za Wilaya na Vijiji hali bado ni mbaya mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya vitisho, mabavu na ukatili wa hali ya juu, habari zilizopatikana katika vyombo vya habari vinasema Dkt. Ulimboka alitekwa na Vyombo vya Dola (Askari Polisi), je, huu ndio utawala bora unaodaiwa kuwepo katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubambikiziwa kesi na kukosa haki zote za msingi za mtuhumiwa ni vitendo vya kawaida kufanywa na sehemu kubwa ya viongozi wa ngazi za Kata na Vijiji. Katiba na sheria nyingine za nchi zinatumika tu pale ambapo kuna maslahi binafsi ya wahusika, matumizi ya fedha yamekuwa ndiyo msingi wa kupata haki yako, kama huna fedha hupati haki hata ikiwa haki hiyo ni stahili yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Mahakama kulalamikiwa sana kwa kiasi kikubwa. Ninashauri Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wa Mahakama ili ubovu huu uondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na wataalamu wake wote kwa maandalizi mazuri ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea na mchango wangu katika hoja hii, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii utakuwa katika maeneo kadhaa yafuatayo:-

Kwanza ni nidhamu ya utumishi kwa watumishi au baadhi ya wafanyakazi imeshuka sana hivyo kuna haja ya Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba kila mtumishi anapaswa kuelewa wajibu wake. Kwa mfano, Mwalimu au Daktari au mtumishi mwingine yeyote anaondoka eneo lake la kazi bila hata kiongozi wake wa eneo kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila ukipita katika maofisi unakuta kuna misururu mirefu ya wananchi wengi wakifuatilia haki zao bila mafanikio wakiambiwa njoo kesho au wiki ijayo pia bila kufanikiwa. Je, Serikali ina mkakati gani kurudisha nidhamu katika maeneo ya kazi? Mtumishi anaondoka kwenda mjini au mahali

popote bila hata ya kibali kutoka kwa kiongozi wake. Waliopewa jukumu la uongozi hawawajibiki ipasavyo kwa woga kwamba wataitwa Nyapara. Ukiwa mkulima kazi yako itapimwa kwa ekari ambazo zimelima kwa siku, je, hata kama hatuwezi kupima kazi za watumishi wengine ofisini ni nani anawajibika kwa ufanisi wa kazi hizo? Kazi ni uhai kwa hiyo kila moja awajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, siku hizi kumekuwa na migomo na maandamano makubwa kila mahali hasa kwa watumishi. Zamani karibu sekondari nyingi, vyuo vikuu, viwandani na maeneo kadha wa kadha inasemekana kulikuwa na Vyombo vya Usalama ambavyo vilikuwa vinatoa taarifa kabla ya mambo kulipuka. Je, siku hizi vyombo hivi havijapewa jukumu hilo? Kwa nini watumishi hao ambao ni muhimu wasiongezwe maana hao wangeweza kusambazwa maeneo mbalimbali ya kazi na kubaini mambo mengi ya kifisadi yanayofanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Vyombo vya Usalama hasa Usalama wa Taifa, TAKUKURU na kadhalika. Watumishi hawa wasambazwe kila eneo hasa kwenye kampuni za madini, vyuoni, mashuleni na viwandani kwa lengo la kusaidia kubaini matatizo na ufisaidi unaofanywa katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha wanazopata wastaafu kila mwezi ni kidogo sana. Hawa ni watu waliolitumikia Taifa kwa muda mrefu na kwa uadilifu sana. Inapaswa waangaliwe kwa jicho la huruma. Viongozi wakubwa wakistaafu sheria inawalinda na wanapata theluthi mbili ya mshahara wa yule aliyeachiwa ofisi. Kwa wastaafu wa kawaida afadhali Muswada uletwe Bungeni wa kuifanya Mifuko ya Pensheni igawe faida inayopata kwenye miradi kwa wastaafu. Mifuko hii inapata fedha nyingi kwenye miradi ya biashara. Wakumbuke kuwa fedha wanayofanyia miradi inatoka kwa wastaafu hawa. Afadhali faida kidogo wagawiwe wastaafu ili fedha wanazopata zifanane kidogo na hali ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwapo watumishi hewa limekuwa likiibuka mara kwa mara. Hii siyo nzuri hasa wakati huu ambapo TEHAMA imekuwa sana nchini, naiomba Serikali ilishughulikie jambo hili *once and for all*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia kwa maandishi bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linayo mahitaji makubwa ya watumishi kupita kiasi. Napendekeza Menejimenti ya Utumishi ijitahidi kuweka majina ya waajiriwa wapya mara tu wanaporipoti kazini, si busara

mfanyakazi mpya kuripoti kazini na akamaliza miezi miwili bila kulipwa kwa madai eti Utumishi na Hazina hawajaweka sawa kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matendo ya Utumishi ambayo yanawakatisha tamaa watumishi katika kuongeza ujuzi wao. Wafanyakazi wengi wamejiendeleza kwa kusoma lakini Utumishi wamekuwa wazito kuwapandisha madaraja. Hali hii inakatisha tamaa wafanyakazi, tunashauri suala hili lirekebishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la mishahara hewa pamoja na taarifa kuwa tatizo la mishahara hewa limepunguzwa sana. Napendekeza na kushauri wale wote waliohusika na mchezo huu mchafu wabadilishwe na wachukuliwe hatua za kisheria na taarifa ziwasilishwe rasmi Bungeni. Ni vyema wahusika wote wakajulikana. Hii itajenga taswira njema ya Serikali na Chama kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la sekta ya watumishi ambao nawaona kama hawawezeshwi. Hili ni kundi la Watendaji wa Vijiji na Kata pamoja na Maafisa Tarafa. Kada hii ikitumika kwa ufanisi, ni dhahiri kuwa utendaji wa Serikali utakuwa na ufanisi wa hali ya juu. Ili kupata ufanisi huo ni vyema kila nafasi ikajazwa yaani kila Kijiji, Kata kiwe na Mtendaji. Watendaji hao wapewe majukumu na mamlaka ili wawajibike pale wanaposhindwa kutimiza wajibu. Yapo majukumu mengi ambayo yangetekelezwa kirahisi kwa kuwatumia watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la malalamiko ya watumishi ambapo mara waendapo utumishi kutafuta suluhu huelezwa kuwa tatizo ni Hazina wakati mwingine wakienda Hazina huwa ni kupigwa danadana wakizungushwa ofisi moja kwenda ofisi nyingine. Nashauri utaratibu uandaliwe ambapo mfanyakazi atawasilisha malalamiko yake ofisi moja na Serikali iwajibike kufuatilia katika Idara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya Serikali kuwa na dhamira ya kuleta wataalamu toka China kuja kuwafundisha wakulima wa Kilosa kilimo chenye tija, naomba na kushauri utaratibu huu usambazwe nchi nzima. Hii ni njia bora ya kuendeleza kilimo badala ya mfumo wa kuita wawekezaji na kuwagawia ardhi. Wazo hili linapokubaliwa kituo cha pili cha Wachina au wataalamu wengine kiwe Mkoani Kagera na ikibidi Jimbo la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kuanzishsa JKT linaendelea kupata kasi na ni dhahiri kuwa litatekelezwa. Pendekezo langu ni kuwa mara tu tunapoanzisha JKT vikosi vyake viwekwe mipakani ili pamoja na kuendesha shughuli za kiuchumi, washiriki kudhibiti uingizaji wa wageni na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee utendaji wa TAKUKURU na hasa inavyoonekana mbele ya jamii. Kitendo cha wafanyakazi wa Serikali kudai na kupokea rushwa, uporaji na unyanyasaji wa wananchi unaofanywa na watendaji wawapo kazini ili hali hakuna linalotendeka inachafua taswira ya Idara hii muhimu. Ni jambo lililo wazi kuwa Polisi wanajipanga

barabarani kutwa wakiomba na kupokea rushwa. Kwa nini TAKUKURU wasiwasihi Jeshi la Polisi ili wawazuie watendaji wao kufanya hivyo? Je, kama Polisi hawataki, kwa nini basi TAKUKURU wasijifiche kama mtengo na kuwabana Polisi hawa? Binafsi nimezungumzia mara nyingi Bungeni jinsi Jeshi la Polisi na Idara ya Uvuvi Mkoani Kagera wanavyonyanyasa wakazi wa visiwani na wavuvi. Hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ilihali kuna Idara hii toka Makao Makuu mpaka Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo tatizo la mifugo (ng'ombe) toka nchi za jirani kuja kuchungwa nchini. Ng'ombe hawa huvushwa kwa makundi makubwa yenye ng'ombe kati ya 3,000 – 5,000. Ilikadiriwa kuwa ilikuwepo mifugo karibu 200,000 Mkoani Kagera mwaka jana toka nchi jirani. Lawama kwa TAKUKURU hapa ni kuwa ni kwa vipi mifugo hii imevushwa? Mifugo hii inachungwa kwenye Hifadhi za Taifa na Ranchi, je, kwa nini TAKUKURU isiwahoji na kuwawajibisha waliopewa dhamana?

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sekta ambazo zina upungufu mkubwa wa watumishi (sekta ya madini kwa mfano) Serikali iandae na kutekeleza mkakati wa kupata watumishi wa kutosha na hasa wataalam. Mkakati huo uziruhusu sekta hizo ziajiri wataalam moja kwa moja kutoka chuoni ili kuhakikisha zinapata wataalam mahiri na wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa sasa wa kutangaza nafasi (nafasi za kuingilia kwenye ajira) zinapata wataalamu dhaifu kwani wale wazuri wanakuwa wamechukuliwa na sekta binafsi. Sababu kubwa ya kupata wataalam dhaifu ni kuwa ajira (mamlaka) wanahitaji vyeti halisi ambavyo mara nyingi hutolewa baada ya miaka miwili hadi vyeti vinatolewa wataalam wenye sifa nzuri za masomo wanakuwa waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa limesongwa na kukandamizwa na rushwa kutokana na Watanzania kutoitambua rushwa kuwa ni dhambi kubwa, Watanzania wengi wamekosa uadilifu kabisa. Rushwa imeota mizizi katika jamii yetu ya Kitanzania ambapo baadhi ya viongozi wakubwa kwa wadogo, wa kisiasa, kiserikali na kijamii wanaikumbatia rushwa kwa kujilimbikizia mali na vitu kwa njia za kutoa na kupokea rushwa. Hali hii inahitaji tuiangalie kwa namna ya pekee kwa kuanza sasa kujenga Taifa jipya lenye waadilifu walio wengi. Dawa ya kweli ya rushwa ni kuijenga mioyo (hasa) ya Taifa iogope rushwa na kuiona kama dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufanya hivyo kwa kutunga na kutumia mitaala yenye kufundisha ubaya wa rushwa kwenye ngazi za shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu. Mtaala hiyo (uraia) itasisitiza ujenzi wa utaifa na kuchukia rushwa. Nina uhakika baada ya miaka kati ya kumi na kumi na tano, tutajenga Taifa jipya lenye uadilifu na utaifa halisi kwa kuwa na Watanzania waliobadili mioyo. Naishauri Serikali iandae mitaala hiyo. *PCCB*, ikishirikiana na

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Taasisi ya Kukuza Mitaala waanze sasa kushughulikia suala hili lenye umuhimu wa pekee. Tujenge Taifa jipya kwa kutoa elimu ya uraia inayokataa rushwa na kujenga uadilifu na utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mishahara ya watumishi, ukurasa wa 55, katika vipengele vya 45, 46 na 47, hasa kipengele cha 46 na 47 havielezi ongezeko la mishahara ni kiasi gani. Naomba kujua iwapo mwaka 2012/2013, Serikali inaongeza mishahara au haiongezi? Iwapo inaongeza ni kiasi gani? Iwapo haiongezi ni kwa sababu zipi wakati Serikali inakusanya kodi za watumishi wa Serikali na sekta binafsi? Aidha, kipengele cha 46, ukurasa wa 55 kinaeleza kuwa shilingi 3,781,100,000,000 zitagharamia malipo ya mishahara, upandishwaji vyeo, kulipa madai ya mapunjo ya mishahara kwa watumishi wa umma na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuandaa mwongozo wa kutoa motisha, ni maajabu makubwa sana kuona na kusikia kuwa katika mwaka 2012/2013 Serikali itatia mkazo katika kuandaa mwongozo wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu pamoja na kufanya utafiti kuhusu mishahara na maslahi ya wafanyakazi baina ya sekta binafsi na Serikali kwa lengo la kuwianisha na kuoanisha mishahara ya watumishi wa umma (Ukurasa wa 56 kipengele cha 47). Swali, Kamati au Tume za akina Ntukamazina zilizoundwa na Mheshimiwa Rais miaka

kati ya 2006-2009 hazifai au Serikali inadhani Wabunge na watumishi wa umma hatujui kwamba tabia hii ya kuja na vitu vipya mara kwa mara ni kutuhadaa? Serikali itueleze ukweli kuhusu namna bora ya kuboresha maslahi ya Wabunge na watumishi mbalimbali wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi na haki za Wabunge baada ya kustaafu. Hivi inawezekanaje viongozi wafuatao baada ya kustaafu wanalipwa 80% ya mishahara ya wale waliopo madarakani, kwa mfano, Waziri Mkuu Mstaafu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Mstaafu), Spika na wengine wastaafu, Wabunge hatumo katika orodha hiyo baada ya kustaafu? Serikali itaacha lini ubaguzi huo kwa wastaafu wake tukiwemo Wabunge na umuhimu wa Wabunge wote wastaafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu na Madaktari, Serikali iache kuwalaghai watumishi wa umma hususan Walimu na Madaktari, pamoja na wengine kama vile Polisi katika kuwalipa madai yao. Nasema hivyo kwa sababu wapo watumishi wengi wanaolalamika kutolipwa madai yao kwa mfano Walimu wengi wanakataliwa malipo ya madai yao na ofisi za Wakurugenzi ambazo huieleza Serikali kuwa uhakiki umefanywa vizuri na kwamba hakuna tatizo. Waziri wa Utumishi upo ushahidi wa mambo hayo. Ninakumbuka mimi mwenyewe nilipokuwa Mwalimu Manispaa ya Kigoma Ujiji miaka iliyopita, hali hiyo ilinikuta na hadi ninaacha kazi ya Ualimu sikulipwa kwa sababu ya uzembe na chuki za ofisi za Wakurugenzi katika Halmashauri zetu. Hali ipo hivyo hivyo hata

katika sekta na taasisi nyingine kama polisi na Madaktari. Swali, Serikali inatoa kauli gani katika hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho madaraja ya Walimu, haiingi akilini Mwalimu anayejiendeleza kitaaluma mathalani anafikia kiwango cha *Degree* katika Daraja E yaani *TGTS E,* kama ngazi ya mshahara, miaka zaidi ya 10 kazini ngazi ya mshahara *TGTS E,* elimu *Degree*, hivi ni haki kweli? Ni uonevu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya hoja zangu.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira vitolewe mapema na aidha vibali katika sekta ya afya na elimu viongezwe. Vibali vya kuajiri kama vya Madereva na Wahudumu viwe *specified*, vitolewe kwa Wilaya husika tu, hapa nina maana kwamba Madereva na Wahudumu wengine wa kawaida iwe *specifically* kutoka ndani ya Wilaya hiyo tu. Ni kwa nini Madereva na Wahudumu wa Wilaya nyingine wanakwenda kuajiriwa Wilaya nyingine wakati ndani ya Wilaya husika kuna *Drives* ambao wangeweza kuajiriwa? Kuna kazi za *profession* kama Wahasibu, Madaktari, Walimu na kadhalika hawa wanaweza kuajiriwa popote lakini *Drivers* ni vema vibali vinapotoka waajiriwe kutoka ndani ya Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya JKT ni muhimu yarudishwe tena, tena yawe kwa muda wa mwaka mmoja. Mafunzo ya JKT yaliwafanya vijana kuwa wakakamavu, kuwa na *despline* na kufanya kazi kwa moyo na kujitolea. Vijana wa sasa hawana *despline* hata utendaji wao wa kazi hauridhishi, wana fujo, vurugu hata uzalendo hawana kabisa na hivyo kushusha kiwango cha uwajibikaji ndani ya Taifa letu. Ajira isitolewe kwa mhusika kama hajapitia mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuhamisha wafanyakazi na watumishi wa umma. Kumekuwa na tatizo la uhamisho kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine. Utaratibu wa kuhamisha watumishi kama kubadilishana ufutwe kwani kuna wakati mtumishi ambaye ni mzawa wa Wilaya fulani anahitaji kuhamia katika Wilaya yake aliyozaliwa na katika Wilaya hiyo kuna uhaba wa watumishi hao, ni kwa nini huyu mtumishi asihamishwe akaenda katika Wilaya aliyozaliwa na ambayo anahitaji kufanya kazi, akaamrishwa kufanya hivyo na hivyo kuziba mapengo ya watumishi ambao walipangiwa katika Wilaya hiyo na hawataki kwenda ndani ya Wilaya hiyo badala ya kutafuta mtu wa kubadilishana? Je, ikitokea kwamba mtumishi huyu hana mtu wa kubadilishana naye na anahitaji kuhama atafanyaje? Napendekeza taratibu za uhamisho zisibanwe na kanuni hii, kwamba mtu hawezi kuhama mpaka ampate mtu wa kubadilishana naye, hii si haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyotolewa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za kada za chini kuruhusiwa kufanywa na Halmashauri husika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba nafasi za ajira zinatangazwa na kusimamiwa na Sekretarieti ya Ajira kwa uwazi na kuhakikisha kwamba wanapatikana na kuajiriwa wale wenye sifa zilizotukuka na ushindani mkubwa. Kwa bahati mbaya sana, utaratibu huu badala ya kutenganisha kada kwa kuzingatia uhalisia katika utendaji kazi kwani haiingi akilini kwamba nafasi kama za Madereva, Makarani, Watendaji wa Vijiji na Kata na nafasi nyingine kama za Wauguzi, Wapishi zinafanywa na Sektetarieti ya Ajira iliyo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii haikubaliki wala haina tija kwani tumeshuhudia nafasi zinaendelea kubaki wazi kwa watumishi walioajiriwa Dar es Salaam na kusambazwa Mikoani kwenda kuripoti na kulipwa pesa za posho za kujikimu na kuondoka kwa visingizio vingi badala ya kuwatumikia wananchi. Hali ni mbaya zaidi kwa Mikoa ile yenye mazingira magumu. Naishauri Serikali irudishe baadhi ya ajira kufanywa na Halmashauri husika baada ya kuainisha mahitaji kulingana na ikama na baadhi ya kada kuendelea kuwa chini ya Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF),* lengo la uanzishwaji mfuko huu ni zuri sana lakini kwa bahati mbaya sana utekelezaji wake umekuwa ukiishia mijini pasi kufika vijijini. Mimi Mbunge katika Wilaya mpya ya Kalambo na Jimbo zima la Kalambo hakuna hata sehemu moja ambayo fedha hizi zimewafikia wananchi hususani vijana ili kupunguza wimbi la vijana kuendelea kukimbilia mijini kwa kukimbia hali ngumu ya maisha vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kuhakikisha elimu ya ujasiriamali inafikishwa kwa wananchi wote na hasa walio vijijini ambao fursa kama hizi zimekuwa haziwafikii ukilinganisha na wale walio mijini ambapo taasisi mbalimbali zimekuwa zikijikita kwa kutoa elimu na uwezeshaji kifedha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Kamati na wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri na mpango na maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumishi ifanyiwe *thorough decentralization* na watumishi wote katika Halmashauri, waajiriwe, wadhibitiwe, walipwe na kuwajibishwa katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hewa waondolewe katika *payroll* na wahusika wachukuliwe hatua. Serikali iunde Tume ndogo ya watafiti na kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni na masharti ya utumishi yapitiwe upya ili kubainisha maeneo yanayohitaji kurekebishwa ili kuweza kukidhi mahitaji mapya ya utumishi wa leo. Hii itasaidia kupunguza matatizo na migogoro ya utumishi kama ya migomo, wizi na kutowajibika kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imeanza kuweka Dira katika mipango ya nchi yetu. Tume ya Mipango ione jinsi ya kuwa na mapendekezo ya *ration* kwenye bajeti ili kusiwepo na tofauti kubwa sana kati ya Wizara na Wizara, sekta na sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango itoe mapendekezo ya kuundwa *Budget Endowment Fund* ama *Budget Designated Fund (BDF*). Mfuko huu ungetunishwa kwa njia ya *reserve* zetu, mikopo na *pre-finances* kutoka sekta za gesi, machimbo ya madini, vitalu vya uwindaji na hisani yza nchi marafiki. Mfuko huu ungekuwa na jumla ya shilingi 25-30 trilioni na ungetumika ku-*fund budget* yetu. Makusanyo ya mwaka husika yangepelekwa ku-*replenish* mfuko wa *budget*. Utaratibu huu ungeondoa changamoto ya kushindwa kutekeleza *budget* inayoidhinishwa na Bunge. Faida nyingine ya utaratibu huu ni kukamilisha miradi ya kiuchumi kwa wakati na kuruhusu miradi hii iweze kuanza kuchangia kwenye uchumi na kusaidia kulipa madeni ya mfuko husika.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza masikitiko yangu kuhusu utendaji kazi wa TAKUKURU kama kweli inafanya kazi yake sawasawa kulingana na maana ya jina lake.

Taasisi hii imekuwa haitimizi majukumu yake sawasawa kwani badala ya kuzuia rushwa, taasisi hii imekuwa ikisubiri rushwa zitolewe na yenyewe ikisubiri ushahidi na kama inavyoeleweka rushwa hufanywa kwa kificho kikubwa lakini mazingira ya rushwa huwa yapo wazi. Ni kwa nini Taasisi hii isiwe inatumia ushahidi wa mazingira kuwatia watoa rushwa na wapokea rushwa nguvuni? Kwa nini Taasisi hii haifanyi kazi ya kuzuia rushwa bali inakalia kudai ushahidi bila kutimiza wajibu wake? Kama kweli inapambana na kuzuia rushwa tusingesikia kwamba kuna vigogo wakubwa wameficha mamilioni ya dola Uswisi, tusingesikia kuna mikataba tata ya madini, nishati na kadhalika, yote hii ingezuiliwa kabla ya watu kujipatia fedha kwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la rushwa ya ngono ni kubwa kuliko inavyofikiriwa. Imekuwa ni kawaida kusikia malalamiko mengi hususan kwa watoto wa kike hasa wanapotafuta kazi kuombwa rushwa ya ngono na mabosi wao na hata wanapokuwa kazini ili wapandishwa cheo, wanadaiwa rushwa ya ngono. Wanapochukua hatua ya kupeleka suala hilo TAKUKURU wanaambiwa walete ushahidi! Sasa ushahidi wa kuombwa rushwa ya ngono ni upi zaidi ya mdaiwa rushwa hiyo mwenyewe? Naomba ushahidi wa mazingira utumike ili kuwatendea haki wanawake na hata wakati mwingine vijana wa kiume pia nao hudaiwa rushwa hii na mabosi wanawake, mifano ipo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Maadili ya Viongozi ya Umma ipitiwe upya ili iwe inaweka wazi mali za viongozi kwa wananchi wote ili nao wajiridhishe

kwamba ni kweli mali alizonazo kiongozi fulani wa umma ni kweli maana wao ndiyo wanaishi nao na kuwafahamu zaidi na kwa undani. Kuwepo na uwazi katika suala zima la kufuatilia, namna ambayo viongozi wanapata mali zao hasa wanapokuwa kwenye utumishi wao. Kama kuna mashaka, wananchi wawe wa kwanza kutoa ushahidi wa mali hizo. Hii itaondoa ufisadi mkubwa ambao viongozi wengi wa umma wamekuwa wakihusishwa nao hasa katika suala la kujilimbikizia mali, mashamba, majumba, magari, viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu malimbikizo ya madai ya watumuishi wa umma hususan Wauguzi na Waalimu. Serikali imekuwa kila mara ikitoa ahadi kwamba itatekeleza malipo na malimbikizo ya watumishi hawa lakini kila mwaka deni linazidi kuongezeka na malalamiko yanazidi kuongezeka na kusababisha migomo kama huu unaonukia wa Waalimu nchi nzima. Serikali ije na majibu sahihi kuhusu namna bora ya kuwalipa watumishi wake kwa wakati na bila kulimbikiza madeni. Hali hii inajitokeza hata kwa watumishi wanapopandishwa daraja, hukaa muda mrefu zaidi ya miaka hata miwili, bila kulipwa mishahara ya madaraja mapya. Hii maana yake nini kama si kudumaza morari ya watumishi wa nchi hii.

Mheshimwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina toka kwa Waziri

ili niweze kujiridhisha na niondokane na wasiwasi wa kulipwa wafanyakazi hewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 90, Jedwali la Sita, Septemba 11 Askari 72 walilipwa shilingi 21,291,780.00 lakini Juni 12, Askari 24 walilipwa shilingi 72,154,083.00. Ukurasa wa 90 Jedwali la Sita, Juni 12, Askari 24 walilipwa shilingi 72,154,083.00 lakini Machi 12, Askari 120 walilipwa shilingi 75,524,368.50. Ukurasa wa 90, Jedwali la Sita, Desemba 11, Askari 118 walilipwa shilingi 183,513,975.00 lakini Februari 12 Askari 214 walilipwa shilingi 173,973,178.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inakuwaje kwamba watumishi wa kada au taasisi moja lakini wanapitana kimaslahi kama ilivyooneshwa hapa, kwani pia inawezekana kwamba Askari hao wote walikuwa ni wa vyeo vya chini kwa kuwa kwa Maafisa sio rahisi hata kidogo maslahi yao kucheleweshwa kama ambavyo imeoneshwa, naamini wote hao ni Askari na watumishi wadogo. Kama hali hiyo ni sahihi na ya ukweli, Serikali inasema nini juu ya kuondoa tofauti hiyo kubwa sana ya kimaslahi kwa watumishi wa kada moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Celina Kombani kifungu 50, ukurasa wa 57 ameeleza kwamba wanahitaji kujenga Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa, si jambo baya lakini kama lengo ni kuvifanya vizazi vipate kumbukumbu, inatosha kuwa ni kumbukumbu kwa vizazi vijavyo kuwepo kwa kiwanja cha kimataifa cha ndege cha Mwalimu Julias Nyerere, Chuo cha Mwalimu kilichopo

Kigamboni na kadhalika lakini pia Uwanja wa Ndege wa Karume, Pemba, Chuo cha Karume, kilichopo Unguja na kadhalika, itoshe kuwa ni kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Naomba kuishauri Serikali kwamba vielelezo hivyo na vingine vitoshe kuwa ni kumbukumbu na ukumbusho kwa vizazi na kwamba fedha za wananchi tuzielekeze katika mambo ya maendeleo kwa faida ya wananchi wetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu iliyopita ya mwaka 2011/2012, tafiti zilichelewa na kukosa ufanisi kutokana na wafadhili kuchelewesha kutoa fedha na kwamba kwa sasa pia kuelekea 2012/2013 taarifa ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba shilingi 4,465,809,000/= ni *OC* pamoja na tafiti. Kwa wasiwasi huo basi naomba pia kwamba kwa kuwa fedha za maendeleo ambazo ni shilingi 2,124,733,000/= zinategemea kutoka kwa wahisani, hii ni wazi kwa Wizara hii tusitegemee mabadiliko. Hapa ndipo tunapoitaka Serikali kutilia mkazo na nguvu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kukidhi matumizi ya kawaida na tuweze kuwa na bakaa itakayosaidia katika shughuli za kimaendeleo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Celina O. Kombani kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposikiliza hotuba ya Wizara hii huwa na shauku kubwa ya ongezeko la mishahara ya wafanyakazi mbalimbali hasa kwa kuwa hali ya maisha imepanda sana. Je, ni kiasi gani mishahara imepanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa rushwa katika nchi yetu haijapungua hasa katika Jeshi la Polisi na Mahakama lakini hatuoni TAKUKURU ikichukua hatua. Hii inadhihirisha kuwa ama TAKUKURU mbinu za kupambana na rushwa hawazijui au wao wenyewe wamekuwa wala rushwa. Je, Serikali ina mikakati gani wa kuondoa aibu ya kuwa Taifa linalosifiwa kwa rushwa wakati TAKUKURU wapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri *TASAF* inafanya kazi nzuri ya kupeleka fedha za miradi iliyoibuliwa na wananchi lakini cha kushangaza ni kuwa miradi hiyo sio endelevu, mara tu baada ya *TASAF* kumaliza mchango wake haifuatilii kuona kuwa miradi hiyo inapambana na changamoto gani ili iweze kusaidia kukwamua, matokeo yake baadhi ya miradi ya *TASAF* hufa baada ya kuanzishwa. Naiomba Serikali ifanye tathimini ya kina ya *TASAF II* kabla ya *TASAF III* haijaanza ili kuepuka makosa yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, malengo ya Sekretarieti hii hayajafanikiwa sana kwa sababu taarifa za viongozi za kumiliki mali na madeni, hayako wazi, ripoti zao zinakuwa siri mno, yaani kati yao na Serikali tu. Hivyo kuna tuhuma kwa Serikali kuwalinda baadhi ya watumishi. Tunaishauri Serikali iziweke wazi taarifa hizo ili yeyote anayetaka kuziona, ili raia wema wasaidie kutoa taarifa sahihi kama ushahidi wa yaliyoandikwa. Tukifanya hivi, tutaondoa tatizo la wale wenye nia ya kudanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa Serikali, nchi maskini kama Tanzania inapaswa kuwa na mipango imara ya kupunguza matumizi kutoka na kuwa na vianzio vichache vya mapato. Hatua ya kwanza ni kupunguza na kuwa na Wizara chache zaidi kuliko ilivyo sasa na hili linawezekana. Kwa mfano Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ilikuwa sehemu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maliasili na Utalii lakini leo hii bajeti ya Wizara ya Mifugo inapunguzwa kila mwaka. Kwa hivyo, naishauri Serikali iunde Serikali ndogo yenye ufanisi.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu wananchi pamoja na Serikali inapiga kelele juu ya wafanyakazi hewa hali ambayo inasababisha fedha nyingi za Serikali kupotea kutokana na udanganyifu huo. Pia Serikali iliahidi kufanyia kazi suala hilo la wafanyakazi hewa. Ninachoomba kwa Serikali inipe maelezo, zoezi hili la kuwatambua wafanyakazi hewa limefika wapi? Ninataka nielewe wafanyakazi hewa kwa kila Wizara wapo wangapi na fedha kiasi gani zimepotea kutokana na kadhia hiyo? Je, marekebisho gani yamechukuliwa kuhusiana na suala hilo la wafanyakazi hewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekabiliwa na mfumuko wa bei kwa bidhaa mbalimbali kutokana na hali hiyo ule mshahara ulioongezwa mwaka 2011/2012, kwa mfumuko wa bei za bidhaa za hivi sasa, ongezeko hili la mshahara kwa mwaka 2011/2012 hauna maana sana. Je, Serikali inasemaje juu ya ongezeko la mishahara ya utumishi wa umma kwa mwaka

2012/2013? Ongezeko hili likoje? Je, litakidhi huu mfumuko wa bei unaotukabili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utumishi wa umma mbele ya wananchi hauna sura nzuri. Shughuli zote wananchi wanazozitaka kwa kupitia utumishi haziendi kwa haraka na ufanisi. Leo mwananchi anapohitaji huduma yoyote kwa taasisi za Serikali inachukuwa muda mrefu mno na wakati wengine huduma hiyo mwananchi hukosa kabisa, bado katika hospitali zetu baadhi ya wafanyakazi ni wenye jeuri. Ipo haja utumishi wa umma ujipange upya ili wawapatie wananchi utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la madai ya malimbikizo ya fedha kwa wafanyakazi likoje? Mbona Serikali haionekani kuwa iko makini katika kulimaliza tatizo hili? Serikali sasa inaahidi nini katika suala hili la madeni ya wafanyakazi ambao wanaidai Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina jumla ya Wauguzi wenye taaluma 30,000 na hawa wanachukua asilimia 60 ya watumishi wote wa afya. Wauguzi hawa ni Jeshi Kuu kwa sababu wao ndiyo walio karibu na mgonjwa wakitoa huduma kwa masaa 24 wakiachiana katika *shift* za asubuhi, mchana, na usiku. Wauguzi hawa kuanzia ngazi ya Hospitali ya Kitaifa – Rufaa, Hospitali za Mikoa na Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati hufanya kazi katika mazingira yasiyo rafiki. Hawana vitendea kazi, vichache walivyo navyo ni duni.

Wanafanya kazi bila madawa ya kutosha, Wauguzi hawa wanayo malalamiko mengi yanayohusiana na kwamba mishahara yao haitoshi, wana malimbikizo sugu ya madai mbalimbali kama vile posho ya likizo ya mwaka, posho ya uhamisho toka kituo kimoja hadi kingine na pengine si mara moja, posho ya matibabu, posho ya *uniform*, *On Call Allowances*, *promotions* hawapati, Wauguzi hawapewi nyumba lakini Madaktari ndiyo wanaopewa lakini ikumbukwe kabisa kwamba Madaktari bila Wauguzi hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa jambo la kufaa kama Wauguzi wangekuwa na Kurugenzi yao pale Wizarani (kama ilivyo kwa Madaktari) inayoongozwa na Mkurugenzi ambaye ni Muuguzi, ili malalamiko ya Wauguzi yafikishwe kwa Mkurugenzi Mkuu anayezifahamu *Nursing Ethics and Etiquettes,* anayefahamu Uuguzi na vitendea kazi sahihi wanavyohitaji Wauguzi, lakini pia wananchi wapate mahali pa kupeleka malalamiko yao dhidi ya Wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba cha Waziri, ukurasa 44, kifungu cha 8 kinasema kazi nyingine zitakazofanyika katika kipindi cha mwaka 2012/2013 ni pamoja na kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi. Naomba Serikali katika hili isikilize rufaa na malamiko ya Wauguzi na yatatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika ukurasa wa 55, kifungu cha 46, panaonyeshwa kiasi cha Sh. 3,781,100, 000,000 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia malipo ya mshahara, upandishwaji vyeo na kulipia

madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali na kwamba kiasi hicho kimepanda kufikia 510,807,000,000 (15.6%). Naomba katika kulipa gharama na madai mbalimbali, Wauguzi wapewe kipaumbele kama wenzao Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja 100%.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu wa maoni katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ijitahidi kuhamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii ili tujikomboe na umaskini na hivyo tuondokane na kuzitegemea nchi nyingine kutusaidia maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa 5, majowapo ya nchi washirika wa maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafaniko tuliyopata ni pamoja na Ethiopia, Misri, Malaysia na kadhalika. Eneo kubwa la Misri ni jangwa, lakini ni nchi mojawapo shiriki katika maendeleo yetu.  Tujifunze kutoka kwao, wao wanafanya nini kupata maendeleo yao. Tunafahamu kwamba Misri inategea sana umwagiliaji na sisi Watanzania tuyatumie maji tuliyo nayo kufanya

umwagiliaji ili tuzalishe zaidi na hivyo kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kiasi fulani imeshindwa kufanikisha majukumu yake. Nchi yetu bado iko juu kwa habari ya rushwa. Jeshi letu la Polisi bado linapokea rushwa ndogo ndogo. Baadhi ya Polisi wanapokea rushwa katika Jeshi hilo na TAKUKURU haijaweza kudhibiti utoaji na upokeaji wa rushwa hapa nchini. Napendekeza TAKUKURU ifumuliwe na watu wabadilishwe na kuwekwa wengine, kwa sababu TAKUKURU imeshindwa kuishauri Serikali namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu kusimamia vizuri kitengo cha mishahara ya watumishi wa Serikali ambapo kwa miaka mingi watumishi hewa wanalipwa mishahara. Duniani pote huu ni wakati ambapo shughuli za kiofisi hufanywa kwa *computer*. Napendekeza mfumo wa malipo/mishahara uwe *computerized* ili kuweza kudhibiti watumishi hewa kwa kuwaondoa waliosimamishwa, waliokufa na hivyo kutolipa mishahara hewa na uchunguzi ufanyike watakaobainika kulipa mishahara hewa washtakiwe Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza waliohusika kulipa shilingi bilioni hizo tisa (Sh.9 bilioni) ambazo ni mishahara hewa kwa watumishi hewa wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na napenda kusema kwamba siungi mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ilikuwa baada ya kusikiliza hoja nzito za Waheshimiwa Wabunge katika Wizara hizi mbili. Waheshimiwa Mawaziri wanatakiwa waanze kujibu na Waheshimiwa Mawaziri kwa mujibu wa Kanuni wakati wanawasilisha Hotuba zao, kila Waziri alitumia saa moja. Kwa hiyo na katika kujibu kila Wizara inatakiwa ipate saa moja.

Sasa jinsi walivyojigawa ilikuwa tuanze kumsikiliza Naibu Waziri wa Fedha, yeye atajibu hoja zinazohusu Tume ya Mipango. Halafu tunaye Mheshimiwa Mkuchika atajibu hoja zinazohusu Utawala Bora na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi naye atapatiwa muda. Sasa ilikuwa tumpe Naibu Waziri wa Fedha dakika 30 ama 25 na sasa tumebakiwa na dakika 25. Busara za Kiti changu zinaniambia kwamba ili tuweze kumaliza hoja hii leo jioni nitamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha achukue nafasi sasa aanze kujibu hizo hoja na nitatumia mamlaka ya kiti kuongeza dakika chache aweze kumalizia ili tutakapofika jioni tumpe nafasi moja kwa moja Waziri wa Utawala Bora. Akimaliza tumpe nafasi ya saa nzima Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na baada ya hapo tuingie kwenye mafungu. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Naibu wa Fedha halafu tutaendelea.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, pamoja na hayo yote nimepokea sahihisho la Hotuba kama

nilivyokuwa nimeagiza jana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na nadhani kwamba nakala hizo mtazipata kusudi twende sawasawa na msije mkafikiri hajawasilisha mezani sahihisho lake la Hotuba, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira iliyowasilishwa Bungeni kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Fungu 66 kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Spika kwa kifo cha Bibi yake mlezi. Aidha, natoa pole kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira kwa kifo cha Mama yake mzazi kilichotokea hivi karibuni. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutumia nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia hotuba hii kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Fungu 66 kwa mwaka 2012/2013, iliyosomwa tarehe 2 Julai, 2012. Napenda pia kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Wajumbe wa Kamati hiyo, Msemaji wa Kambi

ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba hiyo kwa kuzungumza na kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge kumi na mbili wamechangia ambapo Waheshimiwa Wabunge nane walichangia kwa kuzungumza na wanne kwa maaandishi. Napenda sasa kuwatambua Wabunge waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni; Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu na Mheshimiwa John Charles Mwijage.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole–Nangoro na Mheshimiwa Joelson Mpina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge katika mtiririko ufuatao: Hoja za Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa njia ya kuzungumza hapa Bungeni na zile zilitolewa kwa njia ya maandishi.

Nitataja hoja yenyewe pamoja na maelezo ya hoja yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chini ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka, Serikali ihakikishe miradi yote iliyopendekezwa na Tume ya Mipango kwenye Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2012/2013, inatekelezwa na Wizara husika kama ilivyopangwa. Maelezo ya hoja; Serikali imepokea ushauri huu, msingi wa kurejea utaratibu wa Mipango ya Maendeleo ya vipindi maalum ni nia ya dhati ya Serikali kuachana na mazoea na badala yake kuweka utaratibu mahususi wa kusimamia utekelezaji na uwajibikaji. Kwa msingi huu, baada ya bajeti ya maendeleo ya kila Wizara kuridhiwa na Bunge kila Wizara, Idara na Taasisi zimeagizwa kuandaa mpango kazi yaani *action plan* wa kutekeleza miradi ya maendeleo na baadaye kuandaa taarifa ya utekelezaji wake kwa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ifanyike kila baada ya miezi sita ya utekelezaji wa mipango. Maelezo ya hoja; ni kuwa Serikali imepokea ushauri wa Kamati, mpango wa maendeleo wa mwaka 2012/2013 umebainisha utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ambapo miradi ya Kitaifa ya kimkakati itafanyiwa ufuatiliaji na tathmini na Tume ya Mipango kushirikiana na Taasisi husika, miradi iliyo chini ya sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itafanyiwa ufuatiliaji na tathmini na Mamlaka husika pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na taarifa

zake kuwasilishwa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ishirikiane na Wizara ya Fedha kuweka vigezo vya mgao wa bajeti ya Serikali ya kila mwaka ili kuhakikisha kuwa vipaumbele vya Kitaifa na vya kimkakati vinatengewa fedha za kutosha. Majibu ni kuwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Fedha na Tume ya Mpango unazidi kuimarika na tutaendelea kuimarisha ushirikiano huo ikiwa ni pamoja na kuweka vigezo vya mgao wa bajeti ya Serikali kama inavyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa kutoa na kupata taarifa uboreshwe kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Ni kweli bado tuna changamoto katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali imechukua hatua za kuboresha na kuimarisha mfumo wa upatikaji na utoaji wa taarifa za kuboresha na kuimarisha mfumo wa upatikanaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kutoa mwongozo mahususi wa utayarishaji taarifa za utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Aidha, Sheria namba 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango inafanyiwa marekebisho ambapo vipengele vya utoaji na upatikanaji wa taarifa vitauhishwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitengo vya uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha vipewe jukumu la kutoa elimu juu ya miradi yote iliyoainishwa kutekelezwa kwa ubia na sekta binafsi katika mpango

wa maendeleo wa mwaka 2012/2013 pamoja na mipango yote iliyopo katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano. Jibu ni kuwa vitengo hivi vinawajibu huu na vimeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuelimisha wadau juu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Mkakati utekelezaji wa miradi ya ubia kwa ujumla ikiwa ni pamoja na miradi iliyobuniwa katika mpango wa 2012/2013 na ule wa miaka mitano. Aidha, kila Wizara na Taasisi zinazojitegemea na Wakala wa Serikali zimeteua maafisa wa dawati la *PPP*. Mkakati ni kuelimisha maofisa hawa ili wawe watoaji wa elimu hii kwa umma, utoaji wa elimu utaendelea kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iachane na Utamaduni uliozoeleka wa kufanya uhamisho wa fedha (*reallocations)* kutoka mafungu yenye fedha za miradi ya maendeleo pindi yanapojitokeza mahitaji ya fedha yaliyo nje ya bajeti ya Serikali na Bajeti ya maendeleo ilindwe. Jibu lake ni kwamba, wakati akiwasilisha hali ya Uchumi na mpango wa mwaka 2012/2013, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali tayari imefanya uamuzi wa kulinda yaani *ringfence,* fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango iangalie itakavyofanya kazi katika ngazi ya Wilaya, Mikoa hadi Taifa ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jibu lake ni kwamba, Tume ya Mipango kama kitovu cha mawazo rejea, *that is a think tank,* muundo wake ni mdogo na hivyo inafanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ili kuratibu

mipango katika ngazi za Halmashauri, Wilaya na Mikoa, juu ya bajeti ya Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha ili kazi zote za Tume pamoja na tafiti zikamilike kama ilivyopangwa. Jibu lake ni kwamba, bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013, imetengwa kulingana na hali halisi ya bajeti ya Serikali, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya Tume kulingana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja juu ya Watumishi wa Tume ya Mipango, Serikali ishughulikie kwa haraka maombi ya Tume ya kuongezewa Watumishi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Jibu la hoja hii ni kuwa, katika ikama ya watumishi ya mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango imeidhinishiwa ajira mpya za Watumishi 21. Aidha, Serikali itaendelea kuijengea uwezo Tume kulingana na bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu *programme* za kuwapatia mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Tume ziendelezwe kama ilivyopangwa. Ushauri huu utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni juu ya marekebisho ya Sheria namba 11 ya 1989, Tume ya Mipango ikamilishe haraka marekebisho ya Sheria inayounda Tume ili yaweze kuwasilishwa Bungeni mwaka wa fedha 2012/2013. Kama Hotuba iliyowasilishwa ilivyosema kazi ya kurekebisha Sheria

inaendelea na marekebisho haya yanatarajiwa kuwasilishwa katika Bunge la mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Bungeni Mheshimiwa Profesa Kahigi, hoja yenyewe inahusu Watumishi wa Tume ya Mipango, rasilimali watu katika Tume ya Mipango ni ndogo na haikidhi majukumu iliyopewa. Jibu ni kuwa, katika ikama ya watumishi ya mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango imeidhinishiwa ajira mpya za watumishi 21 aidha, Serikali itaendelea kuijengea uwezo Tume kulingana na bajeti itakavyoruhusu.

Kuhusiana na bajeti ya Tume, bajeti ya Tume ya Mipango ni ndogo na inazidi kupungua. Mfano, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa ni shilingi bilioni 8.0 na kwa mwaka 2012/2013, fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 8.0 ikiwa ni upungufu wa shilingi milioni 32. Maelezo ya hoja, bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013 imetengwa kulingana na hali halisi ya bajeti ya Serikali, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya Tume kulingana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zote zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tume ni fedha kutoka nje. Jibu la hoja ni kwamba, miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Wizara husika kwa mwaka 2012/2013, inagharimu kiasi cha shilingi trilioni mbili mia moja ishirini na nne milioni mia saba thelathini na tatu elfu fedha za nje. *UNDP* wanagharamia miradi miwili; Mradi wa *Pro Poor Growth* kwa trilioni moja milioni mia mbili na mradi wa *National Capacity Development* ni milioni mia nne tisini na tatu *point* tisa.

*UNFPA* wanagharamia mradi mmoja wa *Population Planning* shilingi milioni mia nne thelathini mia saba hamsini elfu na miradi hii yote inalenga kujenga uwezo wa Wizara katika kutekeleza majukumu ya msingi hususan katika maeneo ya usimamizi ya uchumi, kupambanua vigezo vya kuondoa umaskini na idadi ya watu. Hata hivyo, ushauri utazingatiwa kutenga fedha za ndani kwa shughuli za maendeleo ya Tume kadri ya uwezo wa Serikali utakavyoimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kuhusiana na mpango wa maendeleo, Tume ya Mipango chini ya Mwenyekiti wake ambaye ni Mheshimiwa Rais irekebishe dosari mbili zilizojitokeza kwa mwaka 2012/2013, ambazo ni mpango wa 2012/2013 ambao haukuzingatia kwa ukamilifu Mpango wa Taifa wa miaka mitano. Pili, bajeti ya mwaka 2012/2013, haikuzingatia viwango na mgawanyo wa fedha kwa mujibu wa mpango wa Taifa. Maelezo ya hoja hii ni Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013 ulikwishapitishwa na Bunge hili na hoja za mpango na bajeti zimezingatiwa wakati wa hitimisho la hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa mwaka 2012/2013, ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano. Vipaumbele vya Mpango wa mwaka 2012/2013 ni sawa na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ambavyo ni Miundombinu ambayo ni nishati ya umeme, barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege, TEHAMA, kilimo, viwanda, biashara na utalii na maendeleo ya rasilimali watu. Mpango wa mwaka 2012/2013 ni wa mwaka

mmoja, hivyo itakuwa vigumu kwake kuweza kuzingatia yote yaliyopangwa katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, dhamira ya Serikali ya kuongeza kiwango cha bajeti ya maendeleo itaendelea kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina la mtoa hoja lilikuwa Mheshimiwa John John Mnyika; hoja yenyewe ilikuwa Mpango wa mwaka wa Maendeleo unakinzana na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano mfano, Mpango wa mwaka hauoneshi kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mradi wa maji na barabara za pembezoni za Dar es Salaam kama ilivyoainishwa katika Mpango wa miaka mitano. Maelezo ya hoja ni kwamba, kama ilivyofafanuliwa wakati wa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013, katika Jiji la Dar es Salaam ikiwemo Jimbo la Ubungo limetengewa shilingi bilioni 118.4 ikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 68.8, fedha za nje kwa ajili ya mradi wa maji wa Ruvu Juu na Ruvu Chini, shilingi bilioni moja, fedha za ndani na shilingi bilioni 29.9, fedha za nje kwa ajili ya Mradi wa Maji Kimbiji na Mpera na shilingi bilioni 3.3.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali naomba uketi kusudu tufuate taratibu za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, halafu utaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Sawa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni namba 28(1) mpaka (7) hivi zinahusu muda wa vikao vya Bunge na Kanuni namba 28(2) ndiyo inahusu hasa muda wa vikao vya Bunge kwa kipindi hiki cha asubuhi. Kama nilivyosema napenda kumuacha Mheshimiwa Naibu Waziri amalize kazi yake yote Asubuhi hii lakini muda hauturuhusu na ili tuweze kuruhusiwa na muda ni lazima sasa nimuite Waziri na nitamwomba Kaimu Waziri wa Nchi, Bunge aweze kutoa hoja ya kutufanya tuweze kuongeza muda sasa toka saa saba hii mpaka pale Mheshimiwa Naibu Waziri atakapokuwa amemaliza maelezo yake ili tutakapokuja jioni tuweze kuendelea na mambo mengine, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (2) naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kuongeza muda tuendelee kumsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka pale atakapokamilisha hoja yake zaidi ya saa saba kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa idadi inayotakiwa kwa mujibu wa kanuni, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki kwamba muda huu wa Bunge usisitishwe saa saba bali uongezwe, tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri apate kutoa maelezo ya Wizara yake mpaka pale atakapokuwa amemaliza.

Basi wale wote wanaoafiki waseme ndiyo na wasioafiki waseme siyo, wasioafiki wameshindwa, walioafiki wameshinda. Kwa hiyo naongeza muda huo na nampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri aendelee na hoja yake kwa dakika thelathini nilizokuwa nimempangia.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa kwenye hoja ya Mheshimiwa John John Mnyika na nilikuwa niko katikati ya maelezo ya hoja kuhusiana na bajeti zilizowekwa kwa ajili ya mradi wa maji, naomba niirudie tu yote, kama ilivyofafanuliwa wakati wa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo mwaka 2012/2013, katika Jiji la Dar es Salaam likiwemo Jimbo la Ubungo limetengewa shilingi bilioni 118.4 ikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 68.8; fedha za nje kwa ajili ya mradi wa maji wa Ruvu Juu na Ruvu Chini, shilingi bilioni moja, fedha za ndani ni shilingi bilioni 29.9 na fedha za nje kwa ajili ya mradi wa Kimbiji na Mpera ni shilingi bilioni 3.3, fedha za ndani na shilingi bilioni 1.8, fedha za nje kwa ajili ya mradi wa bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni Mbunge alizungumzia Tume ya Mipango ifike Vijijini. Maelezo ya hoja; Tume ya Mipango kama kitovu cha mawazo rejea yaani *think-tank,* muundo wake ni mdogo na hivyo inafanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuratibu mipango katika Halmashauri Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alizungumzia vitabu vya Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano vinavyozingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la hoja ni kuwa Kitabu cha Mpango, Toleo la Juni 2012 kinachozingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kimekamilika na Waheshimiwa Wabunge watagawiwa nakala katika Mkutano huu wa Bunge. Aliongezea pia kuwa Tume ya Mipango iliahidi kuishauri Serikali kupunguza matumizi yake, kwa nini matumizi ya Serikali yanazidi kuongezeka? Jibu la hoja hii ni kuwa, kwa kuwa Serikali imejikita katika kutekeleza miradi ya Kitaifa ya kimkakati na ile muhimu kwa ukuaji wa uchumi, matumizi ya kawaida hayawezi kukwepeka kwa kuwa, baada ya uwekezaji kutahitajika gharama kwa ajili kuendeleza uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imeanza kuchukua hatua katika kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na yasiyo na tija. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 68 aya ya 111 Serikali imeainisha maeneo ambayo tunaweza kuanza katika kupunguza matumizi hasa katika magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Mpina ni kwa nini fedha za sekta binafsi na wafadhili hazijaoneshwa kwenye Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa 2012/2013? Maelezo ya hoja ni kuwa, Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013, kimeonesha fedha za wafadhili na

sekta binafsi. Mfano, katika miradi ya Miundombinu, Bandari na Uchukuzi; kuna miradi kama ya ujenzi wa Kituo cha Uchukuzi na Biashara Kurasini *that is Kurasini Trade and Logistic Habour* ambacho kuna shilingi bilioni 640 kutoka kwa mwekezaji binafsi kutoka China. Vile vile Kituo cha Uchukuzi wa Mizigo Kisarawe na ujenzi wa Bandari ya Mtwara kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa 2012/2013, Sura ya Tatu. Aidha, mpango pia umeonesha fedha za wafadhili katika sura hiyo hiyo kama vile miradi ya umeme ya Kinyerezi na mtambo wa umeme wa Hale ambao unafadhiliwa na *SIDA* ya Sweden.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu alitoa hoja kuwa Tume ya Mipango ione jinsi ya kuwa na pendekezo la vigezo vya mgawanyo wa rasilimali katika bajeti ili kusiwepo tofauti kubwa sana kati ya Wizara, Sekta na sekta na baina ya maeneo. Maelezo ya hoja hii ni kama ifuatavyo: Ugawaji wa bajeti na tofauti ya bajeti kati ya sekta moja na nyingine inategemea zaidi mahitaji ya sekta husika. Hivyo, ni vigumu kuwa *ratio* kati ya sekta kutegemeana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole- Nangoro na yeye alitoa hoja hiyo hiyo na kwa hali hiyo, jibu ni hilohilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Charles Mwijage alitoa hoja kuwa yanayofanyika katika kituo cha majaribio cha kilimo kwa msaada wa Wachina yapelekwe pia Karagwe. Suala hili linatakiwa

kufanyiwa uchambuzi ili kukuza uhalisia wake, Tume itaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika kutafakari pendekezo hili kwa lengo la kuboresha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi.

Mtoa hoja alikuwa Mheshimiwa John John Mnyika na hoja yenyewe ilikuwa mpango elekezi wa miaka 15 uwasilishwe Bungeni kuthibitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 (2) na (3) ili kuwezesha Bunge kusimamia Serikali na kuhakikisha utekelezaji wake. Maelezo ya hoja hiyo ni kwamba, mpango elekezi wa miaka 15 tayari umeridhiwa na Kamati ya Fedha na Uchumi kwa niaba ya Bunge wakati wa kikao cha Juni, 2012. Kamati ya Fedha na Uchumi ilielekeza Tume kuchapa mpango elekezi na kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa John John Mnyika alitoa hoja kwamba, Tume ya Mipango itoe maelezo kwa nini mfumo wa kuandaa mpango 2012/2013 haukukamilika mwezi Februari, 2012 na mpango wa mwaka ukaandaliwa mwezi Aprili kama Kanuni za Kudumu za Bunge zinavyohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya hoja hii ni kuwa, Bunge lilipitisha, Serikali ilete Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka 2012/2013 mwezi Aprili. Hata hivyo, baada ya kupitia utaratibu huo ilipendekezwa kuwa turejee katika utaratibu wa kuwasilisha

mapendekezo ya mpango wa mwaka mwezi Februari kila mwaka kama Kanuni ya Bunge inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Godfrey Zambi alitoa hoja kuwa mipango mingi inayopangwa na Tume ya Mipango haieleweki kwa Watanzania ndiyo sababu hata utekelezaji wake huwa ni mgumu sana. Maelezo ya hoja ni kwamba, Tume ya Mipango imekuwa ikitoa elimu juu ya mipango mbalimbali ya nchi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa semina juu ya mipango hiyo kwa Wakuu wa Wilaya, Mikoa pamoja na Maafisa Tawala wa Wilaya na Mikoa kwa lengo la kujenga uelewa wa mipango ya nchi. Vilevile Tume ya Mipango imekuwa ikitumia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo vipindi vya runinga, redio, magazetini na tovuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kutoka kwa Mheshimiwa Zambi ni kuhusu vipeperushi vilivyochapishwa kwa lugha ya Kiingereza ni kwa faida ya nani? Maelezo ya hoja ni kama ifuatavyo: Tume ya Mipango ilichapisha vipeperushi kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa lengo la kuelimisha makundi mbalimbali ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Zambi ni kwamba, vipaumbele vya Kitaifa viko lukuki hivyo kusababisha fedha kidogo za maendeleo kutawanywa katika maeneo mengi sana ambako matokeo yake yaani *impact* kwa maendeleo ni ndogo, Tume iishauri Serikali kuja na vipaumbele vichahche kama vile Miundombinu, Maji, Nishati, Kilimo na Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya hoja ni kuwa, vipaumbele vya Mpango vipo vitano ambavyo ni uwekezaji mkubwa katika Miundombinu, Nishati, Usafirishaji, TEHAMA, maji safi, maji taka na umwagiliaji, kilimo ili kuweza kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada nje ya nchi, maendeleo ya viwanda hasa vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini, maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi hasa katika Sayansi na Teknolojia na Ubunifu, uendelezaji wa huduma za utalii biashara na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole- Nangoro alitoa hoja kuwa Tume ya Mipango itoe mapendekezo ya kuunda *Budget Endowment Fund,* Mfuko uanze na jumla ya shilingi trilioni 25 mpaka thelathini. Maelezo ya hoja ni kuwa wazo hili litazingatiwa na litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Tume ya Mipango inathamini na inaahidi kuyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nawaomba na kuwahimiza waendelee kuishauri Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Oo oh! kuunga mkono hoja, wameniandikia vibaya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaanza kuunga mkono halafu unatoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Naunga mkono hoja na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo anatoa hoja kwa niaba ya Waziri wa Mipango. Yuko sahihi kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Niaba ya Waziri wa Mipango ametajwa kwenye hotuba hii. Alitajwa kwenye *order paper.* Kwa hiyo, lazima atoe hoja naomba, uje uje utoe hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira naunga mkono hoja na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kama mnavyokumbuka kwamba hotuba zilizosomwa hapa Mheshimiwa Mkuchika alisoma Hotuba ya Uhusiano na Uratibu kwa niaba ya Mheshimiwa Stephen Wasira kwa hiyo leo hoja hiyo imejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa George Mkuchika yeye hatatoa hoja kwa sababu hotuba yake iko ndani ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi. Kwa hiyo, hapa mlitaka kum–*mislead*. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru kuwa una uelewa mkubwa na umeshazoea kanuni za Bunge. Nilikuwa napokea

maelezo hapa kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri wawili kama nilivyosema hoja hizi mbili zilituchukua saa moja katika kuziwasilisha kila mmoja na katika kuzihitimisha inatakiwa tutumie masaa mawili pia kwa mujibu wa utaratibu ambao Serikali imejiwekea. Tayari Mheshimiwa Naibu Waziri ameshatumia nusu saa, tutakaporudi jioni Mheshimiwa Mkuchika naye atatumia nusu saa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini tutampa nafasi Mheshimiwa Celina Kombani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yeye atatumia saa nzima kusudi aweze kufafanua hayo masuala yote ya Utumishi wa Umma ipasavyo ili Watanzania wote wapate nafasi ya kusikia na kuelewa vizuri. Kwa hiyo, baada ya kumaliza hiyo saa moja na nusu Bunge litaingia kwenye Kamati na tutaweza kupitisha hotuba hiyo na mafungu hayo, kifungu kwa kifungu kadri itavyokuwa inaonekana ili tuweze kuhitimisha hoja hiyo leo.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumerudi katika kipindi cha jioni, tunaendelea na Mkutano wetu wa Nane na Kikao hiki cha Kumi na Tano lakini kwa heshima na taadhima naomba nitambue uwepo wa

Waziri Mkuu. Kwa takriban siku kama mbili alikuwa anaendelea na kazi nyingine nje ya ukumbi huu wa Bunge, lakini jioni hii amerejea na tupo naye.

Waheshimiwa Wabunge niliwapa Mwongozo mchana kabla sijasitisha shughuli hizi, niliwaambia tukirejea jioni hii tutampa Waziri wa Nchi, Utawala Bora dakika thelathini ili naye achangie hoja ambayo ilikuwa imewekwa mezani na baadaye tutampa nafasi mtoa hoja kwa saa moja aweze kuhitimisha hoja yake.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Gorge Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kuchangia kama ulivyosema hoja iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) ndani yake yakiwemo masuala ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kusema hapa Bungeni, nizungumze na Watanzania wenzangu juu ya mustakabali wa nchi yetu, juu ya masuala ya utawala bora katika nchi yetu, ambayo Rais amenipanga nimsaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, napenda kumshukuru Ndugu yangu Profesa kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Nataka pia niwashukuru pia wale wote waliochangia Bungeni

kwa hotuba na wale ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Celina Kombani mtoa hoja atawatambua kwa majina wale wote ambao wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema kwamba, nasimama hapa nikiwa na fahari kwamba Bara letu la Afrika miongoni mwa nchi ambazo zinazingatia utawala bora ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kuorodhesha mambo mengi yanayoonesha jinsi tulivyo makini katika utawala bora, mambo ambayo hayapo katika nchi zingine. Lakini niseme machache kwa mfano, Katiba yetu inatutaka tufanye uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kila baada ya miaka mitano, ni nchi hii tangu enzi ya Baba wa Taifa hatujawahi kuahirisha uchaguzi mwaka wowote, kila baada ya miaka mitano tunafanya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hii tunaheshimu mihimili mitatu, Serikali, Bunge na Mahakama. Imo ndani ya Katiba na tumeendelea kufanya hivyo na Watanzania ni mashahidi, Serikali yenu inavyoheshimu mgawanyo wa madaraka, jinsi inavyoheshimu shughuli za Bunge, jinsi inavyoheshimu na kutekeleza maagizo ya Mahakama, huo ndio utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika nchi yetu hii tumekubaliana kurudi katika mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, nadhani Watanzania wanashuhudia ni jinsi gani ambavyo watu wana uhuru wa kuingia katika Vyama wanavyovitaka, kusema wanavyotaka ili mradi hawavunji sheria. ila wengine unawashuhudia wanavyovunja sheria, wanavyovuka mipaka, wanavyosema maneno ambayo hata wakati mwingine ukifikiria haingii katika akili. Lakini mnaona ni jinsi gani nchi yetu ambavyo ina uhuru wa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Waziri wa Habari, Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na vyombo vingi vya habari. Nchi nyingine ni vyombo vitatu ama vinne, tena vinadhibitiwa na Serikali, lakini Tanzania anayetaka gazeti la mpira haya, anayetaka gazeti la sinema haya, gazeti la siasa haya, tuna magazeti ya kila aina na mnaandika mnavyotaka na mnavumiliwa kweli! Sijapata kuona nchi ambayo ina uhuru wa kuandika mambo, ningekuja hapa na magazeti nikaonesha mngelisema kwamba kweli Serikali ya CCM ina uvumilivu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani Bungeni tumeshuhudia kwamba kila mwaka tunakutana hapa kujadili taarifa ya *Controller and Auditor General*. Rais ndiye aliyekuwa anapelekewa siku za nyuma, lakini Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ndiye aliyeagiza kwamba kuanzia sasa naagiza taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ipelekwe Bungeni ili Wabunge waijadili na wananchi wajue nchi yao inavyokwenda. Huu ndiyo utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, hapa ndani ya Bunge moja katika sifa ya nchi inayozingatia utawala bora ni kuruhusu zile Kamati zinazoshughulikia mambo ya Fedha kuongozwa na Wapinzani, Wabunge wa CCM wapo wengi humu ndani tungesema kwamba Cheyo asiwe Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali tungefanya hivyo, lakini tumesema hapana, waachieni Wapinzani waongoze hizi Kamati. Mheshimiwa Zitto Kabwe anaongoza Kamati ya Mashirika ya Umma, Kaka yangu Mrema pale wakati mwingine namuita mwanangu maana mtoto wangu mwingine anaitwa Augustino wakati mwingine namuita baba, yeye anaongoza Kamati ya Serikali za Mitaa, *all the oversight Committees* zinaongozwa na *Opposition*. Mko wachache hivi tuwapeni nini zaidi ya hapo, sisi tunakaa tunawasikilizeni, mnatuongoza. Huo ndiyo utawala bora.

Mheshimwia Mwenyekiti, tuna uhuru wa kuabudu, tuna uhuru tunapenda tunavyotaka, ndani humu kuna watu wanaopenda Simba, wanaopenda Yanga, ndivyo tunavyoishi. Kwa hiyo, nasema utawala bora ndiyo kigezo kikubwa tunachozingatia katika Serikali ya CCM kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Ofisi ya Rais, Utawala Bora ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inatawaliwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Kama wapo watu ama wanakuwa barabarani ama kwenye majukwaa wanasema wanataka wafanye mambo kuhakikisha kwamba Tanzania haitawaliki, hawa hawaitakii mema nchi hii, watu wanaoitakia

mema nchi hii ni wale ambao wanataka Tanzania pawe mahali pazuri pa kuishi na mahali pa amani. Anayetaka kumwaga sera za *CUF* amwage, sera za CCM, Sera za CHADEMA, *NCCR* amwage, huo ndiyo utawala bora, *Political tolerance* (kuvumiliana).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba aliyoitoa juzi, mwisho wa mwezi maana naogopa nisije nikasahau mambo yapo mengi. Napenda nichukue nafasi hii pia niwapongeze sana ndugu zangu Madaktari ambao kwa wingi wamerejea kazini jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani kama mtu unataka kujitafutia umaarufu kwa watu kufa basi mtu wa namna hiyo tumwogope kama tunavyoogopa ukoma au kama tunavyoogopa UKIMWI. Hatuwezi watu kujitafutia umaarufu wakati watu wanakufa, *we can't accept that!* Kwa hiyo, nawapongeza Madaktari waliorudi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma magazeti hayo hayo, gazeti lingine linatoa takwimu jinsi gani Madaktari Muhimbili walivyorudi kwa wingi, gazeti lingine linasema *Aluta continua*! Ndiyo hao tunaowasema. Kwa hiyo, nakumbusha kwamba Serikali yetu inaheshimu uhuru wa sheria na kwa mujibu wa mgawanyo huu, sisi Bunge tunatunga sheria, mwenye mamlaka ya kutafsiri sheria ni Mahakama, ndiyo maana Mahakama ikisema jamani uamuzi ni huu, Serikali tunaheshimu. Sasa kama vile Serikali tunavyoheshimu tunaomba na Watanzania wengine

wote waheshimu maamuzi ya Mahakama. Haiwezekani Mahakama ikasema hakuna mgomo, mgomo ni batili, *stop this*, halafu watu wanakwenda kinyume na Mahakama. Halafu na wewe Mwanasiasa kwa kujitafutia umaarufu unakwenda kuwaunga mkono watu wanaopinga amri ya Mahakama, mnaipeleka wapi nchi hii jamani! Sivyo alivyotulea Nyerere. Tulikotoka haya mambo hatukuwa nayo, tunaona mambo ya ajabu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nawapongeza Madaktari, wakati Watanzania wanateseka mahospitalini, liwe ni jambo la aibu kwa mtu yeyote, kikundi au Chama cha Siasa au *NGO's* yeyote, kushabikia mgomo wa Madaktari. Naomba tuungane na Serikali yetu kumaliza tatizo hili ili kuokoa maisha ya Watanzania wasio na hatia wanaokufa. Nawaomba Watanzania wote kama nilivyosema wale wanaoshabikia mambo haya tuwaogope kama vile tunavyoogopa ugonjwa wa ukoma au kama tunavyoogopa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kurejea baadhi ya mambo ambayo yametajwa humu ndani, yapo mengi siwezi kuyamaliza yote, lakini katika yale maeneo ambayo namsaidia Rais kuyaongoza nitapenda kuyasemea. Kwa upande wa Utawala Bora napenda kupokea pongezi za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, zilizotolewa na Kamati kwa Serikali kujiunga na Mpango wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Shughuli za Kiserikali *Open Government Partnership*. Kwa niaba ya Serikali nimepokea ushauri, Serikali inaahidi

kutekeleza mpango huu kwa makini. Upande wa Kambi ya Upinzani, Msemaji anasema wake za Marais kuwa na taasisi binafsi, hiyo ni hoja kwamba, inakuwaje wanakuwa na taasisi binafsi kila anayekuja anakuwa na taasisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake ni kwamba, kuundwa kwa Taasisi hizi ni uamuzi wa hiari wa wake za Marais. Kila mmoja anajishughulisha na shughuli za kimaendeleo walizoamua kujishughulisha nazo na wakati mwingine ambazo wana-*profession* nazo. Huwezi kwenda kuanzisha taasisi ya Uhandisi wewe mwenyewe wala hujui Uhandisi. Pamoja na mambo mengine Mama Anna Mkapa alijikita zaidi katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Mama Salma Kikwete amejikita katika kuwawezesha watoto wa kike kupata elimu ili wajenge msingi imara wa kujiendeleza. Mpaka sasa *WAMA* wamejenga shule ya Sekondari ya wasichana kule Nyamisati, Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sishangai dada yangu Mama Kikwete kuanzisha *WAMA* na kushughulika na mambo ya shule, maana ni Mwalimu by *Profession*. Ndiyo maana unaposema ulazimishe kila mke wa Rais basi wawe na *NGO* moja, wawe wanapokezana, kwanza *NGO* maana yake ni jambo la hiari, sasa huwezi ukasema ili mradi wewe ni mke wa Rais utashughulika na hili. Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba, wake wa Marais wana uhuru wa kuamua shughuli gani wanayoifanya, taasisi hizi ni shughuli binafsi wala haziendani na bajeti ya Serikali na ndiyo

maana hapa hatujawahi kuja Bungeni kuomba fedha za *EOTF* wala *WAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la udini, ukabila na ukanda kuingizwa kwenye siasa, Serikali itoe tamko kukemea hali hii. Nadhani udini, ukabila, ukanda ni masuala yanayopigwa vita na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Serikali yetu haina dini tumesema, bali watu wake wana dini. Tumezungumza hapa awali uhuru wa kuabudu, kwa kuzingatia hali hiyo, Idara ya Mahusiano ina utaratibu wa kukutana na Taasisi za Dini mara kwa mara na nchi yetu ni nzuri, lipo jopo la Mashekhe, Maaskofu na Viongozi wa Dini mbalimbali wanakutana mara kwa mara kuzungumzia amani ya nchi yetu, kuzungumzia uhuru wa kuabudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kusema kwamba udini ukiwepo mahali au ubaguzi ukiwepo mahali, husemi kwamba hapa kuna ubaguzi, wale walioona, wale wanaoona, wale wenye macho, wale wanaokuhesabuni jinsi mlivyojipanga ndiyo wanaojua kwamba hapa kuna tatizo. Kwa hiyo, wakati mwingine kuona tatizo wala siyo lazima useme mimi mkabila, mimi ni mdini, hapana! Yale matendo unayoyafanya, unavyojipanga katika *group* lako ndiyo inayofanya watu wakutilie mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inasema baadhi ya viongozi kufanya kazi kwa msingi wa kisiasa. Suala hili tumesema kwamba taasisi ya uongozi inatambua umuhimu wa maadili kama sehemu muhimu ya uongozi, mwongozo wa kuimarisha uwezo *Leadership Development Framework* ambao unalenga

kumjenga kiongozi kwa ujumla wake ndiyo unaoongoza mchakato wa kubuni na kutengeneza programu za kozi na mafunzo ya mbinu za kuzitoa au kuzifundisha. Mwongozo huu unatambua kuwa uwezo wa kiongozi unajumuisha maarifa, ujuzi, maadili na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari programu zinazohusisha moja kwa moja mafunzo yanayolenga kumjenga Kiongozi kimaadili zimekamilika na mafunzo yatatolewa katika mwaka huu 2012/2013. Kwa hiyo, Serikali inaikubali hiyo hoja na ndiyo maana tunaangalia hayo. Serikali itaendelea kuboresha huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengine nafikiri hawa niwachanganye, Ndugu yangu Mbilinyi, Mheshimiwa Rashid Ali, hawa wamezungumza habari ya kutekwa kwa Daktari Ulimboka, mambo ya vitisho na nini. Unajua kurudia mambo yale yale yaliyokwishasemwa wakati mwingine tunapoteza muda. Serikali ilikwishatoa tamko la kulaani kwa nguvu zake zote, kitendo cha kutekwa na kuumizwa Daktari Ulimboka. Vile vile vyombo vya usalama vimeunda Tume ya Kuchunguza tukio hili. Matokeo ya uchunguzi huo yanatakiwa haraka ili wahusika wachukuliwe hatua. Hakuna haja ya kuundwa kwa Tume ya Bunge kwani itakuwa ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali kufanya kazi ambayo tayari inafanyika. Hapa nataka niseme Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alisema Tume huru ya Bunge iundwe kuchunguza suala hili kwa sababu Serikali haiaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani alisema Serikali haiaminiki! Hivi mwaka 2010 hatukwenda kwenye kura, tukaomba kura, ni nani walipewa kibali cha kuunda Serikali? Hivi kuaminika ndani ya nchi si kigezo chake ni kura? Mlipata kura ngapi mnaosema hivyo? Naomba jambo ambalo lilishatolewa ufafanuzi lipo bayana tusiende mbele halafu tunarudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah anasema Rais aingie mkataba na Mawaziri wake ili kuimarisha uwajibikaji na utendaji. Rais anafanya kazi kwa ukaribu sana na Mawaziri wake, Mawaziri zaidi ya kuwepo kwa mkataba kuna mawasiliano ya mpango wa bajeti hii, haya tunayoyaleta hapa Bungeni yamepita kwenye Baraza la Mawaziri na Rais anapotosheka kwamba huyu hafanyi vile ninavyomkusudia anambadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze inajipangaje kuhusu utawala bora hasa uwajibikaji, uwazi wa Serikali na ushirikishwaji wa wananchi. Haya mambo tumeyaeleza kwamba ni kweli utawala bora ni nguzo muhimu katika uongozi na uendeshaji wa nchi, nchi yetu tangu uhuru imekuwa ikiongozwa na kuzingatia misingi ya utawala bora na pale nilipoanza mwanzoni kusema nimeeleza ni jinsi gani tunazingatia utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu hapa Rajab Mbarouk Mohamed kutoka Baraza la Wawakilishi anasema Serikali kuendelea kusifia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wakati wananchi walio wengi hawautaki kwani hauzingatii utawala bora.

Nimemsikitia kweli ndugu yangu, maana mimi najiuliza kama si Muungano angekuwa humu ndani saa hizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichomtoa mtu kutoka Pemba unakuja Bungeni Dodoma ni Muungano, umo ndani ya Muungano. Nataka ku-*declare interest*, mimi na Muungano damu damu. Nilimwona Mzee Nyerere, nilimwona Mzee Jumbe, wakati wanaanzisha Muungano nilikuwa *TANU Youth League* madhubuti na sasa naendelea kuwa Mzee shupavu wa CCM. Naunga mkono Muungano.

Nataka nikukatalie kabisa, labda pengine ulimi uliteleza, hivi kusema kwamba watu wengi hawautaki Muungano, siamini. Nchi hii nimetembea mikoa yote, kituo changu cha mwisho ilikuwa Sumbawanga, Rukwa. *Guest* moja kule Ikola Karema, Ziwa Tanganyika inamilikiwa na Mpemba, ametoka Pemba anafanya biashara Ikola, Mtwara wapo wanafanya biashara ya mbao wanapeleka Zanzibar, wananunua njugu wanapeleka Zanzibar. Nafikiri wenzetu ndiyo mngesema loh! *Alhamdulillah* Muungano tunaufaidi, hivi Wamakonde wangapi wanafanya biashara Pemba? (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mwambie huyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu umeyasema maneno haya muda muafaka, una watu wa kuwahamasisha kuukataa Muungano, nenda kawahamasishe, kuna Tume inazunguka. Lakini nataka

nikuhakikishie *Wallah* wale watakaokataa Muungano hata mmoja kwa mia hawafiki. Nchi hii watu wanautaka Muungano.

**MBUNGE FULANI:** Watajuta!

**MWENYEKITI:** *Order* tafadhali, Mwacheni Waziri aendelee na kujibu hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa wewe huupendi Muungano unaruhusiwa kupeleka maoni yako kwenye Tume ya Katiba ingawa sera ya chama chako CHADEMA inataka Muungano wa Serikali tatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri huyo ni Mbunge wa Chama cha *CUF* siyo CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumradhi, Ndugu zangu wa CHADEMA kumradhi. Nakusudia kusema kwamba tumemsikia Katibu Mkuu Maalim Seif na Uongozi wa *CUF*, Sera ya *CUF* Muungano wa Serikali Tatu. Sasa anapokuja Mbunge wa CHADEMA anasema Muungano hautaki mimi nakushangaeni. Sasa ilikuja hapa hoja inayohusu Usalama wa Taifa. Mimi nataka kusema hivi, sisi tuna haki kujua kinachoendelea katika nchi yetu. Lakini kuna mambo mengine ukitaka kuyasemea lazima uwe una uhakika nayo. Mimi nimemshiba Mao Tse-Tung, nimemsoma vizuri sana, anasema: "*No research no right to speak*". Watu mmezungumza habari ya Usalama wa Taifa hapa, wengine wakienda wakaandika na makala, sijui

uvunjwe vunjwe, ukarabatiwe! Hivi unaweza kuagiza kukarabati jambo ambalo ndani kinachofanyika kila siku hukijui? He, jamani, hee! Ndugu zanguni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushukuru kwamba chombo hiki unapozungumza usalama wa nchi hii tangu mwaka 1961 mpaka leo, na Zanzibar mwaka 1964 mpaka leo, waliotusaidia kufika hapa katika vyombo vya Ulinzi na Usalama; tulivyo ni pamoja na Usalama wa Taifa wa Nchi hii. Mnazungumza habari, hamjasikia Usalama wa Taifa umekwenda kumkamata mtu, kazi yao ni kupeleleza, kutoa taarifa, kutoa tahadhari. Siyo kazi ya Usalama wa Taifa kwenda kumkamata mhalifu, hiyo ni kazi ya watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wahamiaji Haramu Mheshimiwa Rais amelitolea maelezo juzi kwamba, kwa sababu vyombo vyetu hivi viko madhubuti, ndiyo wahamiaji haramu wameamua sasa kupitapita porini, wanavikimbia vyombo vya usalama. Sasa hoja ambazo zilikuwa zimetolewa nyingi, siyo nyingi sana za kwenye masuala haya ya usalama, lakini walikuwa wanasema tu kwamba, ahaa, kama vyombo vyetu viko imara, mbona uhalifu unatokea? Hivi kama hoja ni hiyo, hivi kuna mahali kuna vyombo imara kama Marekani? Osama hajakwenda kuvunja ile *World Trade Centre* katikati ya Mji? He, Jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zinazohusu masuala ya TAKUKURU ziko nyingi. Lakini la kusema tu kwa kifupi,

maana naona na muda umekwisha, yale makofi utaniongezea dakika mbili. Naona muda umekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU tufuatilia maeneo yote yenye harufu yanayojihusisha na rushwa. Nasema maelezo haya ya nini? Tumefanya katika kesi mbalimbali, yako wazi, hapa tumeyachapa, tutawapa Wabunge. Nasema muda niliopewa ni mfupi, lakini moja nilifafanue. Moja, mmesema, mbona TAKUKURU kesi wanazopeleleza ni nyingi, walizopeleka Mahakamani kidogo? Lakini walizoshinda, ni kidogo. Ndiyo utawala bora huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa TAKUKURU wanapeleka kesi Mahakamani, akaamua na yeye, huo siyo utawala bora. TAKUKURU anapeleleza. Kwanza TAKUKURU anapokea kesi nyingi, watu wengi wanapeleka, baadaye wanaangalia, hivi hapa ni ugomvi wa mtu na mtu, au kuna kesi ya kujibu? Tayari zinapungua. Wakishakamilisha upelelezi, ndiyo zinakwenda Mahakamani. Sasa anayeamua kwamba kesi hii sasa iwe mwisho, siyo TAKUKURU. Ni chombo kinachoitwa Mahakama *(Rule of Law),* chombo cha kuheshimiwa katika mihimili mitatu. Kwa hiyo, ukikaa unauliza: Mbona TAKUKURU hamalizi kesi? Unamwonea TAKUKURU. Sasa yameulizwa hapa, jitihada za dhati hazijaonekana kushughulikiwa watumishi wa umma waliotajwa kwenye orodha ya mafisadi, waliohusika na kashfa za KAGODA, Meremeta, *Richmond* na *IPTL*. Maelezo yapo, uchunguzi wa *deep green* ulianza mwaka 2007, siyo miaka 10 iliyopita. Uchunguzi huu umechukua muda mrefu kwa sababu unahusisha nchi za Afrika Kusini, Mauritius ambako bado taarifa muhimu

zinahitajika kutoka nchi hizi. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 13 ziliokolewa kwa kuzuiliwa Benki kutokana na uchunguzi huo.

Suala la Meremeta lilikwishatolewa maelezo na Waziri Mkuu na jambo akishalizungumza mkubwa, wewe mdogo una ubavu gani tena wa kulisema? Suala la *Richmond* tumelizungumza hapa Bunge, tumelimaliza hapa kwenye Bunge. KAGODA kwa sasa uchunguzi unafanywa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini akiwa na timu ya Wajumbe kutoka Polisi na Usalama wa Taifa. Kuhusu *IPTL,* uchunguzi wa tuhuma hii ulihamishiwa Jeshi la Polisi kuendelea na uchunguzi baada ya TAKUKURU kukamilika uchunguzi wake.

Imetokea hoja hapa, Mbunge mmoja anasema Bunge kuhusishwa na vitendo vya rushwa, TAKUKURU ihakikishe kuwa pamoja na kuwakamata watuhumiwa wengine, iendelee kuchukua hatua kulisafirisha jina la Bunge katika kashfa hii nzito inayoliondolea heshima mbele ya jamii. Sasa mimi nasema, TAKUKURU haiwezi kulisafisha Bunge katika mambo ya rushwa, ni sisi Wabunge hapa ndani kuhakikisha kwamba hapa Bungeni ni *corrupt free zone*. Akijihusisha mtu kwa matendo ya rushwa, kwa sababu ya kura hizi, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria. Uwe Mbunge, uwe Waziri, uwe nani tutakukamata, tutakufikisha kizimbani. Kwa hiyo, namna ya sisi kujisafisha, tushirikiane wote tusijihusishe na matendo ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lile la kwamba watu wameweka fedha Uswizi, nadhani lilikwishajibiwa

kwamba TAKUKURU wamepeleka taarifa. Kuna taratibu za kuwasiliana TAKUKURU na nchi za nje. Wamepeleka taarifa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuanza kufanya mawasiliano na huko zilikowekwa fedha, sasa zoezi linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Sekretarieti ya Maadili, mimi naona hapa Sekretarieti ya Maadili moja. Napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mmesema tuikarabati sheria, Sekretarieti ya Maadili iwe na nguvu, iwe na meno. Ushauri huo Serikali imeupokea. Tunawashukuru sana, mmesema Sekretarieti ya Maadili Bajeti yake ni ndogo. Nawashukuru sana. Bahati nzuri Bajeti ya mwaka huu nimekuta wenzangu akina Chikawe wamekwishaitengeneza. Nataka kuomba rai mapema, mwakani tutakapofika kifungu hiki, mniongezee fedha maana haya maneno mmeyasema wenyewe leo hapa, kwamba Sekretarieti ya Maadili ina fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhana ya kutenganisha uongozi na biashara kufuatia maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeanza kufanya utafiti juu ya namna kupata mfumo bora utakaotumika katika nchi yetu. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Sekretarieti itaendelea kufanya utafiti wa namna bora ya kutenganisha biashara na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lingine ni kwamba Sekretarieti ya Maadili inaongozwa na watumishi ambao wengi wamestaafu. Hili jambo siyo kweli. Sheria

inamruhusu Rais wa Nchi kumteua Kiongozi, Mtumishi aliyebobea kuwa Kiongozi wa Taasisi. Lakini wanaofanya kazi chini yake ni watumishi wa kawaida wengi tu. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wote wanaofanya kazi pale ni wastaafu.

Lingine limerudiwa kuhusu upungufu wa bajeti; imerudiwa hoja kwamba hii Sekretarieti ya Maadili inashughulika tu na wale watu waliotajwa kwa mujibu wa sheria. Wale ambao hawakutajwa, hata kama akijilimbikizia mali namna gani huwa hashughulikiwi. Sisi rai hiyo tumeisikia na tutaizingatia wakati wa kufanya mapendekezo ya kuboresha chombo hiki, kwamba siyo vizuri ukashughulika tu na wale ambao wamejaza fomu ukipata taarifa ya watu ambao pia hawakujaza fomu, lakini hawamo katika ile orodha, washughulikiwe kama vile ambavyo unavyowashughulikia wale wa kwenye fomu. Sasa kuongeza orodha ya watumishi wengine wa umma watakaowajibika na Sheria ya Maadili, hilo tumekubali tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imerudiwa hapa tena Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, zifanyiwe marekebisho Sekretarieti iweze kufanya kazi yake vizuri. Baada ya Viongozi kutojaza mali walizonazo, tumeanza utaratibu pale kwenye Sekretarieti ya Maadili, tunafanya ufuatiliaji na tukibaini kwamba wewe hujajaza au umetudanganya, tunakwambia urekebishe, ama tunakupeleka kwenye Baraza la Maadili. Lakini bado watu wengi wanasema adhabu inayotoka ni ndogo, tutazingatia haya katika kufanya mabadiliko yale tunayotaka kuyapendekeza katika kuiboresha sheria hii.

Halafu lingine, Serikali lini itafungua Ofisi za Sekretarieti katika Mikoa? Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inadhamiria kufungua Ofisi katika Mikoa yote, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, ilianza kufungua Ofisi za Kanda sita ikiwa ni Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Tabora na Mwanza. Hivi karibuni inatarajia kufungua Ofisi ya Kanda pale Chalinze na tutawaomba fedha hapa mtupatie kwa ajili ya kuharakisha zoezi hili la Chalinze.

Ndugu yangu Mheshimiwa Mkosamali anashauri Serikali kupanua wigo wa kuangalia mali kwa viongozi wa utumishi wa umma. Takwimu halisi ya Madiwani wanaoshughulika na Serikali ya Maadili na Viongozi wa Umma 4,485, aidha, katika mwaka 2011 jumla ya Madiwani 10 walifikisha mbele ya Baraza la Maadili ambapo kati ya hao mmoja alipata onyo kali, wanne walipewa onyo, wanne hawakupatikana na hatia na mmoja shauri lake halikusikilizwa kwa sababu zisizoweza kuzuilika. Kwa hiyo, nataka nikushukuru tu ndugu yangu Mheshimiwa Mkosamali, umetoa ushauri mzuri kufuatilia na tutajitahidi kufanya hivyo. Lakini naamini pia kwamba utatuunga mkono katika kutuongezea mafungu.

Halafu Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema - Naibu Waziri Mkuu Mstaafu wa Nchi hii, anasema Serikali ichukue hatua za Viongozi kutenganisha bishara na uongozi. Kweli kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi imekwishaanza kufanya utafiti wa namna ya kupata

mfumo bora utakaotumika katika nchi yetu katika mwaka wa fedha 2012/2013. Sekretarieti inadhamiria kwenda kujifunza katika nchi zinazotumia mfumo huu ili kupata mfumo utakaofaa katika mazingira yetu. *(Makofi)*

Sasa ndugu zangu, Sekretarieti ipatiwe bajeti ya kutosha. Hii imejirudia. Viongozi ambao ni asilimia saba ya Viongozi wa Umma mwaka 2011: Je, zaidi ya kuandika barua hatua, gani zimechukuliwa? Viongozi ambao baada ya kuandikiwa barua za kurejesha matamko yao na kushindwa kurejesha watafikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa mujibu wa kifungu cha 15 (a) na 26.

Kuhusu uhakiki wa rasilimali na madeni ya Viongozi ni muhimu Sekretarieti kupata mamlaka, kupata taarifa za kibenki, *TRA* na *BREILA*. Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma 398 inafanyiwa marekebisho ili kuipa nguvu. Aidha, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Viongozi hawa wametakiwa kuthibitisha na kurekebisha matamko yao na wakishindwa kufikishwa mbele ya Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hoja zilikuwa ziko nyingi, mimi nimepata faraja kubwa sana, ni Waziri Mgeni katika Wizara hii, yale niliyoyapata jana na leo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge imekuwa darasa kubwa kwangu. Nawaahidi kwamba nitayafanyia kazi, sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Captain Mstaafu George Mkuchika - Waziri mwenye dhamana ndani ya Ofisi ya Rais, akishughulikia utawala bora. Tunashukuru sana kwa majibu yako katika hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mtoa Hoja ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, yeye atatumia muda wa saa moja kujibu hoja mbalimbali zilizohusu ofisi yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kunifikisha siku ya leo na kuniruhusu kujibu hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamenisaidia kwa njia moja au nyingine katika kutoa hoja mbalimbali. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuhakikisha nazijibu moja baada ya nyingine na zile ambazo hatutazijibu, tutahikikisha kwamba tumeziandika na tutazileta mbele ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema katika kipindi hiki cha siku mbili. Nakushukuru sana na majadiliano naona yamekwenda vizuri na umetutendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee niwashukuru wazazi wangu walionilea kwa hekima na busara ingawa wako mbele ya haki, lakini Watanzania wanafaidi matunda ambayo nawatumikia kwa kiasi kikubwa. Napenda kumshukuru mume wangu, watoto wangu na wajukuu zangu kwa kunivumilia hasa katika kipindi hiki kigumu cha miongozo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wangu walitaka kuja Bungeni, lakini bahati mbaya wameogopa kweli miongozo. Sasa nikawaeleza kwamba vijembe kwenye siasa ni kitu cha kawaida, naomba mtuone tukitoka pale nje sisi huwa ni wamoja na wengine wanakwenda *disco* pamoja, wanakunywa pamoja. Kwa hiyo, niwaambie tu kwamba wasiliogope Bunge hili, ndivyo ilivyo kwa mfumo wa vyama vingi. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru kipekee Mheshimiwa Pindi H. Chana ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue Wabunge ambao walichangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Dkt. Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa

Suzan L. A. Kiwanga, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Paul P. Lwanji, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Yusuph A. Nassir na Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu. Hao ndio waliochangia moja kwa moja kwenye hotuba yangu na wengine walichangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Napenda pia niwatambue waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Goodluck J. Ole – Medeye, Mheshimiwa Hamoud Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa John P. Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Christowaja G.

Mtinda, Mheshimiwa Hamad Ali Rashid, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay na Mheshimiwa John P. Lwanji. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Dkt. Omari R. Nundu, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Anthony G. Mbassa, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Amina M. Mwidau, Mheshimiwa Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Lwakatare, Mheshimiwa Angellah J. Kariuki, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Lolesia M. Bukwimba na Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba radhi wale pengine kwa njia moja au nyingine sikuwataja majina yao, lakini natambua michango yao yote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa kuongea walichangia Wabunge hao niliowataja kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali na wale waliochangia kwa maandishi nimewataja kwenye jedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kujibu hoja kama ifuatavyo:-

Kwanza nitajibu yale ambayo yalijitokeza kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, nitakwenda sehemu ya *TASAF* baadaye *MKURABITA* na mwisho nitamalizia na Mfuko wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana kumpongeza Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake aliyoitoa juzi tarehe 1 Julai, 2012 kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, yeye ndiye anayesimamia Watumishi wote wa Umma. Kwa hiyo alikuwa na uhalali wa kuitoa hotuba hiyo kuwaasa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwanza nianze labda na kutoa tafsiri au taratibu za migomo kwa mujibu wa Sheria. Sheria ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura 105 inafafanua utaratibu utakaofuatwa wakati Watumishi wa Umma watakapotaka kufanya mgomo au kumfungia nje mwajiri na katika kifungu cha 26 (1)

na (2) cha Sheria hii, vinatoa haki na masharti ya kufuata pale Mtumishi wa Umma anapotaka kujiunga na mgomo. Masharti hayo ni kama yafuatayo:-

(i) Kuwepo na mgogoro au malalamiko;

(ii) Mgogoro huu uwe umeshindwa kupata suluhu;

(iii) Kura ya kufanya mgomo iwe imepigwa na watumishi wengi wa sekta husika chini ya usimamizi wa Afisa kazi; na

(iv) *Notice* ya siku 60 ya kusudio la kufanya mgomo iwe imewasilishwa Serikalini baada ya siku ya kura ya nia ya kufanya mgomo.

Mtumishi anapokiuka utaratibu huu anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na Kifungu cha 27 cha Sheria hiyo, kinaeleza kuwa Sheria hii, hairuhusu mtumishi yeyote wa Umma kufanya mgomo endapo mgomo huu utahatarisha uhai, afya na usalama wa jamii nzima au sehemu ya jamii. Hayo ndiyo masharti ambayo yanatakiwa kufuatwa wakati wa kufanya mgomo wowote. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, sisi ndiyo tunaotunga sheria, tunatakiwa kuzisimamia Sheria zetu ambazo tunazitunga. Nasema hivi kwa nini? Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, sisi ni watunga Sheria, hatuzisimamii Sheria zetu tunazozitunga, tunaipeleka nchi yetu kubaya. Tunatakiwa kuzisimamia Sheria hizo. Kwa hiyo, tunapowashawishi watumishi wa Umma kuhusu

kugoma, tuwaeleze na hiyo Sheria ili waweze kuifuata. *(Makofi)*

Aidha, nawaasa Watumishi wa Umma kwamba mgomo siyo suluhu. Wafanyakazi wawe na subira, wawe watulivu, wawe wanafanya mambo yao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe tunachunga ndimi zetu wakati wa michango mbalimbali. Kwa sababu wakati mwingine unaweza ukasema sentensi moja tu ambayo inachochea au inakuwa na viashiria vya vurugu, fujo katika nchi yetu ambavyo havitakiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la motisha na mishahara kwa Watumishi wa Umma; kwanza tuangalie motisha ni nini? Motisha ni kitu chochote kinachotolewa au kufanywa na mwajiri ili kuongeza ari ya kazi, na motisha inaweza ikawa ni fedha, vitu, maneno au maandishi ya pongezi. Kwa kawaida, motisha hutolewa kutokana na utendaji bora wa mtumishi. Sasa katika Sera yetu ya malipo ya mshahara na motisha, malengo ya Sera hii ni:-

(i) Kuongeza uwezo wa Serikali kuvutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watumishi wenye sifa zinazohitajika;

(ii) Kuoanisha na kuwianisha malipo ya mishahara kwa Taasisi za Serikali zisizopata ruzuku kutoka Serikalini;

(iii) Kuondoa tatizo la upungufu la watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha kunakuwepo na uwiano mzuri wa watumishi;

(iv) Kuwe na mfumo mahususi wa maslahi kwa Watumishi wa Umma;

(v) Kuanzisha mfumo wa masilahi ambao utadhibiti posho;

(vi) Kuongeza uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali watu; na

(vii) Kuimarisha utendaji wa kazi na tija katika Utumishi wa Umma.

Kwa hiyo, motisha sio fedha tu. Motisha ni pamoja na kuboresha mazingira. Hata nikisema ahsante, ile ni motisha tosha kwa wafanyakazi. Hayo ndiyo yaliyokuwa mambo ya kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niruhusu niweze kutoa majibu kwa hoja moja moja. Wengi walichangia kuhusu ukubwa wa Serikali kwamba Baraza la Mawaziri ni kubwa. Naomba nilijibu hili kwa urefu kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais ndiye mwenye mamlaka ya kuanzisha Wizara na kuzipangia majukumu kupitia Hati ya Mgawanyo wa Majukumu *(Instrument)* anayoitoa kila anapoingia madarakani. Aidha, ukubwa au udogo wa Serikali unazingatia mambo yafuatayo:

ukubwa wa nchi, idadi ya watu, vipaumbele vya maendeleo ya nchi, agenda muhimu za kiuchumi na maendeleo ya jamii, pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Yote haya lengo lake ni kukidhi matakwa ya wananchi. Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali za Kimataifa kuhusu ukubwa wa Serikali unaofaa kwa nchi, yaani “*optimal size of Government*”, ukubwa wa Serikali hupimwa kwa kuangalia uwiano kati ya matumizi ya Serikali (kwa maana ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa) na Pato la Taifa. Kwa kutumia kigezo hicho, nchi huhesabika kuwa na ukubwa wa Serikali unaokubalika iwapo uwiano kati ya matumizi ya Serikali na pato la Taifa ni kati ya asilimia 17 mpaka asilimia 30.

Matokeo ya tafiti hizo ya hivi karibuni yaliyochapishwa na Shirika la Fedha Duniani *(IMF),* kupitia jarida lake la “*Regional Economic Outlook for Sub-Saharan Africa*” toleo la mwezi Aprili, 2012, uwiano kati ya matumizi ya Serikali na pato la Taifa kwa nchi yetu ni asilimia 27.1. Hivyo, ni dhahiri ukubwa wa Serikali yetu, Taifa lenye eneo la 945,000 $km^2$ za mraba ni himilivu na uko ndani ya viwango vinavyokubalika Kimataifa. Kwa ulinganisho, uwiano huu kwa nchi ya Kenya ni asilimia 29.7, Msumbiji asilimia 34.4, Malawi asilimia 36.5 na Uganda asilimia 22.9.

Hata kwa vigezo vingine pia, Serikali yetu bado ni ndogo ukilinganisha na baadhi ya Serikali za nchi nyingine kwa kuangalia idadi ya watu, ukubwa wa eneo la nchi na kiwango cha maendeleo ya nchi husika ilivyokwishafikia. Mfano, nchi ya Kenya ukubwa wake ni 582,646 $km^2$ na watu milioni 41.6. Kwa Uganda

ukubwa wake ni 241,038 $km^2$ na watu wake ni milioni 33.8; Rwanda ina 26,338 $km^2$ na watu wake ni milioni 10.9 ambazo jumla ya ukubwa wa maeneo yao haufikii ukubwa wa eneo la Tanzania 945,087 $km^2$ na watu wake takribani milioni 45 na nchi hizo zina Wizara nyingi kuliko nchi yetu ambao inao Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa mfano Kenya inazo Wizara 46 na Mawaziri na Naibu Mawaziri 85; Uganda inazo Wizara 27 na Mawaziri na Naibu Mawaziri 75; Rwanda inazo Wizara 22 na Mawaziri na Naibu Mawaziri ni 41. Vile vile ukilinganisha ukubwa wa eneo la mraba la nchi yetu na idadi ya watu ni dhahiri kuwa mahitaji ya maendeleo yetu ni makubwa kuliko nchi hizo na hivyo uhitaji Watumishi wa Umma ni mkubwa ili kutoa huduma stahiki. Hili lilichangiwa na wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi na motisha kwa Watumishi wa Umma, hili kwa kweli lilichangiwa na Wabunge wengi, wengine walisema kima cha chini cha mshahara kiwe Sh. 315,000/=, wengine wamesema motisha kwa asilimia 50, waongezewe tu Sekta ya Afya na Elimu, wengine walisema mazingira magumu walipwe asilimia 50 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa pendekezo hili utahitaji kwa mfano, tukisema tu kwamba tutekeleze hiyo azama ya kima cha chini kiwe Sh. 315,000/=, tutahitaji Shilingi trilioni 6.9. Sasa kwa kuzingatia bajeti yetu ya mwaka 2012/2013 tulizotenga sisi kwa ajili ya mishahara ni Shilingi trilioni 3.1. Kwa hiyo, ukiangalia hiyo Shilingi trilioni sita na mapato yetu ya

ndani utakuta kwamba ni asilimia 60 tunaichukua kwa ajili ya mishahara tu. Bado hapo hatujaangalia *other charges*. Kwa hiyo, hilo pendekezo la Sh. 315,000/= haliwezi likatekelezeka. Aidha, mishahara ya watumishi itarekebishwa, na kila mwaka tunairekebisha kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ambapo linajumuisha Vyama vya Wafanyakazi wa Serikali. Kwa mwaka huu tumekaa, tumekubaliana, kwa hiyo, wale ambao wanauliza kima cha chini ni Shilingi ngapi, nenda kwenye Chama chako cha Wafanyakazi, kaulizie, watakwambia kima cha chini ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tanzania ndiyo inalipa viwango vikubwa vya mshahara ikilinganishwa na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii isipozingatiwa katika kuainisha viwango vya mishahara, itakuwa na athari zifuatazo:-

(i) Itaongeza gharama za uzalishaji katika uchumi wetu;

(ii) Bei za bidhaa zetu zitapanda na hivyo kuchochea mfumuko wa bei na kuathiri ushindani wetu katika Soko la Afrika Mashariki na kwingineko;

(iii) Wawekezaji wa ndani na nje watashindwa kuwekeza kutokana na gharama za mishahara na hivyo kuhamia kwa washindani wetu pia; na

(iv) Itaongeza tatizo la ukosefu wa ajira kutokana na kuondoka kwa wawekezaji na hivyo kuathiri ukuaji

wa uchumi. Tukipandisha mishahara hiyo kiholela athari zake ndiyo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine waliosema kwamba kada ya Afya na Elimu waongezewe asilimia 50 ya mazingira magumu; mazingira magumu yanagusa kada zote. Hayagusi kada mbili tu, ndiyo maana tumeanzisha ile Bodi ya Mishahara ili iwianishe mishahara ya wafanyakazi wote, na ikiangalia motisha katika mazingira magumu, iangalie motisha kwa watumishi wote na sio kuangalia kada moja. Tukifanya hivi, tutakuwa tunawagawa watumishi. Kwa hiyo, ndugu zangu wa kada ya Elimu, kada ya Madikatari, hiyo Bodi ya Mishahara itaangalia na kada nyingine zozote. Kwa sababu anayefanya kazi katika mazingira magumu sio daktari peke yake, na sio Mwalimu peke yake. Ndugu yangu Mheshimiwa Keissy, kule anakosema Nkasi wanakwenda kwa mitumbwi: Je, ni Madaktari tu na Walimu? Hakuna watumishi wengine? Inabidi tuangalie watumishi wote kwa ujumla wake. Kwa hiyo, hilo tumelisikia na tumeshaanza kulifanyia kazi. Mimi nina uhakika kwamba baada ya muda suala hili tutaliwianisha na tukumbuke kwamba kila mtumishi ana umuhimu wake.

Hapa mmesema kwamba Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji wanafanya kazi nzuri sana, wanatusaidia kule Vijijini, nao wanaishi katika mazingira magumu, nao wanahitaji motisha. Mtisha kama nilivyosema, siyo lazima iwe fedha. Unaweza ukampa mtu fedha, lakini barabara mbovu, hakuna nyumba ya kupanga, hakuna huduma muhimu, kwa hiyo, hata ile hela unayompa ni sawa na kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Watumishi wa Umma kujihusisha na Siasa, napenda kusema kwamba Watumishi wa Umma wanayo haki ya kikatiba kushiriki katika masuala ya kisiasa kwa mujibu wa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2000. Hata hivyo, hakuna haki isiyokuwa na wajibu au uhuru usiokuwa na mipaka. Ushiriki wa Watumishi wa Umma katika siasa ni lazima uzingatie misingi ya kutekeleza wajibu wao bila ya upendeleo, kuwa na utii kwa Serikali na Chama kilichopo madarakani na kutoa huduma kwa misingi ya haki na usawa bila ubaguzi ya misingi ya kisiasa. Kwa hiyo, waraka huu umejieleza wazi kwamba mtu anaweza akajishughulisha na siasa lakini siyo mahali pa kazi. Ndiyo maana tumevunja matawi ya Vyama mbalimbali katika Vyuo Vikuu na mahali pa kazi. Kwa hiyo, hilo naomba waajiri wawaangalie wale watumishi ambao wanajihusisha na siasa mahali pa kazi waweze kuwashughulikia na kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi hewa, hilo limeongelewa na Waheshimiwa wengi sana. Watumishi hewa wanatokana na nini? Watumishi hewa wanatokana na watumishi halali waliokuwa katika orodha ya malipo ya mishahara katika kipindi fulani na baadaye ajira zao zikahitimishwa kutokana na sababu mbalimbali bila kuondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara kwamba bado ni watumishi wa Serikali. Malipo hewa yapo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya mishahara batili kwa watumishi ambao utumishi wao

ulikwishakoma na malipo haya kufanywa kupitia *Accounts* zao za benki kwa kipindi chote cha malipo. Utumishi huu unakoma kwa kufukuzwa kazi, kutokana na kifo au kutokana na utoro kazini. Malipo ya Mishahara kwa watumishi hawa ni batili na malipo haya mara nyingi huweza kurudishwa Hazina na Taasisi husika. Taasisi hizo hutumia fedha hizo kwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kutumia fedha hizo kulipa mishahara ya watumishi wapya kinyume na taratibu za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya mishahara kwa watumishi ambao utumishi wao umekoma na mishahara yao imerejeshwa Hazina bila kuwaondoa katika orodha ya *Payroll* watumishi hao; hatua za kukabiliana na watumishi hewa zilizochukuliwa; kwanza nipende kutoa takwimu kwamba kuanzia mwezi Julai, 2011 mpaka tarehe 31 Mei, 2012 jumla ya watumishi wa Serikali 12,549 wamefutwa katika orodha ya malipo ya mshahara wa watumishi wa Umma *(Payroll)* kutokana na sababu mbalimbali. Watumishi 4,442 ambao wangelipwa Sh. 418,624,812/= hao watumishi walikuwa wamefukuzwa kazi na wameondolewa kwenye *payroll.* Waliokuwa na makosa ya kinidhamu, 5,747 nao walifutwa katika *payroll* na watumishi waliostaafu kwa mujibu wa Sheria 2,239 na wao wameondolewa katika *payroll*. Kwa hiyo, watumishi 12,000 karibuni wameondolewa kwenye *payroll* kutokana na mfumo ambao tumeuanzisha pale Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha uwajibikaji, Serikali sasa imeamua usimamizi wa *payroll* uwe moja kwa moja chini ya Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi

wa Umma badala ya kusimamiwa moja kwa moja na Hazina. Hatua hii itawapa Waajiri na Maafisa Utumishi wao kuwa na nguvu ya usimamizi wa Watumishi wao badala ya kuwatumia Wahasibu kama ilivyokuwa hapo awali.

Kama nilivyokuwa najibu maswali yangu, Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara, yaani *Human Capitali Management Information System – HCMIS,* unaendelea kuimarishwa ambapo waajiri wote Serikalini na katika Taasisi zake watahusika moja kwa moja katika kuingiza katika mfumo huo taarifa zote za kiutumishi. Huo mfumo unasaidia sana. Ina maana kwamba tumefunga huo mfumo pale Utumishi, tume-*centralize* taarifa zote za Watumishi. Kwa hiyo, mafaili yote ya Watumishi wa Umma sasa hivi unaweza ukayakuta Utumishi na unaweza ukayakuta kwa mwajiri. Huo mfumo umesaidia sana. Iwapo *file* halikuonekana kwenye *computer* ya Mwajiri, *file* sisi kule Utumishi tunakuwa nalo kwenye *computer*. Kwa hiyo, hiyo nayo pia imepunguza suala la watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua gani zimechukuliwa? Hatua zifuatazo zimechukiliwa kwa wale waliohusika kwa njia moja au nyingine katika kusababisha suala la watumishi na mishahara hewa.

(i) Watuhumiwa sita walifikishwa Mahakamani kipindi cha mwaka 2011/12;

(ii) Hadi sasa kesi 21 zinaendelea Mahakamani, zikiwemo 15 za miaka ya nyuma; na

(iii) Majalada 83 yanaendelea na uchunguzi na pindi yatakapokamilika, hatua stahiki zitachukuliwa. Kwa hiyo, ndugu zangu, hatua zinachukuliwa kwa wale ambao wamesababisha mishahara hewa na watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni malimbikizo ya mishahara kwa watumishi. Hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malimbikizo ya mishahara yanatokana na sababu zifuatazo: Kuchelewa kwa mtumishi kuingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara, madai ya malipo ya nusu mshahara baada ya hitimisho la suala la kinidhamu la mtuhumiwa akionekana kwamba hana hatia, kuchelewa kuingizwa kwa mabadiliko ya mshahara baada ya kupandishwa cheo. Lingine ni mtumishi kutolipwa mshahara wake katika kipindi cha uhamisho au wakati wa kwenda likizo. Kwa hiyo, kuanzia Julai, 2011 hadi mwezi Juni, 2012, Serikali imekwishalipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi jumla ya Sh. 72,351,994,390.92 na mchanganuo tumeutoa hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengine walichangia kwamba, walivyoangalia kwenye jedwali Na. 6, ukurasa wa 90, wameona kwamba, kuna tofauti ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba, malipo ya madai ya Maaskari na hata kwa Watumishi wengine, hutegemea kiwango chake cha mshahara, muda wa madai na muda ambao Viongozi wa Watumishi wanapoidhinisha ulipaji wa madai husika. Kwa hiyo, lazima hiyo itatofautiana kulingana na mshahara wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya pensheni. Hilo lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, mafao na hitimisho la kazi kwa Watumishi wa Umma, hutofautiana kulingana na mfumo ambao Mtumishi anachangia kulingana na masharti ya ajira yake. Kwa mfano, Mifuko ni *PPF* kwa ajili ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, *PSPF* kwa ajili ya Watumishi wa Serikali Kuu, *LAPF* kwa ajili ya Watumishi wa Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, kutokana na kuwepo kwa tofauti hii, Bunge lilitunga Sheria ya Usimamizi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sheria Na. 8, ambayo tumeipitisha mwaka 2008 kwa ajili ya kuainisha mafao na mifumo ya utoaji wa mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa hapo kwenye mafao ya uzeeni, wanasema kwamba Mheshimiwa Mrema alikuwa Naibu Waziri Mkuu kipindi hicho, hajapewa mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria, hastahili. Lakini *Administratively,* hilo tutazungumza na Mheshimiwa Mrema mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa wataalamu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba urudie tena hapo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIIMENT YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria, Mheshimiwa Mrema, hastahili. Lakini *Administratively,* tunaweza tukazungumza naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Wataalamu ambao huzingatia vipaumbele, tunasema kwamba, katika mwaka 2012/2013 Serikali imetoa kipaumbele kwa kada ya Elimu, Afya, Kilimo na Usalama wa Raia. Kwa hiyo, Serikali, itaendelea kufanya tathmini ya vipaumbele kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa Watendaji, hilo tumesema kwamba, kwa mwaka huu tutalitekeleza. Zile Kada ambazo mmesema zirudi kwenye Halmashauri, hilo tumeliona na tutarekebisha sheria.

Waheshimiwa Wabunge, lakini tunapotunga Sheria, tusiseme tu ipite, ipite, ile Sheria tulitunga sisi wenyewe; kusema kwamba, Sekretarieti ya Ajira, iajiri, sasa hivi tutairudisha basi Bungeni tena, ili mtoe maoni yenu.

Mheshimwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira magumu, hilo nimeshaliongelea. Nakumbuka Mheshimiwa Keissy katika mchango wake, yeye amenichorea mpaka mtumbwi, unaokwenda kwenye visiwa vyake. Nimesema hilo tutaendelea kulitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jitu Soni, alisema kwamba tusiwabague Watumishi. Tumewafanyia *re-categorisation* Watumishi wa Wizara ya Elimu, kwa nini watumishi wengine hatujawafanyia hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jitu Soni, hilo tumeliona na huenda tukalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kombo, yeye ameelezea kwamba, Sekretarieti ya Ajira ifungue Tawi Zanzibar. Hilo tumelipata na tutafungua Ofisi kule kwenye Sekretarieti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Watumishi wazembe kuondolewa, hili limeongelewa sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pia Mheshimiwa Hawa Ghasia, ameliongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulishauriwa kwamba mishahara iangaliwe upya, tumesema Bodi ya Ajira itafanya kazi hiyo ya kuhuisha mishahara katika kada zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu kutosajiliwa, Sekretarieti ya Ajira imeshaanza kusajili namba ya Wahitimu wa Vyuo

Vikuu, tunaijua sasa hivi. Mpaka sasa hivi tunajua tuna wahitimu karibu 21,000 ambao wako Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaohoji Mamlaka ya Rais kuteua Makamishna, Wakurugenzi, na kadhalika, nikasema Profesa Kahigi, tungoje Katiba Mpya. Katiba yetu inamruhusu kufanya hivyo.

Kwa hiyo, ni vyema tukawaambia watu wetu tungoje Katiba Mpya, labda hiyo itakuwa mwarobaini. Lakini nayo Katiba Mpya itaangalia, ni wengi wape ambao watakaosema kwamba madaraka haya ni makubwa sana, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu mmoja alisema kwamba, Wabunge tunapostaafu, kwa nini tusipewe 80%?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema tunaotunga Sheria, ni sisi. Tukiona kwamba, tunagandamizwa, ni vyema tukaleta hiyo Sheria ili tuone kwamba, tutafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, hayo ndiyo ambayo yaliongelewa kwa ujumla katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nitakuwa sijatenda haki nisipojibu masuala ya *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizotolewa kwenye *TASAF* ni kwamba, malengo ya *TASAF II* hayajafanikiwa, kwani bado inakabiliwa na changamoto kadhaa, yakiwemo maombi mengi ya

miradi ya jamii yenye thamani kubwa kuliko uwezo wa *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba, ni kweli, *TASAF II* kumekuwa na mahitaji mengi ya miradi ya jamii kuliko uwezo wa kifedha. Hiyo ilijionyesha bayana kwa tathmini zilizofanyika na ndiyo chanzo cha kuanzishwa kwa *TASAF III.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yalikuwa ni mengi sana. Baada ya kuona kwamba, maombi ni mengi na miradi mingi haijakamilika, ndizo changamoto ambazo tuliziona kwenye *TASAF II,* ndiyo maana tukaanzisha *TASAF III,* ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi wetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kapuya, lile suala lako la Kijiji cha Kazaroho, litazingatiwa kwenye *TASAF III.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walichangia kwamba, mpango madhubuti uandaliwe kwa ajili ya utekelezaji wa *TASAF III* ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa, utekelezaji wa shughuli za *TASAF III* unakuwa chini ya usimamizi wa *TASAF* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea huo ushauri na tumeuzingatia. Katika Muundo wa *TASAF III* ambapo kila Halmashauri itakuwa na Afisa wa *TASAF* wa kusimamia utekelezaji, tathmini na ufuatiliaji.

Aidha, semina za uhamasishaji zitaendelea katika ngazi zote, kabla ya kuanza *TASAF III.* Kwa hiyo, yule *co-ordinator* katika Halmashauri, atarudishwa tena. Kama mtakumbuka pale mwanzoni wakati wa

majaribio, kulikuwa na *co-ordinator* wa *TASAF* kwa kila Halmashauri. Sasa hilo limezingatiwa na atarudishwa katika mpango wa *TASAF III.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* kulingana na malengo yake ya kupunguza umasikini, bado imeshindwa kutokana na kukumbwa na changamoto za ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya *TASAF* kwa Wilaya ambazo zimefanya vizuri, Miradi ya *TASAF* imesaidia sana. Kwa Wilaya ambazo hazikufanya vizuri, kwa kweli *impact* yake huwezi kuiona.

Waheshimiwa Wabunge, nakumbuka tulikuwa na Semina moja mkaisifu sana *TASAF,* mkasema kwamba, mpango ule wa *TASAF* ingefaa miradi yote ingeiga ule mfano wa *TASAF.* Kwa hiyo, sehemu zilizokuwa na ubadhirifu zilikuwa na ubadhirifu, lakini kwa kiasi kikubwa imekidhi lengo lake la kuondoa umasikini. Ndiyo maana unaona Waombaji ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kapuya alisema kuhusu mradi wake ule wa Kijiji cha Kazaroho; nimesema kwamba, utazingatiwa katika awamu ya *III* ya mradi huo wa *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Keissy, yeye amesema kwamba, miradi iliyopatiwa fedha, hailingani na pesa zilizotolewa kwa miradi hiyo. Miradi mingi ilihujumiwa sana kule kwake Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, tunapokea hiyo taarifa kwa masikitiko. Ni kweli, miradi 50 ilikwenda kule na Shilingi milioni 822.0 zilikwenda kule. Kwa hiyo, kwa kuwa ametoa hiyo rai, sisi tutapeleka Wataalamu wetu kule Nkasi, kuangalia kama miradi iliyotekelezwa inalingana na fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zambi alisema *TASAF I* na *II,* ilitekelezwa chini ya viwango. Ninachotaka kusema ni kwamba, kama miradi hiyo inatekelezwa chini ya viwango, ni tatizo la Halmashauri, kwa sababu wao ndiyo waliotakiwa kutoa utaalamu. Sasa kama hawakutoa utaalamu stahiki, wanawaachia wanavijiji, wanavijiji sio ma-injinia, wanavijiji wao wanachofanya ni kubuni mradi. Usimamizi ni wa Halmashauri, na *TASAF,* ilitoa 5% kwa ajili ya *supervision.* Kwa hiyo, ile 5% ndiyo inayotakiwa kusimamia miradi hiyo. Kwa hiyo, Halmashauri ingefaa itimize wajibu wake wa kuhakikisha kwamba miradi hiyo inafanyika kwa kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Salim Hemed Salim, alisema kwamba, miradi iliyoibuliwa na wananchi na kufadhiliwa na *TASAF* ni mizuri, lakini siyo endelevu. Nakubaliana naye, lakini uendelevu wa mradi unatokana na Halmashauri husika. Serikali imeweka miundombinu, yaani huo mradi wa *TASAF,* imewapa mradi wa maji ya bomba; sasa mnataka bomba likiharibika *TASAF* Makao Makuu waje wawatengenezee? Hapana. *Maintainance* ni suala la Kijiji na suala la Halmashauri husika. Kwa hiyo, huo ndiyo uendelevu wenyewe. Mkichimbiwa kisima,

msitegemee kwamba, *TASAF* itakuja kufanya *maintainance,* bali wananchi wenyewe au Halmashauri husika itahusika na mambo ya *maintainance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamepongeza miradi hiyo ya *TASAF.* Kama nilivyosema, kwa kweli kwa Wilaya zile zilizofanya vizuri, mambo yamekuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Shekifu, amesema *TASAF* imefanya kazi nzuri, lakini Watendaji wake ni wabovu. Yeye amesema atanieletea orodha, nami nasema kwamba, Mheshimiwa, alete tu kwamba, miradi ile ambayo ilikuwa haikufanikiwa vizuri, ni vyema akatuletea ili *TASAF* Makao Makuu, waweze kuipitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, yeye anasema aah, Mfuko huu bado unaonekana ni wa Chama kimoja. Mimi nasema siyo kweli. Hivi kisima kikichimbwa pale Kijijini, wanaokunywa maji ni *CCM* peke yao? Au *CHADEMA* peke yao? Au *CUF* peke yao? Wote tunakunywa yale maji. Darasa likijengwa, wala hakuna itikadi pale, darasa tunalitumia wote. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba miradi ya *TASAF* inakwenda kichamachama. Kwa kweli hilo naomba nisikubaliane naye kwamba kwa maji, shule, barabara, wala hatubagui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Yussuf Abdallah Nasri, yeye amesema Korogwe, ikumbukwe. Tunasema kwamba,

tunatambua kabisa kwamba, kuna Korogwe Mji na Korogwe Vijijini. Kwa hiyo, miradi nayo itakwenda kulingana na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mng'ong'o, yeye anasema kwamba, programu ya Kaya Masikini sana kwa majaribio katika Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo, Chamwino na Kibaha, ni nzuri. Ni vizuri sasa zikasambazwa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, ushauri wako umepokelewa, na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge *(MKURABITA).* Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, Serikali, isambaze mpango wa *MKURABITA* kwa nchi nzima, na lingine, *MKURABITA,* itafute fedha nje ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunasambaza mpango huu katika nchi nzima. Lakini tunatumia vigezo kwa sababu, rasilimali ni chache. Lakini habari njema ni kwamba, sasa hivi *MKURABITA* imekamilisha Mpango wa Miaka Mitano, utakaotumika kutafuta fedha nje ya bajeti ya Serikali, kama mlivyoshauri ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanzisha Mfuko wa Urasimishaji wa Wilaya. Tutasisitiza kwamba, Mfuko huu uanzishwe kila mahali ili uweze kuwasaidia

wananchi wengi zaidi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi *MKURABITA* inabidi itumie vigezo tu kwa sababu, rasilimali zenyewe ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine limesema Kamati, ilikuwa imeshauri kwamba, Serikali, kupitia Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuanzisha Masijala za Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba, tunaomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanapojenga Ofisi za Vijiji, wahakikishe kwamba, Masijala ya Ardhi, imejengwa katika sehemu husika, kwa sababu ni kigezo kimojawapo ambacho kinawafanya *MKURABITA* waende katika Vijiji hivyo, kwa sababu vinakuwa vimeshakuwa na Ofisi na zile Hati Miliki zinahifadhiwa katika Ofisi. Hata Mabenki yanakuwa na imani iwapo Ofisi zinakuwepo. Kusipokuwa na Ofisi, ina maana kwamba zile Hati, kila mtu anaziweka sehemu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine wamesema kuhusu Serikali kuhakikisha kuleta Bungeni Sheria ya Ardhi Na. 113 na Sheria ya Ardhi Mjini na Ardhi Vijijini, Sura Na. 114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limezingatiwa na marekebisho haya tumeshaanza kuyafanyia kazi, na baada ya muda tutaleta marekebisho hayo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge, wanasema zoezi la urasimishaji liende sambamba na utoaji wa elimu ili liwe zoezi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba, *MKURABITA* imeendelea kutoa elimu na mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kutumia Vyombo vya Habari, machapisho na maonyesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Mheshimiwa Mohamed Missanga, anasema mbona Singida,sasa haionekani, hasa kwenye Wilaya ya Ikungi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, tatizo ni uhaba wa fedha, ndiyo maana tunakwenda kwa Vijiji vichachechache na Halmashauri chachechache. Fedha zitakapopatikana, kwa kweli ni nia ya mpango huu kuhakikisha kwamba tunafikisha hizo rasilimali kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Zambi amesema kwamba, *MKURABITA* una changamoto tangu ulivyoanza. Sisi tunakubali kwamba hakuna mpango ambao hauna changamoto.

Kwa hiyo, changamoto zipo, tumeziona, na ndiyo maana umeona ushauri mlioutoa kuhusu kupata fedha nje ya bajeti, na kadhalika. Ndiyo maana tumekubaliana na ninyi. Lakini amesema kwamba,

kuna baadhi ya Watendaji, wanaomba rushwa; tunasema kama anao ushahidi, ni vyema tu akaleta, ili tufuatilie kwa wahusika au wahusika wapelekwe moja kwa moja kwenye vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa wa Mkanyageni, amesema *MKURABITA,* itafika lini Mkoani Pemba, katika Jimbo la Mkanyageni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mnyaa, nimesema kwamba, tatizo ni rasilimali, ndiyo maana tunakwenda katika Vijiji vichachechache. Lakini tukishapata fedha, hata Mkanyageni, tutafika. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mrema, anaishauri Serikali iendelee na utaratibu wa kushughulikia kutengeneza na kutoa Hati Miliki za Kimila kwa wamiliki wa mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, kazi hiyo itafanyika. Tunaendelea kutoa Hati za Kimila Wilaya kwa Wilaya, hasa zile Wilaya nane ambazo sisi tumeshazifanyia kazi, sasa ziko katika hatua ya kufika mwisho ya kupata Hati Miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mchuchuli, yeye anasema kwamba, *MKURABITA,* imeshindwa kufanya kazi kule Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, angeshukuru kwamba, mpango huu umefika Wilaya ya Rufiji,

mambo mengi yamefanyika. Ni kitu kitu kidogo tu kwamba, bado wananchi kukabidhiwa hati zao, lakini zile hatua za awali zimeshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge, waliotoa michango kuhusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Kamati ya Katiba na Sheria, imesema Mfuko bado unatoza riba kubwa kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba, Mfuko unatoa riba kubwa. Ni kutokana na vyanzo vyake vya mitaji, ambapo nao wanachukua kwenye mabenki ambayo yana riba kubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana na wao wanakuwa na riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Kamati imesema imeihimiza Serikali, kujitahidi kusambaza huduma za Mfuko huu kwa nchi nzima na kutafuta vyanzo vya mtaji wenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumelipokea kama ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati iliagiza Serikali kutoa ufafanuzi wa utekelekezaji wa mikopo ya uwezeshaji au maarufu kwa jina la mabilioni ya JK. Mfuko huu nao ulipata fedha hizo Shilingi milioni 688 na wamekopesha *SACCOS* mbalimbali katika Wilaya ya Mkuranga, Rufiji, Morogoro Mjini na Vijijini, na sehemu nyingine za vijijini.

Upande wa upinzani wamesema mfuko umeshindwa kabisa kufikia malengo; kwanini mfuko huu usifanye kazi ya kutengeneza mazingira mazuri ya ukopeshwaji ili watu wengine wakope kwenye mabenki moja kwa moja? Tunasema kwamba mfuko unatoa elimu ya awali kwa wanachama wake na pia kuwawekea uwezo na utamaduni wa kujiwekea akiba na kukopa ili hapo baadaye wawe na sifa za kukopa kwenye mabenki.

Wateja wa mfuko huu ni wale ambao hawawezi kutimiza masharti ya kukopa kwenye mabenki. Mfuko huu unawalenga hasa wale wasiokuwa na uwezo. Wakishapata uelewa, wakishapata nguvu, ndio hao wanapanda ngazi, wanakwenda kukopa kwenye mabenki. Lakini kwa kuanzia, kwa kweli inakuwa ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Mussa Haji Kombo wa Chake Chake yeye amesema kuanzishwa kwa mfuko huu ni wazo nzuri, lakini lina sura ya kisiasa. Naona hilo linajirudiarudia. Jamani hapo hamna siasa yoyote, anayekidhi vigezo anachukuliwa na ndiyo maana inakwenda katika Wilaya mbalimbali. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa kweli hatufuati vigezo na katika fomu hutakuta kigezo cha Chama gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Wajumbe walioshauri kwamba hiyo mifuko iko mingi, mara *SELF*, mara *Mwananchi Empowerment,* mara nini; kwanini hiyo mifuko isiunganishwe kwa pamoja? Sisi tunachosema ni kwamba, kila mfuko unaanzishwa kwa taratibu zake na una malengo yake. Kwa hiyo, siyo

rahisi kuichanganya yote kwa pamoja wakati kila mfuko una malengo yake. Kwa hiyo, tunasema kwamba suala hili hatuwezi tukaliharakisha mpaka tuangalie malengo ya kila mfuko na wanaolengwa ni akina nani.

Ndugu yangu Kandege yeye amesema kwamba anaomba mfuko huu ufike mpaka vijijini. Mfuko huu unatekelezwa katika ngazi za Mijini na Vijijini na haifuati tu pale Mjini. Nimesema kwamba Mfuko huu utazidi kutoa elimu kwa wananchi, Mfuko huu utazidi kujitanua ili uweze ukawafikia wajasariamali wengi zaidi. Amesema elimu kwa umma: Kama nilivyojibu huko mwanzo, ni kwamba elimu inatolewa kwa ajili ya mfuko huu hasa kwenye Wilaya husika ambazo zimeshafanyiwa kazi. Wachangiaji wengine wamesema kwamba kuna urasimu katika mfuko huu, na wanaolengwa, hauendi chini kwa wale wanyonge. Hauwalengi wale wanyonge, mimi ninachosema, jamani mfuko huu unawalenga wanyonge, hakuna mkubwa hata mmoja hapa ambaye amekwenda kukopa kule kwenye mfuko kwa sababu fedha zinazotolewa ni kidogo sana. Kwa hiyo, zinawalenga wale watu wa chini ili wainuke kidogo waweze wakakopesheka kwenye mabenki.

Mheshimiwa Nassib Suleman Omar, anasema mfuko huu una changamoto nyingi sana. Kwanza, mfuko haufikii wananchi wenye shida, ndiyo kama nilivyosema, unawafikia wenye shida, unatoa mkopo wa kujuana. Nimesema siyo, lakini changamoto nyingine amesema wengine hawarejeshi. Ni kweli hilo nikubaliane naye kwamba kuna watu ambao

hawarejeshi hata katika mabenki makubwa. Kuna watu ambao hawarejeshi fedha wanapokopa.

Mheshimiwa Dkt. Mrema, anasema naomba Serikali ihakikishe fedha zinazotokana na Mfuko wa Rais wa kujitegemea uwafikie wananchi wanyonge. Hilo limerudiwa kwamba lengo la mfuko huu hata ukiusoma unaona kabisa unalenga kwa wale wananchi wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona kwanza nimalize hayo ya *TASAF*, MKURABITA, na mfuko wa Rais na labda kwenye Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kulibaki suala moja kuhusu kwamba, mbona Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ina Tume Tume nyingi, ina Sekretarieti nyingi, lakini tunachosema ni kwamba, pale kila Taasisi ina kazi zake, Tume ya Utumishi wa Umma ina kazi zake na vyombo vingine vina kazi zake. Hili lilichangiwa sana na Waziri Kivuli, anasema kwamba kwanini kisiundwe chombo kimoja? Mna Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira, Bodi ya Biashahara; sasa tunataka kusema kama ifuatavyo: Kazi zinazofanywa na Taasisi hizi siyo kweli kwamba zinafanana, kwani kila taasisi ina majukumu yake yaliyoainishwa bayana katika sheria zilizoanzishwa kama ifuatavyo:-

Kwa mfano, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, jukumu lake kubwa ni kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia msingi wa utawala bora na kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Kwa hiyo, ile ofisi ni *overall*. Tume ya Utumishi wa Umma ina wajibu

wa kusimamia na kuhakikisha kuwa waajiri, mamlaka ya ajira na nidhamu zinasimamia uendeshaji wa rasilimali watu kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Tume hupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko kutoka kwa Watumishi wa Umma ambao hawajaridhika na uamuzi uliotolewa dhidi yao na mamlaka zao za nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, ni kufanya tafiti kuwianisha, kuoanisha na kutoa mapendekezo kwa Rais juu ya kiwango cha mishahara, posho, maslahi kwa ajili ya mihimili mitatu ya dola; aidha, kumshauri Rais juu ya misingi ya miundo ya mishahara katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira, katika utumishi wa umma kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 29(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 18 ya mwaka 2006 ambayo kazi yake ni kutangaza nafasi za kazi zilizotokea katika utumishi wa umma kusajili wahitimu wataalam mbalimbali waliotoka katika Vyuo Vikuu, kuunda majopo kwa kutumia wataalam kutoka katika sekta mbalimbali kwa ajili ya kuendesha usaili na kushauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo ajira. Kwa hiyo, kila chombo pale kina kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliseme hili. La mwisho, Mheshimiwa Rosweeter alisema kwamba hawa Wauguzi ni wengi sana, kwanini nao wasiwe na Kurugenzi yao?

Mimi nasema Mheshimiwa hili sisi kwa kweli tumelipokea, kwa kweli lazima tufanye *job evaluation* na tufanye *job description* ni kweli kuna baadhi ya sehemu tumeshaona kwamba watu wamezidi ndiyo maana wanafanya pengine wanavyofanya.

Kwa mfano, ukienda pale Muhimbili, utakuta watumishi ni wengi kweli. Sasa pale inabidi tuanze na kufanyia *job evaluation* ili tuone nani anastahili kukaa pale, kazi yake ni ipi ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Lakini tukiacha hivi hivi bila kufanya *job evaluation* na kupata *job description,* kwa kweli itakuwa ni tatizo sana. Watu wanalundikana, halafu wanafanya vitu vya ajabu ajabu kwa ajili ya kukosa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana umetuongoza vizuri na kwa kweli Wizara yangu inakushukuru sana kwa kutuliza zile ghasia kidogo, miongozo na kadhalika, kwa kweli ile ni changamoto.

Waheshimiwa Wabunge, tunathamini michango yenu, tunaomba mtuvumilie na kwa wale ambao nimekosea majina yao, naomba wanisamehe, na wale ambao nimeacha majina yao, naomba radhi wanisamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kazi kubwa ya saa nzima, lakini umeweza ku-*manage* na kumaliza na kukuona sasa na glasi ya maji ya kunywa, nadhani unastahili unywe maji sasa.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

## FUNGU LA 20 - OFISI YA RAIS IKULU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kazi nzito ya majadiliano kwa takribani siku mbili toka jana na leo, sasa hebu tuingie kwenye vitabu vyetu tuweze sasa kupitisha mafungu mbalimbali kwa mujibu wa kanuni na Katiba yetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na kitabu cha pili, na kitabu hicho cha pili tunaanza na fungu la 20 Ofisi ya Rais, Ikulu na hilo fungu liko ukurasa wa nne. Katibu.

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management* ........Sh. 9,146,227,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU LA 9 – OFISI YA RAIS BODI YA MISHAHARA NA MASLAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*……… Sh. 2,387,259,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU LA 30 – OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Managemen*t…… Sh. 212,631,738,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 30, programme* ya kumi na kifungu kidogo cha 229900 - *Other operating expenses*, tupo pamoja?

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwanza, kabla sijamwuliza Mheshimiwa Waziri, nataka kusema neno moja kwa ruhusa yako, mimi kama Mwenyekiti wa Chama cha *UDP* naunga mkono kabisa hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 1 Julai, na msimamo wa Waziri wa Utawala Bora na naomba Waheshimiwa Madaktari warudi wafanye kazi mapesa hayawezi yakabadilishwa na uhai wa binadamu. Vyama vya Siasa tuachane na mgomo huu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hilo, nataka kusema kwamba, mengi yamesemwa juu ya usalama wa Taifa, mengi yamesemwa juu ya TAKUKURU, lakini ukiona kitabu hiki kwa kuangalia tu, naona kama pesa zao zote zimewekwa katika *vote* hii 229900 kwa ajili ya

kuonyesha uwazi zaidi, kwa kuwa hizi Taasisi ziko chini ya sheria, sioni kwanini tusiwe na *vote* moja ya TAKUKURU na tuwe na *vote* nyingine ya *TS* ili mambo haya yawe wazi zaidi kwa sababu wanafanya kazi ambayo ni ya maana na kwa ajili ya Taifa letu.

Pili, tunakokwenda, wengi wetu tungependa kuona Taasisi hizi zinapata *functional independence*, uhuru zaidi wa kufanya kazi bila kutegemea Ikulu, nani ni Rais na tunakokwenda hatujui tutapata Rais wa namna gani kwa hali ninayoiona. Kwa hiyo, ni vizuri tukaanza kujenga pole pole Taasisi hizi zikawa imara kifedha na pia zinaweza zikakaguliwa na pia kuwajibika kwa mambo yote ambayo yanafanywa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Cheyo kwa hoja zake. Moja, nataka nikubaliane naye kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinajitanua na vinafanya kazi zaidi.

Pili, nataka nikubaliane naye kwamba katika fungu hilo ndiyo inapatikana mishahara ya *TS* na *PSBB,* tumeiweka hapa kwa sababu najua katika dunia hii hapa siyo vizuri sana ukawatangazia mpaka maadui kwamba sisi watu wetu tunawalipa mishahara shilingi kadhaa, hasa kwa hao ambao mzee Cheyo unawafahamu. Nafikiri nimefahamika. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Fungu la 30 progamu ya 10 *sub vote* ya 1001 kasima 229900 *other operating expenses*.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia, sijakupata vizuri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kifungu 229900 - *other operating expenses*, kifungu hicho hicho ambacho Mheshimiwa Cheyo amemaliza kuzungumza.

Nilikuwa naomba tu kutoa mwito wa Serikali kwenye mwaka wa fedha unaofuata; kwa kuwa Bunge letu limeweka utaratibu wakati wa upitishwaji wa bajeti kwa upande wa bajeti za Jeshi kutokana na unyeti na usiri wake, *briefing* inatolewa kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, hiki kifungu ni vizuri undani wake uwe *treated,* hivyo tofauti na sasa ambapo unafanyika tu dhana ya ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka sana kwa kiwango cha pesa, Usalama wa Taifa kimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 135 mpaka Shilingi bilioni 142 kwa zaidi ya Shilingi bilioni 12. TAKUKURU imeongezeka kwa zaidi ya Shilingi bilioni tano.

Sasa sitahoji hapa kwanini kuna ongezeko hilo, ila ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri; mwaka wa fedha uliopita, niliomba kwamba TAKUKURU na Usalama wa Taifa waingilie kati kwa masuala ambayo niliyaainisha mwaka wa fedha uliopita 2011/2012 kwenye masuala yanayohusu maji na masuala yanayohusu ardhi, TAKUKURU na usalama wa Taifa.

Ningeomba *commitment* ya Waziri kwa kuwa ndiyo ameingia ofisini kwamba vyombo hivi vitashughulikia yale mambo niliyoomba yashughulikiwe

kwa ajili ya maisha ya wananchi kuhusiana na maji, na kuhusu ardhi Jimbo la Ubungo na Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla, naomba ufafanuzi kwa *commitment* ya Serikali kwamba hilo litafuatiliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mambo yaliyojitokeza hapa ni manne, kwa mujibu wa Kanuni utatakiwa kujibu swali moja tu katika hayo manne, chagua lile ambalo unaona unaweza kulijibu. Huo ndiyo utaratibu wa Kikanuni kwa sababu hapa kumezungumzwa mambo ya maji, fedha kuwa nyingi na kuwa kidogo na pia kumezungumzwa ofisi na kadhalika. Kwa hiyo, naomba uchague moja kati ya hayo. Sikutaka kumkatisha Mheshimiwa Mnyika, ninamheshimu sana lakini Mheshimiwa Waziri naomba ujibu moja kati ya hayo, lile unaloona wewe unaweza kulijibu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenisaidia. Awamu ya Kwanza ya Bajeti yetu ilikuwa ni Hotuba na Michango ya Wheshimiwa Wabunge na kuhitimisha, lakini sasa tupo katika mafungu.

Hoja ya kwamba, suala la maji litakuwaje; naamini kabisa ilikuwa ni hoja ambayo ilipaswa izungumzwe wakati wa majadiliano, hapa inatakiwa Mheshimiwa Mbunge ahoji kifungu hiki kinahusu nini na kina shughuli gani, jambo ambalo tayari tumeshalifafanua.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Program 10, Sub Vote 1001,* kifungu kidogo cha 220700 - *Rental Expenses.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi ndani ya Bunge hili niliwahi kuhoji kwamba, Serikali inatumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kupanga kwenye nyumba binafsi kama ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu hiki pesa zilizotengwa ni shilingi bilioni tano, kama naelewa sawasawa, *Rental Expenses* ni kwa maana ya kulipa pango kwa ajili ya majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kila Fungu kuna pesa ambazo zimetengwa kwa madhumuni hayo. Huko nyuma niliwahi kuiuliza Serikali na wakasema kwamba watachukua jitihada ili kuhakikisha kwamba wanaondokana na kupanga kwenye taasisi au kwenye nyumba binafsi kwa maana kwamba Serikali inajenga nyumba zake.

Je, mpaka leo Serikali imechukua hatua gani kwa sababu tunaendelea kutumia pesa nyingi kwa ajili ya kupanga majengo ya watu binafsi ilhali kama tungekuwa na mipango mahususi tungeweza kujenga Ofisi za Serikali na kwa maana hiyo tungeokoa pesa nyingi za Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu hili lipo hapa kwa sababu Serikali inatekeleza maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tulitenga fedha ili kazi ya kujenga nyumba za kudumu tuachane na upangaji imefanyika, Usalama

wa Taifa wamejengewa nyumba za kuishi. Kwa hiyo, sehemu kubwa ya fedha hizi ni kulipa deni *NSSF* ili Watendaji wetu waliopo katika Chombo hiki nyeti wapate makazi ya kudumu waachane na nyumba za kupanga.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ………………………..Sh. 441,780,000
Kif. 1003 - *Policy and Planning*……………………………Sh. 429,560,000
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ……………………………Sh. 276,816,000
Kif. 1005 - *Information and Communication Technology Unit* ……...................................................... Sh. 261,301,000
Kif. 2001 - *Cabinet Secretariat* ……………………........ Sh. 1,469,267,000
Kif. 2002 - *Government Communication* ……......….Sh. 340,270,000
Kif. 2003 - *Good Governance* …………………….……Sh. 484,256,000
Kif. 2004 - *Public Service Appeal* ……………………….. Sh. 430,894,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 - *Public Sector Reform Coordination* …

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2005 Sub vote 2005.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, hatujafika huko ndiyo tunaingia sasa. Katibu!

Kif. 2005 - *Public Sector Reform Coordination Unit* .... Sh. 334,548,000

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub vote 2005*, kifungu kidogo cha 221200 - *Communication and information.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani labda ni kwa sababu ya *system* yetu, ukiangalia kwenye *Votes* zote *Communication and Information* ipo. Ninataka nijue tunaposema *Communication and Information* ni kwa ajili ya jambo gani maana kama ni ofisi moja au kama ni *photocopy* atatumia moja ama kila Idara ni lazima iwe na *photocopier* yake? Ninataka kuelewa,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri; umeiona hiyo? Mheshimiwa kombani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, analolisema ni *Communication and Information* na fungu hili ni kwa ajili ya majarida na magazeti. Sasa ndiyo maana unaikuta karibu kila *Sub vote.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 32 - Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma)

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*......Sh. 12,484,244,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba kaa, Mheshiwa Nassir, Mheshiwa Shekifu, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Keissy Mtaalamu, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Murtaza, Mheshimiwa Jitu, Mheshimiwa Njwayo, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Subira, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Christowaja, Mheshimiwa Christina, Mheshimiwa Paula na Mheshimiwa Machali.

Mheshimiwa Machali tuanze.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nitakwenda kwenye *Vote* 32, *Sub vote 1001, especially* kwenye kasma namba 221400 - *Hospitality Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 30, kitu ambacho inaonekana kwamba hizi nafikiri ndiyo takrima au sijui niziiteje. Ongezeko hili limekuwa kama kubwa kidogo, sasa naomba maelezo ya Serikali ili itueleze ni sababu gani ambazo zimepelekea pesa hizo kuongezeka kutoka shilingi milioni 47,500,000 mwaka jana na kuja mpaka kwenye milioni 90 na shilingi kama 108 hivi.

Vilevile ...

**MWENYEKITI:** Swali ni moja tu kwa mujibu wa Kanuni.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mwenyewe kwamba, fungu hili ni kwa ajili ya takrima Ofisi ya Waziri na Ofisi zote. Pia akiangalia kwenye vifungu vingine vyote fungu hili ni kidogo sana, kwa hiyo, anayehudumia mambo yote ya wageni, takrima  na kadhalika ni Ofisi ya Utawala Makao Makuu, ambayo ni Ofisi ya Waziri. Siyo vyema Mheshimiwa Mkosamali akija ofisini nishindwe hata kumpa soda, itakuwa siyo busara.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuhoji kifungu cha chini ya programu hiyo hiyo, yaani *Program 10, Sub vote 1001.*

**MWENYEKITI:** Naomba msirudie hiyo *sub vote* bali nendeni moja kwa moja kwenye hoja.

**MHE. GODREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa. Nataka kupata maelezo kwenye fungu 227500 - *Other Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha zilizotengwa ni bilioni tisa na milioni kama ishirini, lakini mwaka wa nyuma ilikuwa bilioni sita na mwaka wa nyuma zaidi ilikuwa bilioni kumi. Sasa nataka kupata maelezo kwa sababu kumekuwa na ongezeko la pesa

kubwa sana, yaani hoja yangu ni kwamba, mwaka uliotangulia, yaani 2009/2010, maana yake ilikuwa ni bilioni kumi, mwaka 2010/2011 ilikuwa bilioni sita, mwaka huu wanatuletea bilioni tisa tena. Ninataka kujua ni vitu gani ambavyo vimefanya sasa tupande kutoka bilioni sita kwenda mpaka bilioni tisa; ndiyo maelezo ninayoyataka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili linahudumia wastaafu na mtu akishastaafu akiwa mzee maradhi ni mengi sana; kwa hiyo, huduma kubwa tunayotumia hapa hasa ni kuwatunza wastaafu. Tukumbuke kwamba, Viongozi wetu Wastaafu ni watu wazima, wanahitaji huduma kama ilivyo kwa wengine. Kwa kuwa wameshalitumikia Taifa hili, wanahitaji huduma muhimu na huduma kubwa ni kuwapeleka nje kwenye matibabu na wastaafu nafikiri mnawafahamu.

Kule nyuma kabisa alikosema kwamba mbona ilikuwa bilioni kumi, ni hilo hilo, akumbuke huko nyuma kulikuwa na wastaafu wangapi na sasa hivi wamebakia wangapi. Kwa hiyo, hizo hizo gharama ninazozisema ndizo zilizofanya iwe bilioni kumi ikashuka na sasa hivi tumeongeza tena kutokana na hali halisi ya mwaka uliopita.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri afikirie posho ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji lakini hakulijibu hapo, angalau hata shilingi 50,000 kwa mwezi, kwani

wana kazi ngumu kweli kama kule kwetu Watendaji hawakai vituoni, Wenyeviti ndiyo kwenye michango, kwenye mikutano na kwenye kila kitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali halipo kwenye Wizara yako lakini kama una majibu kwa sababu ni Serikali unaweza ukalijibu. Hili swali halipo kabisa kwenye Wizara yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Wabunge wengi kwamba, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wapewe posho. Tukumbuke kwamba, nchi yetu ina vijijini 12,500, pia ina vitongoji karibu 60,000 na ina mitaa karibu 20,000. Sasa hilo ni lazima tuangalie na tulifanyie utafiti wa kina sana, kwa sababu tulipiga hesabu tukaona ni mabilioni mengi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy, rai yako tumeipokea lakini ukumbuke kwamba, kazi hizi za Wenyeviti ni za kujitolea, ndugu zangu tukisema tuwalipe watu hawa itakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti wa Vijiji waendelee kujitolea mpaka hapo hali yetu ya kiuchumi itakapokuwa nzuri basi na wao watafikiriwa.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba *Report* ya *CAG* ilianza kuletwa Bungeni kujadiliwa ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mughwai ni kifungu namba ngapi?

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana yake, kwa sababu hapa huwezi kuanza tu bila kuonesha ni kifungu gani. Sasa huo mshahara wa Waziri uko kifungu gani?

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub vote 1001.*

**MWENYEKITI:** *Vote* gani? *Item* gani?

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaiweka sawa, naomba niiangalie kwanza.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na anayefuata Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kusema tayari Mheshimiwa Zambi ameshakisema.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Namwita Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo kwenye mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ni *Vote* gani na *Sub vote* gani?

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 1001 Sub vote 210100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliongelea suala la mfumo wa uajiri kwa kada mbalimbali hususan nilikwenda moja kwa moja kwa waajiri wa wachumi. Inaonesha kwamba, sifa za kuingilia kwa wachumi aidha ni wa moja kwa moja kutoka mashuleni ama wanaotoka makazini, wanalazimika kuwa na *major* kati ya somo mojawapo ama *statistics*, uchumi au sayansi ya uchumi, ambayo ipo *specified* kwenye chuo fulani. Kwa mfano, unaweza ukaambiwa uwe na *major* takwimu kutoka Chuo Kikuu cha Mlimani Dar es Salaam, ama sayansi ya uchumi kilimo kutoka Sokoine University. Sasa niliuliza kwamba; je, wale ambao wanakuwa wanasoma nje ya vyuo hivyo ambao hawaja-*major* hayo masomo lakini ndani ya masomo yao wana masomo ambayo yanafanana na *statistics*, uchumi na kadhalika; wanafikiriwaje ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Nafasi zinapotangazwa inatokana na mahitaji halisi, kama wanamhitaji mtu wa *qualification* fulani ni lazima wata-*base* kwenye *qualification* Fulani, ila ninachoshauri wangeiweka hivi; waweke kwamba mwenye *qualification* fulani ana *added advantage*. Kwa hiyo, hilo tunaweza tukalipokea lakini inategemea mwajiri anamhitaji mtu wa namna gani. Sasa yule mwenye *added advantage* anaweza akafikiriwa zaidi,

lakini hatuna ubaguzi wa vyuo wala kitu kingine chochote.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni suala linalowezekana ndani ya Utumishi. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye *Vote 32, Sub vote 1001* na kifungu cha mshahara ambacho ni 210100.

Niliandika kwenye mchango wangu kwamba ni lini Serikali itaanza kuboresha na kulipa wafanyakazi wa vijijini posho maalum kwa sababu mazingira ambayo wanakabiliana nayo ni magumu na huwezi kulinganisha na wale ambao wanaishi katika maeneo ya mijini. Watumishi wale ilistahili kabisa wawe wanapata upendeleo maalum kwa kukubali kuishi katika maeneo ambayo hayawiani na maeneo ya kawaida ambayo wamezoea kuishi. Kwa hiyo, ninaomba nipate majibu ya Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mangungu kwamba ni kweli nchi yetu ni kubwa na ina mazingira tofauti. Kwa hiyo, kutokana na Sera ya Mishahara na Motisha, mazingira hayo yameshatambuliwa, vigezo vimeshawekwa na tunayo Sera hiyo *in place*, sasa kinachongojewa ni utekelezaji tu na utekelezaji wake kama nilivyoeleza; Bodi ya Mishara imeanzishwa na

hiyo Bodi ndiyo itakayoangalia mazingira yote hayo ili kuwapatia motisha.

Waheshimiwa Wabunge, wangeangalia kwamba hata hiyo Sera ya Mazingira Magumu tumeshaanza kuitekeleza; mazingira magumu siyo lazima iwe mshahara tu, sehemu zenye Maziwa, Visiwa kama *Delta,* tumenunua maboti sisi kama Serikali ili kuwarahisishia watumishi usafiri; kwa mfano, Mafia na hata Kilwa na sehemu nyingine kama Kigoma. Kwa hiyo, hiyo Sera imeshaanza kutekelezwa Serikalini.

La ziada ni hilo la motisha na tunaiangalia hiyo motisha siyo lazima iwe fedha tu kama nilivyoeleza, lakini tunaangalia motisha kwa ukubwa wake.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lazima nikiri kuwa, sasa hivi Serikali ya Muungano imeonesha dalili njema ya kushughulikia Taasisi za Muungano. Asubuhi hii tuliambiwa kwamba, Serikali ya Muungano imefungua Ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi. Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake ukurasa wa 66, anaelezea juu ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma katika. Kifungu cha tatu amesema kufungua Ofisi Zanzibar kwa ajili ya ajira za Muungano, ni jambo jema.

Swali langu ni kwamba; je, ni lini atafungua Ofisi hizi na zitafanya kazi katika utaratibu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli

tutafungua Tawi kule Zanzibar na tumesema kwamba, Ofisi hizi tumeshaanza mchakato wa kuzitafuta na zitaanza rasmi katika *Financial Year* hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, tunafungua Tawi kule na tutakuwa tunaenda kufanya usalli kule Zanzibar.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo *Vote 32, Program 10, Sub vote 1001, Item 210100.* Katika mchango wangu wa maandishi, niliuliza sehemu ya kuboresha ile Sekretarieti ya Ajira kwamba, je ni lini itaweza kufika ngazi ya aidha Kanda kwanza na baadaye ngazi ya Mikoa ili huu utatanishi wote ambao unatokea katika mambo ya ajira na vipaumbele ambayo yanatakiwa katika ngazi ya Mikoa na Wilaya iweze kutatuliwa mapema na iwe ni kama *data base* ya Wizara. Je, ni lini itafanyika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina nia nzuri tu ya kuhakikisha kwamba, tunafika kwenye Kanda na kwenye Mikoa. Kama nilivyosema, mwaka huu tutaanza kwa kufungua Ofisi kule Zanzibar, lakini *option* ya pili ni kwamba, tutaleta Muswada hapa ili kubadilisha ile Sheria yetu kwa lengo la kuhakikisha kwamba, zile *common carders* zinaajiriwa na Mamlaka za Ajira husika. Hiyo itakuwa imepunguza huo mlolongo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 32 Program 10, Sub vote 1001.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimesema *Vote 32* na *Program 10* iacheni, nendeni moja kwa moja kwenye *Sub votes.*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 32, Program 10, Sub vote 1001, Item 210100* - Mshahara wa Waziri.

Kimsingi, sina shida sana na mshahara wake, lakini labda nianze kwa kusema kwamba, naipongeza hiyo Wizara kwa sababu siku za hivi karibuni imefungua Tawi la Chuo cha Utumishi wa Umma Mtwara. Chuo hiki si miongoni mwa wale wanaopata mikopo kwa sababu hakipo katika *category* ya *Higher Learning Institutions*. Mtwara sasa hivi kuna mfumko mkubwa wa shughuli mbalimbali za kijamii, kiasi kwamba, wanafunzi wanaosoma pale wanapata shida sana kushindana na watu wa kawaida katika upatikanaji wa mahali pa kuishi ili waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Je, Wizara imejiandaaje kujenga bweni pale ili kupunguza adha wanayoipata wanafunzi hao kwa kipindi hiki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumelipata na tunaomba tulifanyie kazi badala ya kutoa majibu ya haraka haraka hapa.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika, lakini pengine kushika mshahara wa Waziri sikuwa napenda kufanya hivyo, isipokuwa kwa sababu ni *general,* nizungumzie tu kwamba, katika

mchango wangu niligusia suala la uhaba wa Watumishi hasa Wauguzi na Waganga katika Zahanati. Sasa hili sina uhakika kama Waziri anaweza kusaidia maana hajajibu lolote; ni tatizo kubwa, majengo yamejengwa yako pale lakini hayana Watumishi na Sera zinasema tufungue Hospitali kila Kata.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoainishwa kwenye vipaumbele vyetu katika kuajiri Watumishi vitakuwa ni Afya, Elimu na Vyombo vya Usalama. Kwa hiyo, kwa mwaka huu tutazingatia kati ya wale watumishi 56,000 ambao tutaajiri wengi ni wa afya na tutahakikisha tunawapeleka sehemu ambazo hazina watumishi kama ilivyo kwa Walimu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ni *Vote 32,* Kasma 230400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana magari haya yanayotumia *repairs* za gharama kubwa tuyapunguze kuanzia mwaka huu, lakini hapa *routine maintenance and repair of vehicles* naona fedha zinaongezeka kutoka milioni 120 kwenda milioni 216. Sasa inakuwaje kwa nini iongezeke wakati tuna mkakati mzito wa kuuza haya magari ambayo yanatuletea hasara kubwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Tumekubaliana baada ya Bajeti, magari hayo yapo na yanaendelea kutumika, kwa hiyo, yanahitaji hizo fedha. Pale ambapo tutatekeleza uuzaji wa hayo magari, basi gharama hizo zitapungua.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub vote 1001, Item 210100* - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi na Waziri hakutolea ufafanuzi, kuna *trend* imeanza kuonekana watu wengi wanapofika muda wa kustaafu wanaongezewa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili, wakati huo huo tuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu. Pia hata wale wastaafu wengine wakistaafu wanapelekwa kwenye Bodi za Mashirika yetu. Sasa nataka kuuliza; Taifa hili Vijana nao tuna nafasi gani maana kama mtu amefanya kazi miaka 40 amefika wakati amestaafu; hivi kwa nini asiachwe apumzike ili na yeye amalizie maisha yake vizuri? Lazima kweli tuwapeleke kwenye Bodi ama tuwaongezee muda? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Serukamba, kama ifuatavyo:-

Ajira za mikataba ni kwa wale watumishi ambao Serikali bado inawahitaji na siyo mtumishi mwenyewe afanye *lobbying* aongezewe mkataba. Serikali yenyewe ikijiridhisha kwa mujibu wa Sera zetu kwamba,

huyu mtumishi anahitajika Serikalini, tunamwongezea mkataba na si vinginevyo na hasa kwa zile *rare professions* kama Walimu, Madaktari, wao ndiyo tunawaongezea muda na wale ambao kwenye ofisi husika wanamhitaji yule mtumishi na siyo yeye afanye *lobbying.* Naomba nieleweke hivyo kwamba ni Serikali yenyewe inamhitaji na inamwomba aongeze muda wake na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wa kwenye Bodi, Bodi zina miongozo yake. Kwa wale wastaafu tunaowaona wana nguvu, uwezo na uzoefu, sheria haiwezi ikatufunga kwamba tusiwateue Wajumbe wa Bodi.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilioutoa nilitaka nipatiwe ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 15 wa Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kifungu cha pili, zimeelezwa faida za MKURABITA ambapo mashamba 11,014 yalipimwa, lakini Hati za Kimila zilizotolewa ni 7,632. Ukienda kwenye Randama, ukurasa wa sita, ni mashamba 8,388 na Hati za Kimila zilizotolewa ni 2,311.

Naomba maelezo kuhusiana na hili; je, kuna tofauti baina ya randama na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri? Ukweli uko wapi katika hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kama ulivyo kwenye Hotuba yangu katika ukurasa wa 15. Kule kwenye randama walikuwa

hawajajumuisha taarifa kutoka Mikoa na Wilaya nyingine ambako zinatolewa Hati za Kimila.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kwamba, kumekuwepo na tatizo na malalamiko ya Wafanyakazi wa Hospitali ya Mkoa wa Kigoma hususan wale wanaoishi na VVU kwamba, kila mwisho wa mwezi walikuwa wanapewa fedha zao kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa njia ya hundi, lakini sasa hivi wanapewa *cash,* suala ambalo ni kinyume na Waraka wa Serikali na hivyo usiri unakosekana kwa wahusika.

Je, Waziri anatuambia suala hili litatafutiwa ufumbuzi?

**MWENYEKITI:** *Sub vote* gani?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Kifungu 1001, kasma 210100.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imetokana na kwamba, tunataka tuwafahamu wenyewe na wapokee mkononi. Zile hundi zilikuwa zinaleta utata kidogo na ndiyo maana tumebadilisha utaratibu.

**MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub vote 1001, Item 210100.* Kwenye mchango wangu asubuhi ya leo ilikuwa ni pamoja na kuzungumzia *Good Governance*. Nilisema kwamba, sehemu ya *Good Governance* ni pamoja na kutimiza ahadi hasa ahadi za Kiongozi Mkubwa. Nilitoa ushauri ambao haukujibiwa kwamba, ni vyema basi ahadi za Mheshimiwa Rais zikaingia kwenye Bajeti yake. Wakati wa kupewa ufafanuzi nimejibiwa lile la kuachwa Korogwe Mjini kama sehemu ya utawala. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri atufahamishe kama amepokea huo ushauri na anaufanyia kazi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahazi za Rais tumeziweka katika Miaka Mitano ya Uongozi wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nassir asiwe na wasiwasi, ahadi hizo zitatimizwa tu na zitawekwa kwenye Bajeti mwaka hadi mwaka.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 32, Sub vote 1001, item 210100* - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia tatizo linalotusumbua la ucheleweshaji wa mishahara ya Wafanyakazi na nikapendekeza kwamba, kwa nia njema tu tuunde Bajeti ya Dharura mithili ya ile ya umeme wa dharura, tukusanye fungu moja hata ikibidi shilingi trilioni mbili tuwalipe wafanyakazi wote, wawe wa jeshi na wengine, kusudi tumalizane nao na twende mbele. Mheshimiwa Waziri

hakunijibu na ndiyo maana nakamata mshahara wake.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri mshahara wako umekamatwa na Mheshimiwa Mwijage hapo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Samahani Mheshimiwa Mwijage, mambo yalikuwa mengi nilijibu nusu kwamba, malimbikizo yamelipwa kwa kiasi gani.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nasema kwamba, tatizo la malimbikizo litakwisha baada ya kufunga ule mfumo wa kompyuta wa kuingiza malimbikizo moja kwa moja kwenye mshahara mwezi husika na tarehe husika. Malimbikizo haya yalikuwa ya muda mrefu sana na yalikuwa yanafanywa *manually.* Kule kwangu Utumishi, chumba kilichojaa yale makabrasha ya *manual* tumesha-*feed* kwenye kompyuta na wenzetu wa Hazina wanalipa mwezi hadi mwezi. Kwa hiyo, sasa hivi ukienda pale Utumishi kile chumba kilichojaa yale mafurushi ya marekebisho ya mishahara yamepungua kabisa, yamebaki kidogo. Niseme kwamba, hakuna haja ya udharura ya kuunda bajeti nyingine kwani bajeti ya mwaka huu itakidhi mahitaji husika na baada ya muda hili tatizo litapungua sana kulingana na mfumo tuliofunga hivi sasa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub vote 1001*, Kasma 210300 - Mshahara wa wa Waziri. Sina dhamira ya kuondoka na mshahara wa Waziri ila ningependa kupata ufafanuzi au kauli ya kisera.

**MWENYEKITI:** Kasma namba ngapi Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma 210100.

**MWENYEKITI:** Ndiyo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi kuhusu jambo moja la kisera ambalo tumelichangia Mkutano uliopita wa Bunge na Mkutano huu vilevile kuhusiana na kiwango cha kodi kwenye mishahara kwa Watumishi wa Umma *(Pay As You Earn)*, Madaktari, Walimu na Watumishi wote wa Umma. *Commitment* ya Serikali kwenye Mkutano uliopita wa Bunge ilikuwa ni kwamba, suala la kupunguza kodi kwa wafanyakazi italishughulikia kwenye Mwaka huu wa Fedha na mapendekezo yaliyokuwepo ni kutoka asilimia kumi na nne mpaka asilimia tisa na asilimia thelathini mpaka ishirini na saba kwa wafanyakazi wa kima cha juu.

Kwa kuwa kuna tatizo kubwa la maisha magumu kwa wafanyakazi. Je, Serikali ipo tayari kutoa kauli ya kisera kwamba kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha ambayo kwa sasa hicho kifungu hakipo; hilo suala litaingizwa kwa ajili ya kupunguza kodi kwa Wafanyakazi wa Umma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulilipokea na bado tunalifanyia kazi ili tujiridhishe kwamba kweli huo mzigo unamwelemea nani. Kwa

hiyo, bado tunalifanyia kazi na tukishamaliza basi tutatoa Kauli ya Serikali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Natumia *Vote 32, Sub vote 1001,* Kasma Ndogo ya 210100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la *job royalties* na *job descriptions* kwa Watumishi wa Serikali hususan Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao wanateuliwa miongoni mwa Wabunge.

Nilipenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwa kuwa yeye ni Mwakilishi wa Rais hapa kwamba ni kwa nini hao watu wanatokana na Bunge wakati Bunge kazi yake ni kuisimamia na kuihoji Serikali na wakati huo kuna upungufu mkubwa wa ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu wewe mwenyewe ulisitisha maswali Na. 113 la Mheshimiwa Subira Mgalu na Swali Na. 114 la Mheshimiwa Martha Umbulla yasijibiwe kwa sababu hao wako upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipate ufafanuzi kwa nini hili linafanyika wakati Watanzania wengi hawana nafasi za ajira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Kabla hujajibu hatua yangu ya kusitisha maswali haiendani na suala la ajira kama anavyolitafsiri Mheshimiwa Mbunge; ni kama vile Waheshimiwa Mawaziri

walivyoteuliwa kutoka miongoni mwetu Wabunge. Kwa hiyo, utaratibu nilioutumia ni tofauti na hivyo ambavyo Mheshimiwa Mbunge anataka kulinganisha kwenye swali. Nadhani Mheshimiwa Waziri, usijikite katika *reference* ya Mwongozo wangu jana, ujikite katika eneo lingine la swali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umetusaidia kujibu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inamruhusu Mheshimiwa Rais kuteua Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa jinsi atakavyoona inafaa. Sasa kilichotokea jana ambacho Mwenyekiti ulitumia busara kwamba, ukishateuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, wewe ni sehemu ya Serikali, huwezi ukasimama tena kuiuliza maswali Serikali. Kwa uzoefu tu kule nyuma, pengine inawezekana vijana wengine walikuwa bado hata hawajazaliwa, enzi ya Chama Kimoja wakati Wakuu wa Mikoa walipokuwa ni Wabunge humu ndani, mtu akiuliza swali linalohusu Babati basi Mkuu wa Mkoa wa Manyara alikuwa anasimama kujibu kuhusu Babati kwa sababu Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Waziri wote hao wanateuliwa na Rais na wanakuwa ni kitu kimoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit* ………………Sh. 213, 205,000
Kif. 1003 - *Government Communication Unit* …….Sh. 193,327,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ……….. Sh. 143,958,000

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia *Sub vote 1004*, Kifungu Kidogo 220800 - *Training Domestic.*

Hapa Mheshimiwa Waziri ameweka Sh. 400,000 katika kitengo hiki muhimu cha *procurement*. Je, fedha hizi umekusudia kumsomesha nani na wapi?

**MWENYEKITI:** Swali moja tu, Mheshimiwa Waziri hii hela umekusudia kumsomesha nani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili linatosha kabisa hata kumsafirisha yule mtu anayeenda masomoni na kurudi masomoni. *Training per se* ipo kwenye *Vote* ya *Administration*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* ……..................................…..Sh.80,543,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Planning Division* ………….............………...Sh. 276,145,000

**MHE. SELEMANI SAID JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni dogo. Katika *Sub vote 210500 - Personal Allowances In-kind,* naona *variation* ni kubwa, tumetoka milioni 13 tumeenda milioni 35, kuna *variation* ya milioni 22. Nataka *clarification* katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Maelezo kwa nini fungu hilo limeongezeka; Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ni kwa ajili ya *personal allowance* kwenye *utilities,* wale Maafisa ambao wanastahili kulipiwa kodi ya nyumba, simu, maji na umeme. Kwa hiyo, kwenye Idara hii kuna Watumishi ambao wamepata *promotion,* wapo *entitled* kupata hizo *allowance* ndiyo maana kuna ongezeko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Information and Communication Tech. Unit* ............................................................................ Sh. 87,268,000
Kif. 2001 - *Policy Development Division* ……………. Sh. 396,013,000
Kif. 2002 - *Management Service Division* ………… Sh. 342,403,000
Kif. 2003 - *Establishment Division* ……………....……Sh. 584,716,000
Kif. 2004 - *Ethic Promotion Division* ………...…..…...Sh. 158,435,000

Kif. 2005 - *Human Capital Management Division* … ............................................................ Sh. 1,405,332,000
Kif. 3001 - *Human Resources Development Division* ............................................................… Sh.3,731,841,000
Kif. 3004 - *Diversity Management Unit*… ……………..Sh. 103,502,000
Kif. 4002 - *Management Information System Division* …...................................................................... Sh. 957,794,000
Kif. 4003 - *Records and Archives Division* …............. Sh. 787,139,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 - Ofisi ya Rais (Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma)**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* …. Sh. 2,058,627,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Machali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nataka kufahamu kuhusu *Vote* 33, Kasma 220700 kuhusu *Rental Expenses.* Kwa nini zimepanda mpaka milioni 500 kutoka 1,320,000; naona mmeongeza pango au imekuwaje maana ni ongezeko kubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeiona hapo 220700, ukurasa wa 164.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua gharama za pango sasa hivi zinapanda sana na hiyo Ofisi ya Maadili nayo inapanga katika jengo lile. Kwa hiyo, hizo gharama ni kwa ajili ya kupangisha ofisi na kwa ajili ya wale ambao ni *entitled* kupewa kodi ya nyumba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nakwenda kwenye *Sub vote 1001,* Kasma Namba 221400 kwenye *Hospitality Supplies and Services* kwa maana nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kuna ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 45 imetoka kwenye milioni tano. Ongezeko hili sioni kama linawiana katika mazingira ya kawaida, ukifanya *comparison* kutoka kwenye milioni tano kuja ongezeko la shilingi milioni 45, huko ndiko ambako inawezekana fedha nyingi zinapotea hazitumiki kama zilivyopangwa. Sasa nilikuwa naomba Serikali itupe ufafanuzi ni kwa nini kunakuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia sijui mia ngapi huko wakati tukiangalia kwenye maeneo mbalimbali tungezichukua hizi fedha zikaenda hata kusaidia kukarabati Vyuo mbalimbali vya Ualimu kama vile Kasulu. Sasa fedha nyingi milioni 45 zinaongezwa kwa ajili ya *hospitality* (takrima).

Mheshimiwa Waziri, nitatoa shilingi kwenye mshahara wako iwapo hutaweza kutoa maelezo ya kina katika hili. Kwa sababu kule mwanzoni umejibu sijaridhika na majibu yale ila nimekaa kimya. Naomba kwenye hili, milioni 45 kwa ajili ya takrima mnatumia vigezo gani imetoka milioni tano kuja milioni 50; ni asilimia ngapi hizo? Naomba ufafanuzi vinginevyo, naomba kutangaza kwamba nitatoa shilingi yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maadili tulikuwa tumewabana sana kwenye mambo ya *entertainment.* Wajumbe watakubaliana na mimi kwamba, huko nyuma tulisema kwamba hawa watu waongezewe bajeti na sehemu mojawapo ambayo tulikuwa tumewabana sana hao wenzetu wa Maadili ni ya *hospitality.* Kwa hiyo, tumeongeza kwa makusudi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paulina Gekul, hukusimama kipindi kile cha mwanzo. Fungu gani na lipi? Hamkusimama fungu hili walisimama watu wawili tu. Mbona hukusema nilipokuwa nataja majina?

Waheshimiwa Wabunge, naomba niendelee kwa kweli jicho langu halikukuona tunaendelea na fungu linalofuata.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ……................…..Sh. 214,519,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation*

*Unit*…..........................................................................Sh. 129,425,000

**MWENYEKITI:** Fungu hili nimemwona Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipate ufafanuzi, *Sub vote 1003,* Kifungu Kidogo 220100 - *Office and General Supplies and Services*, lakini chini yake kuna masuala ya *Utilities Supplies and Services* hiki hakina namba au ni nini? Hilo moja.

Pili, huko kuna *zero* ni kwamba hii *utilities* kwa mwaka huu hakuna kitu?

**MWENYEKITI:** Swali moja tu Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Sasa basi niulize hiki kifungu cha *Utilities Supplies and Services* ni kwamba kwa mwaka huu hakutakuwa na mahitaji ya *Utilities*, *Supplies and Services*?

**MWENYEKITI:** Washa *mic* Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kwa kweli hii *Sub vote* imerukwa. *Utilities, Supplies and Services* ni kifungu cha peke yake. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, aende kwenye *Administration Utilities, Supplies and Services* ataona hao watu wa *Planning* wanapata *utilities* zao katika *Sub vote* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaeleweshe Waheshimiwa Wabunge, *Utilities and Supplies* ni umeme, maji na kadhalika. Kuna ofisi nyingine jengo ni moja, sasa hamuwezi mkalipa umeme tofauti, maji tofauti, wakati jengo ni moja. Kwa hiyo, hiyo ni sababu tosha ya kufanya iwe katika *Administration* tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa najiuliza kwamba sijui ni lini Vitabu hivi vya Bajeti vitaandikwa kwa Kiswahili maeneo mengine yanaandikwa hatuyajui. Sasa niulize kwenye *Sub vote 1003,* lakini kifungu kidogo cha 210400. Kifungu hicho hakijapangiwa fedha, lakini nilitaka tu nijue imeandikwa *Onal Immigration Training* sasa sijajui ni nini kama wenzangu wanajua basi ni bahati yao kwao. Mimi sijui naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ni nini hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, 210400 kwenye *Planning, Monitoring and Evaluation Unit,* kifungu cha

tatu kutoka juu. *Onal Immigration Training* ni *Zonal, of course,* itakuwa *Zonal* ni *typing error*. Umekiona Mheshimiwa Waziri. Tunaomba majibu anauliza. Washa *mic* Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *Zonal Immigration Training* kwenye Kanda.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1004 - *Government Communication Unit* ……...Sh.127,674,000
Kif.1005 - *Procurement and Management Unit* ......Sh. 150,784,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Internal Audit* ………………......……………Sh. 154,112,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline nimekuona.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub vote 1006*, hiyo Kasma ya 220300, kwanza maelezo yaliyopo hapo hayaeleweki. Maelezo yake ni kwamba, kuna *13, the salaries and ex 5,980,000* hayo ni maelezo, lakini hicho kifungu kimepanda kutoka bilioni moja mpaka bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu kinajichanganya, kwa hiyo, Waziri atueleze kwanza ni cha nini na sababu za ongezeko hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeona hicho kifungu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba, kifungu hiki kimekosewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunaomba sasa utupatie maelezo, kwa maana hiyo hii fedha sasa inaingia kwenye nini ni *typing error* au ni kitu gani hebu tupeni ufafanuzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, ukiangalia kote huko unaona mambo ya *Fuel, Oils, Lubricants* hakuna. Kwa hiyo, 220300 ni *Fuel, Oils, Lubricants*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, muda niliobakia nao ni dakika kumi, lakini Kanuni Namba 104(2) inanipa idhini ya kuongeza muda ili tufanye kazi hii kwa ufanisi. Kwa hiyo, nitaongeza muda wa dakika 30 ili shughuli hii iweze kuendelea na Waheshimiwa Wabunge waweze kuendelea kuchambua Hotuba hii ya Bajeti. Katibu tuendelee.

Kif. 1007 - *Information and Communication Tech.*

*Unit*……..........................................................................Sh. 109,554,000
Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ………………........……....Sh.335,317,000
Kif. 2001 - *Public Service Leaders Division* ………… Sh.512,531,000
Kif. 2002 - *Political Leaders Division* ………………… Sh.560,324,000
Kif. 2003 - Zonal Services ……………………..........…. Sh.1,570,570,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 - Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango)**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* Sh. 1,096,735,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nakwenda moja kwa moja kwenye Kasma Namba 229900 - *Other Operating Expenses*. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie tuweze kupata *justification* anapozungumzia *Other Operating Expenses* anakusudia mambo gani? Kwa sababu hii ni *general term,* tungeomba tupate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hii *Other Operating Expenses* inajumuisha vilevile *research* ambayo ndiyo shughuli muhimu ya Tume hii na kwa hali hiyo ndiyo maana namba zinazoonekana hapo ni kubwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ……...……………Sh. 315,650,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka maelezo kidogo tu, Kifungu 210100 - Basic Salaries imeongezeka sana. Je, ni ajira mpya au ni ongezeko la mishahara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hizi ni ajira mpya. Nafikiri katika mawasilisho yetu asubuhi tumeonesha kuwa, mwaka jana kulikuwa na *analysts* 25 wapya walikuwa wanatakiwa kuajiriwa na kwa hali hiyo kulikuwa na masuala ya nyongeza zao.

Vilevile mwaka huu kumeidhinishwa wataalam 21 nao pia watahitaji kulipwa mishahara mipya. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Planning and Monitoring Division* …….. Sh. 335,981,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murtaza na Mheshimiwa Paulina Gekul. Mheshimiwa Murtaza.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 1003, Kasma ya 220900 - *Training Foreign,* nimeona ipo *zero* na hata fedha ambazo zilikuwa zimepangwa mwaka jana zilikuwa ni *only twelve million*. Sasa hatujui hawa watu wanafanya kazi vipi bila kupata *experience and training overseas*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Masuala ya mafunzo ya nje yanashughulikiwa na *UNDP, UNFPA,* pamoja na Mahusiano ya waliyoingia Tume kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China. Kwa hiyo, kwa hapa hazitaonekana lakini yatakuwa *covered* na kusema kweli mafunzo yenyewe yameshaanza kwa awamu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma 221400 -*Hospitality, Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hii imeongezeka kutoka shilingi milioni saba mpaka shilingi 17,300,000. Ukiangalia Idara ya Utumishi wao wamepangiwa shilingi milioni nne. Idara ndogo tu hii ya *Planning* na *Monitoring* wana shilingi milioni 17, ongezeko kubwa sana kutoka shilingi milioni saba. Naomba Waziri

atupatie ufafanuzi kwa nini hivi vihela vya chai na maandazi vinapandishwa kwa kiasi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Kashfa jamani, maandazi tena yanahusu nini hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufafanua kuwa hii Tume ina machapisho mengi ambayo yanatakiwa yafanywe. Mengine yaliagizwa humu ndani na Waheshimwa Wabunge, ambayo yapo tayari. *Updates* za mipango ile ya miaka mitano, kuna *updates* za miaka 15, kwa hiyo, yote yanaingia katika masuala hayo. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Government Communication Unit* ……. Sh. 398,788,000

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma 220300 - *Fuel, Oils and Lubricants.* Mwaka wa fedha uliopita ilikuwa *8.5 million,* lakini imepanda imefika *17.3 million.* Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; mlinunua magari mengine zaidi au kwa nini hii imeongezeka kwa mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa kwanza wa Tume hii ulikuwa ni mwaka wa matayarisho. Kwa hali hiyo, hizi gharama za uendeshaji zinakuwa nyingi na hiyo ndiyo sababu mojawapo kubwa. Safari zinakuwa

nyingi za matayarisho ya Tume kwa utendaji kazi wake. Ahsanteni.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Sub vote* hiyo hiyo, kifungu kidogo cha 210100 - *Basic Salaries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka juzi na mwaka jana, hii mishahara haikupishana. Mwaka huu anatumia shilingi milioni 199 kwa ajili ya mishahara, ukilinganisha na shilingi milioni 25 ambazo alitumia mwaka jana. Kitu gani ambacho kimesababisha mishahara hii kupanda kiasi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, naomba arudie kidogo.

**MWENYEKITI:** Mishahara kwa nini imepanda Mheshimiwa Naibu Waziri katika *Directorate* hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshazungumza kuwa kumekuwa na ongezeko la wataalamu walioajiriwa. Kwa vyovyote vile na mishahara yao inaongezeka.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 220600. Nauliza kuhusu hizi *Clothing, Bedding, Footwear and Services.*

Mwaka jana hatukutenga fedha yoyote. Mwaka 2010/2011 tulitenga shilingi milioni 800, lakini mwaka huu

tumetenga shilingi milioni 20; kwa nini imetoka sifuri mpaka shilingi milioni 20 kwa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimedondosha Kitabu nimepoteza ukurasa unisamehe. Nivumilie dakika moja tu, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Tume imeanza *operations* upya, ina askari, ina madereva na wahudumu, ambao wote wana *uniform* na hii ndiyo maana imeingia katika gharama hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* … … ... Sh. 210,459,000

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma ya 230700 - *Routine Maintenance and Repair of Office Equipment and Appliances*. Ina maana hizi *appliances* zimeanza kufanyiwa matengenezo sasa hivi, miaka ya nyuma hazikuwepo au ni nini? Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** *Appliances* wakati mwingine zinaongezeka, matumizi au tuseme *maintenance* kwa mwaka wa kwanza mara nyingi siyo kubwa kwa sababu zinakuwa ni mpya. Sasa huu ni mwaka wa pili tunaendelea, kwa hiyo, *maintenance* inakuwepo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*...Sh. 237,253,000
Kif. 1007 - *Library and Documentation Unit*...Sh. 124,081,000
Kif. 1008 - *Management Information System* ........ Sh. 188,744,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Macro Economy Cluster* ... Sh.1,036,909,000

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo machache tu katika kifungu hicho. Ukienda kwenye Kasma 210100 na 210300 nilitaka kupata ufafanuzi

**MWENYEKITI:** Swali moja tu Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** *Sorry,* ukifanya *comparison* mwaka jana ilikuwa shilingi 384,000,000, sasa hivi imekwenda *less* imekuwa shilingi 94,183,000 *then*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Swali ni moja tu huwezi kwenda *then;* nyingine ya nini ni moja tu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndiyo zile Idara zenye

Wataalamu wapya walioongezeka, kwa hiyo na mishahara imeongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa imepungua haijaongezeka. Umeiona hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Naam, *okay sorry.* Unataka kunisaidia? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoona kwenye *Basic Salary* imepungua lakini ukienda chini *Personal Allowances (Non Discretionary)* zimeongezeka.

Wale ni watumishi ambao mwanzoni hatukuwalipa mishahara kulingana na Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Sasa tumewaingiza *direct* kwenye mfumo huo wa Serikali. Kwa hiyo, pale chini tunawalipa *special allowance* ili kuwa-*maintain* katika Wizara hiyo ya Mipango.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Productive Sector Cluster* … …Sh. 485,681,000
Kif. 2003 - *Infrastructure and Services Cluster* …Sh. 442,018,000
Kif. 2004 - *Social Service and Demographics Cluster*Sh. 445,027,000

Kif. 2005 - *International Trade and Econ Relations*…Sh. 474,580,000
Kif. 3001 - *Social Service and HR Development* …Sh. 90,417,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais (Sekretariet ya Ajira Katika Utumishi wa Umma)**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* Sh. 1,045,216,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye *Sub vote* 1001, *Item* 220800 – *Training Domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sekretarieti ya Ajira ya Serikali naiona kama chombo muhimu sana. Watu ambao wanaendesha ajira kwa maana ya *recruitment* kwa ajili ya wafanyakazi wanaoingia kwenye Utumishi wa Serikali wanapaswa wapate mafunzo mazuri na ya ziada pengine kuliko ilivyo sasa. Inashangaza tunapoona Serikali inapanga shilingi 6,000,000 kwa ajili ya shughuli hiyo. Ukiangalia pia *foreign training* ndiyo haipo kabisa. Sasa hata ya ndani unapanga shilingi 6,000,000! Hivi tunataka Sekretarieti hii iwe na wataalamu wa namna gani kama hatuwezi kuendelea kuwafundisha ili waweze kutupa watumishi ambao ni wazuri zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi ya *training* kwenye Sekretarieti yapo *covered* kwenye Kitabu cha Nne kwenye *Development.* Kwa hiyo, kule tutaona kwamba watu wanapelekwa *training foreign* na ndani ya nchi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi niko Kasma 210100 - *Basic Salaries – Pensionable Posts*. Naona hii mishahara inabadilika sana; mwaka 2010 ilikuwa shilingi 102,165,387, ikapanda 2012 mpaka shilingi 233,670,000, sasa hivi imeshuka shilingi 157,619,000; inakuwaje inabadilika kiasi kikubwa hivyo mwaka hadi mwaka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara inabadilika badilika kulingana na mahitaji ya wakati husika.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Najielekeza kwenye *Sub vote* 2 kidogo nina sababu za msingi. Moja ni ile Kasma Namba 227500, lakini pia kwenye Kasma Namba 229900, kuna hizi *terms* ambazo zinatumika; moja ile inaandikwa *Other Supplies and Services*. Pia kuna *Other Operating Expenses.* Pale nyuma wakati tunaangalia *Vote 66* niliulizia kuhusiana na hii *Other Operating Expenses* nikajibiwa kwamba kuna matumizi kama ya *research.*

Naomba Serikali itueleze ni kwa nini haitaki kufanya *specification* kwenye vitabu hivi tujue hizi fedha moja kwa moja zinakwenda kutumika kwenye

*research*. Kwa kuwa haya ni masuala ya *Public Service Recruitment,* naiomba Serikali ...

**MWENYEKITI:** Uko kifungu gani; naomba uwe *specific* uende kwenye kifungu kimoja *directly* halafu uliza swali lako. Usirudi nilipokwisha kuhoji, unavunja kanuni na nitakupiga adhabu yangu. Wewe nenda kwenye kifungu unachokitaka na niambie hoja yako ni nini. Kwa hiyo, kwenye fungu hilo tulilopo sasa unataka nini na kwenye kifungu gani?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Naomba ufafanuzi kuhusiana na Kasma Namba 229900 kuhusiana na *Other Operating Expenses*. Kwa nini Serikali haitaki kufanya *specification*; Naibu Waziri wa Fedha ameeleza kwamba unapozungumzia *Other Operating Expenses* unajihusisha kwenye masuala ya *research* na kadhalika. Nilitaka nijue hizi *Other Operating Expenses* ambazo haziko *specified* ni sababu gani ambazo zinaifanya Serikali isiweze kufanya *specification* ili tujue hizi fedha zinakwenda kufanya shughuli gani moja kwa moja badala ya kuwa na *statements* ambazo ni *too general.*

**MWENYEKITI:** Unaitaka Serikali katika nini; kwenye kifungu hiki sasa hutaki kujua ni kwa ajili ya kazi gani? Wewe unaitaka Serikali kwa ujumla. Sasa kama unataka majibu haya kwa hoja ya Serikali kwa ujumla itabidi usubiri *Finance Bill* wakati tunamalizia. Ulitakiwa umwulize Waziri fungu hilo fedha hiyo umeipanga kwa ajili ya kushughulikia nini?

Sasa kwa sababu suala lako haliko *specific,* naomba tuendelee. Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ………… Sh. 159,478,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation* …Sh. 74,337,000

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilitaka ufafanuzi kidogo tu kwenye Kifungu 202300 - *Fuel, Oils, Lubricants* kwa mwaka huu haikutengewa chochote; ni kwamba hawa watu hawatasafiri, hawa hawatatumia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu; hakuna fedha iliyotengwa kuna matatizo gani kwenye hiyo *Directorate* ya *Planning, Monitoring and Evaluation?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Utawala lipo hilo fungu ndilo litakalohudumia pamoja na *Planning Unit*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Government Communication Unit…* …..Sh.33,373,000

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 220600 - *Clothing, Bedding, Footwear and Services* na wameweka shilingi 7,000,000. Nashangaa ni nani ananunuliwa viatu na nguo huko Serikalini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri lilishajibiwa na Naibu Waziri wa Fedha kwamba, fungu hili ni kwa ajili ya sare za watumishi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Legal Services* … … ............. Sh. 24,924,000
Kif. 1006 - *Procurement Management* ......... Sh. 46,832,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Management Information Systems* … Sh.111,988,000

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 221100 – *Travel Out of Country*. Ningeomba Serikali ianze sasa kutupa ufafanuzi, *Travel*

*Out of Country going to do what?* Wawe wanatueleza ili tuelewe *they travelled for what purpose?*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli Mheshimiwa Waziri hebu jibu lakini haya maswali mengine yanatupotezea muda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa rejea zaidi angeenda kwenye randama atafahamu maana yake ni nini. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma Namba 229900 - *Other Operating Expenses.* Naomba niwe *specific* hapa Serikali inielewe.

Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie kujua kwa nini hamfanyi *specification* kwenye suala la matumizi ya hizi *Other Operating Expenses,* kwa sababu *it is too general.* Ningeomba nijue, kule mmetuambia kwamba kwenye *research*. Tungependa muweze kufanya *specification* kama ambavyo mmefanya kwenye vifungu vingine; *fuel* na kadhalika. Kwa hiyo *note here* sijui kwa nini iko hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tatizo sisi tunatumia *International Standards,* katika *International Financial Standards* huwa kuna *standard* maalum ambayo imewekwa. Sasa huwezi ukasema kwamba *Operating Expenses* za Idara fulani zinafanana na Idara fulani au na Wizara fulani, lazima

itakuwa tofauti. Kwenye Idara ambayo kuna *research* na kwa kuwa hakuna kipengele cha *research* unaweka *Other Operating Expenses.*

Kwa hiyo, utaona hii *Other Operating Expenses* ni sawa na zile *Non Classified Expenses* kwamba haziko kote huko juu ndiyo unaziweka hapo kwenye *Operating Expenses.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine niwaombe ndiyo maana randama za shughuli ya kesho zimeshakabidhiwa hapa Mezani. Kwa hiyo, kama mtu anataka kujua ufafanuzi zaidi anatakiwa awasiliane tu na Ofisi atajua hivi vifungu vyote hapa na kila siku randama zote za Wizara zote ziko hapa. Matumizi hayo hayaoneshwi kwenye hiki Kitabu, yanayoneshwa kwenye randama ambazo tunawaagiza Mawaziri waziweke hapa Mezani. Kwa hiyo, sasa Waheshimiwa Wabunge msiwe wazembe wa kuchukua randama na kuzisoma ili muweze kuelewa vizuri taarifa hizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Internal Audit*… … … Sh. 1,547,215,000
Kif. 2001 - *Recruitment Management Division* Sh. 798,800,000
Kif. 2002 - *Quality Control* … … Sh. 148,509,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 - Ofisi ya Rais (Tume ya Utumishi wa Umma)**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*... Sh. 2,116,437,000
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit* ........................................................................ Sh. 318,860,000
Kif. 2001 - *Civil Service* … …. …. …. …. …. …. ….... Sh. 212,956,000
Kif. 2002 - *Local Govornment Service* … …. …. …. Sh. 268,060,000
Kif. 2003 – *Teachers' Services* … …. …. …. …. …. Sh. 4,595,461,000
Kif. 2004 - *Fire and Immigration Service* … …... …. Sh. 197,719,000
Kif. 2005 - *Health Service* … …. … …. ….. ... … ....… Sh. 228,717,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais (Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri)**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … …. …......... …. Sh. 50,382,037,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote 30, Sub vote 1003,* Kasma 4921 - *Property and Formalization Program*, ambacho ndiyo kifungu cha MKURABITA na mwaka huu wa fedha

kimetengewa bilioni mbili, pungufu ya mwaka uliopita kilipotengewa bilioni tatu. Ninataka nipate ufafanuzi kuhusu jambo moja; nimeangalia mgawanyo kwenye randama wa shilingi bilioni mbili. Kwenye Bajeti iliyopita niliiomba Wizara ifuatilie kwa sababu eneo mojawapo ambalo linashughulikiwa ni Kimara Baruti. Nikaiomba Wizara ishughulikie suala linalohusu ile Kampuni ya *Twiga Chemicals* hekari nane ambazo zilitaka kupokonywa. Sasa kwa kuwa kiwango hiki cha pesa kilichotengwa kwa ajili ya kufanikisha utolewaji wa hati nataka kujua hati zitakazotolewa safari hii katika utekelezaji wa kiwango hiki ni pamoja na hati za hekari nane ambazo inapaswa kuzuiliwa kuchukuliwa na Kampuni ya *Twiga Chemicals* na badala yake ardhi itumike kwa ajili ya wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa pale Kimara Baruti haujakwisha, kwa hiyo, fedha zake hazipo hapa. Ukishakwisha ule mchakato tutampatia kama tutaamua kwamba kweli wachukue wananchi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda dakika zangu zimebakia kumi kabla ya kumaliza, sasa tutapitisha Bajeti hii kwa mafungu yote kwa umoja wake ili tuweze kumaliza kazi yetu. Katibu hatua inayofuata.

## Fungu 32 - Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma)

Kif.1002 - *Administration and HR Management* . … Sh. 3,573,393,000
Kif.1002 - *Finance and Accounts Unit*… … …......... Sh. 100,000,000
Kif.1003 - *Govornment Communication Unit* … ….. Sh. 175,000.000
Kif.1004 - *Procurement Management Unit*… ….. Sh. 450,000,000
Kif.1006 - *Planning Division* … … …. …. …. …. ..…. Sh. 2,762,000,000
Kif.1007 - *Information and Communication Tech. Unit*…...............................................................................
…Sh. 150,000,000
Kif.2001 - *Policy Development Division* ……. … … …Sh. 1,174,010,000
Kif.2002 - *Management Services Division*……. …. Sh. 1,826,370,000
Kif.2003 - *Establishment Division* … … … … … …... Sh. 531,150,000
Kif.2004 - *Ethic Promotion Division* … … … … …..…Sh. 180,360,000
Kif.3002 - *Human Resources Development Unit* … . …...................................................................
..Sh.1,264,284,000
Kif.3002 - *Tanzania Public Service College* … … …............ … Sh. 0
Kif.3004 - *Diversity Management Unit* … … … ….. Sh. 639,000,000
Kif.4002 - *Management Information System*

*Division*........................................................................ Sh. 2,063,000,000
Kif.4003 - *Records and Archives Divion* ... .... ..... ....Sh. 7,521,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Umma**

Kif.1001 - *Administration and HR Management* ... .... ......... Sh. 0
Kif.1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit* ............................................................................Sh. 828,161,000
Kif.1004 - *Governmentt Communication Unit* ... ... ...Sh. 274,850,000
Kif.1008 - *Legal Services Unit* ... ... ... ... ... ... ....... ..Sh. 92,050,000
Kif.2001 - *Public Service Leaders Unit* ... .... ......... ...Sh. 191,874,000
Kif.2002 - *Political Leaders Division* ... .... .... ......... ...Sh. 80,320,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 – Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu)**

Kif.1003 - *Planning and Monitoring Division* ... .... .... ............. Sh. 0

Kif.2002 - *Productive Sector Cluster* ... .... ... ....... Sh.1,200,000,000
Kif.2004 - *Social Srvc and Demographics Cluster* ... ..Sh. 924,733,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Tukae, mtoa hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba nimtambue Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, nilimsahau ambaye alichangia kwa kusema na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais; Fungu 20 – Ikulu, Fungu 30 – Ofisi ya Rais na Baraza la Mawaziri, Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 9 - Ofisi ya Rais - Bodi ya Mishahara na Maslahi kwa Utumishi wa Umma na Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Hoja iliyowekwa hapa Mezani asubuhi inalitaka Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na (Utawala Bora), pamoja na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu), kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Sasa nitawahoji ili muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na (Utawala Bora) pamoja na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu) kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hata ninyi ni mashahidi, walioafiki wameshinda na mafungu haya ya Ofisi hizo zote kama nilivyozisema na zilivyoonekana kwenye *Order Paper* yetu ya leo, yamepitishwa rasmi.

Waheshimiwa Mawaziri, niwatakie kazi njema, utumishi uliotukuka, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa makini na uadilifu mkubwa, kwa maendeleo na manufaa ya Wananchi wa Tanzania wote. Kwa hiyo, nawatakia kila la kheri katika kutekeleza wajibu wenu.

Waheshimiwa Wabunge, nimekataa mwongozo uliokuwa unaombwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja, sijajua ni nani. Asubuhi nilitoa mwongozo wangu kwenye Kiti kwamba, sasa tunaendelea kukiuka taratibu; mtu yeyote anayetaka kusema lolote atasimama kwa kutulia kwenye Kiti chake bila kusema neno na bila ku-*shout*, macho ya Spika yakishamwona ndiyo atampa utaratibu.

Suala hili tumeshaanza kulivunjavunja tena hapa katikati. Sasa nadhani turudi kwenye ule utaratibu ili tuendeleze nidhamu ya Bunge letu.

Naomba niendelee na matangazo niliyonayo hapa; tangazo la kwanza nimeletewa na Uongozi wa Michezo wa Bunge wanasema, Wabunge wa Timu ya *Simba Sports Club* wanakumbushwa kuendelea na mazoezi.

Mechi yao kati ya Wabunge wa Yanga haijaahirishwa kama taarifa hizo zinavyoenezwa na Wabunge wa Yanga kwa kupotosha na kwa hofu kubwa na kipigo wanachokihofia Siku ya Jumamosi. Sasa ukweli wa jambo hili mimi siujui ila nimeombwa sana, kama kuna meseji mmeshaanza kupatapata huko, naomba mjue kwamba hiyo mechi kati ya Yanga na Simba ipo kama ilivyokuwa imepangwa na itaendelea kama ilivyotakiwa ishughulike kutoa burudani kwa siku hiyo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

*(Saa 2.13 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Tarehe 4 Julai, 2012*
*Saa Tatu Asubuhi)*